# Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili

A.G. Were-MWARO

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamifu

Doctor of Philiosophy (Ph.D)

Katika
Idara ya Lugha na Isimu
Chuo Kikuu Cha Egerton
KENYA.

2000

IFRA
IFRA006842

IFRA
No. d'inventaire
Date 06/ 03 /05
Cote WER 410

# UUNGAMAJI

**Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote kile. Ni kosa kutolesha nakala ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi na/au Chuo Kikuu cha Egerton.**

GEORGE AGGREY WERE-MWARO

4.8.2000

**Tarehe**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yangu mimi niliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton kuisimamia.**

PROFESA ROCHA M. CHIMERAH
CHUO KIKUU CHA EGERTON,
IDARA YA LUGHA NA ISIMU,
S.L.P. 536, NJORO-KENYA.

7.8.2000

**Tarehe**

CHUO KIKUU CHA EGERTON, NJORO-KENYA.

# TABARUKU

Kwa Maulama wote wanaotambua ukweli wa usemi huu:

> Kiswahili katika Kenya kinaweza kulinganishwa na tajiri mwenye nguo katika sanduku kumi chumbani, halafu akaingia katika mashindano ya uvaaji huku akiwa amevalia kikoi kilichopasuka akishindana na maskini mwenye kanzu moja maridadi.
> (Wency Cornel, "Taifa Weekly," Nov. 24, 1979).

**SHUKRANI**

Ama kwa hakika masuala ya kiakademia hayakamilishwi 'vivi hivi tu' pasi na usaidizi wa hapa na pale. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati na wala sio za chati kwa wote walionifaidi. Awali ya yote, ninatoa shukrani kwa Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro, kwa kunisajili na kunidhamini ili nifanye utafiti kwa ajili ya shahada ya uzamifu *(Doctor of Philosophy)* katika eneo la isimu ya Kiswahili (Leksikografia) kwa kuzingatia 'usayansi' wa istilahi. Naona fahari kubwa kutaja majina ya watu kadhaa walionifaa, wakanielekeza na kuniongoza na kunifikisha salama kando ya bahari hii tesi yenye mangi masi.

Nawashukuru sana viongozi wa Chuo Kikuu cha Egerton wakiwemo wastahiki wafuatao; Prof. J. Kiptoon (Mkuu wa Chuo), Prof. W.K. Kipng'eno, Prof. A.M. Mutema, Prof. R.W. Mwangi (Makamu wa Mkuu wa Chuo) na Prof. Dankit Nassiuma kwa kunishauri nisikate tamaa, hususani katika nyakati ngumu ambapo fedha ziliadimika chuoni. Vile vile, naona fahari kumtolea kongole **msimamizi** wangu Prof. Rocha M. Chimerah kwa kuisoma, kuikosoa, na kuirekebisha tasnifu hii. Vilevile namshukuru Dkt. Abel G. Gibbe kwa kuiwekea msingi kazi hii. Ama kwa kweli bila ya wao ningekwama. Daima nitakumbuka usaidizi wao na kujitolea kwao kuniongoza katika kufikia ufanisi uliopo.

Kadhalika nawashukuru wahadhiri wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hasa Dkt. R. Mekacha (Mkuu, Idara ya Kiswahili), Dkt. Z.N.Z. Tumbo-Masabo (Mkuu, Istilahi na Tafsiri), Dkt. A. Chuwa (Mkuu, Leksikografia), Dkt. E.K.F. Chiduo, Prof. A.M. Khamisi, na Prof. D. Massamba (Mkuu, Isimu). Pia, natoa shukrani kwa Prof. T.Y. Sengo (Mkuu, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii) wa Chuo Kikuu cha Uislamu-Uganda, Prof. R. Mukama na Dkt. M.J.K. Muranga wa Chuo Kikuu cha Makerere kwa mazungumzo mengi na msaada wao nilipokuwa huko. Siwezi kamwe kuwasahau Prof. H.J.M. Mwansoko (Mwenyekiti, BAKITA), na Prof. J. Mdee wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao walinikimu kwa mengi. Vile vile, shukrani zangu za dhati ziwaendee Bw. R. Wafula , Prof Ireri Mbaabu, Dkt.

P. Musau, wa Chuo Kikuu cha Kenyatta, Bw. R. Mgullu, Dkt. K. wa Mutiso, Dkt. J.H. Habwe, Dkt. Mwenda Mbatiah wa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kujaza kidadisi vizuri na kunipatia mawaidha ya busara. Prof. Mwansoko, Prof. Tumbo-Masabo na Prof. Mdee pia walinifaa sana kwa kunipa tasnifu na vitabu vyao chungu nzima.

Pia nasema kongole kwa Dkt. K.B. Kiingi, Bw. Said Karama, Prof. S.A. Mohamed, Bw. A.S. Nabhany na Sheikh H. Akida kwa kunielekeza ipasavyo. Aidha nawashukuru wakwasi, wahadhiri, na wazami wenzangu Bw. J.K. Mutiti, Bi. Sheila Wandera, Ndg. E.S. Mohochi, Dkt. K. Njoroge, Dkt. C. Kitetu, F.O.B. Aswani, I.Y. Mwamzandi, J. Marani, Siteti wa Ngero, O.J. Ogolla, Bi. R. Liguyani, na Bi. Anne J. Mahero kwa ushakii wao uliobainika katika mijadala yetu ya pamoja na nikapata mawazo yaliyonifaa zaidi.

Kadhalika, sina budi kuwatolea shukrani zangu za dhati wazazi wangu Baba Festus O. Were, na Mama Regina O. Were pamoja na mke wangu mpendwa Bi. Christine J.N. Mwaro kwa usaidizi wao wa hali na mali na uvumilivu wao wakati wote nikifanya utafiti wa tasnifu hii. Katika kundi hili naweka wanangu wapendwa Laura, Tabibu na Olope Humphrey George Mwaro (Jnr.), pamoja na baba mkwe Nelson L. Nakhone kwa uvumilivu na upendo wao. Nawashukuru pia marafiki zangu Bw. Beneah M. Mutsotso, Bw. David Ngaywa, Bw. V.L. Ondedo, Robert Mukwenyu, Francis Okoth, Bi. F. Indede, Robert Oduori, Bi. Lilian Sanya, Martini Simiyu, Stephen Wesonga, L. Muaka, J.N. Michira, Ndg. Joseph Jamoko Madiro, Ndg. Stephen Okwero na Mwalimu G.M. Lubale kwa kunitia moyo na kunishawishi nikaze kamba.

Mwisho, nazitoa shukrani zangu kwa Bwana na Bibi Mwamzandi kwa kuichapisha na kuisoma tasnifu hii.

Kwenu nyote nasema kongole!

# UFUNGUO WA ISHARA, VIFUPISHO, MTINDO WA KIMAANDISHI NA MANENO ADIMU

## Ishara

| | |
|---|---|
| === | Sawa kisemantiki |
| = | Sawa |
| > | Ni kubwa kuliko |
| < | Ni ndogo kuliko |
| /--- | Mazingira |
| O | Mofimu kapa |
| : | Ili kwamba |
| [ ] | Mabano ya bloku |
| ( ) | Mabano ya kijumla |
| / | Ukanusho k.m. ---, ==== |
| ---- | Kitamkwa kinachotajwa |
| + | Ukiongeza |
| R | Kiwango cha kupendekeza kitamkwa kupata Hadhi ya istilahi |
| ---- | Inageuka na kuwa, inakuwa |
| X, X', X," | Vitamkwa |
| P | Jumla ya alama |

## Lugha

| | |
|---|---|
| **Kigiritini** | Kigiriki + Kilatini |
| **Kigirikilatini** | Kigiriki + Kilatini (Greco-Latin) |
| **Sw.** | Kiswahili |
| **Gd.** | Luganda |

**Mtindo wa Kimaandishi/*Coding***

| | |
|---|---|
| *Normal*/Kwaida | Mwandiko wa kawaida wa matamko ya Kiswahili |
| *Bold*/**Mwangazo** | Ufafanuzi wa mada, istilahi, na msisitizo katika nukuu |
| **Italiki** | Tafsiri ya lugha isiyokuwa Kiswahili |

**Vifupisho Vinavyounda Akronimu PEGITOSCA**

| | |
|---|---|
| **P** | Precision (Udhahiri) |
| **E** | Economy (Iktisadi) |
| **G** | Generativity (Uzalishaji) |
| **I** | Internationality (Umataifa) |
| **T** | Transparency (Uangavu) |
| **O** | (Anti-) Obscenity (Ustara) |
| **S** | Systemicity (Utaratibu maalum) |
| **C** | Consistency (Utaratibu ulio sawa) |
| **A** | Appropriateness and Acceptability (Ufaafu na Ukubalifu) |

**Vifupisho vya Vyombo vya Kukuza Lugha**

| | |
|---|---|
| **BAKIKE** | Baraza la Kiswahili Kenya |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili la Taifa (Tanzania) |
| **CHAKITA** | Chama cha Kiswahili cha Taifa (Kenya) |
| **TUKI** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (Tanzania) |

**Maneno Adimu**

| | |
|---|---|
| **Usayansi** | Ni uwezekano wa maneno/istilahi kuweza kufanyiwa utafiti mahsusi na kuelezwa kimantiki ili ubora wake ueleweke kwa walengwa kwa kuzingatia kanuni maalum za uundaji istilahi. |

| | |
|---|---|
| **Kusharabu** | Ni kuswahilisha maneno/istilahi za kigeni baada ya kuzifanyia marekebisho ili zilingane na muundo wa Kiswahili |
| **Uundaji** | Ni uzalishaji wa istilahi/neno mpya kuwakilisha dhana fulani pale ambapo halipo |
| **Ubunaji** | Ni 'uimarishaji' wa istilahi/maneno zilizopo kwa kuzipa sura nyingine, kuzifinyanga au kuzipa muktadha mwingine wa utumizi |
| **Istilahi** | Ni ishara ya kiisimu inayorejelea dhana moja au zaidi. Istilahi yaweza kuwa neno, au kifungu cha maneno, herufi, akronimu n.k. Istilahi, tofauti na neno ambalo hutegemea muktadha, hutegemea **mfumo wa dhana** ambamo dhana hupatikana. |
| **Lugha za Kibantu** | Ni lugha za Kiafrika zinazotumia neno "Bantu." Mifano ya lugha za Kibantu ni Kikuyu, Kiluhya, Kipokomo, Kimijikenda, Kinyamwezi, na nyingine nyingi. |

# YALIYOMO

Ukurasa

UUNGAMAJI....................................................i
TABARUKU....................................................ii
SHUKRANI...................................................iii
UFUNGUO WA ISHARA, VIFUPISHO, MTINDO WA KIMAANDISHI NA
MSAMIATI ADIMU...............................................v
ORODHA YA JEDWALI...........................................xv
*ABSTRACT* (Ikisiri)........................................xvi

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI...................................................1
1.0 Usuli wa Mada............................................1
1.1 Mada ya Utafiti..........................................3
1.2 Azma ya Utafiti..........................................4
1.3 Upeo wa Tasnifu..........................................5
1.4 Nadharia Tete............................................6
1.5 Natija ya Utafiti........................................6
1.6 Dhana za Kinadharia.....................................11
1.7 Njia za Utafiti na Uchanganuzi..........................14
1.7.1 Mahojiano ya Ana kwa Ana..............................18
1.7.2 Kidadisi..............................................20
1.7.3 Machapisho Kuhusu Istilahi za Kiswahili...............24
1.8 Matatizo na Vikwazo Vilivyoshuhudiwa katika Utafiti.....26
1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza.............................28

SURA YA PILI
TATHMINI YA NADHARIA ZA UUNDAJI WA ISTILAHI.................30
2.0 Utangulizi..............................................30
2.1 Mbinu Tendakazi Kiistilahi..............................32
2.1.1 Mbinu ya Kutafsiri....................................32
2.1.2 Mbinu ya Kidhana......................................34
2.2 Nadharia za Uundaji wa Istilahi.........................35
2.2.1 Nadharia Jumla ya Istilahi............................36
2.2.2 Nadharia ya Istilahi za Kisayansi.....................42
2.3 Tathmini ya Nadharia za Uundaji Istilahi................44

2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili....47

SURA YA TATU

UUNDAJI WA ISTILAHI ZA ISIMU YA KISWAHILI....50

3.0 Utangulizi ....50

3.1 Maana ya Dhana ya Istilahi....51

3.2 Maana ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili....55

3.3 Maana ya Usayansi....60

3.3.1 Misingi ya Usayansi katika Isimu ya Kiswahili....60

3.3.2 Usayansi katika Istilahi za Isimu ya Kiswahili....64

3.3.2.1 Misingi ya Felber ya Istilahi....66

3.3.2.2 Misingi ya Pitch na Draskau ya Istilahi....68

3.3.2.3 Misingi ya Mwansoko ya Istilahi....69

3.3.2.4 Misingi ya Kiingi ya Istlahi....71

3.3.3 'Usayansi' katika Mbinu za Uundaji wa Istilahi....80

3.4 Umuhimu wa Uundaji wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili...94

3.4.1 Sababu za Uundaji wa Istilahi....94

3.4.1.1 Sababu za Kimaeneo za Uundaji wa Istilahi....94

3.4.1.2 Sababu za Kijamii na Kiutamaduni za Uundaji wa Istilahi....97

3.4.1.3 Sababu za Kisiasa za Uundaji wa Istilahi....102

3.4.1.4 Sababu za Kihistoria za Uundaji wa Istilahi....104

3.4.1.5 Sababu za Kiisimu za Uundaji wa Istilahi....109

3.5 Muhtasari wa Sura ya Tatu....114

SURA YA NNE

MBINU ZA UUNDAJI WA ISTILAHI ZA KISWAHILI....115

4.0 Utangulizi....115

4.1 Unyambuaji na Uambishaji....118

4.1.1 Unyambuaji....118

4.1.2 Uambishaji....132

4.2 Uambatanishaji na Uunganishaji....133

4.3 Ufupishaji....139

4.3.1 Akronimu....140

4.3.2 Uhulutishaji....143

4.3.3 Ukatizaji....145

4.4 Uradidi....146

4.5 Upanuzi wa Maana za Maneno....................................148
4.6 Ufufuaji na Ujenzi wa Mumo kwa Mumo wa Istilahi.........150
4.7 Uhusishaji wa Dhana na Kitajwa au Kazi Yake.............158
4.8 Ukopaji............................................................159
4.8.1 Maana ya Ukopaji..............................................159
4.8.2 Sababu za Ukopaji wa Istilahi za Kigeni.............161
4.8.3 Pingamizi Juu ya Ukopaji wa Istilahi za Kigeni......167
4.8.4 Uteuzi wa Lugha Changizi.................................170
4.8.4.1 Ukopaji kutoka Kigiriki-latini...........................171
4.8.4.2 Ukopaji kutoka Kiarabu.....................................172
4.8.4.3 Ukopaji kutoka Kiingereza.................................175
4.8.4.4 Ukopaji kutoka Lugha za Kibantu......................177
4.8.4.5 Ukopaji kutoka Lahaja za Kiswahili....................180
4.8.5 Matatizo ya Ukopaji kutoka Kiingereza...............182
4.8.5.1 Usawazishaji Istilahi Mkopo..............................184
4.8.5.2 Tahijia...........................................................185
4.8.5.3 Ukopaji wa Viambishi........................................188
4.8.5.4 Mpangilio wa Istilahi Mkopo zenye Maneno Ambatani....192
4.8.6 Taratibu za Ukopaji............................................194
4.8.6.1 Utohoaji.........................................................195
4.8.6.2 Kaleki.............................................................198
4.9 Muhtasari wa Sura ya Nne.,..................................203

SURA YA TANO

TATHMINI YA MBINU ZA KUUNDIA ISTILAHI ZA KISWAHILI..........206
5.0 Utangulizi..........................................................206
5.1 Tathmini ya Mbinu za Kuendeleza Istilahi za Kiswahili...207
5.1.1 Vyombo vya Ukuzaji wa Kiswahili.........................209
5.1.1.1 Chombo cha Kukuza Istilahi cha BAKITA...........211
5.1.1.1.1 Usanifishaji wa Istilahi...................................214
5.1.1.1.2 Uundaji wa Istilahi: Mbinu za BAKITA.............219
5.1.1.1.2.1 Minyambuliko ya Shina.................................224
5.1.1.1.2.2 Mifito.........................................................224
5.1.1.1.2.3 Mirakabu....................................................225
5.1.1.1.2.4 Ukopaji wa Istilahi za Kigeni...........................227

5.1.1.2 Chombo cha Kukuza Istilahi cha TUKI.............230
5.1.1.2.1 Uundaji wa Istilahi/Mbinu za TUKI...........233
5.1.1.2.1.1 Ukopaji..................................235
5.1.1.2.1.2 Uambatanishaji na Uunganishaji..........240
5.1.1.2.1.3 Unyambuaji na Uambishaji................242
5.1.1.2.1.4 Upanuzi wa Maana za Maneno..............245
5.1.1.2.1.5 Ufupishaji...............................246
5.1.1.3 Chombo cha Kukuza Istilahi cha BAKIKE...........248
5.1.1.3.1 Uundaji wa Istilahi: Mbinu za Nabhany.......250
5.1.1.3.1.1 Ufupishaji: Uunganishaji na Uhulutishaji...............................253
5.1.1.3.1.2 Ufufuaji na Upanuaji wa Maana za Msamiati Asilia...........................254
5.1.1.3.1.3 Ubunaji: Kufasiri Maana za Maneno.......257
5.1.1.4 Ukuzaji wa Kiswahili: Chombo cha CHAKITA........259
5.1.1.4.1 Njia ya Chimerah ya Kuendeleza Istilahi za Kiswahili...............................260
5.1.1.4.1.1 Uhulutishaji na Akronimu................260
5.1.1.4.1.2 Ubunaji: Fasiri ya Dhana za Kigeni......262
5.1.1.4.1.3 Ufufuaji na Upanuaji wa Maana za Msamiati Asili wa Kibantu...............263
5.1.1.4.1.4 Unyambuaji..............................266
5.1.1.4.1.5 Uendelezaji wa Maneno 'faafu' Yaliyoundwa na Watu Wengine.............268
5.1.1.4.1.6 Ukopaji.................................270
5.1.1.4.1.7 Tafsiri Sisisi...........................272
5.1.1.4.1.8 Uwekaji wa Maneno Katika Muktadha wa Utumizi.................................272
5.1.1.4.1.9 Matumizi ya Visawe......................272
5.1.2 Ukuzaji wa Istilahi za Isimu: Mbinu za Mbaabu na Kapinga............................................274
5.1.2.1 Njia ya Mbaabu ya Kuundia Istilahi za Isimu ya Kiswahili..................................274
5.1.2.1.1 Unyambuaji na Uambishaji...................275
5.1.2.1.2 Kufasiri kwa Dhana..........................277
5.1.2.1.3 Maneno 'Pendezi' Yaliyobuniwa na Watu Wengine.....................................278

5.1.2.2 Njia ya Kapinga ya Kuundia Istilahi za Isimu ya Kiswahili....................................282
5.1.2.2.1 Unyambulishaji.............................282
5.1.2.2.2 Mwambatano wa Maneno.......................284
5.1.2.2.3 Kufasiri kwa Maana ya Dhana...............284
5.1.2.2.4 Ukopaji.....................................285
5.2 Usawa katika Mbinu za Uundaji wa Istilahi za Kiswahili..289
5.2.1 Mapitio ya Mbinu za Uundaji Istilahi................298
5.2.1.1 Uunganishaji/Uambatanishaji.......................298
5.2.1.2 Ubunaji/Fasiri ya Maana za Maneno...............300
5.2.1.3 Unyambuaji........................................301
5.2.1.4 Ufufuaji na Uasilishaji wa Msamiati Asilia......302
5.2.1.5 Uhulutishaji......................................303
5.2.1.6 Ukopaji na Utohoaji...............................304
5.2.1.7 Kaleki............................................305
5.2.1.8 Upanuzi wa Maana za Maneno.......................306
5.2.1.9 Uradidi...........................................307
5.2.1.10 Finyazo (Akronimu na Ukatizaji).................309
5.3 Muhtasari wa Sura ya Tano.................................310

SURA YA SITA

TATHMINI YA ISTILAHI ZA ISIMU YA KISWAHILI..................315
6.0 Utangulizi.............................................315
6.1 Misingi ya Kutathmini Istilahi za Isimu ya Kiswahili....318
6.1.1 Tathmini ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili za TUKI..323
6.1.1.1 Utaratibu Maalum na Uzalishaji katika Istilahi..327
6.1.1.2 Matumizi Kimataifa.................................329
6.1.1.3 Udhahiri Kiistilahi................................330
6.1.1.4 Utaratibu Uliosawa Kifonolojia katika Istilahi..333
6.1.1.5 Iktisadi katika Istilahi...........................335
6.1.1.6 Uangavu Kiistilahi.................................337
6.1.1.7 Ufaafu, Ukubalifu katika Lugha na Utusani.......340
6.1.2 Tathmini ya Istilahi za Isimu za Wataalam Binafsi...344
6.2 Nafasi ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili Zilizoundwa na Watu Binafsi........................................355
6.2.1 Nafasi ya Istilahi za Isimu za Mbaabu...............355
6.2.2 Nafasi ya Istilahi za Isimu za Kapinga..............358

6.3 Matatizo katika Ukuzaji wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili....................................361
6.3.1 Matatizo ya Kiisimu....................................362
6.3.1.1 Uwezo wa Kuleta Mabadiliko katika Muundo wa Kisarufi wa Lugha....................................363
6.3.1.2 Visawe vya Kiistilahi....................................364
6.3.1.3 Tatizo la Tahijia....................................365
6.3.1.4 Namna ya Kushughulikia Viambishi vya Kiistilahi....................................367
6.3.2 Matatizo ya Kisiasa....................................370
6.3.3 Matatizo ya Kijamii....................................373
6.4 Muhtasari wa Sura ya Sita....................................375

SURA YA SABA

TAMATI....................................379
7.0 Mchango wa Utafiti huu....................................379
7.1 Mapendekezo....................................381
7.2 Hitimisho....................................386

VIAMBATISHO

Kiambatisho cha 1: Dhana ya Kinadharia ya Istilahi za Kisayansi....................................388
Kiambatisho cha 2: Istilahi za Isimu ya Kiswahili..........389
Orodha ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili Zilizotathminiwa....................................391
Kiambatisho cha 3: Kidadisi Juu ya Mtazamo wa Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili na Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu....................................393
Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili....................................393
Wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu....................................397
Mahojiano Juu ya Mtazamo wa Waandishi (wa Vitabu na Magazeti) na Watangazaji Redioni na Televisheni)........401
Mahojiano na Waandishi wa Vitabu na Magazeti........401
Mahojiano na Watangazaji Redioni na Televisheni.....403

Kidadisi Juu ya Mtazamo wa Wahadhiri wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu....................................405

Kidadisi Juu ya Mtazamo wa Waundaji Istilahi za Kiswahili....................................409

Waundaji Istilahi Binafsi..............................409

Vyombo vya BAKIKE, BAKITA na TUKI....................411

Waundaji Istilahi Binafsi na Maafisa wa Vyombo Waliohojiwa....................................413

MAREJELEO..........................................414

# ORODHA YA JEDWALI

Ukurasa

Jedwali la 1: Usawa katika Mbinu za Uundaji Istilahi........290

Jedwali la 2: Ufaafu wa Istilahi.............................325

Jedwali la 3: Usayansi katika Istilahi za Isimu.............346

Jedwali la 4: Kiwango cha Usayansi Kulingana na Data........348

Jedwali la 5: Mbinu za Uundaji Istilahi za Isimu Kulingana na Data......................................352

Jedwali la 6: Istilahi za Isimu Zisizo na Usayansi Ikilinganishwa na Zile Zilizopendekezwa na Walengwa.......................................358

*ABSTRACT* (Ikisiri)

**The Scientificity of Swahili Linguistic Terminology**

This thesis was on the 'Scientificity" of Swahili linguistic terminology and methods used in word coinage so that we can determine reasons for their acceptability. The principal objective of the thesis was to evaluate scientificity in methods or approaches used in Kiswahili word formation in order to establish how they can be modified so as to develop this language. The study attempted to investigate the extent to which Kiswahili coined terminology are scientifically based by choosing three research institutes (TUKI, BAKITA, BAKIKE) and renown word coiners (Mbaabu, Nabhany, Kapinga).

The study was guided by the Theory of Scientific Terminology (henceforth TST) of **PEGITOSCA** and E. Wüster's General Theory of Terminology (henceforth GTT). TST is a theory which was coined by Kiingi (1989) and it has a scientific scale which can be used to depict the appropriateness, acceptability or rejection of a terminology. It is an acronym of Precision (P), Economy (E), Generativity (G), Internationality (I), Transparency (T), anti-Obscenity (O), Systemicity (S), Consistency (C), and language relative Acceptability (A). For a language whose scientific lexicon is being expanded, it is of cardinal importance to ensure that these criteria are taken into consideration. The study was conceived as a systematic contribution to the solution of the problem of Swahili linguistic terminology elaborations. The thesis makes it possible for Swahili word coiners to think of appropriate method(s) of lexical formation so as to coin easily and internationally acceptable Swahili terminology.

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Usuli wa Mada

Suala la uendelezaji wa leksikoni limewavutia wataalam wengi ulimwenguni (Haugen, 1966; Ferguson, 1971; Fishman, 1974; Daswani, 1989). Kadhalika, juhudi za kuendeleza leksikoni katika nchi za Ulaya na katika mataifa mengi yanayoendelea zimeongezeka maradufu tangu kumalizika kwa vita vya pili vya dunia (Sager na Johnson, 1978). Msingi wa harakati hizo umekuwa ni kuimarisha mawasiliano baina ya mataifa yanayotumia lugha tofauti tofauti na, kwa namna hii, kukuza uelewano lugha wa kimataifa. Miongoni mwa mataifa ambayo yamejaribu kusasaisha na kuendeleza lugha zao za kitaifa kileksikoni kwa matumizi ya kitaaluma ni Sweden (Selander, 1980), Japan (Sugito, 1989), China (Pasierbsky, 1989), Somalia (Andrzejewski, 1983), Israel (Fellman, 1974), India (Daswani, 1989), Ujerumani (Coulmas, 1989) na Tanzania (Mwansoko, 1990). Katika nchi ya Tanzania, shughuli za kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kiistilahi zinafanywa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na waundaji wa maneno binafsi. Vyombo hivi (BAKITA na TUKI) ni vya kitaifa na wala siyo vya kimataifa (Mbaabu, 1991) ingawa vimeendelea sana katika kuunda istilahi za taaluma mbalimbali (kemia, fizikia na isimu) zenye ukubalifu wa kimataifa kwa walengwa wa Kiswahili (Massamba, 1989:67). Nchini Kenya wanaoshiriki katika kazi ya uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili

ni Baraza la Kiswahili la Kenya (BAKIKE), Mashirika ya Kiserikali, na waundaji istilahi binafsi. Mathalani, Nabhany (1982), Mbaabu (1991) na Chimerah (1998), ni miongoni mwa wataalam ambao wamejitokeza na mbinu tofauti za kukuza istilahi za Kiswahili.

Nabhany, badala ya kutumia maneno yaliyoazimwa katika Kiingereza au Kiarabu, anaunda istilahi kwa kutafsiri maana ya viungo vidogo vya maneno vyenye maana kutokana na lahaja kadhaa za Kiswahili. Kwa mfano, **runinga** (*television*), **rununu** (*telephone*), **kijuwo** (*book*) (taz. pia 5.1.1.3 uk. 248).

Naye Kiingi (1989), baada ya kugundua kuwa hakuna mfumo maalum unaofuatwa na waundaji istilahi za Kiswahili, amependekeza kuwa istilahi za kisayansi kama vile kemia, fizikia na bayolojia ziundwe kwa kutazama baadhi ya mofimu zinazoweza kurekebishwa na kunyambuliwa ili zijenge neno jipya. Kwa mfano:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** | **Mifano** |
|---|---|---|
| '*Hydro*' | -maji | '*Hyrogen*'===**kiundamaji** |
| '*-phyte*' | mea | '*Hydrophyte*'===**kimeamaji** |
| | | '*Neophyte*'===**Kimeachanga** |

Hata hivyo, baadhi ya istilahi zinazoundwa na wataalam binafsi hawa na aidha vyombo vya BAKITA, BAKIKE, TUKI zimekataliwa na watumizi wa lugha hii kwa madai kwamba hazina 'usayansi' ama 'mwonjo' (Temu, 1984; Khamisi, 1987; taz. pia 3.3, uk. 60 na 3.3.2, uk. 64).

Kazi hii, kwa hivyo, ilikuwa jaribio la kuchunguza 'usayansi' wa istilahi za isimu ya Kiswahili na mbinu zinazotumiwa kwa minajili

ya kuibua sababu za kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi kwa walengwa wa lugha hii ya Kiswahili wa Afrika Mashariki. Ilhamu ya kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili imetokana na lugha hii kutaka kujieleza yenyewe katika uwanja wa isimu.

## 1.1 Mada ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutalii swala la 'usayansi' katika uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili ili kutatua tatizo kubwa katika ukuzaji wa lugha hii, hasa katika 'isimu'. Katika kujadili istilahi za isimu ya Kiswahili, tulitaka kuchunguza kama istilahi zinazoundwa zinazingatia misingi ya kisayansi. Tulitathmini mbinu zinazotumiwa na BAKITA, BAKIKE, TUKI na wataalam wa Kiswahili hususani Mbaabu, Kapinga na Nabhany, ili kuona kama zinazingatia 'usayansi.' Pia tulitaka kujua kama mfumo wa sayansi unatumiwa katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili.

Maswali yaliyoongoza utafiti huu yalikuwa ni:

- Je, istilahi kukosa usayansi ndani yake huchangia ukubalifu/ ufaafu wake?
- Je, ni mbinu gani inayotumiwa kuunda istilahi zenye usayansi na ukubalifu wa kimataifa?

Maswali haya mawili ndiyo yaliyokuwa kiini cha kazi hii na yalitokana na sababu kwamba istilahi nyingi za Kiswahili zinazoundwa hukataliwa na wataalam na watumizi wa lugha ya Kiswahili (Mdee, 1980). Suala hili la 'usayansi' katika istilahi na mbinu za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili lilikuwa halijafanyiwa utafiti wa kina kirefu. Kabla ya utafiti huu wataalam wa Kiswahili walioshughulikia suala la uendelezaji wa

istilahi za Kiswahili ni, mathalani Ohly (1977), Mdee (1980), Nabhany (1982), Akida (1983), Gibbe (1983), Kapinga (1983), Polome (1983), Temu (1984), Mbaabu (1985), Mutahi (1986), Abdulaziz (1989, 1983, 1981), Mwansoko (1990), Tumbo-Masabo (1990, 1982), Tumbo na Mwansoko (1992). Maelezo ya wataalam hawa wote ya mbinu za kuundia istilahi za Kiswahili, hata hivyo, yalielekea kuwa ya 'kijumlajumla.' Mtindo ulikuwa ni kutaja mbinu zote za uundaji wa istilahi za Kiswahili, na kutoa mifano michache ya istilahi zilizotokana na kila mojawapo ya mbinu hizo. Sisi tulitathmini istilahi za isimu ya Kiswahili na mbinu za uundaji istilahi hizo ili kuona kama zinazingatia usayansi, na, wakati huohuo, ni mbinu ipi inayounda istilahi zenye usayansi, zilizo faafu, na zinazosadifu zaidi kimataifa.

## 1.2 Azma ya Utafiti

Azma ya tasnifu hii ilikuwa kutathmini istilahi za isimu na mbinu zinazotumiwa kuunda istilahi zenye usayansi na ufaafu wa kimataifa, ili kuona kama misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi inatumiwa. Tulidahili iwapo istilahi za isimu ya Kiswahili zinazingatia kanuni na vigezo vya kisayansi vya 'ufaafu' wa istilahi. Kabla ya kutathmini 'usayansi' katika istilahi na mbinu za uundaji wa istilahi ilitulazimu kwanza kueleza kinagaubaga maana ya 'usayansi' wa istilahi, na misingi ya kisayansi katika mbinu za uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Ilitujuzu kuielewa barabara 'dhana ya istilahi' pamoja na mifumo ya sayansi inayotumiwa na wataalam mbalimbali katika kuundia istilahi zenye upeo wa juu wa ubora na zenye ufaafu

mkubwa wa kimataifa. Kadhalika, tuliazimia kupigia mbizi nadharia na taratibu zilizopo zinazotumika katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili ili zieleweke kwa uwazi na ziimarishwe ipasavyo. Pia, ilikuwa azma mahsusi kwamba tasnifu hii ijikite katika isimu ya Kiswahili, ili ionekane wazi kama mfumo wa sayansi unatumiwa katika kuunda istilahi na kufafanua ruwaza za kisayansi na zalishi zitakazoiwezesha lugha hii kujieleza yenyewe kikamilifu katika taaluma ya isimu ya Kiswahii.

## 1.3 Upeo wa Tasnifu

Tasnifu hii ilifungamana na upeo maalum ili kuyatekeleza madhumuni yetu. Katika tasnifu hii, tulifungamana na istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoundwa na wanaleksikografia wa Afrika Mashariki. Tulitathmini istilahi sabini (70) za isimu ya Kiswahili na mbinu za uundaji wa kila mojawapo ya istilahi hizo ili kuona kama zinazingatia usayansi. Ilhamu ya kujibana katika isimu ya Kiswahili ilitokana na umuhimu wa taaluma yenyewe. Istilahi za isimu ya Kiswahili, licha ya kwamba zina upungufu (Mwansoko 1990), hutumika rasmi katika ufundishaji wa wanafunzi wa shule za upili, vyuoni, na Chuo Kikuu, na zinaweza kutathminiwa kwa urahisi. Tathmini ya usayansi wa istilahi, na mbinu za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili, inatokana na haja ya kutaka kuibua sababu za kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi na, kwa namna hii, kuimarisha 'ufaafu' wake katika ufundishaji wa masomo ya Kiswahili. Uteuzi wa fani hii pia umetokana na sababu kwamba somo la isimu hufundishwa hadi ngazi ya Chuo Kikuu nchini Kenya, na katika nchi jirani kama vile

Tanzania, Uganda, Burundi na Rwanda. Hivyo, fani iliyoteuliwa siyo tu inazo istilahi za Kiswahili za kutosha, bali pia inao watumiaji wengi katika karibu kanda yote ya Afrika Mashariki na Kati. Wakati tuliofungamana nao ni kipindi cha kuanzia mwaka wa 1960 hadi 1999. Eneo tulilozingatia ni Afrika Mashariki. Tulidurusu, kadri ya uwezo wetu, mabuku yaliyomo katika vyuo vikuu vya nchi za Tanzania, Uganda, na Kenya, ili kujitokeza na data pana iliyotuwezesha kutekeleza na kufikia malengo yetu.

### 1.4 Nadharia Tete

Nadharia tete za utafiti huu ni pamoja na:

1. Sababu mojawapo ya kutosadifu kwa istilahi za isimu ya Kiswahili ni istilahi na mbinu ya kuundia istilahi kukosa 'usayansi' ndani yake.
2. Uendelezaji wa istilahi za Kiswahili unaweza kuafikiwa kwa kuimarisha mbinu za uundaji wa istilahi.
3. Kiswahili, kama lugha yo yote ile, kinaweza kujiendeleza kiistilahi mumo kwa mumo (yaani katika Kiswahili chenyewe) kwa kuzingatia misingi teule ya kisayansi.

### 1.5 Natija za Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa na manufaa kwa namna nyingi. Faida kadhaa zimejitokeza kutokana na utafiti huu. Tathmini ya usayansi katika istilahi na mbinu za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili zitatuwezesha kutoa ushauri kwa vyombo vya kukuza na kuendeleza Kiswahili-BAKITA, BAKIKE, TUKI, CHAKITA, na kwa

wataalam binafsi wanaounda istilahi. Ushauri utakaotolewa utahusu mbinu ya kisayansi na zalishi zaidi ya kuunda istilahi faafu za isimu ya Kiswahili zenye ukubalifu wa kimataifa kwa walengwa wake. Faida nyingine kubwa iliyopatikana ni kuwa sasa tumeweza kuibuka na vigezo na misingi timilifu na toshelezi ya kisayansi ya kuunda istilahi za Kiswahili. Endapo wana-leksikografia wa Kiswahili watazingatia na kutumia misingi hii, matatizo anuai katika shughuli za kuunda istilahi mpya za Kiswahili yatadadavuliwa. Aidha, itakuwa rahisi kwao kuchagua istilahi zenye usayansi na 'faafu' zaidi kunapotokea ushindani miongoni mwa visawe vinavyotumika kuwakilisha dhana moja.

Kadhalika, kutokana na utafiti huu, ni dhahiri kwamba baadhi ya madai yaliyowahi kutolewa na wataalam wa Kiswahili itabidi yarekebishwe. Mojawapo ya madai hayo ni ya Tumbo na Mwansoko (1992:22), kuhusu uteuzi wa lugha Changizi. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa mchango halisi wa lahaja za Kiswahili na wa lugha nyinginezo za Kibantu katika uundaji wa istilahi ni mdogo sana, na kwamba kuna udhaifu katika pendekezo la BAKITA (taz. *Kakulu* Na.3, 1982:16) la kuunda istilahi kwa kutumia:

1. Kiswahili chenyewe.
2. Lugha za Kibantu.
3. Lugha nyingine za Afrika.
4. Lugha za kigeni.

Tumbo na Mwansoko (1992:22) wanatoa kauli kwamba:

> Ukweli wa mambo ni kwamba lahaja nyingi za Kiswahili na lugha nyinginezo za Kibantu bado hazijafanyiwa utafiti wa kutosha wa kileksikografia ambao ungeziwezesha kuchangia kikamilifu katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili.

Kauli hii ya Tumbo na Mwansoko inapasa irekebishwe kwa kuzingatia nadharia ya istilahi. Utafiti huu umeonyesha kuwa mchango wa lugha za Kibantu ni mkubwa sana. Si tu, imedhihirishwa kwamba Kiswahili kinaweza kujiendeleza kiistilahi mumo kwa mumo (taz. mbinu ya Nabhany) kwa kuzingatia misingi teule ya kisayansi.

Aidha, utafiti huu umebainisha umuhimu wa kuunda istilahi ambazo zitakidhi matakwa ya walengwa wote pasi na kujali tofauti za kielimu. Wasemaji wa Kiswahili ni wamoja tu. Kwa hivyo, madai ya Mwansoko (1990) kuwa istilahi ziundwe kufuatana na viwango vya elimu vya watumiaji wake itafaa irekebishwe. Ni bayana kuwa kuwepo kwa makundi mawili ya kiistilahi katika fani ya isimu; yaani istilahi za wasomi na istilahi za watu wasio wasomi, kutawakanganya watumiaji wake.

Utafiti huu vile vile umejaribu kupiga hatua zaidi kuliko ilivyokuwa hapo mbeleni. Utafiti wa Mwansoko (1990) ndio uliokuwa mpana na wenye kina zaidi kabla ya utafiti huu. Mwansoko, katika utafiti wake, aliazimia kuchunguza ukubalifu wa istilahi za isimu na fasihi kwa watumiaji wa Kiswahili, pamoja na mikabala yao kuhusu sio tu istilahi za isimu na fasihi, bali pia mifanyiko na hatua zinazopitiwa tangu pendekezo hadi kupatikana istilahi sanifu ya Kiswahili. Utafiti huu wa sasa umeazimia kukidhi mahitaji ya juu zaidi katika taaluma pana ya uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Ugunduzi mkubwa uliojitokeza katika utafiti huu ni kwamba msukumo wa uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili umetokana na Kiswahili kutaka kujieleza chenyewe kikamilifu katika uwanja wa isimu, msukumo

ambao utafaulu tu endapo wanaleksikografia watatumia na kuzingatia vigezo, kanuni, na misingi bora ya kisayansi, ya uundaji wa istilahi za Kiswahili. Utafiti huu, isitoshe, utasaidia vyombo vya BAKITA, BAKIKE, TUKI na waundaji istilahi binafsi kuchunguza upya mbinu wanazozitumia kuundia istilahi za Kiswahili.

Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba mbinu inayozalisha istilahi za isimu zenye 'usayansi' ni ile ya uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe, ikifuatwa na uunganishaji na uambatanishaji, unyambuaji na ubunaji. Mbinu za upanuzi wa maana za maneno, ukopaji/utohoaji, uradidi, uhulutishaji na ufupishaji (akronimu na ukatizaji), licha ya kwamba hutumika katika uundaji wa istilahi za Kiswahili, zina upungufu mkubwa, kulingana na misingi ya uundaji wa istilahi (taz. pia Picht na Draskau, 1985).

Aidha, tunasadikisha kuwa utafiti huu utasaidia uendelezaji na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili, iwe kwa waundaji istilahi binafsi, vyombo, asasi, au taasisi, kwa vile unatoa fursa kwa kila mtu kubuni istilahi kwa kufuata mantiki na utaratibu mwelekevu ulio hakika na sahihi. Kwa usemi mwingine utafiti huu, utasaidia sana waundaji istilahi binafsi na vyombo vya ukuzaji wa lugha kuinua kiwango cha uundaji istilahi 'faafu' na zenye 'usayansi.'

Vilevile, utafiti huu wa sasa umeanzisha rasmi harakati za kukomesha vurugu na utata katika istilahi za isimu ya Kiswahili. Ni mwanzo wa safari ndefu na ngumu ya kuleta nidhamu kwenye

Kiswahili cha kitaaluma, hususani, kuhusu matatizo ya mpangilio wa maneno mkopo, tahijia, uundaji wa istilahi moja moja bila kuzingatia ufungamano wa kidhana, na utohoaji wa viambishi vya kisayansi. Ili kupata usawazishaji na usasaishaji mzuri na thabiti wa istilahi za isimu kimataifa, utafiti huu umeonyesha umuhimu wa kuzingatia kwa misingi ya uundaji wa istilahi. Misingi hiyo ikitwe kwenye nadharia za kiistilahi. Tija nyingine muhimu ya utafiti huu ni dhihirisho la hoja ya ukataru kwamba kuna nadharia za istilahi, kinyume na kauli za awali kwamba hakuna nadharia kama hizo (taz. Picht na Draskau, 1985:32). Utafiti huu umejaribu kuziba mwanya wa kinadharia ulioachwa wazi na wataalam wa awali walioshughulikia suala la ukuzaji wa istilahi za Kiswahili. Sasa tumeweza kuibuka na nadharia mbili za istilahi, moja ikiwa ni kama kijalizo cha nyingine (taz. 2.1, uk. 32).

Jambo jingine ambalo linatokana na utafiti huu, ni ugunduzi kwamba istilahi za isimu zinazopendekezwa ama kuundwa na baadhi ya watu binafsi na vyombo vya kukuza lugha, zina kiwango cha chini cha 'usayansi'. Utafiti huu umejaribu kupendekeza kuwa istilahi ambazo hazina usayansi, na hazisadifu kwa walengwa, huenda zikahitaji usahihisho siku za usoni ili ziakisi vilivyo sifa za dhana zinazoziwakilisha. Kutokana na utafiti huu, ni dhahiri pia kwamba *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990) itabidi irekebishwe na kuandikwa upya. Tumeonyesha, katika utafiti huu, kwamba urekebishaji wa kamusi hii utahitaji kuzingatia viambishi vya kiistilahi vilivyobuniwa na kuasilishwa kutokana na lahaja za Kiswahili.

Aidha, utafiti huu umejaribu kumsaidia kila mhitaji wa istilahi ambaye 'hukanganyika' kutokana na lugha hii kulimbikiziwa visawe vya kiistilahi. Imebainika, kutokana na utafiti huu, kwamba katika taaluma ya isimu na sayansi menyu, tofauti na fani anuai za sanaa, na sayansi za jamii na teknolojia, haifai kuunda istilahi mpya pale ambapo tayari dhana moja inarejelewa na istilahi 'faafu' mbili au zaidi. La sivyo, watumiaji istilahi daima wataendelea kulalamikia udhaifu na utata wa istilahi za isimu ya Kiswahili.

## 1.6 Dhana za Kinadharia

Picht na Draskau (1985:32-33), katika kukanusha kwamba hakuna nadharia ya istilahi, wanadai kuwa:

> Matakwa ya kiistilahi katika nchi zinazoendelea hayapaswi kupuuzwa. Hapa... juhudi nyingi zinafanywa ili kuimarisha vifaa vya mawasiliano vya kitaaluma kutokana na lugha asili ambazo kwa sasa hazijaendelea kiistilahi. Maandalizi ya semina katika Afrika na mataifa ya Amerika kusini na kuongezeka kwa maingiliano na mataifa ya Kiarabu na Mashariki ya Mbali (China) yanadhirisha mwelekeo huu. **Lugha hizi siku za usoni zitaathiri kuzuka kwa nadharia ya istilahi**, kuimarika kwa ujuzi mpya, na kusahihisha kasoro nyingi.
> (Tafsiri hii na zote zitakazofuata ni zetu).

Bila kutufahamisha kikamilifu ni nani 'atakayepuuza' mahitaji ya nchi zinazoendelea, Picht na Draskau (1985:3) wanatumaini kwamba msukumo mkubwa wa nadharia ya istilahi utatokana na lugha zenyewe. Pasi na kupuuza matumaini haya, swali ni je, kuna nadharia ya istilahi au la? Wataalam hawa wenyewe wanatoa jibu la swali hili kwa madai kuwa hakuna msingi wa jumla unaotambulikana wa nadharia ya istilahi. Kwa usemi mwingine,

hakuna nadharia ya istilahi, suala ambalo linapasa kufanyiwa uchunguzi wa kina kirefu.

Hata hivyo, utafiti huu uliongozwa na dhana za kinadharia za Nadharia Jumla ya Istilahi (NJI) *(General Theory of Terminology)*, nadharia iliyoasisiwa na Wuster (1931), pamwe na Nadharia ya Istilahi za Kisanyansi (NIK) *(A Theory of Scientific Terminology)* iliyoasisiwa na Kiingi (1989) (Kwa ufafanuzi zaidi taz. pia 2.1). Nadharia ya Istilahi za Kisayansi, ambayo imetumika ili kujaliza nadharia ya NJI, inasisitiza ya kwamba katika uundaji wa istilahi, ni lazima muundaji azingatie vigezo fulani vya istilahi 'faafu'. Hivyo ni nadharia inayotuongoza katika kuunda, kukubali, na kukataa istilahi fulani za Kiswahili (hasa zile ambazo hazina 'usayansi'). Vigezo tisa vinavyojenga **PEGITOSCA** (taz. 2.2.2 kwa maelezo zaidi) ni:
Udhahiri *(Precision)*, Iktisadi *(Economy)*, Uzalishaji *(Generativity)*, Umataifa *(Internationality)*, Uangavu *(Transparency)*, Utusani *(non-obscenity)*, Utaratibu maalum *(Systemicity)*, Utaratibu ulio sawa *(Consistency)* na Ukubalifu/Ufaafu *(Appropriateness)* wa neno linalopata hadhi ya istilahi katika lugha asili husika.
Kulingana na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi, istilahi bora na ya kisayansi ni ile inayokidhi mahitaji ya PEGITOSCA, na ni lazima ipate alama kati ya kumi na mbili (12) (sawa na asilimia hamsini) na ishirini (20). (Rejelea 3.3.2.4, uk. 71, kwa maelezo zaidi).

Kwa mfano:

| | **Mboo (Mboro)** | Kizalisha (Ume- '*penis*') |
|---|---|---|
| **p** | 4 | 5 |
| **e** | 3 | 2 |
| **g** | 0 | 1 |
| **i** | 1 | 2 |
| **t** | 1 | 2 |
| **o** | -3 | 2 |
| **s** | 0 | 0 |
| **c** | 0 | 0 |
| **a** | 0 | 0 |
| **p** | **6** | **14** |

(Kuhusu utoaji wa alama hizi na nyinginezo, rejelea 5.1, uk. 318-21).

Neno **kizalisha** halina ukali (matusi) katika jamii za Kiafrika likilinganishwa na **mboo** ambalo halikidhi sifa ya utusani katika PEGITOSCA. Hivyo tunapendekeza matumizi ya **kizalisha** (kinachomshikisha mke mimba) badala ya **mboo**. Tukitazama U-PEGITOSCA katika visawe vitatu tunapata:

c)

| | **king'ong'o** | **nazali** | **kipua** *(nasal sounds)* |
|---|---|---|---|
| **p** | 4 | 2 | 4 |
| **e** | 2 | 1 | 4 |
| **g** | 4 | 0 | 0 |
| **i** | 2 | 1 | 1 |
| **t** | 3 | 0 | 4 |
| **o** | 0 | 0 | 0 |
| **s** | 0 | 0 | 0 |
| **c** | 0 | 0 | 0 |
| **a** | 0 | 0 | 0 |
| **p** | **15** | **4** | **13** |

Ilivyo, Istilahi **kizalisha** na **king'ong'o** zimekidhi mahitaji ya jaribio la PEGITOSCA kwa kupata alama za juu hivyo kulingana na nadharia hii ndizo zinafaa kutumiwa. Nadharia ya Istilahi za Kisayansi yenye vigezo vya PEGITOSCA tuliitumia kutathmini istilahi za isimu ya Kiswahili, kwa sababu ingetuwezesha kutambua 'usayansi' na ufaafu wa istilahi hizo, pamoja na kiwango cha

ukubalifu ama kutokubalika kwa istilahi za isimu ya Kiswahili, zinazoundwa katika Afrika Mashariki.

## 1.7 Njia za Utafiti na Uchanganuzi

Katika kuchunguza suala la usayansi wa istilahi na mbinu za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili (taz. 1.1 na 1.2 hapo juu), tulitumia mbinu anuai katika utafiti na uchanganuzi wa data iliyopatikana. Mbinu za utafiti zilizotumiwa ni mahojiano ya ana kwa ana, kidadisi, na uchunguzi wa kimaktaba, ambapo tulidurusu na kusoma tasnifu za Kiswahili, vitabu, magazeti, na majarida mbalimbali yaliyokuwa na makala yaliyohusiana na mada ya utafiti wetu. Mbinu hizi ziliwahi kutumiwa na wataalam wa isimu ya Kiswahili na wanaleksikografia waliotutangulia. Tulichunguza mbinu zilizotumiwa na Mdee(1980), Tumbo Masabo (1989), Mwansoko (1990), ambao walishughulikia uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili, na ukubalifu wa istilahi mpya zinazoundwa kwa watumiaji wa Kiswahili. Kazi za wataalam hawa, kama hii yetu, zilijadili mbinu kadha wa kadha za uundaji wa istilahi za Kiswahili. Mathalani, Mdee (1980) alishughulikia mbinu za uundaji wa istilahi kama vile ukopaji wa istilahi za kigeni na uswahilishaji wake, ukopaji kutoka lugha za Kiafrika, akronimu na unyambuaji. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kwamba watumiaji wa Kiswahili walionelea mbinu ya uendelezaji wa Kiswahili mumo kwa mumo, (yaani uundaji unaotokana na lugha enyeji) kuwa bora zaidi. Naye Tumbo-Masabo (1989) alidahili kwa mapana minyambuliko ya istilahi za Kiswahili katika tasnifu yake ya uzamifu ya Ed.D. Mwansoko (1990) alishughulikia mifanyiko

inayotumiwa katika uundaji wa istilahi kama vile matumizi ya:

(i) Lugha yenyewe kwa minyambuliko, miambatano, miungano, na kuongeza maana, au kuyapa maneno maana maalum, na vifupisho.

(ii) Mikopo kutoka lahaja na lugha nyingine, pamoja na tafsiri sisisi.

Kwa kifupi, tasnifu za waatalamu hawa zina mwingiliano mkubwa na kazi yetu hii; hivyo ilitubidi kutalii mbinu walizozitumia kwenye utafiti wao, na uchanganuzi wa data iliyopatikana.

Utafiti wetu ulizingatia mbinu ya mahojiano kwa sababu ya umuhimu wake. Mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu mwafaka zaidi ya ukusanyaji data, kwa sababu humwezesha mtafiti kupata habari kutoka kwa asilimia kubwa ya wahojiwa walioteuliwa kuliko njia nyingine yo yote; kwa mfano, matumizi ya simu, posta, kidadisi na kadhalika. Aidha, si rahisi mhojiwa kukataa kushirikiana na mtafiti au mhojaji wanapokumbana ana kwa ana na kuulizwa maswali, kuliko anapotumiwa, mathalani, kidadisi, kwa njia ya posta, ili akaijaze (Mwansoko, 1990:8). Kuwepo kwa mhojaji huimarisha majibu ya mhojiwa kwa sababu mhojaji huwa na uwezo wa kueleza na kufafanua maswali yasiyoeleweka kwa urahisi na mhojiwa; na majibu yatolewayo na mhojiwa huwa aghalabu ni ya hali ya juu, si ya 'vivi hivi tu', kutokana na uwezo wa mhojaji kuomba afanyiwe ufafanuzi wa jambo lolote asilolielewa barabara (Samarin 1967).

Kwa upande mwingine, njia ya mahojiano ina dosari zake, hususani, muda mwingi unaotumiwa. Fasold (1984:152) anatukumbusha kwamba humchukua mtafiti muda mrefu zaidi kuhojiana na mhojiwa mmoja kuliko kutumia kidadisi katika vikundi tofauti. Ingawa tulifahamu

dosari hii, ilhamu ya kutumia njia ya mahojiano katika utafiti huu ilitokana na kutaka kuwashirikisha kimawazo watu wenye ujuzi juu ya mada yetu, vyombo vya TUKI, BAKIKE, BAKITA na waundaji istilahi binafsi. Utafiti wetu ulizingatia mbinu hii ya mahojiano kwa sababu ya kutaka kuwashirikisha walengwa mbalimbali katika kazi nzima ya kuunda istilahi, badala ya kuwachukulia kama walaji wasioruhusiwa kuingia jikoni (Sewangi, 1996:20). Tathmini ya 'usayansi' katika istilahi, na mbinu za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili, haingekamilika pasi na kuwashirikisha watumiaji wengi wa istilahi za Kiswahili.

Kutaka kuwashirikisha walengwa wengi kulileta pia msukumo wa kutumia mbinu ya kidadisi. Tulitayarisha maswali yaliyoulizwa na kujibiwa na makundi mbalimbali. Maswali mahususi yalielekezwa kwa wataalam na wanaleksikografia wa Kiswahili, vyombo vya TUKI, BAKITA, BAKIKE, waandishi wa vitabu, magazeti, na watangazaji wa redio, Waswahili wasomi, wanafunzi wa Kiswahili wa vyuo vikuu, wahadhiri (wanaisimu pekee), na watumiaji wa Kiswahili wa kawaida.

Kadhalika, utafiti wetu ulizingatia mbinu ya kidadisi kwa sababu ni rahisi kuitekeleza na haichukui muda mrefu, tofauti na mahojiano ya ana kwa ana. Umuhimu mwingine wa kidadisi ni kwamba wahojiwa wanapewa muda wa kutosha wa kujibu kwa makini maswali yaliyoulizwa na mtafiti, kinyume na mbinu ya mahojiano, ambapo mhojiwa hapewi muda wa kufikiria kabla ya kujibu maswali ya mhojaji. Mbinu ya kidadisi, kama ilivyo ya mahojiano, haikosi dosari zake. Kuna uwezekano mkubwa wa mtu anayejibu maswali

katika kidadisi kupotoka au kuenda nje ya mada ya utafiti. Maswali katika kidadisi huenda yakajibiwa vibaya kwa sababu ya mtafiti kuwa na ushabiki wa kutumia istilahi ngumu na zisizoeleweka kwa urahisi na anayedadisiwa. Fauka ya hayo, kutokuwepo kwa mtafiti wakati maswali ya kidadisi yanapojibiwa huleta ugumu katika kuelewa baadhi ya majibu yaliyotolewa, manake mtafiti hawezi kuomba afanyiwe ufafanuzi zaidi. Hutokea pia ukiushi wa majibu yanayotolewa, ukiushi ambao mtafiti hana uwezo wa kuusahihisha, tofauti na njia ya mahojiano, ambapo mhojaji anao uwezo wa kuomba 'tafadhali rudia, sikuelewi,' na kadhalika (Williamson na wenzake, 1977:145).

Katika utafiti huu, data kuhusu usayansi wa istilahi na mbinu za uundaji wa istilahi, zilipatikana katika maktaba za Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki; yaani maktaba za Chuo Kikuu cha Dar-es Saalam (Tanzania), Chuo Kikuu cha Uislamu katika Uganda-Mbale, Makerere (Uganda), Nairobi, Moi, Kenyatta na Egerton (Kenya). Vyuo Vikuu hivi vilichaguliwa kwa sababu ndivyo vinavyofundisha lugha na isimu ya Kiswahili. Tuliwashirikisha watu wenye ujuzi juu ya mada yetu kimawazo kwa kufanya nao mazungumzo ya kiakademia. Pia, wahadhiri wenye ujuzi juu ya mada yetu katika Vyuo Vikuu hivi tulivyovitaja walihojiwa.

Tulitumia simu, na posta, katika ukusanyaji wa data. Vilevile, tulifanya ziara katika sehemu muhimu za pwani ya Kenya (ili kuhojiana na WANAJUNGU KUU) na ya Tanzania kwa sababu ndiko 'Uswahilini' (Shariff 1988:14) na tulikuwa na imani kwamba ndiko ambako kungepatikana data au wataalam wa kushauriana nao. Hapa

tutatoa maelezo ya namna tulivyotumia mbinu hizi katika utafiti huu.

### 1.7.1 Mahojiano ya Ana kwa Ana

Mahojiano ya ana kwa ana yalitumiwa katika kuchunguza 'usayansi' wa istilahi za isimu, misingi ya kisayansi ya uundaji istilahi, na mifanyiko au mbinu za kuundia istilahi zinazotumika katika ukuzaji na uendelezaji wa istilahi za Kiswahili. Utafiti huu ulilenga taaluma mahsusi; na, kwa hivyo, mahojiano yalielekezwa kwa watu wanaohusika na shughuli ya kubuni na/au kutumia istilahi za isimu ya Kiswahili (taz. Besha 1995:64).

Maswali ya mahojiano yalielekezwa kwa makundi yafuatayo:

(i) Watumiaji wa lugha hii (watumiaji wa Kiswahili wa kawaida, Waswahili wenyeji, na wasomi).

(ii) Wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu.

(iii) Wahadhiri wa isimu na lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu.

(iv) Waandishi (wa vitabu na magazeti) na watangazaji redioni na televisheni.

(v) Wataalam wa lugha ya Kiswahili (wanaleksikografia, waundaji istilahi binafsi na vyombo vya BAKITA, BAKIKE, TUKI).

Kwa jumla, wahojiwa walikuwa thelathini (30). Watano (5) miongoni mwa hao walikuwa wataalam na maafisa katika vyombo vya BAKITA, BAKIKE na TUKI; watano (5) wengine walikuwa waundaji wa istilahi za Kiswahili; kumi na wawili (12) walikuwa wahadhiri wa isimu ya Kiswahili; watatu (3) walikuwa waandishi na watangazaji katika shirika la KBC, Kenya; watatu (3) walikuwa watumiaji wa

kawaida wa Kiswahili na wawili (2) wanafunzi wa Vyuo Vikuu (mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Makerere na mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) (taz. Kiambatisho 3 kuhusu maswali ya mahojiano).

Maswali mahsusi ya mahojiano yalitayarishwa mapema na kuelekezwa kwa kila mojawapo ya makundi yaliyohojiwa. Kwa mfano, katika kundi la wataalam wa lugha ya Kiswahili (waundaji istilahi na maafisa wa vyombo vya BAKITA, BAKIKE na TUKI), maswali yaliyoulizwa yalihusu mantiki; sababu za kuunda istilahi mpya; kanuni na misingi inayofuatwa katika uundaji wa istilahi; mbinu zinazotumiwa katika uzalishaji wa istilahi; sababu ya kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi kwa walengwa; iwapo kuna haja ya kufufua Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ya uundaji na usanifishaji wa istilahi, kama chombo cha BAKITA kinajitosheleza kimajukumu; na maswala kuhusu vigezo vya PEGITOSCA; visawe vya kiistilahi, tahajia, lugha changizi ya Kiswahili, na mengine mengi. Maswali ya aina hii pia yalielekezwa kwa wahadhiri wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu vilivyotajwa mbeleni (taz. Kiambatisho cha 3 kwa maelezo zaidi).

Maswali yaliyoulizwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili wa Vyuo Vikuu yalihusu wakati walipoanza kufundishwa somo la isimu ya Kiswahili (kidato gani, au kama ni chuoni, mwaka wa ngapi); vitabu vya rejea vinavyotumiwa kufundishia masomo ya isimu; jinsi wanavyopata visawe vya Kiswahili kwa dhana za Kiingereza; iwapo *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* inatosheleza mahitaji yao au la; na sababu za kupenda ama kukataliwa kwa istilahi mpya. Maswali ya aina hii yalielekezwa pia kwa watumiaji wa Kiswahili na kwa

waandishi wa vitabu, magazeti na watangazaji redioni (taz. Kiambatisho cha 3, kwa ufafanuzi zaidi).

Ingawa maswali ya mahojiano yalitayarishwa mbeleni, hayakusomewa wahojiwa, lakini mahojiano yaliendelezwa kwa utaratibu wa mazungumzo ya kirafiki. Mtindo huu uliimarisha majibu ya wahojiwa kwa vile waliweza kujieleza kikamilifu na kutoa maoni yao katika hali huria. Kila msailiwa/mhojiwa alihojiwa binafsi akiwa afisini, nyumbani na mahali pake pa kazi kwa takribani masaa mawili au matatu, huku tukinakili na kuandika majibu yaliyotolewa katika shajara ya mfukoni.

### 1.7.2 Kidadisi

Kidadisi kilitumiwa katika kuchunguza na kutathmini 'usayansi' wa istilahi za isimu ya Kiswahili, pamoja na mbinu zinazotumiwa katika uzalishaji wa istilahi hizo. Vigezo na misingi ya uundaji wa istilahi faafu na zenye kusadifu kimataifa pia vilichunguzwa kwa kutumia kidadisi. Kidadisi kiligawanywa katika sehemu mbili, yaani sehemu 1 na sehemu 2.

**Sehemu 1**

Sehemu hii ilishughulikia tathmini ya istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoundwa na TUKI (1990) na watu binafsi. Kiasi cha istilahi sabini (70) ziliteuliwa kutoka kwenye orodha kuu ya istilahi za isimu mia nane hamsini na tisa (859) (taz. Irira, 1990:19), na kujaribiwa kwa walengwa mia moja na ishirini (120) katika maeneo mbalimbali. Walengwa hao walijumlisha wanafunzi

hamsini na moja (51) wa mwaka wa tatu (III) wa Chuo Kikuu cha Egerton, wahadhiri na watafiti wa Kiswahili ishirini (20), waandishi wa vitabu na magazeti sita (6), waundaji istilahi watano (5), na watumiaji wengine wa lugha ya Kiswahili thelathini na nane (38). Wanafunzi wa mwaka wa tatu (3) wa Chuo Kikuu cha Egerton walichukuliwa kama wasailiwa faafu kwa sababu walikuwa tayari wamefundishwa somo la isimu linalohusu leksikografia na othografia; kwa hivyo, tuliamini kuwa walikuwa na uwezo wa kujibu maswali yanayohusiana na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili. Kwa jumla, vidadisi mia moja na ishirini (120) vilitumika. Idadi hii ilichukuliwa kuwa toshelezi.

Uteuzi wa istilahi za isimu ulifanywa baada ya kuzipambanua istilahi zote 859 katika makundi mbalimbali. Vigezo viwili vilitumiwa katika uteuzi wa istilahi zilizofanyiwa majaribio, navyo ni pamoja na:

1. Kigezo cha umbo la istilahi (umbo sahili na ambatano).
2. Kigezo cha aina ya mfanyiko uliotumika kuundia istilahi (taz. 6.1.2, uk. 344, kwa maelezo zaidi).

Mbali na kuzingatia kwa vigezo vilivyotajwa hapa, pia istilahi 70 zilipaswa kuwa na sifa zifuatazo:

- Istilahi zenye mashiko na muda mrefu wa kimatumizi katika isimu ya Kiswahili, ama zinazopatikana katika maandishi.
- Istilahi zilizobuniwa kwa mbinu za kisifabia za uundaji wa istilahi kama vile uunganishaji na uambatanishaji, unyambuaji na ukopaji (taz. pia 5.2, uk. 289) (kwa maelezo zaidi na orodha ya istilahi za isimu zilizofanyiwa

majaribio tazama Jedwali 4, uk. 348).

Istilahi zilizoteuliwa ziliainishwa katika makundi kumi, ambapo kila kundi liliwakilishwa na istilahi saba (7) katika tathmini (rejelea uk. 315-6). Istilahi zilizoteuliwa na kuorodheshwa kwenye kidadisi zilikuwa sawa kwa wasailiwa wote pasi na kuzingatia tofauti zao za kielimu. Hii ni kwa sababu kidadisi kilielekezwa kwa watumiaji wenye ujuzi juu ya mada yetu, ama waundaji wa istilahi hizo. Wasailiwa walitakiwa kuandika vigezo ambavyo wanafikiri kuwa kila mojawapo ya istilahi sabini (70) ilisadifu kwenye nafasi iliyotolewa ili kuonyesha kiwango cha usayansi wa istilahi. Hata hivyo, maswali hayakuulizwa kwa ruwaza ya moja kwa moja. Wasailiwa, kwa mfano, hawakuulizwa kwa njia ya moja kwa moja kama wanaikubali istilahi fulani ama kama istilahi ina usayansi au la, lakini orodha ya vigezo vya istilahi faafu (rejelea Kiingi, 1989) ilitolewa na wasailiwa waliulizwa kama walizitambua istilahi hizo. Pia walitakikana waeleze maana yake kabla ya kuandika, kama ilivyotajwa hapo awali, vigezo vya istilahi faafu ambavyo walifikiri kila istilahi iliyoorodheshwa ilikuwa navyo. Kadhalika, pale ambapo istilahi iliyo kwenye orodha haitumiwi, wahojiwa waliulizwa kutaja istilahi wanayoitumia badala yake. Katika kupima 'usayansi' wa istilahi, istilahi iliyopata asilimia hamsini (50) (ambayo ni sawa na alama 12) na kuendelea ilichukuliwa kwamba inakidhi mahitaji ya PEGITOSCA, na, hivyo basi, ni istilahi 'faafu' na inasadifu. Kwa upande mwingine, istilahi iliyopata chini ya asilimia hamsini (50) ilichukuliwa kuwa haina 'usayansi', si istilahi 'faafu,' haisadifu na haikubaliki kwa walengwa.

### 1.7.3 Machapisho Kuhusu Istilahi za Kiswahili

Mbali na mahojiano ya ana kwa ana na kidadisi, machapisho kuhusu istilahi za Kiswahili pia yalitumika kama rejea muhimu. Machapisho hayo ni pamoja na;

1. BAKITA kijitabu cha *Tafsiri Sanifu*, Juzuu 2. (1979), uk.30-33, chenye istilahi 185 za isimu na fasihi.
2. R.F. Besha, *Utangulizi wa Lugha na Isimu* (1994) kitabu ambacho kina istilahi za isimu zilizotoholewa kwa Kiswahili.
3. R.M. Chimerah, *Kiswahili Past, Present & Future Horizons* (1998). Kitabu hicho, pamoja na makala ya mwandishi huyu ya *"Kiswahili Through the Ages: The Question of Lexicon" (1999)*, kina istilahi zilizoundwa na mwandishi.
4. M.C. Kapinga, *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (1983) ambacho kina orodha ya istilahi za mofolojia, uk.205-207.
5. C. Maganga, *Misingi ya Fonetiki-Matamshi* (1979) (mimeo) ambacho kina istilahi za fonetiki, uk.48-50.
6. I. Mbaabu, *Sarufi ya Kiswahili* (1992) kitabu ambacho kina orodha ya istilahi za isimu ya Kiswahili, uk.193-197.
7. A.S. Nabhany, "Kandi ya Kiswahili" (1978) mswada haujachapishwa lakini una msamiati wa istilahi za Kiswahili.
8. F.V.M. Nkwera, *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo* (1978) DSM.
9. TUKI, *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) ambayo ina istilahi 'sanifu' za isimu ya Kiswahili.
10. Z.N.Z. Tumbo-Masabo na H.J.M. Mwansoko, *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili* (1992) kitabu ambacho kina istilahi za isimu na mbinu za uundaji istilahi, uk.1-46.

**Sehemu 2**

Sehemu hii ilikuwa jaribio la kuchunguza mtazamo wa watumiaji wa Kiswahili kuhusu upungufu wa istilahi za isimu ya Kiswahili, uundaji istilahi, na mbinu zinazotumika katika uundaji wa istilahi zenye 'usayansi' na ufaafu wa kimataifa. Baadhi ya maswali yaliyoulizwa yalihitaji majibu mafupi ya "ndiyo" au "la" na mengine yalihitaji mhojiwa kuchagua jibu sahihi kwa kuliwekea alama X miongoni mwa majibu mengi yaliyoorodheshwa kwenye kidadisi. Kadhalika, kulikuwa na maswali yaliyohitaji kujibiwa kwa mpangilio wa viwango vya ubora, yaani, kuanzia 1,2,3,4,5,6, hadi saba. Kwa jumla, maswali katika sehemu hii yaliazimia kuchunguza mambo kadha wa kadha. Kwa mfano:

- Iwapo wahojiwa wameisoma na kuitumia *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI 1990), na kama ilitosheleza mahitaji yao au la.
- Ikiwa wahojiwa wanafikiri kuwa istilahi za isimu ya Kiswahili zinatosha au la.
- Jinsi ambavyo Kiswahili kinaweza kuendelezwa kiistilahi bila 'malalamiko' mengi ili kujieleza kikamilifu, hususani, katika kipengele cha isimu.
- Vigezo vya ufaafu wa istilahi ambavyo wahojiwa walifikiri ni muhimu zaidi katika ukuzaji wa istilahi za Kiswahili.

Kwa hivyo, data iliyochambuliwa katika kazi hii ilitokana na majibu yaliyotolewa na walengwa waliohojiwa.

11. R. Mgullu, *Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili* (1999) kitabu ambacho kina istilahi za isimu ya Kiswahili.

12. D.P.B. Massamba, Y.M. Kihore na J.I. Hokororo, *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu Sekondari na Vyuo* (1999). Kitabu hiki kina istilahi za sarufi na sintaksia ya Kiswahili, uk. 171-186.

Katika kutathmini 'usayansi' wa istilahi za isimu zinazohusika, tulitumia *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (KASAILU) iliyochapishwa na TUKI (1990) kama msingi wa kuanzia tathmini yetu kwa sababu ya kuziona kuwa ni sanifu (taz. Mwansoko, 1997:33). Pamoja na kutumia *KASAILU* kama msingi wa kutathmini usayansi katika istilahi za isimu ya Kiswahili, tungependa kueleza pia kuwa katika sura za kinadharia za tasnifu hii, tulitumia data isiyo ya isimu. Uchunguzi wetu ulihusu lugha ya Kiswahili na, kwa hivyo, data 'faafu' yoyote katika Kiswahili ilitumika ili kubainisha 'ubora' wake kwa kulinganishwa na zile za *KASAILU*. Data zilizotokana na makala mbalimbali za wanaistilahi wa Kiswahili na zilizochapishwa kwenye majarida yatolewayo na asasi za Kanda ya Afrika Mashariki na Kati pia zilitumiwa kama vyanzo vya data. Data tuliyoipata kutokana na machapisho na maandiko anuai ya Kiswahili kutoka Kenya, kwa kiwango kikubwa, ilijumuisha kazi zilizoandikwa na watu binafsi, hususani, Mbaabu, Nabhany na Chimerah. (Kuhusu jinsi tulivyochanganua data yetu, rejelea sura ya tano kwa ufafanuzi zaidi).

Baada ya kutoa usuli huo wa mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data, ni muhimu tueleze matatizo yaliyoshuhudiwa katika utafiti.

## 1.8 Matatizo na Vikwazo Vilivyoshuhudiwa katika Utafiti

Utafiti huu haukukosa vikwazo na matatizo. Idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu vya kitaifa na kimataifa wanaojifunza Kiswahili ni ndogo sana. Katika vyuo vikuu vya kitaifa na kimataifa tulivyozuru, idadi ya wanafunzi wa Kiswahili haitii moyo. Katika Chuo Kikuu cha Makerere, kwa mfano, tulipata wanafunzi watatu (3) tu wanaosoma Kiswahili wa mwaka wa pili. Mambo ni hayo hayo katika Chuo Kikuu cha Uislamu katika Mbale - Uganda. Katika chuo hiki, tulipata wanafunzi sita (6) tu wa Kiswahili wa mwaka wa kwanza ambao hawakuwa na uwezo ama misingi yoyote katika taaluma ya isimu ya Kiswahili. Idadi ya wahadhiri wa vyuo vikuu pia ni ndogo ila tu katika Chuo Kikuu cha Egerton na cha Kenyatta. Katika Chuo Kikuu cha Uislamu-Uganda tulipata walimu watatu (3) wa Kiswahili; na cha Makerere tangu mwaka wa 1987 mhadhiri wa Kiswahili amekuwa ni mmoja (1) tu, na ndiye anayefundisha kozi za isimu ya Kiswahili. Hata hivyo, ingawa tulikabiliwa na tatizo la idadi ndogo ya wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu walionuiwa kujaza kidadisi, shida hii haikukwamisha utafiti wetu. Pamoja na kuwahoji wahadhiri na wanafunzi wachache waliopatikana katika vyuo vikuu vya kimataifa, tuliweza pia kuwahoji wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu vya Egerton na Kenyatta. Kwa namna hii, tulijaza 'pengo' la idadi ndogo ya wanafunzi na wahadhiri wa Kiswahili waliotarajiwa kujaza kidadisi na kuhojiwa ili kuleta ufanisi katika kazi hii.

Aidha, utafiti huu ulikumbwa na tatizo la kifedha. Wakati wa utafiti huu, mdhamini wetu, Chuo Kikuu cha Egerton, kilikuwa na shida za kifedha na ilitubidi kutekeleza kazi yetu hii tukiwa tumebanika kwelikweli. Hii ilimaanisha kuwa hatungeweza kuzuru maeneo yote yaliyokusudiwa, hususani, sehemu ya pwani ya Kenya kama vile Lamu na aidha sehemu nyingine muhimu ya 'Uswahilini' ya Unguja-Tanzania. Katika maeneo tuliyozuru na kufanya utafiti wa nyanjani, baadhi ya wanafunzi, na watumiaji wengineo wa lugha ya Kiswahili walionyesha kutotaka kuifanya kazi ya ujazaji wa kidadisi bila malipo. Hali hii ilitokana na ukweli kuwa mtafiti hakuwa na fedha za kuwalipa wahojiwa au wasailiwa kwa ajili ya kazi hiyo. Hata hivyo, ni baada ya kuwahimiza na kuwaeleza kwamba utafiti huu uliazimia, miongoni mwa mambo mengine, kuendeleza Kiswahili pamoja na kuiwezesha lugha hii kujieleza katika kipengele cha isimu kikamilifu, ndipo wakabadili mikabala yao na kuifanya kazi ya ujazaji. Hata baada ya kuwaomba waifanye kazi hii kwa kujitolea na wakaifanya kwa shingo upande, sio wahojiwa wote walioweza kujaza kidadisi kwa muda ufaao.

Hali kadhalika, utafiti huu, hususani suala la usayansi wa istilahi za isimu na mbinu za uundaji istilahi, ulijengeka katika misingi ya taarifa au ripoti za kibinafsi ambazo huenda si za kutegemewa (taz. Mwansoko, 1990:31). Hata hivyo, majibu yaliyotolewa kwa kidadisi chetu huenda ni ya kutegemeka kwa sababu, mbali na kidadisi kuandikwa kwa mpangilio na muundo sahili, mtafiti pia aliweza kueleza na kuwafafanulia wasailiwa maswali yaliyoonekana kuwa magumu kwao. Hali hii inaondoa shauku katika ubora wa kutegemewa kwa majibu yaliyotolewa kwenye

kidadisi.

### 1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Katika sura hii, tumejadili mambo ya kimsingi yanayosaidia kuelewa, yaliyofanyika, na jinsi yalivyotekelezwa katika tasnifu hii. Hususani, tumedokeza azma yetu kuu katika utafiti huu, yaani kutathmini 'usayansi' katika istilahi za isimu na mbinu za uundaji wa istilahi. Pia tumeeleza kuwa nia yetu nyingine ilikuwa ni kupigia mbizi nadharia za istilahi ili zieleweke kwa mng'aro na ziimarishwe ipasavyo. Tumefafanua, katika sura hii, kuwa tathmini ya 'usayansi' katika istilahi na mbinu za kuundia istilahi ni kwa minajili ya kuibua sababu za kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi. Kadhalika, tumeeleza natija za utafiti, na kusisitiza kwamba utafiti huu utasaidia ukuzaji wa Kiswahili, iwe kwa waundaji istilahi binafsi, au kwa vyombo vya kukuza lugha, kwa vile unatoa fursa kwa kila mtu kuzizalisha kwa kufuata mantiki na misingi ya uundaji wake. Kwa hivyo, tunataraji kuwa weledi wa waundaji istilahi za Kiswahili, wakiirejelea tasnifu hii utapanuka zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Katika sura hii tumeonyesha kuwa kuna nadharia za istilahi na uundaji istilahi hauna budi kukitwa kwenye nadharia hizo. Vilevile, tumetaja, katika sura hii, kuwa tasnifu yetu inajikita katika Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) ambayo inajaliza Nadharia Jumla ya Istilahi (NJI) iliyoasisiwa na E. Wuster (1931). Pia, katika sura hii, tumedahili kuwa vigezo vya PEGITOSCA vinavyojenga NIK ni muhimu katika kupima 'ufaafu' wa

istilahi za isimu ya Kiswahili.

Aidha, sura ya kwanza imebainisha njia zilizotumika ili kupata data, na namna data hiyo ilivyofafanuliwa na kuchanganuliwa. Kudurusu katika maktaba, ziara (hasa Mombasa, Dar es Salaam, Makerere, Mbale), mahojiano ya ana kwa ana na wataalam mbalimbali, matumizi ya kidadisi ni mbinu muhimu zilizochangia kuleta ufanisi wa utafiti huu.

Kwa kifupi, tunatarajia kuwa sura hii itampa mwanga msomaji kuhusu misingi iliyotumiwa katika maandalizi na uandishi wa tasnifu hii. Pia tunatumai kuwa sura hii itakuwa mwongozo wa kufanyia utafiti wa baadaye, hususani kuhusu uendelezaji, usawazishaji, na usasaishaji wa istilahi za Kiswahili. Watafiti wa baadaye huenda pia wakachochewa na kufaidika na mawazo yaliyomo katika sura hii.

# SURA YA PILI

## TATHMINI YA NADHARIA ZA UUNDAJI WA ISTILAHI

### 2.0 Utangulizi

> Kifaa kikubwa kinachotumiwa na wanasayansi katika kuthibiti ukweli wa maswala mbalimbali ya elimu ni kile kitu kinachoitwa 'nadharia' au 'nasaha'. Nadharia ni mfungamano wa mawazo yaliyopangwa ili kumpa mtu mwongozo mzuri wa kudadisi au kutatua swala fulani. Mfungamano huo wa mawazo huibua dhana mbalimbali ambazo ni muhimu katika kutegemeza na kuikamilisha nadharia inayohusika ...Kwa hivyo ni vigumu kuelewa barabara maana kamili na sahihi (ya istilahi) bila kwanza kuelewa barabara nadharia iliyoziibua na kuzitumia
>
> (Mkude, 1989:31)

Dondoo la hapo juu, kwa kiwango kikubwa, linakubalika kati ya wanaisimu na wanaleksikografa kwa ujumla kuhusu umuhimu wa 'nadharia' katika uundaji wa istilahi. Itakubalika kuwa, kwa mujibu wa dondoo hili, istilahi hutegemea nadharia, na ni dhahiri kwamba 'ufaafu' na 'usayansi' wa istilahi yoyote hutegemea pia ufaafu na nguvu za nadharia yenyewe. Na kama alivyosema Mkude (1989:32) "nadharia changa au tepetepe haiwezi kuibua istilahi imara na zenye ufasaha (usayansi) mkubwa." Lakini nadharia changa (k.v. Nadharia ya Istilahi za Kisayansi - NIK) inaweza kuinukia na kupata umaarufu. Ikitokea hivyo, istilahi zenye kuitegemea hupevuka na kupata makali pia.

Uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili yafaa uegemezwe kwenye nadharia thabiti ili, kama asemavyo Mkude (ibid:32):

> ...isije ikawa kwamba istilahi butu kinadharia itapewa makali yasiyoistahili na istilahi kali kinadharia itapewa ubutu

usiofaa. Kwa mfano, kuiita *pronoun* "kiwakilishi" ni kuipa istilahi hiyo ubutu usiofaa.

(taz. tathmini ya usayansi wa istilahi *pronoun* katika 6.1, uk. 318)

Ni kweli kwamba 'usayansi' wa istilahi unapaswa kutathminiwa kwa kuongozwa na nadharia maalum, na kwa kutumia misingi ya kisayansi. Sifa mojawapo muhimu ya tathmini ya kisayansi ni kueleza kwa ukamilifu kile kinachoonekana, na hivyo kinachoweza kuthibitishwa (taz. Besha, 1995:61). Ndiposa misingi ya istilahi na ya uundaji wake haina budi kukitwa katika nadharia za kiistilahi ili kujua kama istilahi hiyo ina 'usayansi' au la (Felber, 1984).

Tathmini ya nadharia za istilahi ina umuhimu wake. Kwa kuwa istilahi huegemea nadharia, haitoshi kujua nadharia iliyoiibua istilahi hiyo bali ni muhimu kujua 'ubora' wa nadharia yenyewe. Tathmini ya nadharia za istilahi husaidia katika kuchagua nadharia bora zaidi kati ya nyingi zinazotumika katika uundaji wa istilahi. Ili zoezi hili la kuunda istilahi liweze kufanyika kwa mifanyiko yenye mantiki ya kisayansi, na sio kiholela, tathmini ya aina hii ni muhimu. Kwa kuwa mbinu tendakazi za kiistilahi ndio msingi wa nadharia za istilahi (Felber, 1984:3), na nadharia za uundaji wa istilahi zimejikita katika utendaji (Tumbo na Mwansoko, 1992:14), hatuna budi pia kushughulikia mbinu tendajikazi za kiistilahi. Hata hivyo, mantiki ya kushughulikia nadharia za istilahi na mbinu tendakazi kiistilahi ni kwamba endapo maswala haya yatafuatwa ipasavyo, nyingi ya istilahi za isimu zitakazozalishwa zitaeleweka kwa urahisi na zitakuwa na upeo wa juu wa ukubalifu wa kimataifa.

## 2.1 Mbinu Tendakazi Kiistilahi

Shughuli ya hali ya kazi ya istilahi ilielezwa kwa mapana kwa mara ya kwanza na E. Wuster katika karatasi yake "Die Vier Dimensionen der Terminologiearbeit" ((Mitazamo Minne ya Kazi ya Istilahi) (taz. Felber, 1984:3-9, kwa ufafanuzi zaidi)). Uendelezaji wa istilahi, kama sayansi, utumiaji wa misingi ya kiistilahi na ushirikiano wa kimataifa katika kazi ya istilahi, kwa maoni ya Wuster, ni hatua muhimu ya kukuza mawasiliano maalum. Kutokana na sababu hii, kuliibuka mbinu tendakazi za istilahi (taz. Picht na Draskau, 1985:160-170). Hata hivyo, mbinu tendakazi kiistilahi zinazotumika sana na wanaistilahi ni mbinu ya kutafsiri na mbinu ya kidhana (Felber, 1980:65-79).

### 2.1.1 Mbinu ya Kutafsiri

Kutafsiri ni kuchukua maneno yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha changizi) na kuweka badala yake maneno (mawazo) yanayolingana (sio maneno yaliyo sawa) kutoka lugha nyingine (lugha pokezi) [taz. Catford, 1966]. Dhana nyingi mpya zinapoingia katika lugha, wanaleksikografia hukabiliwa na tatizo sugu la kutafuta visawe mwafaka vya dhana hizo mpya katika lugha pokezi. Aghalabu, wataalam na watumiaji lugha huchapua kuzipokea dhana hizi mpya pamoja na istilahi zinazoziwakilisha, ama dhana hizo mpya kuundiwa istilahi mpya kwa kufuata mbinu za kisifabia za kuzalisha istilahi mpya (taz. 4.0, uk. 115).

Misingi ya kinadharia ya mtazamo huu iliwasilishwa kwa mara ya kwanza katika mwanzo wa 1930 katika uchunguzi wa E. Wuster (taz. 2.2.1, uk. 36). Hata hivyo, ingawa mtazamo wa kinadharia (au mbinu ya kinadharia) hutumika katika nchi zilizoendelea kama vile Marekani, Ulaya, Ujerumani, Uswidi, na Ufaransa (taz. Mwansoko, 1990:51), ni muhimu ieleweke kwamba dhana na mifumo yake hutofautiana katika lugha mbalimbali, na hivyo kufanya ulinganishaji baina ya lugha kuwa mgumu (Felber, 1984:105).

## 2.2 Nadharia za Uundaji wa Istilahi

Shughuli ya uundaji wa istilahi na baadhi ya istilahi zenyewe za Kiswahili zinazozalishwa zimelalamikiwa na watumiaji istilahi wengi (taz. k.m. Mdee, 1983; Massamba, 1996). Hususani, malalamiko haya yamehusu waundaji istilahi kutofahamu nadharia za istilahi (Massamba, 1989:79). Wengi wao, kwa mfano, hawafahamikiwi na uhusiano uliopo baina ya dhana na kiwakilishi chake. Kutofahamikiwa kwao na nadharia za istilahi, mbali na kukwamisha shughuli ya uundaji wa istilahi 'faafu', pia kumezuia kupatikana kwa ufanisi wa kazi yenyewe. Uundaji wa istilahi zisizo na 'usayansi' (taz. 5.1) unasababishwa na misingi potovu ya uundaji istilahi ambayo haikitwi katika nadharia za istilahi (taz. Massamba, 1996:91-3).

Ili kufahamu chanzo cha malalamiko haya, ni muhimu kuzichunguza, kuzichambua, na kuzitathmini nadharia za kiistilahi zinazotumika katika uundaji na uendelezwaji wa istilahi za Kiswahili. Kinyume na madai yaliyotolewa na Picht na Draskau (1985:32-33) (taz. 1.6,

uk. 11) kwamba hakuna nadharia ya istilahi, nadharia mbalimbali zimetumika kimataifa katika uibuaji wa istilahi imara na uendelezaji wa leksikoni za lugha (taz. Sager na Johnson, 1978:82-4).

### 2.2.1 Nadharia Jumla ya Istilahi

Nadharia Jumla ya Istilahi (NJI) (*General Theory of Terminology*), kama ilivyoelezwa hapo awali, ni nadharia iliyoasisiwa na Prof. Eugen Wüster mwaka wa 1931. NJI kama nyanja ya kisayansi, hutoa msingi wa kisayansi wa kushughulikia kazi ya uundaji wa istilahi, yaani utekelezaji wa misingi ya kiistilahi na mbinu, ambao unapaswa kuwawezesha waundaji istilahi na vyombo vya ukuzaji lugha kutekeleza kazi zao kwa njia bora na yenye ufanisi mkubwa. Nadharia ya istilahi ya Wüster ilitokana na kitabu chake, na pia mhadhara uliohusu "*Einfuhrung in die Terminologielehre und Terminologische Lekikographie*" (Utangulizi wa Nadharia ya Istilahi na Leksikografia Kiistilahi). Machapisho yake mbalimbali na tasnifu yake ya Uzamifu (Ph.D.) iliyochapishwa hadi sasa hutumika kama rejeleo muhimu katika uundaji wa istilahi (Felber, 1984:32). Kitabu cha Wüster kinachotokana na tasnifu yake kina uchunguzi wa kina kuhusu istilahi kama kifaa cha mawasiliano. Vilevile, masuala yanayohusu uasili wa dhana, uhusiano wa dhana, viungo baina ya dhana, sifa za dhana, vijelezi vya dhana, uundaji wa istilahi, usanifishaji wa dhana na istilahi, umataifishaji wa dhana na istilahi, miongoni mwa masuala mengine, yamejadiliwa kwa kina. Kitabu hiki cha Wuster pia ndio msingi wa NJI.

NJI ina sifa tatu maalum zinazohusu lugha na ukuzaji wa istilahi za lugha. Sifa hizo ni pamoja na:

(1) Kazi yoyote ya istilahi inaanza na dhana na wala siyo na istilahi. Lengo lake ni kuwekea mipaka dhana ya 'dhana'. Eneo la 'dhana' ni huru na tofauti na eneo la 'istilahi'. Huku wanaistilahi wakizungumzia kuhusu dhana, wanaisimu huzungumza kuhusu maana ya maneno. Dhana ni kile kinachomaanishwa na istilahi. Uhusiano uliopo baina ya kiashirii na kiashiriwa, kama asemavyo de Saussure (katika Massamba, 1989:79), ni wa sibu.

(2) Ni istilahi za dhana pekee, yaani istilahi mbalimbali, ambazo zina faida kwa wanaistilahi na wala siyo kanuni za uambishaji na sintaksia. Kanuni au sheria za sarufi huchukuliwa kutoka kwa lugha za kawaida.

(3) Mtazamo wa lugha kiistilahi ni wa kisinkronia; yaani maana ya kisasa ya istilahi ndiyo muhimu. Kiistilahi, pia, mifumo ya dhana ndiyo inayofaa katika lugha.

Katika **Nadharia Jumla ya Istilahi**, dhana 'dhana' na uhusiano wake kwa dhana nyingine huchukua nafasi ya kimsingi. Dhana ndio msingi wa NJI na mwanzo wa kazi yoyote ya istilahi. 'Dhana' katika NJI inajelezwa kama elementi ya kufikiria. Ni kiwakilishi cha fikira cha vifaa vya kibinafsi (Felber, 1984:115). Uundaji istilahi na kijelezi cha 'dhana' huathiriwa na **dhamira na upanuzi**. Kulingana na nadharia hii ya NJI, 'dhamira' ni "mkusanyiko wa sifa zote zinazojenga dhana" (taz. ISO/R 1087, na pia taz. Felber, 1984:116 kwa maelezo zaidi ya 'dhamira').

Istilahi 'upanuzi' ina maana mbili: Kwanza, upanuzi wa mfanano unaorejelea mkusanyiko wa elementi zote zinazodhaniwa za dhana inayohusika na kuzitenga. Pia ni mkusanyiko wa vifaa vya kibinafsi vinavyoshughulikiwa na dhana husika (ISO/R 1087). Pili, ni upanuzi wa uunganishaji, ambao ni mkusanyiko wa sehemu zote za tukio kamilifu, zikitazamwa tofauti tofauti (ISO/R 1087) (taz. Picht na Draskau, 1985:41 kwa mifano na maelezo zaidi).

Kipengele cha **uhusiano baina ya dhana** ni muhimu katika NJI. Uhusiano baina ya dhana ni tatanishi na wala si rahisi kuelezeka (taz. Mwansoko, 1990:151). Hata hivyo, kuna aina mbili za uhusiano: uhusiano wa dhana na uhusiano wa somo. Uhusiano wa dhana ni wa mjengo wa uainishaji wa dhana, yaani uainishaji wa somo; na uhusiano wa somo ni wa mjengo wa uainishaji wa somo, yaani uainishaji unaokusudia kuhifadhi hati kama thesaurusi (taz. Mwansoko, 1997). Katika kazi ya kiistilahi, uhusiano kati ya dhana ndio muhimu na hutumika katika kujenga mifumo ya dhana. Uhusiano baina ya dhana unaweza kugawanywa katika makundi matatu makuu: (a) Uhusiano kimantiki, (b) Uhusiano kiujirani, na (c) Uhusiano unganishi.

**(a) Uhusiano kimantiki**

Uhusiano kimantiki umejengeka katika usawa kati ya dhana (taz. Picht na Draskau, 1985:66-8 kwa ufafanuzi zaidi wa aina za uhusiano kimantiki). Kwa kutumia uhusiano kimantiki, ni dhana zenye sifa zinazofanana tu, ndizo zinazoweza kuratibishwa, na ni mbinu na mifanyiko tu ndiyo inayoweza kupangwa kikamilifu. Kwa hivyo, uhusiano kimantiki pekee hauwezi kutumiwa kwa mahitaji ya

istilahi (taz. Felber, 1980).

**(b) Uhusiano Kijirani (Kiontolojia)**

Huu ni aina ya uhusiano unaojengeka kwenye msingi wa ujirani, yaani mgusano usio wa kudumu wa dhana ambao hujenga mfumo. Kuna uhusiano kijirani wa kotekote, na pia kuna uhusiano wa kusaidiana (katika kiwango cha kidhahania); kwa mfano, **mboni ya jicho//nyusi ya jicho**. Uhusiano kijirani hautoshelezi mahitaji ya istilahi, bali unaruhusu tu uratibishaji wa sehemu za tukio kamili.

**(c) Uhusiano Unganishi**

Ni aina ya uhusiano kati ya dhana ambao unaweza kuwa wa kimantiki au kijirani (kiontolojia). Katika uhusiano unganishi, muhimu zaidi ni utambuzi. Dhana huzuiliwa kwa kuongeza sifa nyingine kama mwanajumuiya wa pili wa dhana.

Dhana nyingine muhimu katika nadharia ya Wuster ni **sifa ya dhana**. Sifa ya kidhana hutekeleza dhima muhimu katika kuamua dhamira ya dhana, uendelezaji na uundaji wa vijelezi, upangaji wa dhana katika mfumo, uundaji wa istilahi 'faafu' na, vilevile, katika uteuzi na uchujaji wa visawe miongoni mwa istilahi nyingi katika lugha moja.

Kuna aina mbili za sifa. Sifa hizo ni pamoja na:

1. **Sifa asili:** Ni sifa zinazowakilisha kifaa chenyewe asilia na wala siyo katika uhusiano wake na kifaa kingine.
2. **Sifa zisizo asili:** Ni sifa zinazohusu kifaa katika uhusiano wake na kingine (ISO/R 704).

Katika uteuzi wa sifa bora kama msingi wa dhana, kijelezi chake na istilahi inapendekezwa katika ISO/R 704, kwamba sifa asili ni bora zaidi ya sifa zisizo asili kwa sababu zinaweza kuthibitishwa kwa kukaguliwa na mtu yeyote. Mbali na kujitosheleza zenyewe, sifa asili pia ni nzuri katika kutaja majina ya vifaa sahihi (taz. Felber, 1980:70 na Shirika la Kimataifa la Viwango - ISO/R 704 kwa ufafanuzi zaidi wa umuhimu wa sifa asili ikilinganishwa na sifa zisizo asili).

Dhana nyingine muhimu katika NJI ni **mifumo ya dhana**. Mifumo ya dhana ni kundi la dhana linalounganishwa na uhusiano wa kimantiki au uhusiano kijirani (taz. Felber, 1984:2). Umuhimu wa mifumo ya dhana katika NJI unatokana na manufaa yake katika utekelezaji wa mambo yafuatayo:
Kwanza, utambuaji thabiti wa orodha ya dhana.
Pili, utambuaji wa kiwango cha mlingano kati ya mifumo ya dhana ya lugha tofauti; hii ikiwa ni muhimu katika kutambua visawe vya kiistilahi.
Tatu, uelewaji wa uhusiano baina ya dhana ambao huenda ni muhimu katika uzalishaji wa istilahi.
Nne, uwasilishaji katika kamusi kwa mpangilio bora wa matokeo ya kazi ya kiistilahi (taz. Picht na Draskau, 1985:92).

Suala lingine muhimu katika NJI ni **usanifishaji wa dhana na istilahi**. Wuster aliandaa misingi ya kisayansi ya istilahi na uundaji istilahi. Kuhusu misingi ya istilahi 'faafu,' NJI inasisitiza, kama inavyoelezwa katika ISO/TC 37, uzingatiaji wa vigezo vitano: Yaani, udhahiri, ufupi wa istilahi, uzalishaji wa

istilahi kwa mnyambuliko, utaratibu maalum, na umataifa (taz. 3.3.2.4, uk. 71 na pia taz. Felber, 1984). Hali kadhalika, kulingana na nadharia ya istilahi ya NJI, ambayo inaweza kutumika katika lugha yoyote, dhana mpya zinapoingia katika jamii-tumizi-lugha au sehemu ya jamii, zinafaa kukopwa pamoja na istilahi zake (Mwansoko, 1990:129).

Itafaa kusisitiza kuwa katika NJI, istilahi zilizozoeleka, au zilizozagaa na kuenea katika fahamu za watu kwa muda mrefu hazipaswi kupembuliwa na kubuniwa istilahi mpya mahali pake (Zingatia tathmini ya swala hili katika 2.3, uk. 44). Kadhalika, kwa vile yaliyomo kinadharia ya nyanja maalum kama vile kemia, bayolojia, isimu, husababisha tofauti za kiistilahi za nyanja husika, NJI husisitiza kuwa kazi ya istilahi itengewe au ishughulikiwe na wataalam wa nyanja husika pekee (taz. Mdee, 1990). Kwa usemi mwingine, NJI inasisitiza kuwa kazi ya uundaji wa istilahi ihusishe pande moja muhimu - wataalam wa lugha. Felber (1984:99) hakosei anapodokeza kuwa:

> Katika isimu, mantiki, ontolojia n.k. kuna nadharia tofauti. Kwa hivyo, ni muhimu kuchunguza maendeleo mapya katika nyanja hizo kwa kuzingatia ufaafu wake katika NJI. Ilivyo ni kwamba NJI ni nyanja ya utafiti inayopaswa kuheshimu matokeo ya taaluma nyingine, yanayohusiana nayo na pia yanayotoka kwa wataalam wanaofanya kazi za kiistilahi. Wuster ameweka msingi wa NJI unaopaswa kujengewa kutokana na utafiti wa baadaye.
>
> (Tafsiri yetu)

Nadharia ya Jumla ya Istilahi haijikiti katika uwanja wa isimu pekee inaweza kutumika katika medani za taaluma mbalimbali kama vile mantiki, ontolojia, sayansi ya mawasiliano n.k. Taaluma yoyote, iwe ya mawasiliano au kielimu inahitaji NJI katika

ukuzaji wa istilahi zake.

### 2.2.2 Nadharia ya Istilahi za Kisayansi

Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) ni nadharia changa iliyoasisiwa, kama ilivyotajwa hapo mbeleni, na K.B. Kiingi (1989). NIK ni nadharia ya istilahi ya kisasa, na ilitokana na utafiti wa kina na uzoefu katika fani ya uundaji istilahi uliomwezesha Kiingi kuandika tasnifu ya uzamifu ambayo mada yake ilikuwa: *A Systematic Approach to the Problem of the Expressional Modernisation in the Formal and Natural Science: The Case of Luganda* (yaani, Mtazamo Wenye Utaratibu Maalum katika Tatizo la Usasaishaji wa Vitamkwa katika Sayansi Menyu na Asili: Mifano kutoka Luganda). Tasnifu hii (haijachapishwa bado) pamoja na tasnifu ya baada ya uzamifu - A.D. LITT., pamwe na mihadhara iliyohusu: "*A Theory of Scientific Terminology*"/ "Nadharia ya Istilahi za Kisayansi," aliyoitoa kuanzia mwaka 1996-1998 katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, na kwingineko (k.v. katika semina ya Kiswahili, Eldoret, 10-12/9/97) ndio msingi wa NIK. NIK ina sifa saba maalum zinazohusu lugha na uendelezaji au usasaishaji wa istilahi za lugha. Sifa hizo ni pamoja na;

Kwanza, **dhana za kimsingi:** Kazi yoyote ya ukuzaji na usasaishaji wa lugha ianze na dhana za kimsingi, yaani dhana, kitamkwa na istilahi. Dhana ni za kimataifa, kitamkwa na istilahi si vya kimataifa. Kwa hivyo, NIK inasisitiza, katika kipengele hiki, kwamba dhana mpya zinapoingia katika jamii-tumizi-lugha au sehemu ya jamii, zinafaa kukopwa lakini siyo pamoja na istilahi zake.

Dhana inaweza kukopwa lakini iundiwe istilahi 'faafu' (kwa kuzingatia sifa ya saba ya nadharia hii).

Pili, kile kinachojenga nadharia halisi ni madai yanayokubalika (kuhusu kipindi cha majaribio ya istilahi katika medali ya sayansi). Hapa NIK inasisitiza vipindi 20 na vifungo vya kinadharia 24 (taz. Kiambatisho 1, kuhusu jinsi vipindi hivi vilivyofungamana na vifungo vya kinadharia 24).

Tatu, sheria ya kuongoza uundaji istilahi ya **CFR** (*Conceptual Formation Rule/* Sheria ya Uundaji wa Istilahi (taz. pia Sheria ya Ugeuzamaumbo (TR) ya Chomsky, 1965) huongoza katika kutambua usawa wa sentensi kisarufi na kuwepo au kutokuwepo kwa istilahi fulani katika lugha za kurejelea dhana mpya.

Nne, ni mfumo wa kivipindi wa arki za kidhana. Hii ni sifa mojawapo ya NIK inayojumlisha elementi au arki za kidhana zinazopatikana katika ubongo wa binadamu.

Tano, ni sheria ya uundaji istilahi ya **CTR** (*Conceptual Transformation Rule/* Sheria ya Ugeuzamaumbo Kidhana. Sheria ya **CTR** inasisitiza kwamba istilahi mpya hujengeka au huzalishwa pasi na kuzingatia lugha tunayoitumia katika mazungumzo.

Sita, ni sifa inayohusu kanuni **CBR** (*Conceptual Bridging Rule/* Sheria ya Kidhana ya Kuziba Mapengo (ya Kiistilahi). Kutokana na sifa hii muhimu ya NIK, suala linalosisitizwa ni vitambulishi vya dhana. Waundaji istilahi za Kiswahili wanapaswa kufahamu

vitambulishi *("markers")* vya dhana zilizomo katika Kiswahili na kuundia dhana hizo istilahi mwafaka. Ikiwa lugha za Ulaya zimeweza kufasiri dhana ambazo hazimo katika lugha hizo, Kiswahili pia kina uwezo wa kueleza dhana za kigeni (taz. Kimani Ruo, 1989:99).

Sifa ya saba na ya mwisho, na ambayo ndiyo muhimu, sio tu katika NIK bali pia katika tasnifu hii, ni vigezo vya istilahi 'faafu' vya **PEGITOSCA**. Kiingi, kama alivyofanya Wuster, aliandaa misingi na vigezo vya kisayansi vya istilahi 'faafu' ili kuleta usasa na usawa au upatanisho wa kimataifa katika shughuli ya ukuzaji wa istilahi za lugha mbalimbali duniani (kwa ufafanuzi zaidi wa vigezo vya **PEGITOSCA**, taz. 1.6, uk. 11 na 3.3.2.4, uk. 71).

## 2.3 Tathmini ya Nadharia za Uundaji wa Istilahi

Nadharia za istilahi zilizojadiliwa hapo juu ni nadharia zinazoweza kutathminiwa katika fani anuai, na katika lugha yoyote duniani. Nadharia Jumla ya Istilahi (NJI), kwa mfano, inashughulikia misingi na kanuni za kisayansi bila kujifunga katika fani mahsusi au lugha maalum, kinyume na Nadharia Maalum ya Istilahi (NMI), ambayo ina kanuni za kiistilahi zinazojibana kwenye lugha mahsusi (taz. Felber, 1984). Labda ni kutokana na sababu hii ndipo Mwansoko (1990:149) akatoa madai kuwa: "Kutokana na uzoefu wangu katika fani ya uundaji istilahi, hakuna mwandishi ye yote ambaye ametambua udhaifu katika Nadharia Jumla ya Istilahi na mbinu ya kidhana". Pamoja na umaarufu, uzito, na mafanikio katika shughuli ya uundaji istilahi yaliyopatikana

kutokana na matumizi ya nadharia jumla ya istilahi, nadharia hii haikosi **dosari na udhaifu** kama inavyodhihirika katika mjadala unaofuatia:

Kwanza kabisa, misingi na vigezo vya istilahi 'faafu' vinavyotetewa na NJI ni vichache mno na havikuzama. Kwa mfano, NJI haikuzama katika vigezo muhimu vya kisayansi vya uangavu, utusani, utaratibu uliosawa, na ukubalifu/ufaafu wa istilahi (taz. pia Picht na Draskau, 1985:29).

Pili NJI, kwa kusisitiza kwamba dhana mpya zinapoingia katika lugha changizi zinapaswa kukopwa pamoja na istilahi zake, inabainisha kwamba nadharia hii haitambui ubunifu katika lugha. Dhana hutuunganisha kimawasiliano na huwa mara nyingi sawa katika lugha mbalimbali. Hata hivyo, dhana ni za kimataifa, istilahi si za kimataifa. Ndiposa Mdee (1995:46) hakosei anaposema kuwa:

> Kiswahili cha Kenya na Tanzania kimeanza kutofautiana taratibu kulingana na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili katika nyanja tofauti kwa kila nchi kwa wakati tofauti. Kwa mfano, Tanzania iliposhabihikia siasa ya Ujamaa baina ya 1967 na 1985, ilijiundia msamiati wa kueleza dhana na fikra za kijamaa...Wakenya walipopata Uhuru...walibuni msamiati uliokidhi mahitaji yao ya mawasiliano...

Sifa ya NJI ya kukopa dhana pamoja na istilahi huenda ilinuiwa kuyapa mataifa ya kigeni umbele zaidi na kudumaza mataifa mengine.

Tatu, istilahi kuzoeleka au kuenea katika fahamu za watu kwa muda mrefu si sababu tosha ya kuifanya istilahi isipembuliwe. Kwa mfano, neno 'mazingara' lilibuniwa kimakosa, uzoefu au mashiko

yake ya kimataifa hayamaanishi kwamba tuendelee kulitumia. Hii ni sifa mojawapo ya NJI inayowafunga waundaji istilahi bure wanapotaka kukosoa istilahi makosa na kuunda istilahi 'faafu' za kurejelea dhana mpya kisawasawa katika lugha.

Nne, kwa kusisitiza kwamba shughuli ya uundaji istilahi ihusishe pande moja, yaani wataalam wa fani sadakta husika, NJI inapuuza umuhimu wa walengwa. Uchunguzi uliofanywa na Mdee (1980), Mac William (1985), Sewangi (1996), kuhusu ukubalifu wa istilahi kwa walengwa, umebainisha kuwa wengi wao hawakupendezwa na istilahi zilizoundwa bila kuwashirikisha. Wataalam wa lugha wanaweza kutoa misingi na vigezo vya istilahi na mwelekeo mzima wa kiisimu katika kazi ya uundaji istilahi, mahali ambapo walengwa wanaweza kushirikiana nao (waundaji istilahi) kwa kutoa ufafanuzi wa dhana mbalimbali katika fani inayohusika (taz. Sewangi 1996:19). Kwa hivyo, waundaji istilahi hawana budi kuwashirikisha watumiaji katika shughuli ya kuzalisha istilahi, hususani za isimu ya Kiswahili.

Hata hivyo, ingawa nadharia ya NJI ina dosari na udhaifu uliotajwa hapo juu, bado inaweza kuwa na ubora kwa ajili ya kujaliza nadharia changa ya NIK; mathalani, vipengele vinavyohusu dhana na mifumo ya dhana. Kinyume na NIK ambayo husisitiza kuwa uundaji wa istilahi uanze na dhana za kimsingi, msingi wa NJI ni kwamba uundaji huo uanze na dhana. Aidha, kipengele kinachohusu ujumlishaji wa dhana, au dhana zinazokaribiana kimaana kuundwa pamoja, ni kijalizo muhimu kwa nadharia mpya ya NIK. Ni maoni yetu kwamba nadharia za kiistilahi za NJI na NIK, zikiimarishwa

na wananadharia, zinaweza kuendeleza Kiswahili, ama lugha yoyote ile, kwa njia yenye ufanisi mkubwa. Nadharia ya istilahi za kisayansi ya PEGITOSCA ni yenye usifabia na haijikiti katika Kiswahili au Luganda tu bali inaweza kutumika katika lugha mbalimbali ulimwenguni.

## 2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili

Katika sura hii, tumeeleza bayana umuhimu wa nadharia kwa walengwa na waundaji istilahi, na aidha katika kazi ya kiistilahi kwa jumla. Tumejadili kuwa istilahi hutegemea nadharia, na kwamba nadharia tepetepe haiwezi kuibua istilahi 'faafu', zenye 'usayansi' na zinazokubalika kimataifa. Aidha, tumefafanua mbinu tendajikazi kiistilahi zinazotumiwa na wanaleksikografia, hususani mbinu ya tafsiri na mbinu ya kidhana. Imebainika, kutokana na ufafanuzi huu, kwamba mbinu ya kidhana ndiyo inayopendelewa na wananadharia wengi kutokana na himizo la mbinu hii kwamba istilahi ziundwe katika ufungamano wa kidhana. Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kuwa kuna nadharia za istilahi ambazo ni Nadharia Jumla ya Istilahi (NJI) na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) baina ya nyinginezo. Tumefafanua sifa kuu za kila mojawapo ya nadharia hizi. Imebainika, kutokana na ufafanuzi huu, kwamba katika NJI, dhana 'dhana' na uhusiano wake kwa dhana nyingine huchukua nafasi ya kimsingi. Pia istilahi na dhana muhimu katika nadharia ya NJI, kama vile dhamira, upanuzi, uhusiano baina ya dhana, sifa ya dhana, mifumo ya dhana na usanifishaji wa dhana na istilahi, zimejadiliwa kwa mapana.

Fauka ya hayo, katika sura hii, mna ufafanuzi wa nadharia changa ya NIK na sifa kadha wa kadha zinazojenga nadharia yenyewe. Mojawapo ya sifa iliyojadiliwa na inayosisitizwa katika NIK ni kwamba dhana ni za kimataifa lakini istilahi si za kimataifa (Yaani kila taifa lina uhuru wa kujiundia istilahi zake panapotokea haja ya kufanya hivyo). Kwa hivyo, dhana zinapokopwa kutoka lugha za kigeni, yafaa ziundiwe istilahi mpya. Pia imeelezwa kuwa misingi na vigezo vya **PEGITOSCA** vya kisayansi vya istilahi 'faafu' ni sifa nyingine muhimu inayofanya nadharia ya NIK kupata umaarufu. Aidha, tumeshughulikia tathmini ya nadharia za istilahi. Kutokana na tathmini hii, imedhihirika kwamba nadharia ya NJI (na mbinu ya kidhana), kama nadharia yo yote ile, ina udhaifu, kinyume na madai ya Mwansoko (1990:149) anayesema haina. Tathmini hii pia imebainisha kwamba nadharia ya Wuster ya istilahi (NJI) ni kijalizo muhimu cha nadharia mpya ya Kiingi (NIK).

Kutokana na sura hii, tunatarajia kuwa malalamiko ya muda mrefu yanayohusu udhaifu wa istilahi za isimu ya Kiswahili, yatapungua ama yatakwisha kabisa. Hususani, malalamiko yanayohusu:

- Waundaji istilahi binafsi na vyombo vya kukuza istilahi vya BAKITA, BAKIKE na TUKI kutofahamikiwa na nadharia za istilahi.
- Istilahi za isimu kukanganya na kutapanyisha, kwa vile hazikitwi katika nadharia mufidi za istilahi.
- Istilahi butu kinadharia kupewa makali au kipaumbele.

Kutokana na sura hii iliyoshughulikia nadharia za istilahi, imejadiliwa pia kuwa malalamiko haya hutokea ama hujitokeza kwa

sababu waundaji istilahi na wasanifishaji istilahi hawafahamu na hawazingatii kanuni za istilahi na nadharia za istilahi. Tunatarajia, kwa hivyo, kuwa utafiti huu utawafaa katika kufanya kazi yao kwa ufanisi zaidi. Aidha, tunatarajia kuwa tathmini ya nadharia za istilahi itawafaa watumiaji na wapenzi wa Kiswahili wote watakaosoma kwa makini kazi hii, hususani, katika kuelewa nadharia za uundaji wa istilahi pamwe na kazi za istilahi, bila shida kubwa.

# SURA YA TATU

## UUNDAJI WA ISTILAHI ZA ISIMU YA KISWAHILI

### 3.0 Utangulizi

Wakiandika kuhusu uendelezaji na uundaji wa istilahi za Kiswahili Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:22) wanadai kuwa:

> Ukuzaji wa kudhamiria wa istilahi za Kiswahili ambao umekuwa ukiendelea tokea mwaka 1930 umekuwa ukikabiliwa na matatizo anuwai na hivyo kuufanya usiwe na mafanikio ya kuridhisha. Matatizo hayo yanajumuisha **upungufu mkubwa wa istilahi katika takribani nyanja zote za taaluma; mparaganyiko wa baadhi ya istilahi unaosababishwa na misingi potovu na au isiyotimilifu ya uundaji na usanifishaji wa istilahi** ....ni muhimu (kama suluhisho) kuichambua kwanza misingi, taratibu na mbinu zinazotumiwa katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili.

Maoni ya wataalam hawa yana mashiko na ndio msukumo na msingi wa sura hii. Tunakubaliana na Tumbo na Mwansoko (1992:22) kwamba Kiswahili kina 'pengo' la kiistilahi katika njanja zote za taaluma. Kwa hivyo pana haja ya kuchunguza na kutathmini msingi, kanuni na mbinu za uundaji wa istilahi za Kiswahili ili kutatua tatizo kubwa katika ukuzaji wa lugha hii, hasa katika 'isimu'. Azma ya sura hii, kwa hivyo, ni kuchunguza "usayansi" katika istilahi na mbinu za uendelezaji wa leksikoni ya isimu ya Kiswahili. Tutaanza kwa kutoa vijelezi na kufafanua maana ya dhana ya istilahi, istilahi za isimu ya Kiswahili, maana ya "usayansi," misingi ya usayansi katika isimu na katika istilahi za isimu ya Kiswahili.

Kabla ya kutathmini 'usayansi' katika mbinu zinazotumiwa na vyombo vya BAKITA, BAKIKE, TUKI na wanalugha binafsi akina Nabhany, Kapinga na Mbaabu katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili, tutachunguza misingi na kanuni zinazotumiwa kwa wakati huu ili kutambua chanzo cha 'kuparaganyika na kupwaya kwa istilahi,' upotovu katika misingi hiyo, na baadaye kupendekeza pafanyike nini ndipo misingi ya kisayansi ijitosheleze katika uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Aidha, tutayaibua yale mambo ya msingi katika kujenga hoja za tasnifu hii.

### 3.1 Maana ya dhana ya Istilahi

Dhana ya istilahi ni telezi mno, na kijelezi chake ni suala ambalo limeshughulisha kalamu ya wataalam wengi. Mathalani, Mwangomwango (1977:8) anaeleza "'istilahi' kama maneno ya kitaaluma ambayo yanatumiwa katika kila taaluma na sharti kila taaluma itengewe maneno kwa ajili ya maelezo maalum."

Naye Akida (1975) anaeleza 'istilahi' kwamba ni maneno yanayotumika katika sanaa ya sayansi. Gibbe (1993:144) anatumia neno 'msamiati' kwa maana moja na 'istilahi'. Ingawa tunaamini kwamba mtaalam huyu ana sababu zake za kutotafautisha msamiati na istilahi, sisi tunachukulia istilahi kama sehemu ya msamiati wa lugha inayopaswa kuelezwa bayana na wala siyo 'vivi hivi' tu. "Istilahi" inahitaji maelezo mwafaka yanayopelekea kuitafautisha na "msamiati" au "maneno." Felber (1984:108) katika kufafanua maana ya neno "istilahi" anasema kwamba ni ishara ya kiisimu inayowakilisha dhana moja au wakati mwingine dhana nyingi.

Istilahi yaweza kuwa alama, herufi, neno au kifungu cha maneno.

Isisitizwe hapa kwamba neno 'istilahi' hutumika kwa ufupi wa maneno mengi ya kiufundi kufuatana na ujuzi au elimu fulani kama vile sayansi, siasa, uchumi n.k.; yaani maneno ya kitaaluma au kiufundi. Kwa maneno mengine, dhana ya istilahi imefungamana na dhana ya nyanja maalum katika jumla ya maarifa ya binadamu. Kila uwanja una msamiati wake maalum wa kuwakilisha dhana mahsusi katika uwanja husika (Bwenge, 1996:56).

Wataalam wa taaluma yoyote ile huwa wanafanana kwa ari waliyo nayo ya kujitafutia uhakika wa mambo kwa kufuata kanuni na taratibu imara za kutambua ukweli wa masuala ya elimu yao. Hali hii huwapa ushirikiano wa kipekee na hujibainisha hasa katika matumizi yao ya lugha ya kitaalamu na wala sio ya kawaida. Kwa mfano, wanaisimu wa Kiswahili ni wataalam wanaojishughulisha na kutafuta ukweli wa maswala yanayohusiana na isimu ya lugha ya Kiswahili. Ili kutekeleza dhima hii, huwa kuna ulazima wa wataalam hawa kuwa na istilahi "faafu" za isimu ya Kiswahili za kuwezesha taaluma hii kujieleza kikamilifu katika kipengee cha 'isimu,' kwa kutumia Kiswahili na, kwa namna hii, kufanikisha mawasiliano baina yao na watumiaji wa Kiswahili wanaolengwa.

Felber (1984:3) anaeleza umuhimu wa istilahi kuwa ni:

1. Kuimarisha mpangilio wa maarifa kwa kuzingatia mahusiano ya dhana (dhana na mifumo ya dhana ilingane katika mambo yanayohusu sayansi na teknolojia).

2. Kufanikisha ubadilishanaji wa maarifa, ujuzi na teknolojia (maarifa, ufundishaji, usomaji wa matini ya kisayansi na kiteknolojia).
3. Kuimarisha uundaji na usambazaji wa maarifa kisayansi na kiteknolojia (maandishi ya kisayansi, uhariri, uchapishaji).
4. Kutafsiri katika lugha nyingine makala ya kisayansi na kiteknolojia.
5. Kurahisisha utoaji na uwekaji pamoja wa taarifa husika.
6. Kuhifadhi na kutoa taarifa inayohusu sayansi na teknolojia.

Kutofahamu maana na umuhimu wa istilahi, kwa maoni ya Felber (1984), ni sababu mojawapo inayowafanya watu 'kujiundia' istilahi zao kiholela bila kusubiri kuundiwa na vyombo vya ukuzaji istilahi. Baada ya kuzizoea istilahi zao huwa wagumu kukubali zile walizoundiwa au zile zilizoundwa pasi na wao kushirikishwa.

Felber (1972, 1984:2), Mwansoko (1990:44) na Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:17) wanaelekea kukubaliana kwamba uendelezaji wa istilahi kama sayansi ni sharti uzingatie kanuni na misingi ya kiistilahi pamoja na ushirikiano wa kimataifa utakaoleta makubaliano juu ya dhana na mifumo ya dhana; yaani kuna haja ya kusanifu dhana na mifumo ya dhana katika taaluma na utaalamu, hoja ambayo ina mashiko na, hivyo basi, tunakubaliana nao.

Katika kusisitiza umuhimu wa istilahi, Felber (1984) anadokeza kwamba kuna idadi kubwa ya dhana mpya ambazo huzuka katika nyanja zote za matendo ya binadamu, na ni lazima zielezwe kwa kutumia istilahi zilizoko, ama kuunda istilahi mpya (baada ya kuiangalia

dhana inayohusika kwa makini) kwa kuambatanisha elementi za neno (mzizi na viambishi) katika lugha husika.

Tukumbushane pia kwamba kuna idadi ndogo sana ya elementi za neno ikilinganishwa na dhana ambazo ni mamilioni. Uhusiano huu mbaya, mbali na kukwamiza maendeleo ya sayansi na teknolojia ulimwenguni, hudhoofisha mawasiliano baina ya vyombo mbalimbali vinavyotumia lugha tofauti. Kadhalika, ni ukweli kwamba ubadilishanaji wa maarifa, ujuzi, na teknolojia unawezekana tu iwapo istilahi katika lugha husika zitaendelezwa kwa kuzingatia kanuni misingi na utaratibu maalum wa uundaji wa istilahi. Ingawa umuhimu wa (na dhima ya) istilahi kama unavyoelezwa na Felber (1984) hauhusiani na taaluma yoyote maalum, ukitiliwa manani utatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Vilevile, utafaidi mawasiliano hakika na sahihi katika fikira pevu za kisayansi kama itarajiwavyo, kwa vile kiambato muhimu cha mawasiliano maalum ni "istilahi."

Kadhalika, ingawa tunafahamu kuwa istilahi ni mfumo wa msamiati maalumu unaotumika katika taaluma maalum (TUKI, 1990), sisi katika tasnifu hii tutatumia neno 'istilahi' kwa maana ya taaluma inayoshughulikia nadharia, kanuni, misingi, mbinu na miongozo ya uundaji wa istilahi. Kinachotofautisha 'istilahi' na 'neno' ni ukosefu wa utata, udhahiri, na uangavu (taz. Mwansoko, 1990:162 kwa maelezo zaidi).

## 3.2 Maana ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili

Istilahi za Isimu ya Kiswahili ni msamiati maalum ulioteuliwa, ukapewa umbele, urasmi, na kuingizwa katika kamusi ya lugha sanifu, na unatumika mara kwa mara katika kisanifu. Huu ni msamiati maalum katika taaluma ya isimu unaojidhihirisha katika lugha andishi kwenye matini mamboleo, na katika lugha ya mazungumzo ya kila siku miongoni mwa watumiaji lugha kisanifu, au kusikika katika vyombo vya habari kama vile redio na runinga. Aghalabu istilahi za isimu ya Kiswahili hupatikana katika makamusi ya isimu, hususani *Kamusi ya Isimu na Lugha*, ya TUKI (1990), *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*, TUKI (1996), na katika machapisho ya Kiswahili ya waandishi kama vile Nabhany (1982), Kapinga (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* DSM, TUKI, Mbaabu (1992) *Sarufi ya Kiswahili*, na mengine mengi. Ili kuelewa bayana istilahi za 'isimu' ya Kiswahili, ni muhimu tueleze, angalau kwa kifupi, maana na matagaa ya isimu ya Kiswahili.

'Isimu' ni sayansi ya lugha ijishughulishayo na jinsi lugha mbalimbali zilivyopangika na kusikika katika sehemu tofauti tofauti ili kufanyiza mfumo wenye misingi yake katika kanuni maalum. Isimu inahusu kanuni zote za lugha na arudhi ambazo ndizo mihimili ya lugha yoyote ile.

Isimu ya Kiswahili ina matagaa mengi. Nayo ni pamoja na:

**Fonetiki:**

Ni tawi la isimu linaloshughulikia sauti za vitamkwa ikiwa ni pamoja na kuchunguza ala za sauti, namna ya kutolea sauti, aina

ya vitamkwa, na kusafiri na kusikika kwa sauti. Ni fani inayoangalia utoaji wa sauti, na hali za sauti hizo.

**Fonolojia:**

Ni taaluma inayoshughulikia mpangilio wa sauti katika lugha; yaani namna sauti zinavyotumika, zinavyojumlishwa kwa pamoja na kupangiliwa ili kuunda maneno. Kila lugha ina namna yake ya kupanga sauti zake ili kutofautisha na lugha nyingine zote ulimwenguni. Mathalani, Kiswahili hutumia umbo la KVKV (Konsonanti ikifuatiwa na Vokali).

Fonolojia husaidia katika kutambua lugha, lafudhi, au lahaja ngeni, utamkaji wa sauti ziletazo maana, kuunda maneno/istilahi, na kutambua mabadiliko ambayo hutokea baada ya vitamkwa kukusanyika katika mpangilio au mfuatano katika maneno. Vitamkwa vinapokutana katika mpangilio au mfuatano katika neno, mara nyingi huathiriana na hutokea uwiano wa sauti. Katika uundaji wa istilahi, dhana ya fonolojia ni muhimu sana (Gibbe, 1981: 2).

**Mofolojia:**

Ni tapo la isimu linaloshughulikia maumbo ya maneno. Dhana ya mofu, na mofimu ni sehemu ya mahusiko muhimu ya mofolojia.

**Sintaksia:**

Ni tawi la isimu linaloshughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi.

**Leksikografia:**

Ni tapo la isimu linaloshughulikia utaalamu wa kuunda istilahi na kamusi za namna mbalimbali. Kwa hivyo, isimu ya Kiswahili ni taaluma maalum ambayo ina matagaa mengi na istilahi zake. Katika tasnifu hii, tutashughulikia istilahi za isimu ya Kiswahili zilizosanifishwa pekee, na tathmni ya 'usayansi' wa istilahi hizo

itafanywa bila kujibana katika tagaa moja maalum.

Kuhusu umuhimu wa "isimu," Whorf (1956:232) anasema:

> Isimu bado ni changa.... watu hawajatambua umuhimu na ukwasi wa nyanja zinazoshughulikiwa na isimu na kwamba kanuni zake ndizo huongoza makubaliano ya aina yoyote na uelewano baina ya binadamu... Muda si mrefu isimu, kama afanyavyo hakimu kotini, itakaa na kutoa hukumu kuhusu matokeo ya uchunguzi ufanywao na taaluma nyingine za kisayansi kabla ya maana ya matokeo hayo kubainika.

Licha ya umuhimu huu wa isimu katika kuchunguza lugha kwenye matumizi yake mbalimbali, ikiwamo fasihi, na maeneo ya kisayansi na kadhalika, inaelekea watu hawajali 'usanifu' wa istilahi za Kiswahili katika Afrika Mashariki, na istilahi zinaendelea kubuniwa kiholela (Massamba 1989:69). Kuhusu uundaji huria wa istilahi Mbaabu (1991:112) anasema:

> Ni wazi kwamba, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Baraza la Kiswahili la Tanzania (BAKITA) hazifanyi kazi sawa na ile iliyokuwa ikifanywa na Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ya kuwa kielelezo bora cha matumizi ya Kiswahili **kote** katika Afrika Mashariki. Kutokuwepo na chombo kama hicho kumezusha hali ambayo waandishi wanaandika kwa kile wao binafsi wanachofikiria kuwa ni Kiswahili Sanifu....

Maoni haya ya Mbaabu yana uzito, na tunakubaliana naye kwamba, kufikia sasa, hakuna chombo chenye uwezo wa kutoa ushauri kuhusu matumizi ya istilahi sanifu katika machapisho mbalimbali. Maneno kama vile **walalahoi** (masikini, akina yakhe), **changudoa** (malaya) si sanifu lakini yanapatikana katika magazeti ya Kiswahili nchini Tanzania, na inaonekana wataalam wa BAKITA, na TUKI hawasaidii kurekebisha hali hii. Kwa hivyo, litakuwa jambo bora ikiwa istilahi za isimu ya Kiswahili zitashughulikiwa kwa ushirikiano

wa nchi zote za Afrika Mashariki, na uamuzi wa Kiswahili sanifu na kile kisicho sanifu kutoachiwa waandishi na wachapishaji. Kadhalika, Baraza la Kiswahili la Kenya (BAKIKE) lishirikiane na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) katika chuo kikuu cha Dar es Salaam kwenye miradi ya uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Pia ushirikiano uwepo kwenye uandishi wa kamusi ya isimu na lugha ili kutatua tatizo la uundaji istilahi zisizo kubalika kimataifa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Isitoshe, ushirikiano wa vyombo vya kukuza Kiswahili utasaidia katika kutatua tatizo la **upungufu** wa istilahi za isimu ya Kiswahili unaong'amuliwa na waandishi, wafasiri, wakalimani au walimu katika matini za sanaa, sayansi na teknolojia. Takwimu za istilahi za Isimu (1990) zinaoyesha kuwa ni 859 pekee (Irira 1990:19).

Akida (1990:vi), kwenye dibaji ya *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi*, anasema:

> Nasadiki kuwa Mwongozo huu utasaidia ubunifu na ukuzaji wa istilahi iwe kwa mtu binafsi, asasi au taasisi kwani: (1) Unazingatia vipengee vyote muhimu katika masuala ya istilahi (2) Unatoa fursa kwa kila mtu kubuni istilahi kwa mpango na utaratibu mwelekevu ulio hakika na sahihi...Utasaidia sana watu binafsi na asasi kuinua kiwango cha uundaji istilahi kwa mujibu wa kaida shurutishi na kanuni tama....Hapana shaka kuwa Mwongozo huu utakuwa kichocheo na kisababishi cha harakati za kukuza istilahi kuhusiana na hududi pana ya mawasiliano kitaaluma...

Pamoja na azma hii anayoieleza Akida, Mwongozo huo ulinuiwa kusaidia kudhukuru mambo kisayansi, kupevusha fikira sahihi

na hakika juu ya istilahi na kutoa ndaro ya kukuza ubunifu wa istilahi za Kiswahili kisayansi. Hata hivyo, ni bahati mbaya kuwa *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* (1990) si kiongozi madhubuti cha usanifishaji na uundaji wa istilahi za Kiswahili. Mwongozo umeegemea sana katika uundaji wa istilahi na wala sio usanifishaji ndiposa 'usanifu' wa istilahi ungali unapuuzwa na waandishi na watumiaji wa Kiswahili. Pana haja kubwa ya BAKITA na TUKI kuandika upya Mwongozo wa kuunda na kusanifisha istilahi, kwa kuzingatia misingi ya kisayansi, utakaowafaa sana wanalugha wa Kiswahili na utakaoweka wazi misingi au kanuni za kuikubali istilahi kuwa 'sanifu" na "yenye usanyansi." Kadhalika, istilahi za isimu ya Kiswahili zinazowakilisha dhana, zinazokaribiana kimaana, au zinazotokana na shina moja la neno, zisanifishwe pamoja. Ili kuepuka tatizo la vurugu na utata wa usawazishaji istilahi nusunusu, vyombo vya BAKITA na BAKIKE vitoe agizo rasmi kwa wanaleksikografia wote kupeleka istilahi zao kwa vyombo hivi zikiwa tayari katika ufungamano wa kidhana. Istilahi za isimu ya Kiswahili zitakazoundwa moja moja na kiholela au bila kufuata msingi na kanuni za kisayansi zinyimwe ithibati na mabaraza haya. Ingawa tunafahamu kuwa matumizi ya istilahi zisizosanifishwa si tatizo la lugha ya Kiswahili pekee, na kwamba lugha nyinginezo kama vile Kiarabu hukumbwa na tatizo hili pia, matumizi ya istilahi za aina hii yanapasa yasitambuliwe kirasmi (Ibrahim, 1989), na hayana budi kukomeshwa.

### 3.3 Maana ya 'Usayansi'

Neno "sayansi" kwa mujibu wa maelezo ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981:250) ni:

> Elimu inayotokana na uchunguzi, majaribio, vipimo na kuthibitishwa kwa muda uliopo.

'Sayansi' ni mtaala wa maarifa yanayoweza kufanya mfumo ambao kwa kawaida hutegemea kuona na kujaribisha hoja (Whorf, 1956). Nadharia za sayansi zinazingatia kanuni za kijumla au sheria ambazo hujaribu kueleza ni kwa namna gani na ni kwa nini jambo au tukio fulani limefanyika. Nadharia inayoendelezwa na mwanasayansi haiwezi kukubalika kama sehemu ya elimu ya kisayansi kabla ya kuthibitishwa na uchunguzi wa watafiti wengi. Ili elimu yoyote iwe ya kisayansi hasa, ni lazima ifanyiwe majaribio hadi kupatikana kwamba ni ya kweli.

"Usayansi," kadhalika, ni uwezo wa istilahi na mbinu za uundaji wa istilahi kuweza kufanyiwa majaribio ili 'ufaafu' wake kueleweka. Isisitizwe hapa kwamba majaribio hayo hufanywa kwa kufuata kanuni na misingi maalum inayotumika katika uundaji wa istilahi yenye ukubalifu wa kimataifa. 'Usayansi,' mbali na kuchunguza mfumo ulio sawa wa hoja na nadharia inayoizunguka, pia huonyesha mikabala inayozingatiwa na mwanaisimu kwa muda uliopo kuhusu taaluma yake (Robins, 1989:6).

#### 3.3.1 Misingi ya Usayansi Katika Isimu ya Kiswahili

Suala la misingi ya 'usayansi' katika isimu halijashughulikiwa kikamilifu na wanaisimu wa Kiswahili. Wataalam na wanaisimu

wengi hufafanua maana ya isimu kuwa ni 'sayansi' ya lugha, na hueleza matagaa yake pasi na kuzama katika kipengele cha misingi ya 'usayansi' katika isimu.

Whorf (1956) katika makala yake "*Linguistics as an Exact Science*" anaeleza historia ya isimu. Isimu kihistoria ni sayansi kongwe. Mtaalam huyu anatufichulia kwamba sayansi ya isimu iliasisiwa na mtaalam mmoja kwa jina Panini wa India karne nyingi kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Panini yadaiwa alikuwa mwana alijebra aliyeshughulikia mpangilio wa ishara na alitumia fomyula kwa njia ya kisasa katika kueleza mifumo ya lazima ya Ki-Sanskrit.

Ni maoni ya Whorf (1956) kwamba 'sayansi' huanzia na humalizikia katika mazungumzo. Maneno kama vile 'chambua, linganisha, gundua, fikiria, dai, dhania, onyesha' humaanisha kwamba mwanasayansi anapofanya jambo lolote huzungumzia vitu avitendavyo. Matokeo ya uchunguzi wa mwanasayansi hayana umuhimu kabla ya kuingizwa katika **lugha**. Matumizi ya kisayansi ya lugha huhusishwa na misingi na kanuni za kisayansi zinazochunguza matamko yote; yaani isimu.

Ni ukweli usiopingika kuwa isimu ni sayansi kimajaribio. Data yake hutokana na maono na uchunguzi wa mara nyingi. Majaribio katika 'isimu' kama ilivyo katika fizikia, biolojia, na kemia huongozwa na nadharia za kielimu ila tu hayahitaji vifaa vya kiufundi. Badala ya kutumia vifaa vya kiufundi, isimu hubuni na hutumia taratibu mahsusi (Robins, 1967).

Isimu huunda taratibu ambazo, kama dira, huiwezesha kueleza mifumo kamili inayohitaji kushughulikiwa. Isimu kimajaribio, kama biolojia, huwa na 'wanyama' wa kufanyia majaribio ingawa 'wanyama' wenyewe ni binadamu. Binadamu kama kifaa ndiye msaidizi na mfahamishaji wa mtafiti wa kiisimu na hulipwa kwa kazi yake. Yeye ni zana za kazi na wala si mwalimu wa mtafiti (Whorf, 1956:230). Kwa jumla, kuna 'usayansi' katika isimu. Misingi ya usayansi katika isimu ni pamoja na:

1. Kuchunguza hatua za kitaaluma kwa maono ya mara nyingi.
2. Kutoa misingi na kanuni asilia za jumla ambazo huongoza katika ukusanyaji wa data.
3. Kufanyiwa majaribio kwa data inayokusanywa na kuthibitishwa kwa muda uliopo.
4. Kuchunguza lugha kwa njia sawa kama afanyavyo mwanasayansi anapochunguza fizikia au kemia kwa utaratibu maalum.

Todd (1987:5) hakosei anapokiri kwamba isimu ni 'sayansi' ya lugha kwa kusema kuwa:

> Mwanaisimu azma yake ni kutenda kisayansi, hujaribu kuchunguza lugha kwa njia iliyo sawa na anayoitumia mwanasayansi anapochunguza fizikia au kemia kwa utaratibu maalum. Mwanaisimu hudadisi matumizi ya lugha, huunda nadharia tete kuihusu, hufanyia nadharia tete majaribio na huiimarisha kwa msingi wa ushahidi aliokusanya.

Naye Robins (1989), katika kutetea kauli kwamba isimu ni 'sayansi' ya lugha, anadokeza kwamba 'isimu' hushughulikia nyenzo maalum za lugha. Nyenzo hizo huwa za kimaongezi na kimaandishi zinazowasilishwa kwa umma na kuthibitishwa kwa kurejelea misingi kamili na nadharia inayoweza kubuniwa. Jukumu la isimu katika

mfanyiko huo ni kuchambua nyenzo husika na kutoa kauli za kijumla zinazohusiana na kanuni, kaida, na aina tofauti tofauti (kama vile utamkaji katika uneni au maandishi) ambazo hupatikana katika upeo wake. Katika utendaji kazi na utoaji wa kauli zake, isimu huongozwa na kanuni tatu za kisayansi. Nazo ni:

(i) Ukamilishaji, ushughulikiaji wa kina kirefu wa nyenzo zote muhimu.

(ii) Ulinganifu wa mtiririko, unaosisitiza ukosefu wa kujikanganya kwa kauli zitolewazo na zinazopasa kuzingatia misingi maalum.

(iii) Ikitisadi, ambapo kauli fupi na za mkato au uchambuzi unaotumia istilahi chache kutumiwa badala ya istilahi na kauli ndefu (taz. 3.3.2.4, uk. 71).

Isimu, kama sayansi ya lugha, inachukua nafasi muhimu sana katika taaluma za kisayansi kwa sababu ndiyo huchunguza matukio au hali thabiti za lugha kwa kutumia lugha kuzieleza. Isimu leo hudhamiria kueleza tukio la lugha kama utata wa sehemu zinazohusiana. Ikichukuliwa kama 'sayansi,' isimu inaendelea kukuzwa kiistilahi ili iweze kueleza lugha yote pamoja na matokeo ya lugha kama inavyodhihirika kimuktadha. Lugha mbalimbali ulimwenguni huwakilisha data ambazo zinaweza kuthibitishwa kwa maelezo ya kiisimu. Isimu hutoa maelezo sahihi ya kiuchambuzi kuhusu tukio lolote la lugha. Ni kioo kinachopiga matumizi ya lugha mbalimbali. Mwanaisimu, kama afanyavyo mwanasayansi ye yote, hushughulikia nyenzo zake kwa kuona, kubainisha, kudadisi kaida husika, kubuni nadharia tete azifanyiazo majaribio dhidi ya data zilizoko ili kuthibitisha maelezo ya awali na kutoa hukumu kuhusu maswala kama vile ukubalifu, uhakika, ukweli wa

kauli fulani, na kadhalika. Kwa muhtasari, isimu ni 'sayansi' ya lugha kwa sababu ina malengo maalum na wazi kuhusu machukulizi ya taaluma yenyewe.

### 3.3.2 'Usayansi' katika Istilahi za Isimu ya Kiswahili

'Usayansi,' kama tulivyoeleza mbeleni, ni uwezo wa istilahi kufanyiwa majaribio ili 'ufaafu' wake ueleweke kwa kufuata na kuzingatia taratibu au kanuni maalum za uundaji wa istilahi. Istilahi yenye usayansi ni ile inayokidhi na kuzingatia misingi na kanuni za istilahi, na kwa namna hii, kuwa na ukubalifu wa kimataifa. Usayansi wa istilahi ni jambo muhimu katika mawasiliano ya kitaaluma kwa sababu mbili: kwanza, 'usayansi' hudhihirisha sifa bainifu za istilahi sadifu. Vilevile, huwezesha istilahi zilizokubaliwa na watumiaji wengi kuundwa na kusanifishwa ili zitumike kwa ulinganifu bila kuzibadilisha-badilisha kiumbo na/au kidhana. Pia, istilahi zenye usayansi zinapotumika kwa ulinganifu hurahisisha na huchapusha mawasiliano ya kitaaluma kwa vile washiriki wa mawasiliano, mathalani waandishi wa vitabu vya kitaaluma, wahadhiri, wanafunzi, na walimu, huwa na uelewa mmoja usiopingana (Felber, 1984:1-2).

Katika kuchunguza 'ufaafu' wa istilahi za isimu ya Kiswahili, tutakachosisitiza ni kanuni za istilahi na vigezo vya kisayansi vinavyotumiwa katika uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Uundaji wa istilahi katika lugha zinazoendelea sasa hufuata vigezo maalum vya kisayansi kama mwongozo thabiti katika ukuzaji wa lugha lengwa. Uchunguzi uliofanywa na Mwansoko (1989a, 1989b,

1990) umeonyesha kwamba vyombo vinavyohusika na ukuzaji wa Kiswahili nchini Tanzania, BAKITA, na TUKI, vimeweka na kuorodhesha misingi na kanuni za istilahi ambazo ni za kijumla mno, si toshelezi au timilifu na hazijachapishwa katika chapisho moja maalum. Tunakubaliana na mtaalam huyu kwamba baadhi ya kanuni za istilahi si kanuni hasa bali ni hatua zinazofuatwa katika uundaji wa istilahi za Kiswahili. Kwa mfano, katika kuendeleza istilahi za kisayansi na kiteknolojia, kwa muda mrefu BAKITA imekuwa ikifuata "misingi minne" iliyopendekezwa (taz. *Kakulu No. 3.* 1982:16). Nayo ni (kuunda istilahi kwa kutumia):

1. Kiswahili chenyewe
2. Lugha za Kibantu
3. Lugha nyingine za Afrika
4. Lugha za kigeni.

Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:22) wanadai kuwa:

> Misingi hii, kama inavyooonekana ni ya jumla mno na pengine inaweza kuwapotosha waundaji wa istilahi...

Kwa maoni yetu, hii si misingi wala kanuni za istilahi bali ni hatua au mpangilio unaofuatwa na wanaleksikografia katika kuendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili na kuteua lugha changizi mbalimbali kama inavyofanyika katika lugha nyingi ulimwenguni (taz. Sugito 1989:119).

Inafaa tusisitize hapa kwamba ingawa kitabu cha *Kiongozi cha Uundaji wa istilahi za Kiswahili* ni kazi muhimu inayowekea msingi rasmi harakati za kutokomeza vurugu na utata katika istilahi za Kiswahili, msingi ambao hatuna budi kujenga, waandishi wake hawakutafautisha kanuni za istilahi na kanuni/misingi ya uundaji

wa istilahi za Kiswahili. Kuna tofauti baina ya vigezo vya kisayansi vya ufaafu wa istilahi na misingi ya uundaji wa istilahi. Tumbo na Mwansoko (1992) katika *Kiongozi cha Uundaji wa istilahi za Kiswahili* wanaeleza zaidi misingi (ya jumla na misingi mahsusi) ya uundaji istilahi (Uk. 23-27) na, kwa namna hii, hawaweki wazi mipaka ya kanuni za istilahi na za mbinu za uendelezaji wa istilahi za Kiswahili.

Suala la kanuni za istilahi na vigezo vya kisayansi limewavutia wataalam kama vile Felber (1984), Picht na Draskau (1985), Mwansoko (1989a, 1989b, 1989c, 1990), Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992) na Kiingi (1989, 1997). Ili kuliweka wazi suala la usayansi katika istilahi za Kiswahili, tunaamini itakuwa vyema kujadili mitazamo mbalimbali ya wataalam hawa kuhusu misingi ya uundaji wa istilahi.

#### 3.3.2.1 Misingi ya Felber ya Istilahi

Felber (1984) anadokeza kwamba kanuni za istilahi na mbinu za uundaji wa istilahi ndio msingi wa umoja wa kazi ya istilahi. Kanuni anazozijadili ni za jumla na hazihusu uwanja wowote maalum. Kanuni za istilahi anazozifafanua ni pamoja na:

1. Uchambuzi wa dhana.
2. Kuibua maana za dhana.
3. Kuchunguza uhusiano wa dhana.
4 Ulinganishi wa dhana na mifumo yake.
5. Uundaji wa istilahi mpya zenye ukubalifu wa kimataifa.
6. Uteuzi wa maneno bora au elementi za maneno katika uundaji

wa istilahi.

Bila ya kufafanua, Felber (1984:114) anadokeza kwamba istilahi 'faafu' lazima ikidhi majaribio fulani. Hata hivyo anatutahadharisha kuwa tunapotumia kanuni za istilahi ni muhimu ikumbukwe kwamba kanuni hizo zinaweza kugongana. Kunapotokea mgogoro (ambapo istilahi sharti iwe na udhahiri na iktisadi), uamuzi ufanywe kuhusu kanuni gani ipewe umbele (Kiingi, 1997:6). Mtaalam huyu (Felber, 1984) alishughulikia vigezo vitatu (3) vya istilahi 'faafu.' Navyo ni **iktisadi, ukubalifu kimazoea** na **umataifa**. Kwa maoni ya Felber (1984) **iktisadi** katika lugha ndiyo kanuni ya kimsingi kwa sababu istilahi fupi hutamkwa na hueleweka kwa urahisi. Kadhalika, anasisitiza kwamba pasifanywe mageuzi yoyote bila sababu maalum katika istilahi ambazo zimekubalika na tayari zimepata mashiko, hoja ambayo haina uzito na hatuafikiani naye. Istilahi kupata mashiko, kama ilivyoelezwa mbeleni, si sababu tosha ya kuendelea kutumiwa. Ni muhimu vigezo vingine vya kisayansi vizingatiwe. Kwa mfano utusani. Istilahi ambazo zinabeba maana ya matusi, kulingana na adabu ya lugha ya jamii lengwa, hazina budi kufanyiwa mageuzi, kukataliwa, na istilahi zenye stara kuundwa (taz. 3.3.2.4, uk. 71).

Hata hivyo, tunakubaliana na Felber (1984:176) kwamba **umataifa** ni kigezo kimojawapo muhimu katika ufaafu wa istilahi. Umataifa katika istilahi utiliwe manani istilahi zinapoundwa na kusanifishwa kwa matumizi ya kimataifa. Panapotokea istilahi mbili au zaidi kuwakilisha dhana moja, uteuzi wa istilahi faafu uzingatie umbo la kimataifa (Abdulaziz, 1989:39). Ingawa suala la umataifa katika istilahi halijafanyiwa utafiti wa kutosha na

wanaleksikografia na watayarishaji wa Kamusi za Kiswahili, lugha zetu si mfumoumoja. Kila lugha ni mkusanyiko wa lugha nyingi; kila lugha ni mfumowingi. Kwa hivyo, utandaridhi au utandawazi wa istilahi, mbali na kurahisisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii-tumizi-lugha tofauti tofauti, pia hupunguza vizuizi vya kimawasiliano. Licha ya hilo, huimarisha ubadilishanaji wa maarifa na teknolojia na, kwa namna hii, kufunga mwanya uliopo kati ya mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea. Azma ya nchi yetu ya Kenya ya kuwa taifa la kiviwanda kufikia mwaka wa 2020 itafanikiwa kikamilifu na kutekelezwa barabara tu iwapo Kiswahili kitaendelezwa kiistilahi kwa kuzingatia kigezo cha umataifa wa istilahi (taz. Nedobity, 1989:170, kwa maelezo zaidi). Kanuni za'ufaafu'wa istilahi zilizopendekezwa na Felber (1984), ingawa hazijitoshelezi, si timilifu, na ni za jumla mno, zina ubora wake kwa sababu ziliweka msingi ambao uliendelea kujengwa na wataalam wa baadaye wa isimu ya Kiswahili.

### 3.3.2.2 Misingi ya Picht na Draskau ya Istilahi

Picht na Draskau (1985:114-6) walijadili misingi sita (6) ya "ufaafu" wa istilahi.

Misingi hiyo ni pamoja na:

1. Istilahi iweze kuwa dhahiri, yaani ilenge maana ya dhana inayowakilisha.
2. Istilahi ilandane na muundo wa kimatamshi na kisarufi wa lugha pokezi.
3 Uwezo wa istilahi kuzalisha maneno zaidi kwa mnyambuliko.
4. Ufupi wa istilahi.

5. Istilahi zisiwe na wingi wa visawe au homonimia.
6. Umbo litokane na mpangilio wa kimofolojia wa istilahi ambazo tayari zipo.

Misingi hiyo, kama ilivyo misingi iliyowekwa na Felber (1984) si toshelezi na ni ya kijumla mno katika kuchunguza ufaafu wa istilahi. Hata hivyo, kanuni hizi ni muhimu kwa ajili ya kupanua kikamilifu suala hili la usayansi katika istilahi.

### 3.3.2.3 Misingi ya Mwansoko ya Istilahi

Kwenye makala ya Mwansoko "The Principles, Methods and Procedures of Swahili Terminology Developed in Tanzania: A Re-examination of Basic issues" yaliyochapishwa kwenye *Journal of Asian and African Studies*, No 38, 1989 na makala mengineyo (taz. Mwansoko 1989b, 1989c, 1993, na 1996) ameeleza kuhusu uzingatiaji wa vigezo vya kisayansi vya ufaafu wa istilahi (kanuni za istilahi) katika uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Amesisitiza kwamba inapasa vyombo vya kukuza istilahi vya BAKITA, TUKI, na wanalugha binafsi kufuata kanuni za uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili.

Mwansoko (1989c:8) hakosei anaposema kuwa:

> ...kwa bahati mbaya, tathmini za awali za istilahi za Kiswahili (taz. K.M. Kiingi (1981), Mdee (1983), Mac William (1985) zimeonyesha kuwa istilahi nyingi za Kiswahili zilizoundwa hazikuzingatia vigezo vya 'ufaafu' wa istilahi. Kiingi (1981), kwa mfano, ameonyesha kwamba istilahi nyingi za Kiswahili hazizalishi maneno zaidi kwa mnyambuliko (taz. Picht na Draskau (1985) kanuni ya istilahi ya 3). Mdee (1983) na Macwilliam (1985), kwa upande mwingine, waligundua kuwa istilahi mkopo kutoka kwa

> Kiingereza hazikufuata mfumo maalum na uliosawa zinapoingizwa katika Kiswahili.

Bila kueleza ni kwa sababu gani, Mwansoko (1989c:9) anahimiza wataalam na chombo cha BAKITA kuzingatia vigezo vya ufaafu wa istilahi vya **udhahiri** na **uwiano wa kisarufi** ili istilahi zikubalike kimataifa na watumiaji wake.

Kadhalika, uchunguzi uliofanywa na Mwansoko (1989c, 1993) kuhusu 'ukubalifu' wa istilahi za fasihi na isimu nchini Tanzania ulionyesha kwamba istilahi ambazo hazikuzingatia vigezo na kanuni za istilahi zilikataliwa na watumiaji wa Kiswahili. Kwa mfano, istilahi mkopo **prediketa**==="*predicate*" ilikataliwa kwa sababu haizingatii kanuni ya ulandanaji na muundo wa kimatamshi na kisarufi wa lugha pokezi (Kiswahili). Aidha istilahi **prediketa** haitamkiki kwa urahisi. Istilahi zenye utata na zisizo dhahiri pia zilikataliwa.

Mtaalamu huyu anatutahadharisha kwamba si muhimu kuchunguza kigezo bora zaidi cha ufaafu wa istilahi, kwa sababu hakuna usifabia katika suala hilo (Mwansoko, 1993:187). Hata hivyo, kutokana na uchunguzi wake wa awali (taz. Mwansoko, 1989c; 1990; 1991) ameonyesha kwamba watumiaji wa Kiswahili walipendelea mpangilio wa kanuni za ufaafu wa istilahi zinazokubalika uwe kama ifuatavyo:

1. Kwamba istilahi ziwe na udhahiri.
2. Kwamba istilahi mpya ilandane na muundo wa kimatamshi na kisarufi wa lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo pokezi.
3. Kwamba istilahi itokane na utaratibu ulio sawa.
4. Kwamba istilahi iwe zalishi kwa mnyambuliko.

5. Kwamba ufupi wa istilahi utiliwe maanani.

Hata hivyo, matokeo ya uchunguzi huo (Mwansoko, 1989c:8; 1990) hayakuzama katika vigezo vingi vya usayansi na kanuni za istilahi 'faafu' zenye ukubalifu wa kimataifa. Vigezo vitano alivyovishughulikia havitoshi, na si timilifu katika kupimia kukidhi kwa istilahi.

### 3.3.2.4 Misingi ya Kiingi ya Istilahi

'Usayansi' katika istilahi, kama ilivyotajwa mbeleni, husaidia katika kuchagua istilahi faafu au bora zaidi kunapotokea ushindani wa visawe viwili, vitatu au zaidi vinavyowakilisha dhana moja. Kutokana na uchunguzi wa lugha ya Luganda, Kiingi (1989) anajadili kwa mapana na marefu vigezo tisa (9) vya 'ufaafu'wa istilahi. Vigezo hivyo vinavyojenga akronimu PEGITOSCA ni pamoja na:

1) **Udhahiri - R** p(xi) (taz. 6.1, uk. 318 kuhusu maana ya alama hii na nyinginezo) -kigezo muhimu zaidi cha ufaafu wa istilahi ni udhahiri. Istilahi lazima iwe isiyotatanisha mtumiaji wake. Istilahi 'bora' ni ile inayolenga maana ya dhana inayotumiwa kwa udhahiri bila utata. Katika **(1)**, **(2)** na **(3)**, dhana ya udhahiri imeepukwa. Kwa mfano,

**(1)**

*"salt"*===**chumvi**

Neno **chumvi** linaweza kuwa na utata kwa sababu **chumvi** ni za aina nyingi, kuna zulfati, kloridi, nitrati, fosfati n.k.. Tunaamini kuwa neno **munyu** ingawa linatokana na msamiati asilia wa

Kiswahili, ni dhahiri zaidi na linakubalika na watumiaji wa Kiswahili.

(2)

*"astronomy"*===**unajimu.**

**Unajimu** haiwezi kuwa *"astrology"* na *"astronomy"* kwa wakati mmoja.

(3)

*"term of endearment"*===**istilahi pendezi.**

(2) **Ikitisadi** - Re(xi) -Kigezo hiki kinamaanisha ufupishaji wa istilahi kikundi kwa kuviunga vipashio tenzi vya istilahi hiyo ili kupata istilahi fupi. Kila lugha hulenga ufupi wa matamshi na maneno. Istilahi ndefu mno haisaidii katika sifa hii. Kwa mfano:

(4)

"mwanawingilugha"===**mlumbi**

(5)

*"triangulation"*===**Mwimarishopembetatu**

(3) **Uzalishaji** - Rg(xi) -Istilahi faafu iweze kuzalisha maneno zaidi kwa mnyambuliko. Katika Kiswahili, mofimu '-isha' ni zalishi, inanyambulika na inaweza kutumiwa kuunda istilahi nyingi. Kwa mfano:

(6)

*"nominal"*===**nomino**

*"nominalize"*===**nominisha** au **jinisha**

*"nominalization"*===**unominishaji** au **ujinishaji**

Uzalishaji, kama ilivyo katika (6), ni hatua nzuri inayozingatia unyumbuaji wa leksia za Kiswahili.

(4) **Umataifa** - Ri(xi) -Kwa maana kwamba si lazima istilahi za isimu ya Kiswahili ziswahilishwe kutoka istilahi za Kiingereza zilizotokana na Kigiritini lakini zichukuliwe kama ishara zilizokubalika kimataifa, kama ilivyo katika (7):

(7)

*"xenon"*===**zenoni** (Xe)

*"hydrogen"*===**hidrojeni** (H)

Istilahi iliyo sawa na *"xenon"* na *"hydrogen"* inaweza kutokana na msamiati maalum asilia lakini ishara zinazowakilisha istilahi hizo ni za kimataifa na hazigeuki kamwe (taz. Wuster 1959).

(5) **Uangavu** - Rt(xi) -Kinachochunguzwa hapa ni uhusiano wa istilahi za isimu ya Kiswahili na maana. Istilahi iangaze maana. Uangavu wa istilahi hutegemea mtumiaji wake. Hata hivyo, Abdulaziz (1989:39) na Mwansoko (1996:20) wanakosea, kwa maoni yetu, wanaposisitiza kwamba viwango vya elimu vya walengwa wa istilahi lazima vizingatiwe na waundaji istilahi. Madai yao ni kuwa iwapo istilahi zinazoundwa ni kwa matumizi ya watu wenye elimu ya msingi au "kisomo chenye manufaa," waundaji istilahi wahakikishe kuwa istilahi hizo zinatokana na Kiswahili chenyewe au lugha za Kibantu ambazo zinafanana sana kimaumbile na Kiswahili. Kwa maoni ya Mwansoko (1990:116, 1996) wazungumzaji wa Kiswahili wenye 'kisomo chenye manufaa' watachukulia istilahi za kundi la (a) katika (8), (9), na (10) kuwa ni angavu ilhali wasomi watachukulia (b) katika (8), (9) na (10) kuwa ndiyo angavu zaidi.

(8a) **King'ong'o**

(8b) **Nasali**

(9a) **Kiingizi**

(9b) **Idiofoni**

(10a) **Dalili bainifu**

(10b) **Sifa bainishi**

(taz. Mdee, 1980:8, kwa maelezo zaidi juu ya kigezo cha uangavu wa istilahi). Waundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili inaelekea hawafuati utaratibu uliosawa wanapong'ang'ania uangavu wa kileksia. Hatuelewi sababu yoyote ya kiistilahi inayowafanya wanaleksikografia kutozingatia uangavu katika **(11)** ila tu katika (11a):

(11a) *"quantised"*===**iliyokwantishwa**

(11b) *"photolysis"*===**uvunjikajikimwanga**

*"hydrolysi"*===**majimvunjo**

*"dialysis"*===**dialisisi**

*"pyrolysis"*===**Pirolisisi**

(11c) *"analogy"*===**analojia**

*"anaphora"*===**mrejeosabiki**

*"anaphoric substitute"*===**umbo mrejeosabiki**

*"anaphoric word"*===**umbo mrejeosabiki**

(TUKI, 1990)

(6) **Utusani - R**o(xi) -Kwa maana kwamba istilahi iepuke maana ya matusi kulingana na adabu ya lugha ya jamii lengwa. Istilahi zenye stara zinafaa kuundwa. Istilahi 'chafu' kiutamaduni kama katika (12) haziwezi kukubalika kama istilahi 'faafu' za Kiswahili (taz. Kiingi, 1989:41).

(12)

*"penis"*===**mboo** (**kizalisha**/ume - kinachomshikisha mke mimba) (*oluwasiso* - Luganda

*"vagina"*===**kuma** *(emmana)* - Luganda)

*"anus"*===**mkundu**

(7) **Utaratibu maalum** - Rs(xi) -Istilahi iundwe kuambatana na utaratibu fulani wa kuunda. Istilahi zisiundwe kiholela na bila kufuata utaratibu dhahiri kama (13) inavyoonyesha:

(13)

*"phonemics"*===**fonimiki**

*"phonemic analysis"*===**uchanganuzi kifonimu**

*"phonemic notation"*===**mabano mkwaju**

*"phonemic transcription"*===**unukuzi mpana**

*"phonemic overlapping"*===**usawazishano**

Tatizo la "uholela" katika istilahi za Kiswahili limelalamikiwa na watumiaji istilahi wengi (taz. k.m. Mdee (1983), Mac William (1985), Dunn (1985:43), na Massamba (1989)). Tatizo hili linatokana na usawazishaji nusunusu wa istilahi sanifu uliokithiri katika Kiswahili, na unaosababishwa na usanifishaji wa istilahi moja moja kama zinavyopelekwa kwa BAKITA na waundaji wake (Sager na Johnson, 1978:83). Katika baadhi ya vitabu vya isimu ya Kiswahili, kumekuwa na matumizi ya istilahi zinazokiuka utaratibu wa kawaida unaotumika katika sarufi ya Kiswahili. Tunasema, kwa mfano, **kitenzi**, hatusemi **kitenzo**; tunasema **kielezi**, hatusemi **kielezo**; **kivumishi** bada ya **kivumisho**. Ni kutokana na utaratibu huu wa kuzalisha istilahi ndiposa Massamba, Kihore na Hokororo (1999:xiii-xiv) hawakosei katika madai yao kuwa matumizi

ya **changamano, ambatano, kitambazo,** si sahihi. Wanavyosema, maneno sahihi ni **changamani, ambatani,** na **kitambazi** kwa sababu yanazingatia utaratibu maalum katika sarufi ya Kiswahili.

Kama suluhisho la tatizo hili, Massamba (1989:69) anapendekeza kuwa:

> ...BAKITA litoe agizo rasmi kwa waundaji istilahi wote kupeleka istilahi zao BAKITA zikiwa tayari katika ufungamano wa kidhana. Istilahi zitakazoundwa moja moja au kiholela zinyimwe ithibati ya Baraza.

Maoni ya mtaalam huyu pamoja na ya Mwansoko (1990), ambaye ndiye mwenyekiti wa BAKITA wakati huu, yana mashiko, na endapo yatazingatiwa na Baraza hilo pamoja na Baraza la Kiswahili la Kenya, huenda yatapunguza 'uholela' katika istilahi za isimu ya Kiswahili.

(8) **Utaratibu uliosawa** - Rc(xi) -Ili kubuni istilahi kubalifu kimataifa miongoni mwa hadhira lengwa, kigezo hiki kinasisitiza istilahi kuwa nyofu na kuundwa kuambatana na utaratibu thabiti. Istilahi lazima ziwe na ulinganifu wa mtiririko unaokubalika, kama ilivyo katika **(14)**.

**(14)**

**tabakanje**

**tabakandani**

**tabakamzunguko**

**tabakakati** n.k. (TUKI 1990)

(9) **Ukubalifu na ufaafu** - Ra(xi) -Ukubalifu na ufaafu wa istilahi ndiyo azma ya mwisho ya mwanaleksikografia. Ukubalifu

na ufaafu wa istilahi huambatana na hadhi ya kitaifa au jamii tumizi lugha yenyewe. Kigezo cha ukubalifu na ufaafu kinaweza kugawanywa katika vigezo vitano vifuatavyo: (C, E, S, L, A);

(a) C: Mfumo wa kiutamaduni wa jamii husika.

(b) E: Mfumo wa ikolojia (viumbe katika mazingira maalum).

(c) S: Mfumo wa kijamii (uwezo/ngazi za kijamii huathiri istilahi (Kwa mfano, taz. asili ya maneno **ng'atuka**- "*ritire*", **kabwela, kabaila, katapeli, walalahoi, nyayo**).

(d) L: Mfumo wa kiisimu (masuala yanayokubalika kiisimu).

(e) A: Mfumo wa utendaji kimatamshi wa jumuia lugha pokezi.

Mifumo hii (C, E, S, L, A) huathiri istilahi na huchangia ukubalifu wake (Kiingi, 1997).

Kuhusu mpangilio wa vigezo na kanuni za istilahi kutokana na 'ubora' wa kila mojawapo, Kiingi (1989:33) anatoa hatua tatu kuwa:

(1) **Udhahiri** na **utaratibu maalum** ni vigezo muhimu zaidi na vinachukua nafasi ya kwanza.

(2) **Iktisadi** na **uzalishaji** ni vigezo muhimu vinavyochukua nafasi ya pili.

(3) Vigezo vyote vilivyosalia vinachukua nafasi ya tatu na ya mwisho: **umataifa**, **uangavu**, **utusani**, na **ukubalifu/ufaafu** (Linganisha na mpangilio wa Mwansoko wa kanuni na misingi za istilahi faafu (3.3.2.3, uk. 69).

Kulingana na Kiingi (1989) istilahi 'faafu'/ bora (xi) ni ile inayokidhi mahitaji ya PEGITOSCA, na sharti ipate alama kati ya asilimia 12 na asilimia 20 ($12 < \mathbb{R}(x) < 20$).

Misingi ya 'ufaafu' wa istilahi ya Kiingi (PEGITOSCA), ikilinganishwa na ya wataalam wa awali walioshughulikia suala hili, inadhihirisha wazi kwamba misingi ya awali inayotumiwa kuendeleza leksikoni za Kiswahili haikuwa timilifu.

Mathalani, kanuni za istilahi 'faafu' za Mwansoko (1989c) zilizingatia vigezo vitano (5) tu, yaani:

1. Rp(xi) - udhahiri
2. Rt(xi) - uangavu
3. Rc(xi) - utaratibu ulio sawa/ulinganifu wa mtiririko
4. Rg(xi) - uzalishaji kwa mnyambuliko
5. Re(xi) - ufupi wa istilahi

Mwansoko (1990), katika uchunguzi wake huo, hakuzama katika vigezo vya kisayansi vya istilahi faafu vya I,O,S. na A. Hakuzingatia kanuni muhimu sana kama:

1. Ri(xi) - umataifa (taz. Felber, 1984:176)
2. Ro(xi) - utusani
3. Rs(xi) - utaratibu maalum
4. Ra(xi) - ukubalifu na ufaafu

Wataalam wote walioshughulikia misingi na vigezo vya kisayansi vya istilahi faafu, wakiwemo Tumbo na Mwansoko (1992), Mdee (1985:39), wanaelekea kukubaliana kuhusu umuhumu wa vigezo vya: (P, E, G, T na S)

P - udhahiri

E - ufupi wa istilahi

G - uzalishji kwa mnyambuliko

T - uangavu na

S - utaratibu ulio sawa/ ulinganifu wa mtiririko.

Kwa kuwa Kiswahili ni lugha hai na inakua kiistilahi, aghalabu imedhihirika kwamba ipo haja ya kuimarisha misingi na vigezo vya kisayansi vya istilahi na uundaji wa istilahi faafu zenye ukubalifu wa kimataifa.

Uzingatiaji wa usayansi na kaida asisika za istilahi za isimu ya Kiswahili utasaidia katika kuchagua istilahi faafu zaidi kunapotokea ushindani miongoni mwa visawe vinavyotumika kuwakilisha dhana moja. Kwa namna hii, tatizo la utata na wingi wa visawe katika isimu ya Kiswahili litapunguzwa kama ilivyo katika (15).

(15a)

*"vowel harmanoy"*===**uwiano wa irabu/ vokali**

===**ulinganifu wa irabu**

===**upatanisho wa irabu**

===**tangamano irabu**

(15b)

*"phonological processes"*===**mifanyiko ya kifonolojia**

===**michakato ya Kifonolojia**

===**taratibu za kifonolojia**

(15c)

*"palate"*===**burutio**

===**kaakaa**

(15d)

*"minimal pairs"*===**jozi za mlingano finyu**

===**jozi za sauti**

===**jozi bainifu**

===**jozi za nitoe nikutoe**

Tathmini ya usayansi wa istilahi za isimu ya Kiswahili, kwa kuzingatia misingi na kanuni za istilahi, itadhihirisha 'ufaafu' wa istilahi na mbinu zinazotumika katika uendelezaji wa leksikoni za Kiswahili.

### 3.3.3 'Usayansi' katika Mbinu za Uundaji wa Istilahi za Kiswahili

Maana ya "usayansi katika mbinu" ni uwezo wa mbinu za uundaji istilahi za Kiswahili kufanyiwa uchunguzi, ili kutambua 'ufaafu' wa kila mojawapo, kwa kuzingatia misingi na kanuni za uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Mbinu ya kisayansi ni ile inayotumiwa katika kuunda istilahi 'faafu'/bora na zenye ukubalifu mkubwa wa kimataifa.

Zipo kazi chache ambazo zilishughulikia tathmini ya 'usayansi'au misingi ya kisayansi katika mbinu za uundaji wa istilahi za Kiswahili. Mdee (1980) amefanya tathmini ya ukubalifu wa istilahi za biashara na ofisi katika mji wa Same-Mkoani Kilimanjaro, nchini Tanzania. Uchunguzi wa Mdee (1980) ulionyesha kuwa mbinu ya kuendeleza Kiswahili kiistilahi mumo kwa mumo ndiyo inayounda istilahi zenye ukubalifu mkubwa kwa walengwa. Hata hivyo, uchunguzi wa mtaalam huyu haukuzama katika misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi za Kiswahili. Mwanalugha huyu alishughulikia mbinu nne (4) tu; yaani akronimu, unyambuaji, ukopaji kutoka lugha za Kiafrika, na utohoaji/ Uswahilishaji wa maneno ya kigeni.

Misingi ya uundaji wa istilahi ni suala ambalo limeshughulisha sana kalamu ya Mwansoko (1990:45) ambaye anasema kwamba:

> Uzingatiaji wa kimataifa wa kanuni za uundaji wa istilahi utasaidia wataalam katika nyanja za kiteknolojia kuunda istilahi zinazohitajika kwa utaratibu ulio sawa na bila uholela.... istilahi hizo zitakuwa na kiwango cha juu cha ukubalifu kimataifa na hivyo kuimarisha mawasiliano.

Ni ukweli usiopingika, na tunakubaliana na mtaalam huyu, kwamba misingi ya uundaji wa istilahi husaidia katika kupanua upeo wa 'ubora' wa istilahi zinazoundwa na wanaleksikografia wa Kiswahili. Ndiposa ni muhimu kufanya uchunguzi na kuweka wazi au kubainisha misingi ya uundaji wa istilahi za Kiswahili. Baadhi ya misingi itakayojadiliwa hapa imetajwa na Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992). Licha ya kwamba mchango wao ni mkubwa, kanuni hizo ni za jumla, zinakanganya na sio timilifu. Tutajaribu, katika sehemu hii ya tasnifu, kuziweka pamoja na kwa njia iliyo mufidi, bayana na toshelezi, na baadaye kutathmini 'usayansi' katika kila mojawapo ya mbinu za uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili (taz. 3.4, uk. 95).

Kadhalika, wataalam wa awali walioshughulikia misingi ya uundaji wa istilahi hawakutofautisha, kama tulivyotaja mbeleni, baina ya misingi hiyo na misingi ya istilahi faafu (taz Nedobity, 1989: 171). Ingawa misingi ya uundaji istilahi inaingiliana sana na misingi ya istilahi faafu, ni maoni yetu kuwa inapaswa kutofautishwa ili 'istilahi faafu'na 'mbinu mwafaka' za kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili zipate kutambulikana. Labda suala hili litaeleweka zaidi tukirejelea utafiti wa Mwansoko (1990), na Tumbo na Mwansoko (1992) uliokuwa mpana na wenye kina zaidi,

kabla ya utafiti huu, kuhusu misingi ya uundaji wa istilahi za Kiswahili.

Tatizo la ukosefu wa istilahi za kisayansi halikumbi lugha ya Kiswahili pekee bali ni tatizo la lugha nyingi ulimwenguni (Coulmas, 1989:19). Matatizo ya istilahi za kisayansi yalianza na uvumbuzi, usafiri na mawasiliano kati ya makundi ya watu. Matatizo hayo yaliongezeka wakati wa mapinduzi ya viwanda (Mac Williams, 1985:115).

Majaribio ya kuunda istilahi kinidhamu na kusanifu mfumo wa dhana katika kiwango cha kimataifa yalianzishwa mwaka wa 1931 na Wuster. Matokeo ya utafiti wake kuhusu misingi ya jumla ya uundaji wa istilahi yaliwezesha uchapishaji wa kitabu kilichojulikana kama *Die internationale Sprachnormung in der Technik"* (Usanifishaji wa Kimataifa wa Lugha katika Uhandisi) mwaka wa 1936. Uchunguzi huo ulishughulikia istilahi kama kifaa cha mawasiliano kinachohusu hali ya dhana, uhusiano wa dhana, sifa za dhana, uundaji wa istilahi, usanifishaji wa dhana na istilahi, umataifishaji wa dhana na istilahi n.k. (Felber, 1984: 32). Mwaka huo huo wa 1936 uendelezaji wa kimataifa wa usanifishaji istilahi ulianzishwa na kamati maalumu ya istilahi, "Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Usanifishaji vya Kitaifa" (ISA -International Federation of National Standardizing Associations). Kamati hii iliundwa ili kusanifu na kufafanua misingi ya uundaji wa istilahi ulimwenguni.

Baada ya vita vikuu vya pili (mwaka wa 1951) kamati ya kiufundi ya 37 ya Shirika la Viwango la Kimataifa (1SO), iliundwa badala ya Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Usanifishaji vya Kitaifa. Shughuli za shirika hili zilikuwa ni kuwasaidia wataalam wa nchi mbalimbali katika kuunda istilahi na kuwaonyesha mbinu za uundaji istilahi zilizoeleweka. Mbinu mojawapo iliyopendekezwa ni ukopaji pasi na kubadilisha umbo la neno asilia na uhifadhi wa shina la neno asilia.

Kamati ya kiufundi ya ISO imetayarisha kanuni, mbinu na misingi ya kuendeleza istilahi. Misingi hiyo ni ya jumla na haihusu taaluma yoyote maalum (Felber, 1980; 1984, Sager na Johnson, 1978). Misingi hiyo ya kisayansi, kama wanavyotufahamisha Tumbo na Mwansoko (1992:17-18), ni pamoja na:

1. Uundaji wa istilahi uanzie kwenye dhana na wala siyo istilahi.
2. Dhana hizo zielezwe kwa ukamilifu na wazi.
3. Uhusiano baina ya dhana ndio uwe msingi wa uundaji wa istilahi.
4. Istilahi mkopo zichukuliwe kama zilivyo katika umbo lake asilia kwa kufanya marekebisho machache tu kulingana na sarufi na matamshi ya lugha pokezi.
5. Pale ambapo istilahi asilia haiwezi kukopwa ama ambapo kuna istilahi ya kitaifa, istilahi asilia iandikwe kwenye mabano.
6. Uundaji wa istilahi kwa kutumia Kigiritini (Kigiriki na Kilatini) uendelezwe.
7. Istilahi ziwe fupi iwezekanavyo lakini zieleweke.
8. Sarufi ya lugha inayohusika lazima itiliwe maanani.

9. Istilahi ziwe na muundo unaoeleweka, yaani zifuate mofolojia ya kawaida ya lugha.

10. Uundaji wa istilahi kwa vifupisho na akronimu uepukwe hasa kama istilahi kamili si ndefu sana.

11. Kuunda istilahi kwa kupanua maana ya neno kuepukwe, hasa kama nyanja zinazotumia maneno hayo zinakaribiana ili kuepusha utatanishi.

12. Istilahi zisiwe na sinonimia au homonimia.

13. Istilahi ziundwe kwa njia ambayo itakuwa rahisi kuunda istilahi nyingine kwa mnyambuliko.

14. Istilahi zitolewe kufuatana na mfumo wa dhana; yaani, zianishwe kuliko kuandikwa kwa alfabeti.

15 Pale ambapo misingi inaelekea kugongana, uundaji ufanywe kuzingatia sarufi na matamshi ya lugha inayohusika.

Kuhusu umuhimu wa misingi hii, iliyotayarishwa na Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO), katika uendelezaji wa leksikoni zenye ukubalifu wa kimataifa, Tumbo na Mwansoko (1992:23-24) wanasema:

> Misingi hiyo... inatumiwa na mashirika na kamati nyingi za uundaji istilahi za kitaifa na kimataifa. Matumizi ya misingi ya uundaji istilahi iliyopendekezwa na ISO, ambayo yanahimizwa na umoja wa mataifa kupitia shirika lake la UNESCO, yatapelekea kwenye uzalishaji wa istilahi zinazoeleweka kwa urahisi na wanasayansi wengi, licha ya kutumia lugha zao tofauti za kitaifa, katika mawasiliano ya kitaaluma. Aidha, ubadilishanaji au ukopeshanaji wa istilahi baina ya lugha mbalimbali utarahisishwa....

Mwansoko (1992:23-24) anaendelea kudokeza kuwa:

> ...uendelezaji wa istilahi za Kiswahili ni vema vile vile itumike misingi ya uundaji istilahi ya ISO... baadhi ya misingi hii tayari imo kwenye machapisho na ripoti za semina na warsha mbalimbali za BAKITA na

> TUKI zinazohusu uendelezaji wa istilahi za Kiswahili.

Kutokana na dondoo hili, ni ukweli kwamba uzingatiaji wa misingi ya uundaji wa istilahi utarahisisha mawasiliano baina ya watumiaji wake na kuondoa vurugu na utata katika istilahi. Hata hivyo, Tumbo na Mwansoko hawakueleza udhaifu katika misingi iliyopendekezwa na ISO, ila tu hoja ya sita (6) ambayo anaitazama kama kwamba 'inaweza kusababisha mdahalo kwani inaelemea mno lugha za ulaya' (1992:21). Kadhalika, wataalamu hawa wanaelekea kujikanganya wanaposema kuwa:

> ...ni muhimu wanaistilahi waelewe kuwa misingi hii ya uundaji istilahi sio taratibu za 'kisheria' ambazo lazima zifumbatwe na kila istilahi itakayoundwa...

Bila ya kueleza ni kwa sababu gani, na bila hata uchunguzi wa kina kirefu, wasomi hawa (ibid, 1992:32) wanaendelea kudai kuwa:

> Uzoefu katika harakati za uundaji istilahi utaonyesha **kuwepo kwa istilahi chache ambazo zitakiuka taratibu zilizopendkezwa hapo juu.** (Msisitizo ni wetu).

Baada ya kutambua kwamba misingi iliyopendekezwa na ISO 'imetawanyika mno na si timilifu', Mwansoko (1990:164; 1996:21) alijaribu "kuiweka misingi hii pamoja na kwa mpangilio mzuri zaidi ili iweze kurejewa kwa urahisi na waundaji wa istilahi za Kiswahili".

Misingi hiyo mahususi ni pamoja na:

1. Istilahi yafaa ziakisi sifa bainifu za dhana zilizoziwakilisha (au angalu zidokeze hali hiyo) na ziwe angavu kwa watumiaji wanaolengwa. Msingi huu unamaanisha kuwa katika utayarishaji wa istilahi za Kiswahiii kipaumbele kitolewe kwenye muungo, mwambatano na unyambulishaji wa mizizi ya maneno ya Kiswahili. Aidha msingi huu unasisitiza utayarishaji wa istilahi kwa

kufuata viwango vya elimu na ujuzi wa watumiaji lengwa.

2. Endapo istilahi zitaundwa kwa kutumia mbinu ya uambatanishaji, basi mambo yafuatayo itabidi yazingatiwe:
   a) Idadi ya maneno yanayoambatanishwa yafaa yasizidi mawili (k.m. **sarufimiundovirai**).
   b) Visitari visitumiwe kutenga istilahi ambatani, kwani katika Kiswahili, istilahi za namna hii kwa kawaida hutamkwa kama neno moja, lenye mkazo mkuu kwenye silabi moja tu (k.m. **isimujamii** na wala siyo **isimu-jamii**).
   c) Istilahi za namna hii yafaa zisiwe na silabi zaidi ya nane, kwani kwa kawaida maneno ya Kiswahili yana wastani wa kati ya silabi moja na tano tu.
3. Istilahi sharti ziwe na uwezo mkubwa wa kunyambuliwa ili ziweze kuzalisha istilahi nyingine za kikoa au ukanda unaohusika. Hii itawezesha istilahi zinazowakilisha dhana zinazokaribiana kimaana au zinazotokana na shina moja kuonyesha kimantiki ukaribiano huo (k.m. **sharabu, sharabisha, usharabishaji**)
4. Istilahi (hasa zile zenye vivuli vya maana vinavyoingiliana) sharti ziwe na ulinganifu wa mtiririko unaokubalika.
5. Istilahi sharti ziwe dhahiri au toshelevu, yaani ziakisi vilivyo sifa za dhana zinazoziwakilisha.
6. Istilahi sharti ziwe fupi na zenye kueleweka. Istilahi ndefu hazifai kwani hazizingatii msingi wa iktisadi ya lugha. Kwa mfano, **sintaksia===sarufimiundo (muundomaneno)**

   **semantiki===sarufimaana (umbo-maana)**

   **mofolojia===sarufimaumbo** (taz. Massamba na wenzake,

1999).

7. Istilahi finyazo au mahuluti yafaa ziepukwe kwani etimolojia yake ina uvulivuli. Istilahi za namna hii huwa ngumu kukumbukwa na kutumiwa.
8. Uundaji wa istilahi kwa kutumia mbinu ya kupanua maana ya maneno yaliyopo yafaa uepukwe kwani istilahi za namna hii huwakanganya watumiaji wengi, hasa zinapotumika nje ya muktadha au kwenye taaluma zenye mahusiano ya karibu. Watumiaji wa istilahi za namna hii hutatizika katika kutofautisha vilivyo maana zake za kawaida na zile za kiistilahi zilizoongezewa na waundaji istilahi kwa kudhamiria.
9. Kila dhana yafaa iwakilishwe na istilahi moja tu. Mfumo wa visawe vya kiistilahi sharti uepukwe kwa sababu ni mzigo kwa ukumbuko na unawafanya watumiaji istilahi wadhani kuwa kuna dhana zaidi ya moja (taz. Braun, 1989:163 kwa maelezo zaidi).

Bila kuzingatia umuhimu wa kanuni hii ya 9, Mwansoko (1992:26) anadai kuwa:

> Hata hivyo, dhana moja inaweza kuwakilishwa na istilahi mbili, moja ya lugha enyeji (Kiswahili chenyewe) kwa mfano, **jina** kwa matumizi ya ndani ya nchi na kwa elimu ya msingi na ya kati; na ya pili, ya kimataifa, kwa mfano, **nomino**, kwa matumizi ya kimataifa na elimu ya juu. Utaratibu huu umependekezwa na ISO na unafuatwa katika lugha nyinginezo, kwa mfano, Kiyahudi (Fellman na Fishman 1977:91), Kirusi, Kijerumani, n.k.

Mtazamo wa Mwansoko (1989), na ambao ameutetea sana, kwamba istilahi zitayarishwe kwa kufuata viwango vya elimu na ujuzi wa watumiaji lengwa, kama ilivyotajwa mbeleni, hauna mashiko na hatukubaliani nao kwa sababu zifuatazo: Kwanza, ni msimamo

unaokiuka kanuni na msingi wa uundaji istilahi katika taaluma ya isimu unaosisitiza dhana moja-istilahi moja. Pili, ni msimamo uliojengeka katika taasubi ya kielimu inayowabagua na kuwatenga 'watu wa kisomo cha chini.' Ubaguzi wa viwango vya elimu katika uundaji istilahi utazidisha tatizo la vurugu, utata na wingi wa visawe na, kwa namna hii, kukwamisha juhudi za kimataifa za ulinganifu wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Istilahi faafu ni zile zinazoweza kutumiwa na watu wa aina zote, wasomi kwa wasiosoma; hivyo makundi mawili ya istilahi hayafai, hasa katika taaluma ya isimu ya Kiswahili (Besha, 1986:3).

Mbali na misingi iliyotajwa hapo juu, Mwansoko (1990) anajadili misingi ya uteuzi wa lugha changizi (chasili) ya istilahi. Mtaalamu huyu anapendekeza matumizi ya Kiingereza kama lugha chasili ya istilahi za Kiswahili, na anatoa sababu zifuatazo:

a) Kwanza kabisa, wengi wa watumiaji lengwa wa istilahi za Kiswahili walipata na/au wanaendelea kupata elimu yao kwa Kiingereza. Hivyo wanazipendelea istilahi zenye asili ya Kiingereza kwa sababu si ngeni kwao (Khamisi, 1980).
b) Pili, vitabu vingi zaidi vinavyotumika shuleni, vyuoni na Chuo Kikuu vimeandikwa kwa Kiingereza, ikiwa ni pamoja na kuwepo makamusi ya Kiingereza-Kiswahili ya kurejelewa.

Tofauti na Mwansoko anayetambua Kiingereza kama chanzo muhimu sana cha istilahi za Kiswahili, Abdulaziz (1989:3) anasema:

> Maelezo ya kiisimu ni kwamba kutokana na maingiliano kati ya Waswahili na Waarabu kwa karne nyingi, Kiarabu ni chasili cha Kiswahili kama ilivyo Kigiritini kwa lugha za ulaya. Ukopaji wa moja kwa moja kutoka Kiingereza aghalabu unaonekana kuwa si kawaida na hivyo haukubaliki.

Kutokana na kauli hii, Abdulaziz anaitambua lugha ya Kiarabu kuwa chanzo cha istilahi mkopo za Kiswahili na anatoa sababu kwamba ukopaji kutoka kwa Kiarabu hautambuliki kwa urahisi. Sisi hatuna sababu yoyote ya kuushuku msimamo wa Abdulaziz na Mwansoko. La muhimu na tunaloshikilia sisi ni kuwekwa misingi ya kisayansi madhubuti ya uingizaji istilahi mkopo kwenye Kiswahili pamoja na vigezo vya kutumia katika kuteua lugha chasili (Ehlich, 1989). Ili kupata usawazishaji mzuri na thabiti wa istilahi za mkopo, vyombo vya BAKIKE, BAKITA na TUKI havina budi kuandaa misingi mahususi ya kisayansi ya uundaji istilahi kutoka kila lugha kopeshaji. Kila lugha kopeshaji, iwe Kilatini, Kiarabu, Kigiriki, lugha za Kibantu, Kiingereza n.k., iwekewe misingi yake ya ukopeshaji. Kanuni za sasa ni za jumlajumla tu na matokeo yake ni ukopaji mwingi na usioridhisha wa istilahi. Vilevile, kuna ukosefu wa usawazishaji bora (kisarufi), kutotambua istilahi mkopo zitamkwe na ziandikwe vipi, na kutofahamu vigezo vipi vizingatiwe katika kuteua lugha chasili.

Uchunguzi katika misingi ya uundaji wa istilahi iliyopendekezwa na Tumbo na Mwansoko (1992) unadhihirisha madai yetu ya awali kwamba tofauti baina ya misingi ya istilahi faafu na misingi ya mbinu za uundaji istilahi hazikuwekwa wazi na wataalam walioshughulikia suala hili. Misingi tisa (9) inayotajwa katika

*Kiongozi cha Uundaji Istilahi za Kiswahili*, mbali na kwamba ni ya kijumlajumla, inakanganya na imeegemea sana katika misingi ya istilahi faafu. Mathalani, misingi ya 1. (uangavu), 3. (Uzalishaji), 4. (Ulinganifu wa mtiririko), 5. (Udhahiri), na 7. (Iktisadi) ni mojawapo ya vigezo na misingi inayounda akronimu ya PEGITOSCA (taz. 3.3.2.4, uk. 71) ya 'ufaafu' wa istilahi.

Misingi ya uundaji wa istilahi za Kiswahili katika *Kiongozi cha Uundaji Istilahi za Kiswahili* ni nambari 2, 7 na 8 pekee na inahusu mbinu mahsusi za uundaji wa istilahi. Yaani uambatanishaji, (2), akronimu au ufupishaji (7) na upanuaji maana ya maneno yaliyopo (8). Kwa hivyo, misingi ya uundaji istilahi ya ISO na ya Mwansoko (1990, 1992) haitoshelezi, si timilifu, na haitazami mbinu zote za uundaji wa istilahi za Kiswahili. Tunachojaribu kufanya hapa ni kuiweka misingi hii katika hali ya utimilifu (taz. Abdulaziz, 1972:158) na kwa mpangilio mzuri zaidi ili wanaleksikografia na watumiaji wa Kiswahili wasiendelee kukanganyika katika kutambua mbinu ya kisayansi ya uundaji istilahi za isimu ya Kiswahili. Misingi mahususi ya uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili ni kama ifuatayo:

(a) Uhusishaji wa dhana na kitajwa au na kazi yake ndio uwe msingi wa kwanza na muhimu zaidi wa uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili.

(b) Istilahi za isimu ya Kiswahili ziundwe kwa njia ambayo itakuwa rahisi kuunda istilahi nyingine kwa mnyambuliko.

(c) Upanuaji kimaana wa istilahi zenyewe za Kiswahili, na matumizi ya istilahi asilia pale ambapo hapana neno mwafaka,

uendelezwe. Kwa mfano:

(16a) *"x-ray"*===**uyoka** badala ya **eksirei**.

(16b) *"blood pressure"*===**buhari** badala ya **presha** au **mtuto wa damu** (TUKI 1990).

(16c) *"focus"*===**wiwendu** badala ya **fokasi** (Tol. 2:27).

(16d *"leave"*===**sono** badala ya **livu** au **mapumziko**.

(d) Istilahi za isimu ya Kiswahili ziundwe kwa njia ambayo itaendeleza utaratibu ulio sawa ama ulinganifu wa mtiririko na wala sio kiholela. Kwa mfano:

(17a) *"frequency"*===**kasimawimbi**.

(17b) *"frequency analysis"*===**uchanganuzi vipengere**.

(17c) *"frequency count"*===**uchanganuzi maneno kiidadi**.

(17d) *"fundamental frequency"*===**frikwensi msingi** (TUKI, 1990).

(e) Uundaji wa isitlahi za Kiswahili kwa kutumia lahaja za Kibantu uendelezwe. Kwa mfano:

(18a) *"television"*===**runinga** (televisheni).

(18b) *"radio"*===**bomba/mwengoya** (redio).

(18c) *"science"*===**ulimbe** (sayansi).

(18d) *"mathematics"*===**maenga** (hesabu) (taz. Mdee, 1986).

(f) Uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili kwa kutumia mbinu ya kupanua maana ya maneno yaliyopo yafaa uepukwe kwa sababu istilahi zinazoundwa kwa mfanyiko huu huwatatanisha watumiaji wengi katika kutofautisha maana zake mbalimbali, hasa kama nyanja zinazotumia maneno hayo zinakaribiana.

(g) Uuundaji wa istilahi mpya katika taaluma ya isimu, pale ambapo tayari kuna istilahi mwafaka iliyokubalika, inayowakilisha dhana husika sharti uepukwe. Kila dhana yafaa iwakilishwe na istilahi moja tu kwa vile visawe ni mzigo kwa

ukumbuko na unawafanya watumiaji istilahi kukanganyika kwa kudhani kuwa kuna dhana zaidi ya moja.

(h) Uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili kwa mbinu ya ufupishaji, yaani akroninu, uhulutishaji na ukatizaji yafaa uepukwe. Istilahi finyazo (au za mkato) huwa ngumu kukumbukwa na kutumiwa. Kadhalika, hakuna utaratibu maalum unaofuatwa wa kufanya finyazo.

(i) Uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili kwa kutumia mbinu ya uambatanishaji uendelezwe kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(i) Idadi ya istilahi ambatano yafaa isizidi mbili. Kwa mfano:

(19a) *"excretion"*===**utoajitakamwili** .

(19b) *"syncope"*===**udondoshajisautikati**.

(19c) *"apocope"*===**udondoshajisautitamati**.

(ii) Visitari visitumiwe kutenga istilahi ambatano kwa sababu katika Kiswahili, istilahi za namna hii kwa kawaida hutamkwa kama neno moja, lenye mkazo mkuu kwenye silabi moja tu. Mathalani:

(20a) *"epiglotis"*===**kidakatonge** (sio kidaka-tonge)

(20b) *"exhalation"*===**utoajihewa** (sio utoaji-hewa)

(20c) *"anaphora"*===**mrejeosabiki** (sio mrejeo-sabiki)

(20d) *"apposition"*===**mrejeosawa** (sio mrejeo-sawa)

(iii) Istilahi ambatano yafaa zisiwe na silabi zaidi ya nane (8). Maneno ya Kiswahili kwa kawaida yana wastani wa kati ya silabi moja na tano tu.

(j) Endapo istilahi za isimu ya Kiswahili zitaundwa kwa kutumia mbinu ya ukopaji, basi mambo yafuatayo yazingatiwe:

(i) Istilahi mkopo zichukuliwe kama zilivyo katika umbo lake

asilia. Marekebisho machache tu yafanywe kulingana na sarufi na matamshi ya lugha ya Kiswahili.

(ii) Istilahi mkopo katika Kiswahili ziandikwe kwa mtindo mmoja na wala siyo kwa njia mbili.

(iii) Viambishi vya kiistilahi vipatiwe visawe mahususi vya Kiswahili kwa kufuata utaratibu maalum na viandikwe kulingana na matamshi yake katika lugha chasili. Kwa mfano (taz. Kiingi, 1989:167),

| | **Kiambishi cha Kiingereza** | **Kisawe cha Kiswahili** |
|---|---|---|
| (21a) | '*-ics*' '*-logy*' (*Physics*) | **ia** (fizikia) |
| (21b) | '*-ist*' (*linguist*) | **m, mwana** (**mwanaisimu**) |
| (21c) | '*epi-*' (*epidermis*) | **nje ya** (ngozinje) |

(iv) Mpangilio wa istilahi zinazotoholewa kutoka lugha kopeshi ulingane na sarufi ya Kiswahili. Yaani vivumishi vifuate majina. Kwa mfano, 'sodium chloride' itoholwe kama:

**(22)**

**kloridi ya natiri** badala ya **'natiri kloridi'**

Uzingativu wa misingi hii ya kisayansi ya uundaji istilahi za isimu ya Kiswahili na BAKITA, BAKIKE, TUKI na watu binafsi utapunguza malalamiko juu ya udhaifu wa istilahi zinazoundwa. Vilevile, utaimarisha ukubalifu wa kimataifa wa istilahi kwa walengwa wake. Uundaji wa istilahi, kwa maoni ya Bwenge (1996:65), ni mchakato unaodai kuzingatiwa kwa misingi ya uundaji wa istilahi.

mfano wa Wasamia wanaoishi Kenya na aidha wale wanaoishi Uganda (Busia). Kutoka jamii hii ya Wasamia, kulichipuka vikundi-jamii vya Wasamia wa Uganda (W.U.) na Wasamia wa Kenya (W.K.). Wakati wa mgawo wa mipaka ya utawala na hata miezi au miaka michache baadaye, wakazi hawa hawakuwa na tofauti za kiistilahi. Waliongea lugha sawa sawa. W.U. walikuwa hawajaathiriwa sana na lugha pamoja na tamaduni za Kiganda. Lakini kadri wakati ulivyopita, ndivyo wakazi wa W.U. walivyochomoza na kudumisha tofauti za kilugha (kiistilahi) za kuwatofautisha na W.K. Isisitizwe hapa kwamba mabadiliko ya kiistilahi yalipotokea katika wakazi wa W.U., tofauti nyingine zilitokea hata miongoni mwa W.K. Kijiografia. Maeneo haya yaligeuka. Kiwakati na kimahitaji, wakazi wa maeneo hayo walibadilika. Kwa hivyo, hata istilahi zao zilibadilika. Wakazi wa eneo la W.U. walipounda **upekee lugha** (yaani upekelevu na kujitegemea kwa lugha kikamilifu katika mahitaji ya jamii-tumizi-lugha) mambo huku shinani walikotenganishwa kiutawala yalibadilika pia kutokana na mwachano wa wakati. Kwa usemi mwingine, kutokuwepo mfululizo wa kukutana kwa wanajamii hawa kulisababisha uundaji wa istilahi zilizohitajika kutokana na kutokuweko kwake katika lugha ambazo hapo mwanzo zilikuwa sawa. Kwa mfano:

| **Wasamia wa Uganda (W.U.)** | **Wasamia wa Kenya (W.K.)** |
|---|---|
| **epale** (suruali) | esuruali |
| **maido** (njugu) | enjugu |
| **esigiri** (jiko) | ejiko |
| **ebijanjaro** (maharagwe) | managanda/amaragwe |
| **masima** (uhakika) | obwadieri |
| **kalee** (sawa) | nibilayi |

3.4 Umuhimu wa Uundaji wa Istilahi za Kiswahili

### 3.4.1 Sababu za Uundaji wa Istilahi

Ili kazi hii ieleweke vyema na kuweza pia kuwapa mkabala mzuri wasomaji wetu, ni bora kueleza baadhi ya sababu za uundaji wa istilahi. Sababu za uundaji wa istilahi hazijulikani na hakuna maelezo dhahiri ya sababu za kuunda istilahi mpya. Hata hivyo, wanaisimu na wanaleksikografia wengi wanachukulia kwamba sababu za kuunda istilahi za taaluma yoyote ile zinaweza kugawanywa katika makundi yafuatayo:

1. sababu za kimaeneo (kijiografia).
2. sababu za kijamii na kiutamaduni.
3. sababu za kisiasa.
4. sababu za kihistoria na kisaikolojia.
5. sababu za kiisimu.

Hapa tutafafanua:

#### 3.4.1.1 Sababu za Kimaeneo za Uundaji wa Istilahi

Uundaji wa istilahi ni jambo lisiloweza kuepukika katika lugha yoyote ile. Sababu mojawapo muhimu ni ya kimaeneo. **Uhamaji** na **uhamiaji** husababisha uundaji wa istilahi mpya. Suala hili hutokea iwapo kuna vikwazo kama vile mto mkubwa, bahari, maadui baina ya kikundi kimoja na kingine, au iwapo vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti, haviwafikii watu wote katika pembe zote walizomo. Hata hivyo, suala la **wakati** pia ni muhimu. Wakati hubadilisha vitu vyote, na hakuna sababu yoyote ambayo inaweza kufanya istilahi iepukane na sheria hii ya ulimwengu. Tuchukue

Yafaa tusisitize hapa kuwa lugha inapoongewa katika eneo kubwa sana hubadilika kiistilahi, lakini mabadiliko yanayopatikana katika eneo moja yanaweza kuwa tofauti na yanayopatikana katika eneo lingine.

Wazungumzaji wa lugha ya Kisamia, kwa sababu ya kutokuwepo mfululizo wa kukutana ulioletwa na kuwepo kwa mto Sio na mgawo wa mipaka ya utawala, pametokea maeneo mawili ambapo lugha ya Kisamia inazungumzwa. Kwa mpito wa wakati, pakawa hakuna mawasiliano mengi baina ya watu wa makundi haya, wala hakuna mwingiliano baina yao; kilichofanyika ni kuwa lugha ya W.K. na ya W.U. ilibadilika kileksia katika sehemu yanapoishi makundi haya. Baada ya miaka kadhaa, wanajamii hao waliunda istilahi mpya ili kuleta kufahamiana na kuelewana, na wanaongea lugha iliyo tofauti. Kuna upungufu wa uelewano-lugha. Tazama pia na lugha za Kilatini na 'vilugha' vyake kama lugha ya Kiromania ya kisasa, lugha ya Kifaransa n.k.

**Kilatini**

Kifaransa Kiispania Kitaliano Kiromania

'Vilugha' hivi ni matokeo ya mabadiliko yaliyotokana na utengo wa kijiografia (Arlotto, 1972). Kilatini ndicho 'kizazi' cha lugha za Kiromania.

Ieleweke kuwa, kutokana na umbali wa kimaeneo, inawezekana wazungumzaji wa lugha/lahaja ya **Kimvita** wakafahamiana na wa **Kiamu**, na wazungumzaji wa **Kivumba** wakaelewana na wa **Chi-chifundi**,

lakini wazungumzaji wa **Chi-chifundi** wasielewane na wazungumzaji wa **Kimvita**. Kutoelewana huku, ambako kunasababishwa na utengo wa kimasafa, husababisha pia uundaji wa istilahi ili lugha husika ziweze kutosheleza haja za mawasiliano za walengwa wake (taz. Bakari, 1982; Maganga, 1990 kuhusu usawa katika lahaja za Kiswahili).

Binadamu, katika harakati zake za kutawala mazingira yake popote aishipo, amekuwa akibuni **dhana mpya** ambazo huhitaji kupewa istilahi za kuziwakilisha. Maendeleo ya haraka katika nyanja mbalimbali za maarifa ya binadamu ni sababu moja ambayo imemlazimu kuunda istilahi mpya au hata kubadilisha dhana zilizoko (Daswani 1989:81). Kuna idadi kubwa ya dhana mpya ambazo huzuka katika kila eneo anamoishi binadamu na ni lazima zielezwe kwa kutumia istilshi zilizoko au kuunda istilahi mpya.

### 3.4.1.2 Sababu za Kijamii na Kiutamaduni za Uundaji wa Istilahi

Sababu za kijamii na kiutamaduni huweza kusababisha uundaji wa istilahi. Uhai wa lugha huenda sambamba na wa jamii. Lugha huendelezwa kileksikoni kulingana na mabadiliko katika mahitaji ya jamii. Katika jamii huwa panatokea utengano wa kielimu, kiumri, kiuwana, kitabaka na kiutamaduni. Utengano wa namna hii huchangia katika uundaji wa istilahi mpya za lugha husika. Katika jamii, makundi ya watu yanaweza kusababisha uundaji wa istilahi. Kwa mfano, kundi la wasomi huunda na hubuni 'istilahi angavu' au 'istilahi zenye uvulivuli' zaidi zikilinganishwa na istilahi zinazopendelewa na watu wasio wasomi.

Kuhusu suala la utengo wa kielimu, Tumbo na Mwansoko (1992:43) wanadokeza kuwa:

> ...istilahi siyo msamiati maalum unaomhusu kila mtu, bali ni msamiati kwa ajili ya watumiaji maalum (wasomi kwa wasio wasomi) na katika mazingira maalum. Aidha, si lazima istilahi ileile ikidhi matakwa ya watumiaji wote, pasi na kujali tofauti za, mathalani, viwango vya elimu, mazingira yao na kadhalika.

Wataalamu hawa wanaongeza kudai kuwa:

> ... ili kuhakikisha zinaundwa istilahi 'bora' katika Kiswahili ni muhimu hadhira mahsusi za watumiaji istilahi ziainishwe na istilahi ziundwe kufuatana na viwango vya elimu vya watumiaji lengwa hao.

Kauli ya wataalamu hawa, licha ya kwamba ina udhaifu kama ilivyojadiliwa mbeleni (3.3.3), inadhihirisha kwamba utengano wa kielimu husababisha uundaji wa istilahi (taz. Tumbo na Mwansoko, 1992:26). Wasomi hujiundia istilahi mpya ili kueleza dhana ambazo tayari zina istilahi zenye kuziwakilisha kwa sababu ya **kutoridhika** na istilahi zilizopo na ambazo hazielekei kujali matakwa yao. Mfano mzuri ni wa wasomi kama Kapinga (1983), Mbaabu (1985), na Kiingi (1989). Kiingi (ibid:49) ameunda istilahi za Luganda baada ya kugundua kwamba hakuna ulinganifu wa mtiririko, uangavu na ustara katika istilahi za lugha ya Luganda. Kwa mfano,

**(23)**

(23a) "*AIDS*"===**Kanafuyabusibage** badala ya **siliimu** (UKIMWI)

(23b) "*penis*"===**Olúwasiso** badala ya **embolo**/mboro

(23c) "*vagina*"===**Olulaato** badala ya **emmana**/kuma

Nao Nkwera (1978), Kapinga (1983), na Mbaabu (1985) wameunda istilahi zao za isimu ya Kiswahili zifuatazo:

(24)

| | Kapinga | Mbaabu | Nkwera | TUKI |
|---|---|---|---|---|
| (24a) | vihusishi | vihusiano | viunganishi | vihusiano |
| (24b) | kiashiria | kiashirio | ishara | kiashiria |

(Sengo (1997) ameunda istilahi **"Lugha-wiyati"** kwa maana ya isimu taz. *JUA* Juzuu ya 2. No 1).

Kutokana na "kutoridhishwa" na istilahi za Kiswahili, na kwa kutaka pia kuonyesha bayana kuwa ukwasi wa lugha ya Kiswahili ni mpana sana, Nabhany (1982), amebuni istilahi kama vile:

**(25)**

| | **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| (25a) | *"energy"* | **ngosi** |
| (25b) | *"institute"* | **mwima** |
| (25c) | *"hormone"* | **chocheo** |
| (25d) | *"overtime"* | **koto** |

Suala la umri pia ni muhimu katika uundaji wa istilahi. Vijana, kwa kutaka kujitenga na wakubwa wao, wana istilahi na msamiati wao ambao nchini Kenya hujenga 'lugha' ya Kisheng. Vijana wamejiundia maneno kama mfano huu unavyodhihirisha:

**(26)**

| | | |
|---|---|---|
| (26a) | **Kobole** | (shilingi tano) |
| (26b) | **Mapero** | (wazazi) |
| (26c) | **Washitobe** | (wasichana) |

(Taz. Kamusi ya Sheng' 1993)

Matumizi ya maneno ya Sheng' yameathiri sana lugha ya Kiswahili. Tofauti na vijana, wazee ni wahafidhina na wanaelekea

'kutoridhika na istilahi za vijana.' Kundi la wazee hupendekeza kwamba Kiswahili ni lugha kamili na ikiwa haina msamiati maalum wa kutajia kifaa fulani, jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua katika lahaja zote za lugha hii. Aidha, wazee hupendelea kwamba maneno yenyewe ya lugha yapanuliwe (Besha, 1986). Kwa kutafuta na kubukua msamiati asilia katika lahaja za Kiswahili panaweza kupatikana istilahi za kuendeleza lugha hii. Kwa mfano, wazee wanapendelea matumizi ya msamiati asilia ufuataο:

| **Msamiati wa zamani** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **mafumo** | mikuki |
| **mwango** | sauti |
| **mswaji** | mke anayenyonyesha |
| **utayo** | sifa |

(taz. K. wa Mutiso, 1985:255)

Kwa hivyo, uundaji istilahi wa wazee una mwelekeo wa ukale katika matumizi ya lugha.

Jinsia ni suala muhimu pia katika uundaji wa istilahi. Wasichana hutofautiana na wavulana kisauti na kiistilahi. Katika jamii nyingi za Kiafrika, wanawake nafasi yao ni jikoni tu. Hivyo istilahi zao aghalabu zina mwelekeo wa maji, kuni, mtungi, sufuria na kulea watoto. Hii ni taasubi ya kiume ambayo ingali ina mizizi mirefu katika jamii zetu, mizizi ambayo jamii ya sasa inafanya kila juhudi kizing'oa katika kujenga jamii mpya yenye usawa na haki kwa kila mwanadamu. Utengano upo katika jamii zetu. Watu wa tabaka la juu, istilahi zao ni tofauti na za watu wachochole. Watu wenye uwezo wa kiuchumi na kisiasa huunda

istilahi ambazo hupata mashiko kwa haraka sana (taz. mfano, katika uk. 103-4)

Aidha, uundaji wa istilahi husababishwa na masuala ya kibinafsi. Hisia za kijamii zina mwelekeo wa kutotaka kutaja waziwazi sehemu za kizazi za binadamu. Katika jamii zingine watu, kwa uoga, huwa hawataji jina la Mungu moja kwa moja, ama matukio mabaya kama vile kufa. Ndiposa badala ya neno "kufa" kulitokea uundaji wa maneno (au tasfida) **aga dunia, kutupa mkono, kupotea, kupiga dunia teke, kuenda wasikorudi**, na kadhalika.

Miiko na utamaduni ni sababu nyingine inayoweza kusababisha uundaji wa istilahi. Kutokana na sababu kwamba jamii tofauti za watu zina utamaduni tofauti uliowalea, baadhi ya dhana zimekuzwa zaidi. Dhana ambazo zimekuzwa istilahi zao zimeimarishwa zaidi kwa kuundiwa nyingine mpya katika lugha husika kuliko dhana ambazo hazina umuhimu wa kiutamaduni, na kwa hivyo, msamiati wazo umepotea ama kufa.

Njia nyingine ya kuelezea kigezo cha miiko ni kwamba kunazo istilahi nyingine ambazo jamii hairuhusu zitumiwe hadharani kwa sababu labda hazina mbeko au hazizingatii adabu ya lugha. Mathalani, neno **"makende"** lina 'uchafu' kiutamaduni. Huenda likaepukwa na watumiaji wa Kiswahili, na mahali pake pakachukuliwa na neno lenye stara litakaloundwa na kukubaliwa na wanajamii au wazungumzaji wa Kiswahili.

### 3.4.1.3 Sababu za Kisiasa za Uundaji wa Istilahi

Katika kujadili sababu za kisiasa za uundaji wa istilahi, Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:15) wanadai kuwa:

> ...Sababu ya upanuzi wa matumizi ya lugha huambatana na sababu za kisiasa. Ili kujenga utaifa, hasa baada ya kutawaliwa na lugha ya watawala kutumika kwa mapana, nchi nyingi huona haja ya kuendeleza lugha zao wenyewe ili zitumike badala ya lugha hizo za watawala.

Kauli ya wataalam ina mashiko na tunakubaliana nao kwamba nchi nyingi zimesasaisha na kuendeleza lugha zao kiistilahi mumo kwa mumo kutokana na sababu za kisiasa (Abdulaziz,1989:43). Mifano ya nchi ambazo zimejishughulisha na uundaji wa istilahi ni Ufini na Uswidi katika Ulaya; Indonesia, Malaysia na India katika Bara Asia; Uyahudi katika Mashariki ya kati; China na Japani Mashariki ya Mbali; Tanzania, Kenya, Afrika Kusini, Madagascar na Somalia katika Afrika Mashariki na Kusini.

Kwa maelezo zaidi tusisitize hapa kwamba Uswidi ya kusini, kama historia inavyotueleza,ilikuwa sehemu ya Denmark hadi kufikia mwaka wa 1658, na lahaja zilizokuwa zikizungumzwa katika sehemu ya Scandinevia zilikuwa kama lahaja za Kidanishi. Lakini kwa sababu za kisiasa sehemu hii ikawa ya Uswidi na baada ya miaka arubaini (40) hizo lahaja za Kidanishi zikawa za Uswidi na hivyo basi pakatokea haja ya Uswidi kujiendeleza kileksia kwa kuunda istilahi mpya. Kadhalika, kwa sababu ya kutaka kujenga utaifa, (Mwansoko, 1990:70) istilahi asilia za Kihebrania zilifufuliwa na zingine mpya kuundwa kwa misingi ya lugha hiyo yenyewe (Rabin, 1989:27). Juhudi za kuunda na kusambaza istilahi za Kihebrania

zinafanywa na Akademia ya lugha za Hebrew (Aqademiyah la-lashon ha-ivrit) iliyobuniwa mwaka wa 1890 mjini Jerusalem. Njia nyingine ya kuendeleza suala la kisiasa ni kwamba wanasiasa wanaweza kuieneza, kuikuza ama kuidunisha lugha kiistilahi.

Temu (1983) anaita sababu za kisiasa kwamba ni "mabadiliko ya msamiati kufuatana na viongozi". Istilahi za Kiswahili, kwa maoni ya Temu (ibid) zinadunishwa na falsafa ya viongozi wanaoshikilia hatamu. Mathalani, kuna tofauti kati ya istilahi zilizotumika kuwataja au kuwaita viongozi wa kikoloni na wale viongozi wa baada ya ukoloni. Aghalabu istilahi huathiriwa na falsafa ya tabaka tawala. Katika kutilia uzito hoja hii, Temu anatukumbusha kwamba wakati wa ukoloni, tabaka tawala lilikuwa lenye madaha na lenye kupenda ubwana. Msamiati/istilahi zao ziliathiriwa na maringo hayo, kama ilivyo hapa;

(27)

(27a) *"Distict Commissioner"*===Bwana Shauri (Mkuu wa Wilaya)

(27b) *"Agricultural Officer"*===Bwana Shamba (Afisa wa Kilimo)

Maneno haya "Bwana Shauri," "Bwana Shamba," na mengine mengi kama vile 'boi' (mfanyikazi wa nyumbani), 'mnyapara' (mlinzi), ilibidi yaepukwe kutokana na maendeleo ya kisiasa. Maneno yasio ya 'ubwana' yaliundwa na kukubaliwa na watumiaji wa lugha hii ya Kiswahili.

Baadhi ya maneno ambayo yamechimbuka na/au kubadilika kimaana kutokana na siasa ni kama vile, **harambee**, **kandarasi**, **upinzani**, **programu**, **sekretariati** (ukatibu), **kinyangarika**, **magendo**, **ukupe**, **kung'uta**, **mgombea**, **ujamaa**, **bepari** (taz.Massamba, 1988:138).

Maneno kama haya yameundwa ama kugeuzwa maana yake asilia na wanasiasa "mashuhuri." Ni mifano ya maneno ambayo yamepata mashiko katika jamii za Afrika Mashariki kwa sababu ya uigaji unaofanywa na wafuasi wa viongozi fulani wa kisiasa (Mdee, 1995). Kuhusu kuigizwa na kutoigizwa kwa baadhi ya maneno haya na mengine mengi, kama vile **matatu** (Kenya), **unepaji**, **kikwamuzi**, **daladala** (Tanzania) katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu tazama Khamisi (1989:111), Habwe (1995:14), na Okombo (1995:73).

#### 3.4.1.4 Sababu za Kihistoria za Uundaji wa Istilahi

Sababu za kihistoria za uundaji wa istilahi ni suala linalohitaji kuelezwa kwa kuzingatia dhana ya ubunaji. Fikira ya kimsingi zaidi ya ubunaji ilitolewa na de Saussure (1916) katika ufafanuzi wake wa dhana ya lugha. Kwa maoni ya de Saussure, mwanaisimu lazima atambue kwamba kila lugha huvua istilahi tofauti tofauti katika tabaka la sauti zilizopo ndani ya *"langage."* Kutokana na sauti hizo, yeye huunda kwanza istilahi au nomino katika uhusiano wa kiupekee ambao kwa upande wake huunda kwanza *"parole"* kisha *"langue,"* na jinsi wakati unavyopita, dhana hizi mbili hudumu katika uhusiano wa kutegemeana (taz. Mwaro, 1993).

Katika kueleza dhana ya lugha, de Saussure alitumia dhana zifuatazo:

*Langage* – *Langue* / *Parole*

*Saikronia* / *Daikronia*

*"Langage"* - ni ghala la lugha zote ulimwenguni. Katika ghala hili ndipo kuna misingi na kanuni za mifumo ya lugha zote ulimwenguni. Katika *"langage"* tunapata *"langue"* na *"parole"* pamoja na sifabia za lugha za ulimwengu wote. Ieleweke kwamba kutokana na "langage" kila jamii-tumizi-lugha (langue) na kila mtu-binafsi (parole) hunyopoa vipande-sauti kulingana na uwezo, ujuzi wake na mahitaji yake mbalimbali. Unyopoaji au uchaguzi huo ndio husababisha uundaji wa istilahi mpya za lugha husika.

Mbali na jinsi nyingine za kutazamia lugha, de Saussure alibainisha kati ya lugha ikifikiriwa kama *"langue"* na kama *"parole."* *"Langue"* ni lugha dhahania, ni mfumo-lugha imara au lugha mahsusi na kanuni ya mawasiliano katika (au ya) jamii-tumizi-lugha fulani. Ni lugha iliyo 'mfumo imara' ambao hauwezi kubadilishwa 'vivi hivi tu,' na lazima pawe na makubaliano ya jamii nzima inayotumia lugha hiyo; mathalani, lugha ya Kiingereza, Kiswahili, Kifaransa na kadhalika. Tumuelewavyo Saussure ni kwamba mtu mmoja hawezi kuibadili *"langue,"* na vivyo hivyo, hafai kuiundia lugha istilahi pasi na ushirikiano wa wanajamii wa lugha lengwa.

*"Parole"* ni lugha-tumizi au lugha katika hali ya matumizi. Ni tabia au njia ya mtu-binafsi ya kutumia lugha (langue) kimaongezi au kimaandishi (taz. mchoro kwa maelezo zaidi).




Kutokana na madai ya de Saussure, *"parole"* ni kitu binafsi au halisi kinachotokea mtu anapozungumza ama kuandika kinyume na *"langue"* (mfumo-lugha) ambayo ni **mali ya jamii nzima**. *"Parole"* (lugha-matumizi) ni lugha inayomhusu **mtu-binafsi** (Mohamed, S.A. 1995:33). Ubainishi wa de Saussure una mwingiliano mkubwa na ubunaji unatokea katika kuunda istilahi za lugha yoyote ile.

Suala la sababu za kihistoria za uundaji wa istilahi linaweza pia kuhusishwa na mtazamo wa Chomsky (1965) katika dhana za "umilisi-lugha" na "utendaji." Kwa maoni ya Chomsky, mwanalugha ana uwezo-lugha (umaizi-lugha) ambao ndio msingi wa utendaji wa kiisimu. Tunakubaliana na Chomsky anapodokeza kwamba mwanalugha anao umilisi-lugha anaoutumia katika utendaji kubadilisha lugha kileksia na kuzalisha miundo isiyo na idadi kutokana na miundo yenye idadi maalum. Kwa mfano, kutokana na sauti thelathini katika Kiswahili, mwanalugha anaweza kuunda istilahi zisizo idadi, mpya mpya na, kwa namna hii, kuiendeleza kileksia.

Maelezo ya maulama hawa, Chomsky na de Saussure, kuhusu swala la ubunifu yana mashiko na tunakubaliana nayo. Jamii ina uwezo wa kutomruhusu mtumiaji lugha fulani kujitokeza na istilahi fulani alizozibuni. Hivyo, de Saussure hajakosea kwa kuihusisha lugha na *"langue"* (mfumo wa lugha imara wa jamii). Kadhalika Chomsky hakosei anapoihusisha lugha na *"parole"* (utendaji). Ubunifu wa istilahi, kutokana na maelezo ya de Saussure, unapatikana katika *"parole"*. Ubunifu ni uwezo wa kujitokeza na fikira za kiisimu zinazomwezesha mwanaleksikografia kuunda istilahi mpya ambayo haijawahi kutolewa hapo awali kutoka ujumla-lugha (Chomsky, 1965).

Kuhusu swala la ubunifu wa istilahi, Kitsao (1989:52) hakosei anaposema:

> Kuna pia na kupanua lugha kwa kuibunia maneno mapya. Hapa mwanalugha, wataalam... huunda maneno kufuatana na muundo (mofolojia) wa lugha hiyo na kuyapa maana inayohitajika ili kuziba pengo lililopo katika mawasiliano kwa lugha hiyo...

Tumetangulia kusema kwamba dhana za "daikronia" na "sinkronia" zilifafanuliwa na de Saussure na ni muhimu katika kujadili sababu za kihistoria za uundaji wa istilahi. "Sinkronia" ni kuangalia jinsi lugha ilivyo au ilivyokuwa katika kipindi maalum wakati fulani maalum. "Daikronia" ni kutazama mabadiliko ya lugha kihistoria katika viwango mbalimbali kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na kadhalika. Mathalani, tunaweza kutazama maendeleo ya lugha ya Kiswahili kutoka karne ya kumi na moja hadi karne ya ishirini na, kwa namna hiyo, tukagundua namna matukio ya kihistoria yalivyoathiri lugha kiistilahi. Tuseme kwa mfano, watu waendapo vitani hubadilisha

istilahi zao asilia kwa kutumia istilahi fiche kama vile **kupotea** badala ya **kufa**. Mfano wa maneno yanayotokana na sababu za kihistoria au maendeleo na mabadiliko ya mambo ni:

(28)

(28a) **mlanguzi** - maana asilia ni mfanyi biashara wa kati.
- kwa sasa ni mwuza bidhaa kwa bei ya haramu.

(28b) **magendo** - maana asilia ni mikono ya kaa ya mbele.
- kwa sasa linatumiwa kwa mtu anayefanya biashara isiyo halali.

(28c) **hamaki** - maana asilia ni ujinga.
- maana ya sasa ni hasira.

(28d) **bazazi** - maana asilia ni mfanya biashara.
- kwa sasa ni mtu mjinga.

(28e) **husudu** - maana asilia ni kuchukia.
- kwa sasa linatumika kwa maana ya kupenda.

(28f) **mtumba** - maana asilia ni furushi la nguo.
- kwa sasa ni kitu au mtu mzee asiyependeza.

(28g) **gari** - maana ya awali ni chombo chenye magurudumu cha kusukumwa kwa mikono.
- hivi leo, **gari** lina maana kadhaa: motokaa, gari-moshi, mkokoteni n.k. (Massamba, 1988:137).

La muhimu hapa ni kwamba binadamu kihistoria ni mbunifu, ndiposa huunda istilahi mpya katika kuendeleza na kukuza umilisi-lugha wake. Ndiposa pia Kapinga (1996:46) hakosei anapodai kwamba kila mmoja wetu aweza kubuni maneno fulani fulani ili kutoa maelezo yake, mradi tu maneno yanayobuniwa yawe yameundwa kulingana na sheria za lugha husika.

#### 3.4.1.5 Sababu za Kiisimu za Uundaji wa Istilahi

Sababu za kiisimu ni zile zinazotokana na muundo wa lugha. Kila lugha ina muundo wake. Muundo ni mfuatano wa maneno na uhusiano kati ya maneno (Khamisi, 1988:96). Sababu za kumbo hili la isimu zinaweza kugawanywa katika vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, na kisemantiki.

Kutokana na udhaifu wa binadamu, istilahi zilizo ngumu kutamkwa huepukwa, na hutokea haja ya kuunda istilahi mpya na zinazotamkika kwa urahisi. Watumiaji wa 'lugha zinazoendelea' huepuka matumizi ya sauti au istilahi ngumu, na hupendelea sauti au istilahi rahisi. Tunafahamu kuwa msamiati mwingi asilia wa Kiswahili umesahaulika (taz. Mwaro, 1993; Mutahi, 1988:145), na mwingine mpya kubuniwa kwa sababu ya 'ugumu' wa msamiati huo wa awali, kama ilivyo katika (29):

| | Istilahi Mpya | Kisanifu |
|---|---|---|
| (29a) | **vihisishi** | viingizi |
| (29b) | **kielezi** | advebo |
| (29c) | **kirai** | kikundi/kifungu |
| (29d) | **sarufimaumbo (umbo-neno)** | mofolojia. |

Kadhalika, istilahi zisizotamkwa kwa urahisi husababisha uundaji wa istilahi mpya ambazo si ndefu na zinazotamkika kwa urahisi. Kuhusu suala hili, Massamba (1988:142) anasema:

> ...ili kuweza kukidhi haja ya kuwepo kwa iktisadi ya maneno mwanadamu hujaribu kadri awezavyo kuyatumia maneno ya asili ya lugha yake kuwakilisha dhana mpya...

Madai ya Massamba (ibid) kwamba iktisadi ya istilahi ni muhimu katika uundaji wa istilahi ni madai yenye mtazamo mpana na

tunakubaliana naye. Istilahi ndefu zaidi huwa na silabi tisa (9) katika Kiswahili. Ni muhimu ifahamike, kwa manufaa ya kueleweka kwa kazi hii, kuwa sababu za kisiasa, kihistoria, kijamii, kiisimu pekee hazitoshi katika kueleza uundaji wa istilahi za lugha yoyote ile. Visababishi vingine ni vya **kimawasiliano** (Habwe, 1995:14). Uundaji wa istilahi hufanywa ili kukidhi haja za mawasiliano katika fani anuai za sanaa, sayansi za jamii, sayansi menyu, ufundi na utaalamu, elimu ya juu na shughuli zinazohusu serikali na teknolojia (Fishman, 1977; Opalka na Pasierbsky, 1977:74).

Uundaji wa istilahi mpya za Isimu ya Kiswahili ni muhimu sana kwa sababu utaiongezea lugha hii uhai kwa kuiwezesha kutumika kwa mapana na wanasayansi wengi. Juhudi zozote za kuendeleza jamii ya Kiswahili na lugha ya Kiswahili haziwezi kufaulu endapo lugha hii haitaundiwa istilahi za Kiswahili zenye ukubalifu wa kimataifa (Mutahi, 1988:145). Uundaji wa istilahi mpya, hususani za isimu ya Kiswahili, utaiwezesha lugha hii kupata usasa pamoja na kuweza kutafsiriwa na lugha nyinginezo katika kutekeleza haja za mawasiliano miongoni mwa jamii za kisasa (taz. Abdulaziz, 1989:42).

Kadhalika, uundaji wa istilahi mpya za isimu ya Kiswahili utaiwezesha lugha hii kujieleza kiteknolojia, kusambaza ujuzi wa kisayansi na kiteknolojia na kwa namna hii kutosheleza mawasiliano ya kimataifa. Kasi ya maendeleo ya istilahi za isimu ya Kiswahili ni ndogo mno ikilinganishwa na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Uchunguzi wa makini wa lugha nyingi za

ulimwengu kama vile Kijerumani, Kiingereża, Kihindi na nyingine nyingi ambazo zimekomaa na zinaelekea kutosheleza haja za mawasiliano ya kisasa katika taaluma za kisayansi na kiteknolojia, unaonyesha kuwa nazo pia zilikuwa hazijitoshelezi kiistilahi (Massamba, 1989:7). (Kuhusu maendeleo ya Kijerumani kiistilahi, taz. Coulmas (1989:183)). Baadhi ya istilahi mkopo zilizoingizwa katika Kiswahili ni pamwe na **video, chalaza, bomba, machela, safari,** na **shondo.** Ili isimu ya Kiswahili iweze kueleza lugha yote pamoja na matokeo ya lugha kama inavyodhihirika kimuktadha, na pengo la istilahi liweze kuzibwa, lugha hii haina budi kuendelezwa kileksikoni kwa kuzingatia hatua zifuatazo:

(1) Kupekuapekua miongoni mwa lahaja za Kiswahili istilahi 'faafu' asilia zilizosahaulika kutokana na usanifishaji na ambazo hazitumiki mara nyingi ingawa zipo.

(2) Pale ambapo istilahi 'faafu' na mwafaka kuhusu dhana za kisasa za kisayansi na kiteknolojia hazipatikani, basi tupekuepekue miongoni mwa lugha za Kibantu na kunyumbua mofimu za Kiswahili chenyewe.

(3) Uswahilishaji na uasilishaji (nativisation) wa istilahi za kigeni ufanywe (kama ilivyo katika Kichina (Pasierbsky, 1989:102)) ambapo dhana za kigeni zinakopwa lakini kabla ya dhana kuingizwa katika mfumo lugha, 'ugeni' wake unaondolewa na ku-Chinaishwa)

(4) Iwapo njia nyingine hazifaulu, ubunaji na uundaji wa istilahi mpya ufanywe kwa kuzingatia misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi 'faafu.' (Kuhusu taratibu za kuunda istilahi za kisayansi taz. pia Abdulaziz (1989:38) na Massamba (1996:91).

Ili hatua hii ya nne (4) ifaulu na ieleweke, ni muhimu kuchambua kwa mapana na marefu "usayansi" katika mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika kuendeleza Kiswahili na kuweza kujitokeza na ruwaza za kisayansi zinazozalisha istilahi zenye upeo mkubwa wa ukubalifu. Tathmini ya 'usayansi' katika mbinu za uundaji istilahi itatuwezesha kutambua mbinu muhimu sana katika uundaji wa istilahi za Kiswahili zinazohitajika katika mwanda wa sayansi, ufundi na teknolojia, mwanda ambao Besha (1972:30) na Mukwaya (1996:69) wanakosea kudai ni mgumu kuwasilishwa kwa Kiswahili.

Shughuli za kuunda istilahi za Kiswahili, hususani za isimu, zinapaswa kuendelezwa na wanalugha weledi wa istilahi pamoja na vyombo vya TUKI, BAKITA, na BAKIKE kwa sababu istilahi za lugha hii hazitoshi na ni chache sana (taz. Mwansoko, 1990:114). Kulingana na Irira (1990), takwimu za istilahi zinaonyesha kuwa kuna jumla ya istilahi 20,975. Istilahi hizo zinahusika na fani zifuatazo:

| **Fani** | **Idadi ya Istilahi** |
|---|---|
| Agronomia na ufugaji | 869 |
| Biashara na uchumi | 1005 |
| Biolojia | 1175 |
| Fasihi | 357 |
| Fizikia | 1226 |
| Hisabati | 737 |
| Historia | 198 |
| **Isimu** | **859** |
| Jiografia | 632 |
| Kemia | 1432 |

| | |
|---|---|
| Michezo | 162 |
| Saikatria | 285 |
| Saikolojia | 328 |
| Sayansi Kimu | 1990 |
| Siasa | 187 |
| Teknolojia | 7982 |
| Tiba | 187 |
| Uendeshaji na Uongozi | 1478 |
| Uhandisi Kilimo | 543 |
| Utafiti | 62 |
| **JUMLA**........................................ | 20,975 |

(taz. Irira, (1990) *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* wa BAKITA Uk. wa 19

Kutokana na orodha hii ya istilahi za Kiswahili, tatizo la 'uchache' wa kiistilahi ni mufidi na wazi. Istilahi mpya za isimu ya Kiswahili zinahitajika kuundwa kwa kuzingatia misingi ya kisayansi ili kukidhi mahitaji halisi katika:

(i) Ufundishaji masomo mbalimbali ya isimu ya Kiswahili.

(ii) Uandishi wa makala, majarida, magazeti na vitabu vya Kiswahili.

(iii) Tafsiri za matini ya fani mbalimbali.

(iv) Utangazaji kwa redio na runinga.

(v) Usambazaji wa ujuzi wa kisayansi na kiteknolojia na utoshelezaji wa mawasiliano ya kimataifa.

Mojawapo ya hatua inayopasa kuchukuliwa katika ukuzaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili ni kutathmini mbinu zinazotumiwa na TUKI, BAKITA, BAKIKE na wanalugha binafsi ili kuona kama zinazingatia 'usayansi' na kama zinaunda istilahi faafu na zenye

ukubalifu wa kimataifa. Ilinuiwa kwamba maelezo na ufafanuzi wa sababu mbalimbali za kuunda istilahi za Kiswahili ungeleta motisha na kudhihirisha kuwepo kwa haja ya kuchunguza mbinu za uundaji wa istilahi za Kiswahili.

### 3.5 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Katika sura hii, tumejadili misingi ya usayansi katika uundaji wa istilahi za Kiswahili. Tumeeleza maana ya 'istilahi,' 'usayansi' na misingi ya usayansi katika isimu ya Kiswahili. Tumesisitiza kwamba waandishi wa awali hawakutofautisha kanunu za 'ufaafu' wa istilahi na misingi ya uundaji wa istilahi. Kadhalika tumetathmini misingi ya kupimia 'ubora' wa istilahi iliyowekwa na wanalugha kama vile Felber (1984), Picht na Draskau (1985), Mwansoko (1989), na Kiingi (1989). Imebainika, kutokana na tathmini, kuwa misingi iliyoshughulikiwa haikuwa timilifu. Sababu za uundaji wa istilahi zimejadiliwa katika sura hii. Tunatarajia kuwa wapenzi wa Kiswahili huenda watafaidika katika kuelewa misingi ya kisayansi ya kupimia kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi bila shida kubwa.

# SURA YA NNE

## MBINU ZA UUNDAJI WA ISTILAHI ZA KISWAHILI

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumejadili sababu mbalimbali za uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Imefafanuliwa kwamba, istilahi makosa, japo zimepata mashiko, ziundiwe nyingine 'bora' ili lugha ya Kiswahili ijitosheleze, hususani, katika taaluma ya isimu. Pana haja ya lugha hii kuundiwa istilahi 'faafu.' Suala la mbinu za uundaji wa istilahi za Kiswahili ni muhimu sana na limewavutia wasomi na wataalamu mbalimbali kama Polome (1967), Ohly (1977), Temu (1972, 1984), Nabhany (1982), Gibbe (1983), Kapinga (1983), Mbaabu (1985), Mdee (1986), Mwansoko (1989, 1990, 1993) na Tumbo na Mwansoko (1992), miongoni mwa wengine. Maelezo yao ya mbinu za kuendeleza Kiswahili kama ilivyotajwa mbeleni, yameelekea kuwa ya 'kijumla' (taz. 1.1, uk. 3). Mtindo umekuwa ni kutaja mbinu zinazotumika katika lugha nyinginezo za kuunda istilahi, na kutoa mifano michache ya istilahi zilizotokana na kila mojawapo ya ruwaza zinazozalisha istilahi za Kiswahili.

Ni jambo la kustaajabisha kwamba hadi sasa inaelekea hakuna mbinu 'bora' zaidi na yenye usayansi ambayo imetambuliwa kuwa itumike katika kutunga istilahi za Kiswahili zenye ukubalifu wa kimataifa. Wanaleksikografia wa Kiswahili kufikia sasa hawana kitu cha kujivunia, manake ni vigumu dhana mpya katika Kiswahili kupewa majina au istilahi za kuziwakilisha bila ya kuzua tatizo la ukubalifu kutoka kwa wataalamu na walengwa wake. (Maelezo

zaidi kuhusu maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania kwa muda wa miaka thelathini (30) iliyopita tazama Mwansoko [1996]). Ni kutokana na tatizo hili ndipo azma yetu katika mada hii ikawa kutathmini mbinu zinazotumiwa kuunda istilahi ili kuona kama misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi inatumiwa. Kwanza tutashughulikia mbinu za uundaji istilahi zenye usifabia na zinazotumika pia katika lugha nyinginezo. Baadaye tutatathmini mbinu za BAKIKE, BAKITA, TUKI na za wataalamu binafsi za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili. Neno 'uundaji' linatumiwa hapa kwa maana ya uwezo wa lugha kukuza na kujenga istilahi zake katika mpangilio wake maalum. Pia, uundaji ni uzalishaji wa istilahi mpya kuwakilisha dhana fulani, pale ambapo hazikuwepo awali.

Mbinu za uundaji wa istilahi zitakazochunguzwa ni pamoja na unyambuaji, uambatanishaji, akronimu, uhuluti, ukatizaji, uradidi, ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo, ukopaji kutoka lahaja za Kiswahili na lugha nyingine, kaleki, utohoaji na uhusishaji wa dhana na kitajwa au kazi yake. Katika kujadili mbinu hizi za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, tutazingatia zaidi ruwaza zenye usayansi, zalishi na zinazounda istilahi 'faafu' za isimu ya Kiswahili na zenye ukubalifu wa kimataifa.

Ni muhimu isisitizwe hapa kwamba wataalamu wa awali walioshughulikia mbinu za uundaji wa istilahi (k.v. Ohly, 1981; Tumbo, 1982; Mwansoko, 1990; na Tumbo-Masabo na Mwansoko, 1992) waliziainisha mbinu hizo katika makundi mawili. Nazo ni njia zitokanazo na 'Kiswahili chenyewe' kama vile minyambuliko,

miambatano, miungano, uongezaji au upaji maana mpya kwa maneno yaliyopo, ufupisho au akronimu; na njia ya "kukopa" istilahi kutoka lahaja na lugha nyinginezo. Katika kazi hii uainishaji wa mifanyiko inayotumiwa katika uundaji wa istilahi ni tofauti na haujafungiwa katika makundi hayo mawili (ya 'Kiswahili chenyewe' na "ukopaji") kwa sababu ya kutaka uwanja huu wa istilahi ueleweke kwa mng'aro. Aidha, mtazamo na uelewa wetu wa uundaji wa istilahi kutokana na 'Kiswahili chenyewe' au mbinu za mumo kwa mumo ni tofauti (taz 3.4.2.3, uk. 69) kama itakavyodhihirika baadaye.

Kiango (1984:14), katika uchunguzi wake wa mbinu za kuunda istilahi za Kiswahili, anadai kwamba hakuna mbinu 'bora' inayopaswa kuzingatiwa katika kuendeleza leksikoni za lugha hii kwa sababu kila mojawapo ya mbinu hizo ina udhaifu. Kadhalika, mtaalam huyu hakutambua mbinu 'faafu' zaidi kuliko nyingine zote maanake zote zina mtagusano, zinachangiana na zinaingiliana, madai ambayo, kwa maoni yetu, hayana mashiko na hatukubaliani nayo.

Ni ukweli usiopingika kwamba kila mojawapo ya mbinu za kuendeleza istilahi za Kiswahili ina dosari na udhaifu (taz. Temu 1984, Mdee 1986). Hata hivyo, ni ukweli pia kwamba tathmini ya mbinu za uundaji istilahi za Kiswahili inaweza kuwasaidia wanaleksikografia kutambua na kuteua mbinu 'bora', ya kisayansi, zalishi na inayofaa kutumiwa katika kukuza istilahi zenye ukubalifu kwa walengwa wake.

Uchunguzi wa awali (taz. Mdee (1986), Yambi (1988:152), Mwansoko (1989:168), Tumbo-Masabo (1989), Kapinga (1996)) umeonyesha kuwa mbinu zalishi zaidi za kuzalisha istilahi za Kiswahili ni uambatanishaji, unyambuaji, upanuzi wa maana za maneno, na ukopaji. Endapo Temu (1972:1) hakosei anapodai kuwa:

> Maoni yangu ni kuwa Kiswahili kinaweza kuunda maneno yote yanayohitajika kueleza yote kinachotaka katika nyanja zote zikiwemo za kisayansi...

basi kinachohitajika, na ambacho wataalamu wa awali hawakuzingatia, ni kutathmini kila mojawapo ya mbinu za kuunda istilahi za Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, kuna uwezekano wa kujitokeza na njia ya kisayansi na mwafaka ya kujenga na kuendeleza istilahi za Kiswahili zenye ukubalifu wa kimataifa (taz. Abdulaziz, 1989:41).

Ili shughuli za uundaji wa istilahi zinazofanywa na taasisi na vyombo mbalimbali pamoja na watu binafsi zikamilike, tena kwa urahisi mno, hatuna budi hapa kupigia mbizi mbinu za uendelezaji istilahi za Kiswahili. Ushughulikiaji wa swala hili kwa mapana utatuwezesha pia kuona kama mbinu hizo zinazingatia 'usayansi' na mbinu ipi inayounda istilahi za isimu ya Kiswahili zinazokubalika na watumiaji wa Kiswahili.

### 4.1. Unyambuaji na Uambishaji

#### 4.1.1. Unyambuaji

Mbinu ya unyambuaji na uambishaji ni muhimu sana kama inavyodhihirishwa na wataalamu walioshughulikia suala la uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Wataalamu na wanaisimu

waliojadili mbinu ya unyambuaji, na wanaelekea kukubaliana kwamba ni njia zalishi katika Kiswahili, ni Polome (1967), Myachina (1981), Kapinga (1983, 1996:46), Mbaabu (1985), Mdee (1986), Abdulaziz (1989), Khamis (1989), Mwansoko (1989, 1990, 1996), Tumbo na Mwansoko (1992), na Bwenge (1996).

Wataalam hawa wote kwamba walitambua umuhimu wa mbinu ya unyambuaji na wanaafikiana kuwa istilahi za kitaaluma zinazoundwa kutokana na unyambuaji hueleweka kwa urahisi na walengwa wake. Hata hivyo, mtazamo wao, ijapokuwa Polome (1967), kuhusu dhana ya unyambuaji hauna mashiko. Tunasema hivi kwa sababu mbili muhimu: Kwanza, hawakufaulu kutofautisha baina ya unyambuaji na uambishaji. Pili, hawakuzingatia kwamba uambishaji hauwezi ukatupa neno au istilahi mpya. Wasomi hawa, ingawa wamewekea msingi suala hili, msingi ambao tunanuia kuujenga, hawatuonyeshi unyambuaji ni kuyaunda vipi maneno au iwapo ni kuyaunda upya maneno yale yale.

Kapinga (1983:26), katika sura iitwayo '**mnyambuliko**', anasema kwamba **mnyambuliko** ni neno linalotokana na nyambua. Kunyambua ni kurefusha kitu kama mpira. Mnyambuliko ni hali ile ya kulipa neno maana nyingine, kwa kuongezea viambishi fulani fulani. Baada ya kutambua udhaifu katika ufafanuzi huu, Kapinga (1996:47) anadokeza kuwa:

> **... mnyambuliko ni tendo la kuambatisha viambisho kwenye mzizi au mashina ya maneno ili kupata neno jingine lenye maana, lakini si kila mwambatisho wa viambisho ni mnyambuliko** ... izingatiwe kwamba viambisho-idadi vya ngeli, viambisho vya nyakati za tendo, viwakilishi-nafsi au viwakilishi virejeshi havifanyi mnyambuliko. Maneno

ambayo yanaweza kutoa maneno mapya kwa njia ya mnyambuliko ni ya aina ya majina, vivumishi, vielezi na vitendo. (Msisitizo ni wetu)

Mwansoko (1990:53) na Bwenge (1996:66) wanajeleza unyambuaji kwamba ni uundaji wa istilahi kwa kuambatisha viambishi kwenye mzizi au shina la neno. Kauli ya wataalam hawa, kama ilivyotajwa mbeleni, haina uzito kwa sababu ya kutofaulu kwao kutafautisha baina ya unyambuaji na uambishaji na kutozingatia kwao kwamba uambishaji hauwezi ukatupa neno jipya ila hutumiwa katika kujenga jina la kategoria ile ile.

Katika kazi hii, tumechukulia **unyambuaji** kuwa ni mbinu ya kuunda istilahi za Kiswahili ambapo viambisho vifuatilizi huongezwa kwenye mzizi wa neno fulani ili kujenga neno au istilahi mpya au yenye maana tofauti.

Unyambuaji, kama mbinu ya kuendeleza istilahi, umetumika katika lugha nyingi kote duniani. Katika Indonesia, kwa mfano, viambishi awali **"ke-"** na **"pe"** na kiambishi tamati **"-an"** hutumiwa mara kwa mara kuunda istilahi nyingi zinazowakilisha mawazo ya kidhahania kama vile umataifa, uananchi, mmenyo wa chakula, rutubisho, na kasimwelekeo n.k. Tazama kwa mfano:

ke-bangsa-an (bangsa - watu, mbari, taifa) - **utaifa**

pe-cerna-an (cerna - menya) - **mmenyo**

ke-cepat-an (cepat - kasi) - **kasimwelekeo**

(taz. Alisjahbana, 1976:73)

Mbinu ya unyambuaji pia ni zalishi katika Kirusi na Kipolishi, (Mwansoko, 1990:54) kama ilivyo katika lugha nyingi za Kiafrika,

hususani za Kibantu (Abdulaziz, 1989:41; Batibo, 1988:58). Njia hii ya uundaji istilahi hutumika sana katika Kiswahili. Karibu kila kitenzi au kivumishi kinaweza kunyambuliwa na kuambishwa na, kwa namna hii, kuunda istilahi mpya.

Khamisi (1989:113), katika uchunguzi wake wa unominishaji katika **Kamusi ya Kiswahili Sanifu** (KKS), alijitokeza na ruwaza zifuatazo za minyambuliko:

**(30)**

| | | |
|---|---|---|
| (i) | ku- | kucheza |
| | | kujibu |
| (ii) | x-ji | uchezaji |
| | | mbatizaji |
| (iii) | x-o | mchezo |
| | | andiko |
| | | ufunguo |
| | | mkwaruzano |
| (iv) | x-zi | ufunguzi |
| | | maamuzi |
| | | pongezi |
| (v) | x-shi | mapishi |
| | | upishi |
| (vi) | x- | masaza |
| | | mchinja |
| (vii) | x-i | mneni |
| | | msomi |
| (viii) | x-e | kihame |
| | | mtume |

(ix) - chapa

hesabu

hiari

(x) x- (vu) maumivu

(fu) uangalifu

(x = kiambishi awali mahususi).

Maumbo yote katika **(30)** yanawakilisha mifumo anuai ya kunominisha vitenzi viliyo na asili ya lugha za Kibantu.

Naye Tumbo-Masabo (1990), katika kuangalia istilahi za hisabati, aligundua ruwaza za minyambuliko zifuatazo;

**(31)**

1. a) ki + mzizi wa kitenzi/ kielezi + e: - kigawanye

kinyume

b) ki + mzizi wa kitenzi + i: kifuasi

kitambulishi

kitambazi

c) ki + mzizi wa kitenzi + o: kigawanyo

kichapuo

d) ki + shina la kitenzi: kifundo

kiunzi

kirai

2. ku + shina la kitenzi: kutenga

kugawanya

3. u + shina la kivumishi/ jina: ukubwa

utaratibu

utanzu

4. ma + mzizi wa kitenzi + o: maendeleo

makisio

5. m-/ mw- + mzizi wa kitenzi + o: mkokotoo

mwendo

6. u- + mzizi wa kitenzi + o: uwiano

uonyesho

7. - + mzizi wa kitenzi + o: kanusho

kadirio

8. ny- + shina la kitenzi: nyongeza

9. u- + mzizi wa kitenzi + aji: ugawanyaji

10. u- + mzizi wa kitenzi + i: uchambuzi

Polome (1967:77) alijitokeza na kauli kwamba:

> Katika Kiswahili majina huundwa kwa kutumia mizizi ya vitenzi pekee.

Kauli hii, kwa maoni yetu, inapotosha na ni finyu mno. Tunavyojua ni kwamba ingawa maneno na istilahi nyingi za Kiswahili huundwa kutokana na mizizi ya vitenzi kwa kutumia mofimu maalum pamoja na viambisho vitangulizi vya ngeli, kuna nomino kadhaa ambazo huundwa kutokana na misingi au mizizi ya vivumishi na majina mengine. Pamoja na vitenzi kuweza kugeuka kuwa nomino, kwa kutumia taratibu zinazojitokeza, maneno mengine kama vivumishi na nomino pia huweza kugeuka kuwa nomino kama mfano huu (32) unavyoonyesha:

(32)

| | **Kivumishi** | **Nomino** |
|---|---|---|
| (32a) | zuri | u-zuri |
| (32b) | tamu | u-tamu |
| (32c) | kaida | u-kaida |

| | | |
|---|---|---|
| (32d) | kavu | u-kavu |
| (32e) | kame | u-kame |
| (32f) | tata | u-tata |
| (32g) | moja | u-moja |
| (32h) | baya | u-baya |

Kiambishi awali u- **(32)** huweza kunominisha takribani vivumishi vyote ila tu katika baadhi ya maneno ya mkopo ambayo hayachukui kiambishi awali u- (taz. Mdee 1985:134 kwa maelezo zaidi). Kiambishi u- hudokeza hali (unyong'onyevu) au nchi (Urusi) au utaifa (Ukenya, Utanzania) au udogo (ujia) au jina la sifa (ukwasi, umahiri).

Istilahi nyingi katika herufi **u** zimetokana na uambishi wa u-dhahanishi kwenye nomino inayohusika. Kwa usemi mwingine, kategoria nyingine (mbali na kitenzi) huruhusu unominishaji, (kutoa neno au istilahi katika kategoria moja na kuliingiza katika kategoria ya nomino) ama uundaji wa istilahi mpya kama mfano ufuatao unavyodhihirisha:

**(33)**

| | **Nomino** | **Nomino** |
|---|---|---|
| (33a) | mtu | utu |
| (33b) | mbabe | ubabe |
| (33c) | mtendi | utendi |
| (33d) | mgeni | ugeni |
| (33e) | mneni | uneni |
| (33f) | amilifu | uamilifu |
| (33g) | buye | ubuye |
| (33h) | mjarabati | ujarabati. |

Lugha ya Kiswahili imefanikiwa pia kuunda istilahi nyingi za isimu kwa kutumia kiambishi awali **m+** mzizi wa kitenzi + kiambishi o au -i. Kwa mfano,

**(34)**

| | | |
|---|---|---|
| (34a) | -sigana | msigano |
| | -gusa | mgusano (wa lugha) |
| | -tetemeka | mtetemeko |
| | -suguana | msuguano (baina ya ala za sauti) |
| | -ungana | muungano (wa sauti) |
| | -lingana | mlingano/ mlinganuo |

| | | |
|---|---|---|
| (34b) | -andika | mwandishi |
| | -bainika | mbainishi |
| | -chambua | mchambuzi |

Kiambishi m- huweza kudokeza mtu (mkulima) au kitu (mkutano) au hali (mkao). Utumiaji wa viambishi vitangulizi na viambishi tamati ni muhimu sana katika uundaji wa istilahi za Kiswahili. Myachina (1981) anasema kwamba maneno yanayonyambulishwa kudokeza mtenda jambo huundwa kwa kuongeza viambishi vitangulizi vya ngeli ya 1 na 2 kama ilivyo katika mfano huu:

| | |
|---|---|
| [som] | msomi |
| [sem] | msemaji |
| [und] | mwundaji |
| | muunda |

Hata hivyo, hatukubaliani na Polome (1967) na Myachina (1981) kuhusu madai yao kwamba neno **mganga** limeundwa kwa kuongeza kiambishi cha ngeli [m-] na kiambishi kifuatilizi a- kwenye mzizi wa kitenzi [gang]. Vokali a- katika neno **mganga** inaonyesha hali

ya kitenzi. Mbaabu (1985:109) analifafanua suala hili anaposema;

> Vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kibantu huishia kwa irabu a. Kuunda nomino kutokana na vitenzi hivyo vyenye asili ya Kibantu kunawezekana kwa kutumia viishio ambavyo ni irabu zingine zote isipokuwa hiyo a ambayo ni kiishio cha vitenzi vyote vyenye asili ya Kibantu.

Anachofafanua Mbaabu hapa, na tunakubaliana naye, ni kwamba vokali a- haitumiwi kuunda nomino kutokana na vitenzi vyenye asili ya Kibantu.

Aidha, ruwaza nyingine inayoonyesha utajiri wa unyambuaji kama mbinu zalishi ya kuendeleza leksikoni za isimu ya Kiswahili ni matumizi ya kiambishi awali **ki+** mzizi wa kitenzi + kiambishi tamati **-i**, **-o** au **-a**. Mathalani;

(35)

| | | |
|---|---|---|
| (35a) | wakilisha | **kiwakilishi** |
| | vumisha | **kivumishi** |
| | tenda | **kitenzi** |
| | ambisha | **kiambishi** |
| | eleza | **kielezi** |
| (35b) | daka | **kidako** |
| | tenga | **kitengo** |
| | ziba | **kizibo** |
| | yeyusha | **kiyeyusho** |
| | nyambua | **kinyambuo** |
| (35c) | fuliza | **kifulizwa** |
| | kwamiza | **kikwamizwa** |
| | tenda | **kitendwa.** |

Istilahi za Kiswahili zinazoundwa kutokana na kiambisho

kitangulizi [Ki] aghalabu hudokeza kitu kinachotenda au kinachofanya jambo fulani (taz. S.A. Mohamed 1988:88 kuhusu Ki-ya Kiswahili). Vilevile, kiambishi hiki hudokeza au huashiria dhana ya msingi au kitu kama vile:

(i) **kiolwa** kwa mfano, kivuko, kiakisishi, kitumi, kibofu, kidonge.

(ii) **udogo** kwa mfano, kidubini, kijumba, kijitu, ini (kiini).

(iii) **uatilifu** kwa mfano, kichomi, kitambi, kisonono, kizunguzungu.

(taz. Mwongozo wa BAKITA wa Usanifishaji Istilahi 1990:13).

Kuhusu ruwaza ya kiambishi **ku-** [taz. mfano **(31)**.2] + shina la kitenzi, Khamisi (1989:117) anasema kwamba kiambishi **ku-** kina uwezo wa kubadili kitenzi cha aina yoyote na kukifanya nomino. Ruwaza hii ina uwezo usiokuwa na kikomo wa kuundia istilahi mpya za Kiswahili. Haijalishi kama kitenzi hicho ni cha silabi moja:

**(36)**

(36a) -wa **kuwa**

(36b) -fa **kufa**

(36c) -la **kula,**

au cha silabi zaidi ya moja

**(37)**

(37a) beba **kubeba**

(37b) penda **kupenda**

(37c) egemeza **kuegemeza**

(37d) eneza **kueneza**

(37e) changanua **kuchanganua.**

Kama kitenzi kimekopwa:

(38)

| | |
|---|---|
| (38a) nakili | **kunakili** |
| (38b) sajili | **kusajili** |
| (38c) bughudhi | **kubughudhi** |

au kimetokana na unyambuaji,

(39)

| | |
|---|---|
| (39a) jichana | **kujichana** |
| (39b) pigilia | **kupigilia** |
| (39c) fungulia | **kufungulia** |
| (39d) nyatia | **kunyatia** |
| (39e) shambulia | **kushambulia.** |

Unyambuaji shina kuunda istilahi huweza kutumia fomyula majumui kupata istilahi, jina, kitenzi au kivumishi. "Fomyula" hiyo, kwa mujibu wa *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* (1990:12) huwa kama ifuatavyo:

| Jina, au kitenzi au Kivumishi | Kiambishi awali (+ au 0) | + | shina (+) | + | Kiambishi tamati (+ au 0) | Istilahi |
|---|---|---|---|---|---|---|

Kwa mfano,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (i) | m- | tetem- | -o | **mtetemo** |
| (ii) | ki- | angat- | -wa | **kiangatwa** |
| (iii) | u- | hus- | -ianifu | **uhusianifu** |
| (iv) | m- | kem- | -ia | **kemia** |
| (v) | 0 | pitu | -a | **pitua** |
| (vi) | ki- | ene- | -zi | **kienezi** |
| (vii) | 0 | akisi- | -shi | **akisishi** |
| (viii) | ki- | kanz- | -i | **kikanzi** |
| (ix) | u- | hui- | -shaji | **uhuishaji** |

(x) u- atili- -fu **uatilifu**

Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kwamba utumiaji wa viambisho vifuatilizi [i], [ji], na [zi] ni muhimu katika kuendeleza istilahi za Kiswahili. Mofimu [i] kwa mfano, huunda istilahi za isimu ya Kiswahili zenye maana tofauti kutegemea kiambishi kitangulizi kinachotumiwa. Kiambishi tamati [i] kinapotumiwa pamoja na kiambishi cha ngeli ya 1. na 2. huonyesha mtendi wa tendo linalohusika, kama mfano huu wa **(40)** unavyoonyesha:

**(40)**

(40a) /m-som-i/ **msomi**

(40b) /m-sem-i/ **msemi**

(40c) /m-chum-i/ **mchumi**

(40d) /m-lew-i/ **mlevi**

(taz. Batibo 1988:59)

Utumiaji wa [i] pamoja na kiambishi cha ngeli ya 6 **(ma)** umezusha mjadala mrefu miongoni mwa wanalugha wa Kiswahili. Mdee (1986:79) anasema:

> Vitenzi vyenye kuchukua kiambishi tamati -i pamoja na viambishi awali **ma-** au **u-** hujenga majina yenye kudokeza hali ya tendo.

Naye Polome (1967) anadai kwamba baadhi ya nomino ambazo hutumia [i] pamoja na kiambishi cha ngeli **(ma)** huonyesha ile hali ya utimilifu wa tendo fulani. Mathalani:

/ma-zik-i/ **mazishi.**

/ma-pik-i/ **mapishi.**

Kiambishi tamati **zi** pia hutumiwa katika kuzalisha istilahi za isimu ya Kiswahili ingawa kumekuwa na tashwishi miongoni mwa wataalamu kuhusu matumizi yake. Myachina (1981) anadokeza kwamba

[zi] yaweza kuwa sura nyingine ya [ji] na hutumika pale ambapo mzizi wake unamalizikia kwa vokali.

Khamisi (1989:120) anaelekea kukubaliana na Myachina (ibid) kwamba kuna uhusiano wa usawa wa maana ambapo kinominishi **-zi** kinaingiza dhana ileile kama kinominishaji -ji kinavyofanya;

**mfagiaji===mfagizi.**

**utatuaji===utatuzi.**

Khamisi (ibid:121) anaendelea kudai kwamba kuna uhusiano wa kutoana ambapo kinominishi kimoja kinapoingiza dhana kingine hakiwezi kufanya hivyo. Mathalani:

**mlimaji** na wala siyo **mlimizi**

**ugubikaji** na wala siyo **ugubikazi**

**uhulutishaji** na wala sio **uhulutishazi**

**uchopekaji** na wala sio **uchopekazi**

**utendaji** na wala sio **utendazi**

Isitoshe, kuna uhusiano wa ubobezi na wa utobwe ambapo mofimu **-zi** inaingiza dhana ya kubobea katika jambo, na mofimu **-ji** inaingiza dhana ya kutenda jambo bila kuwa na mashiko au ubingwa au uzoefu nalo. Mfano:

**mlindaji** **mlinzi**

[tobwe] [bobezi]

(taz. pia Polome, 1967:88)

Inasisitizwa hapa kwamba kila lugha ina muundo wake wa silabi unaopendekezwa. Kiswahili hupendekeza muundo wa **KV KV** (Konsonanti ikifuatiwa na Vokali). Kwa hivyo, katika baadhi ya istilahi, /z/ huongezwa ili kuvunja mfululizo wa vokali. Kwa mfano:

nyoa ——— /ki-nyo-i/ ——— **kinyozi**

lea ——— /m-le-i/ ——— **mlezi**

Mofimu -zi mwishoni mwa nomino vile vile inatokana na athari ya /z/ ambayo hubadilisha konsonanti za mtuo na kuzifanya za mkwaruzo. Mfano,

d ——— z /-i mpenzi (siyo **mpendi**)

g ——— z /-i (jenga) /m-jeng-i/ **mjenzi**

b ——— z /-i (iba) /m-ib-i/ **mwizi**

Ruwaza nyingine ya unyambuaji, ambayo imetumiwa sana katika uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, ni ya kiambishi tamati -ji (Polome, 1967 anaiita ruwaza hii kuwa j na Batibo, 1988 anaiita kiambishi tamati cha -aji). Mofimu -ji ni maarufu sana na matumizi yake yamezagaa. Kwa mfano,

**(41)**

(41a) **uainishaji**

(41b) **uambishaji**

(41c) **unyambuaji**

(41d) **utatuaji**

(41e) **ufifiaji**

(taz. Khamisi (1987b) kwa malezo zaidi juu ya kitenzi -ji katika Kiswahili).

Ruwaza za istilahi mnyambuliko ni nyingi. Baadhi ya ruwaza ambazo hazikujadiliwa hapa zitashughulikiwa baadaye. La muhimu ni kwamba istilahi za isimu ya Kiswahili zinazoundwa kutokana na unyambuaji ni nyingi (Myachina, 1981:14). Ukubalifu na "usayansi" wa istilahi zitokanazo na unyambuaji kwa walengwa ni suala ambalo litashughulikiwa katika 5.2 (uk. 289). Istilahi za isimu ya

Kiswahili zinazoundwa kutokana na mbinu ya unyambuaji hueleweka kwa urahisi na walengwa na watumizi wa Kiswahili kwa sababu hunyambuliwa kutokana na mizizi ya Kiswahili chenyewe.

### 4.1.2 Uambishaji

Kama tulivyodokeza hapo awali, wanaisimu wengi walioshughulikia suala la mbinu za uundaji wa istilahi za Kiswahili hawakufua dafu katika kutofautisha dhana ya unyambuaji na uambishaji. Katika *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990:32) uambishaji unaelezwa kuwa ni:

> Utaratibu wa kuweka viambishi kwenye mzizi wa neno ilikulipa maana mahsusi.

Uambishaji ni aina ya uundaji wa istilahi ambapo **viambishi awali** huongezwa kwenye mzizi wa jina ili kuunda istilahi ya kategoria ile ile. Katika ufafanuzi huu, tunasisitiza matumizi ya viambishi awali vya ngeli kwa sababu, kinyume na unyambuaji, ni maoni yetu kwamba katika uambishaji ni viambishi awali tu ndivyo hutumika. Kwa mfano, kutokana na mzizi [**ti**] tunaweza kuunda majina yafuatayo:

**mti** (umoja)

**miti** (wingi)

**jiti**

**kiti**

**viti**

Kutokana na mzizi [**tu**] tunaweza kuunda majina yaletayo dhana ya udogo kama vile **kijitu**, **vijitu**, kwa kuongeza kiambisho [**ki**] katika umoja na [**vi**] katika wingi (Polome 1967:95).

Mbinu ya uambishaji, ingawa si zalishi, inatumika katika lugha nyingi, kwa mfano, Kichina (Pasierbsky, 1989) na Kirusi (Kadukov, 1979).

## 4.2 Uambatanishaji na Uunganishaji

Dhana ya uambatanishaji, katika isimu, ni telezi mno kama inavyodhihirishwa na kuwepo kwa visawe vifuatavyo vya Kiswahili vyenye kuirejelea:

(i) **maneno pacha**
(ii) **istilahi za upacha**
(iii) **vikundi jina**
(iv) **vikundi nomino**
(v) **maneno ungana** (Kiingi, 1982)
(iv) **mikarabu** (Gibbe, 1981)
(vii) **mwambatano wa maneno** (Kapinga, 1975, 1983, 1996)
(viii) **mikarabu** (Mdee, 1981; BAKITA, 1990)
(ix) **kuunganisha maneno** (Kakulu, No.3, 1982)
(x) **maneno ambatani/mwambatano**

Kuwepo kwa visawe vingi kwa dhana ya uambatanishaji kunawakanganya watumiaji wa Kiswahili (Mwansoko, 1990:99).

**Uambatanishaji** wa istilahi ni utaratibu ambao unahusu kuteuliwa na kuchukuliwa kwa maneno mawili (au zaidi) yenye maana na yaliyo huru na kuyaunganisha ili kuunda jina moja lenye dhana moja mpya. Aghalabu, muungano huu huwa katika msingi wa uhusiano bainishi (Marchand, 1969:11). Mathalani, katika mwambatano **mpigo kifua** '*chest pulse*' **mpigo <-pigo** ni kibainishi kinachoongoza

kibainishwa **kifua**. Tumbo na Mwansoko (1992:19) hawakosei kwa kudokeza kwamba:

> mfanyiko huu (mwambatano) hutokana na hulka ya binadamu ya kuona kuwa vitu vinafanana lakini vilevile kutofautiana. K.m. **viazi mviringo** kwa msingi ni **viazi** lakini havina umbo la viazi tulivyovizoea. Mara nyingine, mwambatano wa maneno hutumiwa ili kuelezea zaidi dhana kwa nia ya kuitofautisha na nyingine inayoshabihiana nayo...

Uambatanishaji ni mfanyiko ambao hutumika kwenye lugha nyingi ulimwenguni [k.v. Kiingereza (Bauer, 1983), Kiindonesia, Kirusi, Kichina na Kijerumani (Opalka na Pasierbsky, 1977)] kama mifano ifuatayo inavyodhihirisha:

**Kichina:** *hui yuan* (mwanajamii)

**Kirusi:** *jazykovederne* (isimu)

*zeleznaja doroga* (reli)

**Kiindonesia:** *buku sekolah* (kitabu cha shule)

*Orang bumi* (mwenyeji)

**Kijerumani:** *Schutzmann* (polisi);

*renaissancemensch* (mwanamapinduzi)

(taz. Opalka na Pasierbsky, 1977:78-85)

Hata hivyo, inaelekea waandishi wengi katika uwanja wa uundaji wa istilahi hawaafikiani kuhusu fasiri ya dhana ya uambatanishaji. Tumbo-Masabo (1989:45-46) anashikilia kwamba maneno ambatani hutokea tu "wakati maneno mawili au kundi la maneno linapounda istilahi, bila au na viunganishi, huku kila neno likiwa huru; k.m. **zao mtiririko kutokana na zao na mtiririko**". Hivyo mwanalugha huyu anamaanisha na kuchukulia uambatanishaji gotanisha (yaani usio na kiunganishi cha **-a**) unaoandikwa kama neno moja, uko nje ya mfanyiko wa uambatanishaji.

Tumbo-Masabo anaainisha uambatanishaji gotanisha katika kundi la **uunganishaji** (ambapo maneno mawili au zaidi huunganishwa ili kubuni istilahi moja). Uunganishaji au muungo ni utaratibu wa vipashio zaidi ya kimoja kuungana kujenga kipashio kimoja kikubwa zaidi. Mathalani **ushabihimiundo, kiinitete, msogeomwisho, mrejeosabiki, uirabuunganifu.** Naye Ohly (1977) anatambua maneno ambatani kwa misingi ya uhusiano ya kisintaksia wa maneno. Mtaalam huyu anachukulia viziada vya vitamkwa kama vile **pipa la moo ya mtoto** '*Heisswasserspeicher*', **kopo la maji ya mvua** '*Dachriane*' (Ohly, 1977:66) kwamba ni maneno ambatani, msimamo ambao, kwa maoni yetu, ni dhaifu na hauna mashiko.

Katika tasnifu hii, sisi hatutachukulia viziada vya vitamkwa kama miambatano na wala hatutatofautisha **uambatanishaji** na **uunganishaji.** Mifanyiko hii itachukuliwa kama visawe kwa sababu inaingiliana na kutegemeana. Kwa usemi mwingine, uambatanishaji na uunganishaji, kama miungano ya maneno au mofimu au maumbo unganifu, ili kupata neno au istilahi mpya kwa ajili ya dhana mpya, ni mifanyiko isiyofaa kutenganishwa.

Wanaisimu na wanalugha wengi (k.v. Myachina (1981), Tumbo (1982, 1989), Kiango (1984), Temu (1984), Mac William (1986), Mwansoko (1989, 1990, 1993, 1996), Goetschalckx (1989), Tumbo na Mwansoko (1992), na Bwenge (1996)) wanakubaliana kuwa mbinu ya uambatanishaji ni zalishi, huunda istilahi angavu na zinazoeleweka kwa urahisi na walengwa. Kabla ya kujadili umuhimu wa mbinu ya uambatanishaji katika uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili, inafaa kusisitizwa hapa kuwa maneno mawili au zaidi

huunganishwa kuwa neno moja na mkazo ambao hutokea kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa neno la pili. Ndiposa tunakubaliana na Polome (1967:81) anapodai kwamba silabi ya pili kutoka mwisho wa neno la kwanza hupata mkazo dhaifu sana. Kwa mfano, **mlariba** - kutokana na **la** + **riba** kwa kuongeza kiambisho cha ngeli ya 1 - (M). Neno **mlariba** lina zaidi ya mzizi mmoja; lakini hutumika kama neno moja, hivyo ni mwambatano.

Kuna sababu kadha wa kadha zinazofanya mbinu ya uambatanishaji kupendelewa kama mfanyiko mojawapo wa kuendeleza istilahi za Kiswahili. Kwanza kabisa, uambatanishaji huunda istilahi angavu, faafu na zinazokubalika kwa walengwa (taz. 6.2, uk. 355) kwa sababu aghalabu maana ya kiambatanishi huenda na maana ya sehemu zake. Pili, mbinu hii hurahisisha na huharakisha ubunaji wa istilahi kwa kutumia mizizi ya Kiswahili asilia (na/ au kuswahilisha mizizi ya mkopo). Chombo cha BAKITA kinapendekeza kwamba istilahi za Kiswahili ziundwe kutokana na Kiswahili chenyewe (KAKULU, No.3, 1982:15) (taz. 5.1.1.1.2, uk. 219).

Ruwaza za miambatano ni suala ambalo limeshughulikiwa kwa mapana na Ohly (1977), Temu (1984) na Mwansoko (1989, 1990, 1996). Kwa hivyo hapana sababu maalum za kutufanya tujadili kwa undani suala hili, ila tu tutasisitiza hapa ruwaza zinazoelekea kuwa zalishi katika Kiswahili. Ruwaza **mwana** + jina linalobainisha mtu na kazi yake, ni zalishi hasa katika kutaja dhana zinazohusiana na siasa, pamoja na kutaja taaluma mbalimbali kama mfano huu unavyodhihirisha:

**(42)**

(42a) mwanaisimumuundo.

(42b) mwanafilolojia.

(42c) mwanasarufi.

(42d) mwanaleksikografia.

(42e) mwanasemantiki.

(42f) mwanafonolojia.

(taz. Polome, 1967:81; Myachina, 1981:16-17)

Ruwaza ya **uambatanishaji kwa kugotanisha** pia imepata mashiko hivi majuzi na ni zalishi katika Kiswahili. Mfano wa uundaji wa istilahi kwa ruwaza hii ni:

**(43)**

(43a) **isimushule** isimu ya shule.

(43b) **sarufimaumbo** sarufi ya maumbo ya maneno.

(43c) **faridikifonolojia** faridi ya kifonolojia.

(43d) **isimujamii** isimu ya jamii.

(43e) **isimuushairi** isimu ya ushairi.

[taz. *Mulika No. 16*, (1984)]

Ruwaza nyingine inayotumika (ingawa kutokana na haja ya iktisadi matumizi yake yanafifia kwa sasa) katika kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili ni: **Nomino** + **Kiunganishi** + **Kibainishi** kinachoonyesha umilikaji au yambwa inayorejelea. Mathalani:

**(44)**

(44a) mkondo wa sauti.

(44b) istilahi za mkopo.

(44c) takriri ya sauti.

(44d) alama ya kiarudhi.

(44e) taaluma ya isimu.

(44f) kanuni za ufasiri.

(44g) mfumo wa lugha.

(44h) mazingira ya kifonetiki.

Aidha, ruwaza nyingine ya uundaji mikarabu ni ile inayohusisha **kiambishi awali cha jina** (Noun prefix) + **mzizi wa kitenzi unaoishia kwa -a** + **yambwa** au **kijalizo** kama ilivyo katika mfano ufuataao:

**(45)**

(45a) **kidakatonde** < daka + tonge

(45b) **kipasuandani** < pasua + ndani

(45c) **kilegezapumzi** < legeza + pumzi

(45d) **kibanapumzi** < bana + pumzi

(Kwa maelezo zaidi juu ya ruwaza zalishi za miambatano tazama Ohly (1977), Temu (1984) na Mwansoko (1990, 1996)).

Kwa ujumla maneno ambatani yaweza kuwa ni:

jina + jina - (elimuumbo/**mwanawiyati**) [taz. Nchimbi, (1997:5)],

jina + kitenzi - (nuktatulia/ sitiarifiche/ alasogezi),

jina + kiambishi - (**ulughai** [Sengo (1997)],

jina + kivumishi - (fundisanifu/ kiinitete),

kitenzi + kitenzi - yeyusha + ungano ( myeyungano),

Kitenzi + kiambishi - (chachisha/ unururishaji).

(taz. Temu, 1984; Abdulaziz, 1989:41; BAKITA 1990:12)

Mbinu ya uambatanishaji licha ya kwamba ni zalishi katika Kiswahili na huunda istilahi zenye ukubalifu kwa walengwa ina

matatizo anuai yanayopaswa kutatuliwa na wanalugha wa Kiswahili (Abdulaziz, 1989:37-8).

Mwansoko (1993:67) anataja matatizo matatu:

1. Idadi ya maneno yanayopaswa kuunganishwa na kuambatanishwa,
2. Tahajia - maneno ambatani yaandikwe kama neno moja (**kiangamitamati** *'enclitic'*) au kama maneno mawili tofauti (**kiangami tamati**), na
3. Urefu wa maneno ambatani.

   (Kama suluhisho la matatizo haya tazama misingi ya uundaji istilahi iliyopendekezwa katika kazi hii (3.3.1, uk. 60)).

Msimamo wa Mwansoko, na sisi tunakubaliana nao, ni kwamba maneno ambatani inafaa yasizidi mawili (k.v. **lugha ambishi tamati**) na istilahi ambatani zisiwe na silabi zaidi ya nane (**pembetatukisarufimaana** au **pembetatukisemantiki**) ili sifa muhimu ya iktisadi isikiukwe. Kadhalika, visitari visitumiwe kutenga istilahi ambatani (**kibinua-ulimi**) ambazo zinafaa kuandikwa, kama zinavyotamkwa, kama neno moja (taz. **4.2**, uk. 133). (Kuhusu kasoro na udhaifu wa mbinu ya uambatanishaji na uunganishaji ya kuunda istilahi za Kiswahili tazama **5.2.1.1**, uk. 298).

### 4.3 Ufupishaji

**Ufupishaji** au **vifupisho** ni matumizi ya sehemu za maneno katika kuunda istilahi. Hii ni mbinu mojawapo muhimu katika uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili kwa sababu huzingatia sifa ya iktisadi (taz. **4.3.1**, uk. 140) ya istilahi faafu. vilevile, hurahisisha utamkaji wa majina marefu na tatanishi ya mashirika,

taasisi na makampuni mbalimbali. Wataalam walioshughulikia mbinu ya ufupishaji ni Temu (1984), Mwansoko (1990), Tumbo na Mwansoko (1992), Bwenge (1996) na Kapinga (1996). Kuhusu suala hili, Kapinga (1996:53) anasema:

> Siku hizi ufupisho ni njia moja ya kutunga maneno. Watu huchukua herufi au silabi za mwanzoni, badala ya kuandika maneno kwa urefu. Silabi zote zinazopatikana kwa "njia hiyo huunda neno au jina jipya... Katika kamusi mna vifupisho kama vifuatavyo: **taz** - tazama, **k.v.** - kama vile..."

Mwanalugha huyu anatoa mifano katika vyama na mashirika, ya **TANU** - Tanganyika African National Union, **UDA** - Usafiri Dar es Salaam, **UMATI** - Uzazi wa Majira Tanzania kwamba ni maneno ya ufupisho. Ufafanuzi huu, pamoja na maelezo ya Bwenge (1996:66) kwamba ufupishaji ni "ufupishaji maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa **kuchukua herufi za mwanzo tu** za maneno hayo," kwa maoni yetu hauna mashiko kwa sababu hautofautishi baina ya akronimu, uhulutishaji na ukatizaji.

Ili utaratibu wa ufupishaji ueleweke barabara, hatuna budi kujadili aina tatu za ufupishaji. Nazo ni pamoja na:

(a) akronimu,

(b) uhulutishaji, na

(c) ukatizaji.

### 4.3.1 Akronimu

Wanalugha walioshughulikia dhana ya akronimu [k.v. Adams (1973), Temu (1984), Felber (1984), Mukwana (1988), Mwansoko (1990), Njeru (1990)] wanadokeza kwamba akronimu ni uundaji wa istilahi

kwa kuunganisha herufi au/na silabi za mwanzo za jina la kitu, au chombo kama asasi, taasisi, shirika, kampuni, idara, wizara, na kitengo.

Maelezo ya wataalam hawa yana upungufu. Mbali na kwamba hawakuweka wazi dhana za akronimu, uhuluti, na ukatizaji, maelezo yao juu ya msingi wa finyazo kuwa akronimu hayana uzito, na yanakanganya watumiaji wa Kiswahili. Adams (1973) anadai kwamba akronimu inahusisha maneno yanayotamkika k.m. *UNESCO*, pamoja na mfuatano wa herufi k.m. BBC. Naye Baker (1983:237) anashikilia kwamba "kila finyazo siyo akronimu: ili iwe akronimu neno jipya si lazima litamkwe kama mfuatano wa herufi lakini kama neno", madai ambayo yana mashiko na tunakubaliana nayo.

Irira (1990:7) katika *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* wa BAKITA anadokeza kuwa:

> Msingi mkubwa wa finyazo ni herufi au/na silabi za mwanzo za jina la kitu au asasi.

Mtaalam huyu anaendelea kututahadharisha kwamba:

> Kuchukua finyazo ya jina la Kiingereza na kuiweka finyazo yake hiyo na jina la Kiswahili ni upotoshaji wa dhamira na ukweli. Ni bora na sahihi kuambatisha finyazo ya Kiswahili na jina la Kiswahili au finyazo ya Kiingereza. Kuchanganya lugha mbili katika maandishi rasmi ni kudhalilisha lugha moja, hususani Kiswahili wakati kina uwezo wa kuwa na finyazo zake sahihi na hakika.

Ukweli kwamba lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kuwa na finyazo zake haupingiki. Hata hivyo, inafaa isisitizwe kwamba tatizo la finyazo litaweza kutatuliwa tu endapo wanalugha wa Kiswahili watajitokeza na kijelezi mwafaka cha akronimu.

Ufafanuzi wa akronimu unaozingatia herufi na/au silabi za mwanzo tu za jina la kitu au asasi una udhaifu. Udhaifu unatokana na wazo kuwa inawezekana akronimu ikatokana na kuunganisha zaidi ya herufi moja, za mwanzo wa neno moja au maneno zaidi katika kishazi kama ilivyo katika **msikwao** (**m**tu asiye na **kwao**).

Katika kazi hii, kwa hivyo, akronimu inachukuliwa kwamba ni aina ya ufupishaji ambapo jina, istilahi au **neno linatengenezwa na ufupisho wa maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa kuchukua silabi ya kwanza, silabi mbili za mwanzo, silabi tenzi za kati au hata neno zima.**

Kwa msingi huo mifano ya akronimu ni kama ifuatayo:

(46)

(46a) CHAKINA - **Cha**ma cha **Ki**swahili cha **Na**irobi.

CHAKA - **Cha**ma cha **K**iswahili cha **A**frika.

CHAKU - **Cha**ma cha **K**iswahili **U**ganda.

KASAILU - **KA**musi **SA**nifu ya **I**simu na **Lu**gha.

MKUI - **M**kutano wa **K**imataifa wa **U**sanifishaji wa **I**stilahi (za Kiswahili).

(46b) BBT au BEBITA - **B**enki ya **B**iashara ya **T**aifa.

WF au WIFE - **W**izara ya **F**edha.

WBV au WIBIVI - **W**izara ya **B**iashara na **V**iwanda.

BKK au BAKIKE - **Ba**raza la **Ki**swahili la **Ke**nya.

Inasisitizwa hapa kwamba katika uundaji wa maneno kwa mbinu ya akronimu, dhana mpya huwa hazibuniwi lakini ni ishara tu ambazo hufupishwa. Mfanyiko huu hutumika katika lugha nyingi ingawa ufaafu na uzalishi wake huwa ni tofauti kutoka lugha moja hadi

nyingine.

### 4.3.2 Uhulutishaji

Uhulutishaji ni mfanyiko wa kuendeleza istilahi ambapo **mofimu huru mbili au zaidi huchanganywa au huungwa ili kuunda neno** jipya ambalo hubeba kwa pamoja maana zote za mofimu huru husika. Polome (1967), Fromkin na Rodman (1974), na Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992), ni miongoni mwa wataalam walioshughulikia mfanyiko wa uhulutishaji.

Fromkin na Rodman (1974:39) wanadokeza kwamba uhulutishaji ni 'uambatanishaji' ambao ni 'mdogo kuliko' uambatanishaji. Maelezo haya yanatokana na mwingiliano na ukaribiano wa mbinu ya uhulutishaji na uambatanishaji (taz. 4.2, uk. 133). Naye Mwansoko (1990:56) anadai kwamba istilahi mahuluti huundwa kutokana na sehemu za maneno mawili (au zaidi), kwa hali ambapo hakuna uchambuzi angavu katika mofu.

Fromkin na Rodman (1974:39), Marchand (1969:451), Bauer (1983:234) wanatoa mifano ifuatayo ya istilahi mahuluti katika Kiingereza:

**(47)**

(47a) *smog* kutokana na ***smoke*** + *fog*

(47b) *motel* kutokana na ***motor*** + *hotel*

(47c) *ballute* kutokana na ***balloon*** + *parachute*

(47d) *chunnel* kutokana na ***channel*** + *tunnel*

(47e) *urinalysis* kutokana na ***urine*** + ***analysis***

Katika Kiswahili, istilahi mahuluti huungwaungwa kufuatana na mapenzi ya wale wanaoziunda (Tumbo na Mwansoko 1992:36). Mifano ya istilahi mahuluti ni kama hii ifuatayo:

**(48)**

(48a) **vitegauchumi** - kutokana na **tega** + **uchumi**

(48b) **mnyanyumbuko** - kutokana na **mnyambuko** + **mnyumbuko** (ambapo - **nya** ni 'pungua' na **nyu** ni 'zidi').

(48c) **deltao** - kutokana na **delta** kama **tao**

(48d) **siunganishi** - kutokana na **isiyo** na **viunganishi**

Polome (1967:82) anadai kwamba istilahi mahuluti huundwa inapounganishwa na '**mfanyi**'. Kuunganisha 'mfanyi' na vifaa aghalabu huonyesha kazi inayofanywa na wahusika kama mfano huu unavyodhihirisha;

**(49)**

(49a) **mfanyibiashara** - kutokana na **mfanyi** + **biashara**

(49b) **mfanyisaa** - kutokana na **mfanyi** + **saa**

(49c) **mfanyikazi** - kutokana na **mfanyi** + **kazi**

(taz. Mbaabu 1992:64. Kwa maelezo zaidi juu ya '**mfinyo**')

Kutokana na mifano hii ya uhulutishaji, ni dhahiri kwamba hakuna taratibu madhubuti zinazofuatwa za kuundia istilahi mahuluti. Ndiposa mfanyiko huu hautumiki sana katika uundaji wa istilahi za kiteknolojia katika lugha nyingi zinazoendelea, k.m. Kimalaysia (Omar 1978:238-239), Kiindonesia (Alisjahbana 1976), Kipoli (Cienkowski 1983) na Kiswahili (Mwansoko 1990:105-107).

Ili mfanyiko huu utumike sana katika uzalishaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, pana haja ya kufanyiwa uchunguzi zaidi na

kujitokeza na misingi na kanuni maalum za kuundia istilahi mahuluti faafu, zinazoeleweka na kukubalika kwa walengwa.

### 4.3.3 Ukatizaji

Katika *Kamusi ya Isimu na Lugha* (TUKI 1990:12) neno "ukatizaji" linafafanuliwa kuwa ni:

> Hatua ya kufupisha neno kwa kuondoa sehemu za mwanzoni na mwishoni.

Wataalam walioshughulikia mbinu ya ukatizaji ya uundaji istilahi za Kiswahili [k.v. Temu (1984), Njeru (1990), Irira (1990)] wanakubaliana kuwa ukatizaji ni aina ya ufupishaji, ambapo **neno hujengwa kimkato kwa kuondoa sehemu ya mwanzoni au mwishoni mwa neno hilo**, pasi na kubadilisha maana yake. Sisi hatuna sababu ya kutoafikiana na maoni ya wanalugha hawa.

Hata hivyo inafaa tusisitize hapa kwamba mfanyiko huu hutumika sana katika Kiswahili, na lugha nyinginezo, (Kiingereza taz. Felber 1984:178) kwa sababu hurahisisha matamshi na mawasiliano kwa jumla. Ni tabia ya binadamu kupenda majina mafupi sana (iktisadi) ili yatamkike kwa urahisi. Maneno katizi, kwa kawaida, huundwa kwa kuchukua herufi tatu, na pengine zaidi kama yana zaidi ya herufi nne huku sehemu fulani (hasa silabi ya kwanza) za neno asilia zikihifadhiwa. Mifano ni kama ifuatayo:

(50)

(50a) mof. = **mofimu**,

fon. = **fonimu**,

prag. = **pragmatiki**.

Pale ambapo maneno mawili au zaidi yanachangia herufi tatu au

zaidi za kwanza, inabidi lile muhimu na maarufu zaidi lipewe herufi tatu au zaidi za awali, na mengine yapewe tano au zaidi ili kutofautishwa (taz. Irira 1990:5). Mathalani:

(50b) mofol. = **mofolojia**

mofof. = **mofofonolojia**

fonol. = **fonolojia**

filol. = **filolojia**

Mfano huu unabainisha udhaifu wa maneno katizi wa kutofuata muundo wa Kiswahili wa Kv Kv. Maneno katizi yanaweza pia kuundwa kwa kuchukuliwa kwa herufi moja moja ya kila neno la kirai (kirai ni kipashio cha kimiundo chenye neno moja au zaidi lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima kiarifu (Massamba na Wenzake, 1999:80)) kama mifano ifuatayo inavyoonyesha:

(50c) k.n.y. = kwa niaba ya

m.y. = maana yake

i.k. = ipeleke kushughulikiwa

m.m. = mrejeshee mpelekaji

(kuhusu dosari na udhaifu wa mfanyiko wa ukatizaji katika kuundia istilahi za Kiswahili tazama **5.2.1.10**, uk. 309).

## 4.4 Uradidi

Uradidi ni mojawapo ya mifanyiko inayotumiwa katika uundaji wa istilahi za Kiswahili ambapo neno, jina, mofimu, silabi au mizani hurudiwarudiwa katika nomino. Wanalugha walioshughulikia dhana ya uradidi (.v Ashton, 1944; Polome, 1967; Kapinga, 1983; Mbaabu, 1992; Rubanza, 1996) wanaafikiana kwamba ni mfanyiko muhimu sana katika uundaji wa istilahi za Kiswahili. Ni mfanyiko unaoonyesha

kutendeka kwa mifanyiko au kitu au jambo mara kwa mara, yaani ile hali ya mazoea hudhihirika wazi.

Mbaabu (1992:65), katika sura iitwayo "uradidi," anadokeza kwamba uradidi au "uradufu" katika usemi ni jambo ambalo linajitokeza kwa wingi katika lugha za Kibantu. Naye Polome (1967:94) amejadili dhana ya uradidi kwa kuzingatia taratibu za kifonolojia. Tunakubaliana na mtaalam huyu kwamba uradidi ni tendo la kukariri sauti katika maneno na huathiri mzizi wa kitenzi (ni njia ya kurejelea mzizi wa neno).

Aina ya uradidi ni suala ambalo limefafanuliwa na Ashton (1944:316), Polome (1967:105) na Mbaabu (1992:66) kwa kina,na hapana sababu ya kutufanya sisi turadidi yaliyoelezwa na wataalam hawa. Hata hivyo,isisitizwe hapa kwamba kutendeka mara kadha kwa jambo moja husababisha haja ya msisitizo, na kurudiwa kwa mizani ya kwanza (ambazo katika baadhi ya istilahi huwa sawa na mizani ya pili). Kwa mfano:

(51)

(51a) tatanisha.

fufua.

chembechembe.

Mifano zaidi ya maneno ya uradidi ni kama hii:

(51b) nomino - pikipiki, tingatinga.

vitenzi - chambuachambua, tangatanga, nyanyasa, lialia.

vivumishi - sawasawa, ndefundefu, upesiupesi.

vielezi - fofofo, kochokocho.

viwakilishi - yayohayo.

vionyeshi - vivihivi, vivyohivyo, yaya kwa yaya.

(taz. Mbaabu, 1992:66).

Pia, ni muhimu kutaja kwamba kitenzi chochote chaweza kurudiwa ikiwa kitenzi hicho kimetanguliwa na mofimu /ku/ ya kuonyesha nia isiyotajwa. Kinachorudiwa huwa ni mzizi wa kitenzi pamoja na kishio chake (vokali /a/) kama mfano huu unavyodhihirisha:

(51c) kupikapika

kutangatanga

kuchambuachambua

kuonjaonja

(haya ni matendo yanayoendelea kufanyika kila mara)

Uradidi ni mfanyiko ambao si zalishi katika Kiswahili. Hata hivyo, utaratibu huu hutumika katika lugha nyingi ulimwenguni, k.v. Kiingereza (Bauer, 1983), Kirusi (Kodukov, 1979) na Kijerumani (Coulmas, 1989). (Maelezo kuhusu ufaafu na usayansi wa mfanyiko wa uradidi tazama **4.4**, uk. 146).

## 4.5 Upanuzi wa Maana za Maneno

Upanuzi wa maana za maneno ni mfanyiko mmojawapo muhimu wa kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, ambapo neno lililopo kwenye lugha hupewa maana zaidi ya maana yake ya awali. Mbinu hii ya kuongeza maana maalum za kiistilahi maneno ya kawaida ya Kiswahili imewavutia wataalam wengi [k.v. Falk Julia, 1973; Pei, 1967; Myachina, 1981; Massamba, 1988; Mwansoko, 1989, 1990), Tumbo na Mwansoko (1992), Bwenge (1996)]. Wanalugha hawa wanaelekea kukubaliana kwamba upanuzi wa maana za maneno ni mfanyiko zalishi katika Kiswahili.

Ni muhimu kusisitiza kwamba kuongeza maana au kuyapa maneno maana finyu kuliko ile ya awali haufanywi 'vivi hivi tu,' bali kwa kufuata mantiki ya uhusiano kati ya maana ya kawaida, au ya msingi na ile ya kiistilahi (Mwansoko, 1992:32). Myachina (1981:17) anadai kwamba mfanyiko huu unatumika katika kukuza istilahi za Kiswahili na anatoa mfano wa maneno kama vile **ndege, tawi, piga kura** na **mtego** ambayo maana yake asilia imebadilika kutokana na kuongezwa kwa maana na matumizi maalum ya kisasa.

**(52)**

**kiini** - maana asilia ni undani wa kitu; kwa sasa neno hili linatumika kwa maana sawa na **mzizi**.

Mfanyiko wa upanuzi wa maana za maneno ni zalishi siyo tu katika Kiswahili bali pia katika Kiingereza (Falk Julia, 1973), Kisomali (Andrzejewski, 1983) na Kirusi (Kodukov, 1979). Mifano ya maneno ya Kiingereza yaliyoongezwa maana maalum ni:

*lust* (uchu) - maana asilia ni furaha na utashi ilhali maana ya sasa ni uzinifu.

*rent* - maana asilia ni mapato, ambapo sasa maana ya neno hili imepunguzwa na ni 'mapato yatolewayo na wapangaji wa nyumba.'

*garbage* - maana asilia ni mabaki ya chakula. Hivi sasa linatumika kurejelea kitu kisicho na faida, au takataka.

(taz. Pei, 1967 kwa maelezo zaidi).

**Kisomali:**

*magas* - maana asilia ni kitajwa *(name)* na maana ya sasa ni nomino *(noun)* (Anderzejewski, 1983).

**Kirusi:**

*Plenit* - kufanya mtu awe mfungwa (maana asilia).

- pendeza, mvuto - maana iliyopanuliwa ya sasa. (Kodukov, 1979:219).

**Kigiriki:**

*Presbuterus* - mtu mzee (maana asilia).

- mhuburi/padri - maana ya kisasa. (Massamba, 1988:120).

Istilahi zinazoundwa kwa mfanyiko wa upanuzi wa maana za maneno mara nyingi huwa si angavu na hutatanisha walengwa, kwa sababu ni vigumu kutofautisha maana mahsusi ya neno kutoka kwa maana zake za kawaida (pia taz. 4.5, uk. 148 kwa maelezo zaidi).

## 4.6 Ufufuaji na Ujenzi wa Mumo kwa Mumo wa Istilahi

"Ufufuaji" ni kurudisha katika matumizi msamiati au istilahi ambazo hazikufikiriwa katika Kiswahili sanifu. Msamiati kiasili au wa zamani huwa upo, lakini hautumiki katika maandishi ya kila siku. Msamiati asili unapatikana katika kamusi za zamani za Kiswahili, lahaja na kazi za kale za fasihi ya Kiswahili kama vile **Utenzi wa Tambuka** (1928) ulioandikwa na Bwana Mwengo, **Utenzi wa Hamziyah** (1649) au (1650), **Utenzi wa Mwana Kupona**, **Al-Inkishafi** (1810-1820) na katika mashairi ya Muyaka, kazi za Fumo Liyongo, M.H. Mbega na A.N.J. Bhalo.

Ufufuaji wa msamiati ni mfanyiko ambao haujapewa uzito na wataalam wa Kiswahili walioshughulikia uendelezaji wa istilahi za lugha hii. Ieleweke tangu mwanzo kwamba ufufuaji wa istilahi

ni sifa mojawapo ya lugha. Kuunda kwa maneno mengine 'yanayofaa' zaidi badala ya yaliyokuweko kabla kumesababisha 'kufa' kwa maneno asili ya Kiswahili. Hata hivyo, pana haja ya kufufua msamiati wa zamani wa Kiswahili ili kuweza kuendeleza leksikoni ya lugha hii (taz. Mwaro, 1993; 1999).

Mfanyiko wa ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo wa msamiati wa Kiswahili umewavutia na kushughulikiwa na wataalam wengi (k.v Besha, 1972; Nkwera, 1978; Nabhany, 1978; 1982; ), Baruwa, 1979; Mbega, 1979; Ruo, 1979). Msimamo wa wanalugha hawa, (na wanaelekea kuungwa mkono na Sengo T.S.Y. wa Chuo Kikuu cha Uislamu nchini Uganda, na Akida, H. kama walivyotuarifu), ni kwamba kuijenga lugha ndani ya lugha ndiko kuikuza lugha.

Ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo wa istilahi ni mbinu ambayo hutumika katika lugha nyingi duniani [k.v. Kihebrania (Rabin, 1989), Kichina (Pasierbsky, 1989), Kijapani (Takada, 1989; Sugito 1989) na Kijerumani (Coulmas, 1989; Ehlich, 1989) kwa sababu ya umuhimu wake:

Kwanza, msamiati asili wa Kiswahili unaodhaniwa 'ulikufa' ukifufuliwa utaweza kutumiwa pale ambapo hapana neno mwafaka. Kwa mfano, dhana ya 'brother' ina pengo. Kuna **dada** na **kaka**. **Dada** ni **ndugu mkubwa wa kike**. **Kaka** katika muktadha huu ni moja tu **ndugu mkubwa wa kiume**. Pengo la kimsamiati katika dhana ya *'brother'* linaweza kuzibwa kwa kufufua msamiati asili wa Kiswahili na kuupanua kimaana.

Pili, ufufuaji wa msamiati asili ambao ulisahaulika katika Kiswahili sanifu utasaidia katika kuijenga lugha hii katika misingi ya Kiafrika na wala si ya kigeni. Ndiposa Besha (1972:23) hakosei anapodai kuwa:

> Si lazima lugha ichukue maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya la kueleza. Maneno yenyewe ya lugha yanaweza kupanuliwa.

Nkwera (1978) anadokeza kuwa ili juhudi za uundaji wa istilahi za Kiswahili zifanikiwe barabara, ni bora chemchem au chimbuko la istilahi liwe Waswahili wenyewe. Mtaalam huyu anasisitiza kuwa mwelemeo mkubwa katika kujenga istilahi mpya uwe kwenye:

(a) Lugha zenzake za Kiswahili,

(b) Lugha za makabila ya Kibantu, kuliko kuelekea kwenye lugha za kigeni kama inavyofanywa sana leo.

Tatu, ufufuaji wa istilahi asili uliosahaulika katika Kiswahili sanifu utathibitisha kwamba lugha hii haijawahi kuwa na "pengo kubwa" la kiistilahi, na kwamba ukwasi wake wa kiistilahi ni mpana zaidi. Mbega (1979) anauliza:

> Maneno **karakhana** (karakana), **zahanati**, **kabaila**, **kipuri** n.k ni maneno ya wapi? Hiki Kiswahili cha mpetompeto ni cha nini? Kwa nini tunakikuza Kiswahili kwa maneno ya kudondoza? Kwani tumechimbua ukale wa Kiswahili na kupata kuwa hatuna hazina ya maneno? ... hiki si Kiswahili bali ni mpochongo wa maneno.

Ili kuondoa tatizo hili la matumizi ya 'mpochongo wa maneno,' ni muhimu istilahi za Kiswahili ziundwe mumo kwa mumo, na kwa namna hii kuirudishia lugha hii 'ukale' na uasili wa kiistilahi.

Nabhany (1982) amebuni na kukusanya msamiati asili wa Kiswahili. Kwa mfano:

(53)

| | Kiswahili Asili | Kiswahili Sanifu (Maneno Yaliyoazimwa) |
|---|---|---|
| (53a) | **uhazigi** | zahanati |
| (53b) | **udandi** | kalamu (penseli)/kalamu ya mate |
| (53c) | **mwiya** | wakati |
| (53d) | **shokori** | stihizai |
| (53e) | **matayo** | lawama |

(taz. Nabhany (1978) katika *Kandi ya Kiswahili*)

Baruwa anadokeza kuwa:

> ... tulisema neno lizaliwe katika maneno yake asili au likiwa ni jina la kitu kipya basi lizaliwe neno katika mnasaba wa kitendo chake. Kuijenga lugha ndani ya lugha yenyewe ndiko kuikuza.

Kauli ya Baruwa ina uzito na tunakubaliana naye kwamba hapana dharura yo yote inayotushurutisha kuunda istilahi mpya ama kutohoa na kukopa za kigeni. Wanalugha wanahitajika tu kupekuapekua miongoni mwa Waswahili wenyewe na kupata msamiati faafu wa kutumika pale ambapo hapana neno mwafaka. Kwa kufanya hivyo, hazina ya istilahi ya lugha hii itachangiwa zaidi.

Nne, sababu nyingine inayofanya mfanyiko huu upendelewe na utumike ni kwamba msamiati asili ukifufuliwa utasaidia katika kuikuza lugha ya Kiswahili katika mwelekeo mmoja. Kikwamizi kikubwa cha uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili kinatokana na wanalugha kuunda istilahi mpya ilhali tayari zipo istilahi asili zinazopatikana katika lugha hii. Kwa mfano:

*blood pressure* = **presha**

= **buhari**

= **mtuto wa damu**

Wazee wa Mombasa kwa muda mrefu sana wamekuwa wakilitumia neno **buhari** kwa maana ya *"high"* na *"low bloodpressure"*. Hivyo hapakuwa na haja yo yote kwa Watanzania na vyombo vya TUKI na BAKITA kuunda **mtuto wa damu** ama hata **presha** iwapo hasa kusudi ni kuikuza lugha hii kwa mwelekeo mmoja.

Kadhalika, katika taaluma ya isimu ya Kiswahili, istilahi za kundi la B zimeundwa, japo istilahi za kundi la A tayari zimepata mashiko, kwa sababu aidha ziliundwa kimakosa, ama pengine zinafaa zaidi:

| **Kundi la A** | **Kundi la B** |
|---|---|
| isimu | **lugha wilayati** [Chuo Kikuu cha Uislamu - Uganda] (Isimu ni neno la Kiarabu. Maana yake halisi ni jina, -taz. *Ma ismi ka?* - jina lako ni nani?) |
| kaakaa | **burutio** *(palate)* [Chuo Kikuu cha Moi] |
| kijalizo | **kikamilishi** *(complement)* [Chuo Kikuu cha Makerere] |
| mfanyiko | **mnyumbusho** *(process)* [Chuo Kikuu cha Makerere] |
| sarufibia | **sarufi ya kilimwengu** *(universal grammar)* [Chuo Kikuu cha Makerere] |
| Kiarifu | **prediketa** (Besha, 1994) |
| hali | **aspekti** (Chuo Kikuu cha Nairobi) |
| ulumbi/usemaji fasaha | **wingilugha** (Vyuo Vikuu vya Moi na Egerton) |
| uwililugha | **ujozilugha** (Chuo Kikuu cha Moi) |

| | |
|---|---|
| mwanalughambili | **mjozi-lugha** (Chuo Kikuu cha Moi) |
| isijumla/isiyojumla | **isimujumlifu** (Chuo Kikuu cha Egerton) |
| mlumbi/mtondozi (mtu fasaha wa maneno) | **mwanawingi-lugha** (Chuo Kikuu cha Nairobi) |
| kongomeo | **koromeo** (Vyuo Vikuu vya Egerton na Moi) |
| vizuiwa | **vikatizwa** (Chuo Kikuu cha Kenyatta) |
| kopa | **sharabu** (ni kujaa zaidi ya pomoni) (Chuo Kikuu cha Moi) |

Ubunifu zaidi unahitajika kwa upande wa wanalugha wa isimu ya Kiswahili pamoja na haja ya kuchunguza katika ghala la istilahi za isimu ya Kiswahili ili kupata zile ambazo ni 'faafu,' na zenye usayansi.

Juhudi zote zinazofanywa na vyombo vya TUKI, BAKIKE, BAKITA na watu binafsi, akina Mdee, Temu, Mwansoko, Mbaabu, Akida, Kapinga, na wengineo, zinafaa zizingatie kwa kadri inavyowezekana, mfanyiko wa ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo wa msamiati wa Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, lugha hii itakuwa na istilahi faafu na bora, ambazo ziliangamizwa kwa sababu ya haraka za kuzifuata lugha za kigeni.

Badala ya kukopa istilahi za kigeni (Kiingereza, Kiarabu n.k.) na kuziswahilisha [kama wanavyopendekeza Abdulaziz (1989), Mwansoko (1990), Tumbo na Mwansoko (1992)] kwa madai kuwa hakuna lugha ulimwenguni isiyowahi kukopa istilahi za kigeni, inatupasa tupekuepekue miongoni mwa lahaja za Kiswahili - Kiamu, Kimvita,

Kipemba, Kimtang'ata n.k. na kufufua msamiati asili wa Kiswahili ilimuradi utumike pale ambapo hapana istilahi za kisayansi faafu za kutumika.

Aidha, pale ambapo hatupati istilahi mwafaka kuhusu dhana za kisasa za kisayansi na kiteknolojia, waundaji istilahi wafikirie zaidi, wawe wabunifu na, ikibidi, wanyambue mofimu za Kiswahili (Kiingi 1989). Kwa mfano:

*"family"* - **kizazi** (badala ya **familia**) (TUKI, 1990)

*"subfamily"* - **kijizazi** (badala ya **sabfamilia/ familia ndogo**)

*"infrafamily"* - **kikijizazi** (badala ya **familia ya chini**) (taz. mfano 63, uk. 188-9).

Msamiati asili unaweza kuhuishwa na kupewa matumizi mapya. Kwa mfano, neno **funda** ambalo kwa sasa limepanuliwa kimaana limo katika kamusi ya zamani ya F. Johnson (1939) na yaonekana limepanuka kimaana wakati huu. Neno "funda" lina maana kadhaa: Kwanza, ni kumea matiti kwa msichana aliyevunja ungo, na pili, ni kufunganisha vitu fulani pamoja (tazama **fundika, fundo, mfundo, kifundo**). Pia linatumika sasa kwa maana ya kinywaji chochote kile; 'kupiga funda moja.' Aidha, 'funda' ni **shavu.**

Mbali na msamiati asili kusaidia katika kuikuza lugha hii katika mwelekeo mmoja, kama ilivyotajwa mbeleni, pia utasaidia katika kuepuka kuunda istilahi mpya kwa dhana ambazo tayari zina msamiati kiasili wenye kuziwakilisha. Mathalani (54):

| | Kiingereza | Maneno yaliyoazimwa | Maneno ya Kiswahili Asili |
|---|---|---|---|
| (54a) | *leave* | mapumziko | **sono** |
| | *hospital* | hospitali | **gango** |
| | *fish* | samaki | **nswi** |
| | *vitamin* | vitamini | **ndisha** |

Nabhany (1978, 1982) amependekeza matumizi ya maneno asili yafuatayo:

| | Kiswahili | Kiingereza |
|---|---|---|
| (54b) | **jopo** | *panel* |
| (54c) | **tindikana** | *vacuum* |
| (54d) | **skuli ya uyezi** (malezi) (**skuli ya vidudu/ chekechea, skuli ya watoto wachanga, skuli ya toratora,** (taz. Akida, 1977)). | *nursery school* |
| (54e) | **uwote** | *college* |
| (54f) | **ndaki** | *university* |

(Maelezo kuhusu nambari za zamani za Kiswahili tazama Mwaro (1993:122) na Nabhany (1978) katika *Kandi ya Kiswahili*)

Ni muhimu kutaja hapa pia kwamba istilahi za isimu ya Kiswahili ambazo hazifuati nidhamu fulani (taz. 3.3.2, uk. 64), ama ziliundwa kimakosa, zisiingizwe katika matumizi ya kila siku, na mahali pake pachukuliwe na istilahi angavu, faafu, asilia, na ziwezazo kupanuliwa kimaana.

## 4.7 Uhusishaji wa Dhana na Kitajwa na/au Kazi Yake

Uhusishaji wa dhana na kitajwa vilevile hutumika sana kuzalisha istilahi za Kiswahili (Tumbo-Masabo, 1990). Hata hivyo, wataalam wengi wa Kiswahili (Tumbo, 1982; Mc William, 1985) wanasita kuafiki mfanyiko huu wa kuendeleza istilahi, kwa madai kwamba unakiuka tabia ya asili ya uundaji istilahi katika lugha ya Kiswahili. Madai ya wasomi wenye msimamo kama huu hayana mashiko, hasa kutokana na umuhimu wa mfanyiko huu ambao umetambulikana katika mataifa yaliyoendelea kama vile Marekani, Ujerumani, Ufaransa, na Uswidi (Tumbo, 1982). Mfanyiko huu unahusu uundaji wa istilahi ambazo zina maana inayohusiana na dhana inayowakilishwa kimaumbile, kitabia au kimatumizi.

Mbinu hii inatumiwa pia na mashirika ya kimataifa yanayoshughulikia uendelezaji wa leksikoni (taz. Tumbo 1982:89) kama vile *"International Electronical Commission," "Directorate for Translation and Terminology Services of the European Parliament,"* n.k. Hapana sababu, kwa hivyo, ya kuwafanya wanalugha wa Kiswahili kutoizingatia mbinu hii katika harakati zao za kuendeleza istilahi za Kiswahili. Kwa mfano, jina **msichana** lina visawe vyake kama vile **mrembo**, **kisura**, **kipusa**, n.k. Majina haya yote yanayomweleza msichana, yanahusiana kwa namna fulani na kitajwa (msichana). Kwa kawaida, msichana hujirembesha (ni **mrembo**) ili apendeze na atamanike. Kadhalika, **sura** yake huwa nzuri na ya kuvutia wavulana. Hivyo, msichana ni kiumbe chenye thamani kubwa sawa na **kipusa** (pembe ya faru) kwa wavulana. Katika hali hii, kuna na istilahi [kama vile **masagego** (premolars)]

ambazo zimeundwa kutokana na kuhusisha dhana na kazi.

## 4.8 Ukopaji

Dhana ya ukopaji, au kusharabu, imetajwa na baadhi ya wataalam wa Kiswahili [k.v. Temu (1984), Abdulaziz (1989), Irira (1990), Mwansoko (1989, 1990, 1996), Tumbo na Mwansoko (1992), Bwenge (1996), Sewangi (1996), na Chimerah (1998) kwa juujuu bila kujadiliwa kwa kina. Hapa tunakusudia angalau kuziba pengo katika mojawapo ya maelezo yanayolengalenga kwa kina. Miongoni mwa maswala ambayo ni muhimu na yatashughulikiwa ili yawe mufidi na wazi ni pamoja na:

- Maana ya ukopaji.
- Sababu za ukopaji wa istilahi za kigeni.
- Pingamizi juu ya ukopaji wa istilahi za kigeni.
- Uteuzi wa lugha changizi.
- Matatizo ya ukopaji kutoka lugha ya Kiingereza.
- Mifanyiko ya ukopaji (utohoaji na kaleki/ukopaji sisisi).

### 4.8.1 Maana ya Ukopaji

Katika *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990), neno "ukopaji" linaelezwa kama:

> kitendo cha kuhamisha kipashio kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine.

Bwenge (1996:66) anaeleza "mkopo" kama:

> ...uundaji wa istilahi kwa njia ya kutohoa istilahi ya lugha changizi katika lugha lengwa...

Katika kazi hii, tunachukulia 'ukopaji' kwa maana ya uchukuaji wa dhana mpya kutoka lugha nyingine pamoja na jina lake.

Uchukuaji wa istilahi ya kigeni aghalabu huhusika na hatua nne:

(i) Lugha asili ya istilahi inayochukuliwa tu.

(ii) Mfanyiko wa uasilishaji au utohoaji wa neno la kigeni kwa mujibu wa sarufi ya Kiswahili.

(iii) Istilahi matokeo, maana yake sanifu, na maelezo ya muktadha wa matumizi yake.

(iv) Uhusianifu wake na istilahi nyingine katika mfumo wa istilahi, hususani katika fani au uga wa taaluma husika (taz. Irira, 1990:14 kwa ufafanuzi na maelezo zaidi).

Istilahi ngeni huingizwa kwenye mfumo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili baada ya kupewa umbo na tabia ya Kiswahili.

Kabla hatujatoa mifano ya istilahi mkopo za Kiswahili, na baadhi ya sababu za ukopaji, ni muhimu kusisitiza hapa kwamba mfanyiko wa ukopaji umeungwa mkono, na vilevile umepingwa, na wataalam wengi. Miongoni mwa wataalam wanaotetea mfanyiko wa ukopaji kwamba ni 'zalishi' ni Khamisi (1981), Myachina (1981), Temu (1984), Mc Crum, Cram na Mc Neil (1986), Shariff (1988), Abdulaziz (1989), Coulmas (1989), Mwansoko (1990), na Chimerah (1998). Kundi la 'wahafidhina' linalopinga vikali mbinu ya ukopaji wa istilahi za kigeni linawahusisha wanalugha kama vile Khalid (1977), Nabhany (1978, 1982), Mukhwana (1988), Kiingi (1989), miongoni mwa wengine (k.v. akina T.S.Y. Sengo na H. Akida). Ingawa si lengo letu kujiingiza katika 'mzozo' na mjadala wa ukopaji na uswahilishaji wa istilahi za kigeni, ni

muhimu tueleze baadhi ya sababu (na hoja zinazotolewa) za ukopaji ili dhana hii ieleweke wazi.

### 4.8.2 Sababu za Ukopaji wa Istilahi za Kigeni

Mfanyiko wa ukopaji (au kutazama 'nje') wa lugha pokezi umetetewa sana. Mojawapo ya sababu ya ukopaji inayotolewa ni kwamba ukopaji **ni sifa ya lugha zote na kila lugha hukopa.** Kuhusu swala hili, Likhako (1991:33) anasema:

> ...ingawa Kiswahili kina maneno mengi ya mkopo, hili silo jambo la aibu kwani lugha nyingi duniani zimekopa msamiati kutokana na lugha zingine. Kiingereza kina asilimia 85 ya maneno ya kukopa...

Kundi la "kama Kiingereza" linaongozwa na wanalugha (k.v. Mc Crum na wenzake (1986), Abdulaziz (1989), Chimerah (1998)) wanaoshikilia kwamba Kiingereza kinajimudu au kinajitosheleza kileksia, kwa sababu kinazidi kukopa istilahi za kigeni. Ni maoni ya wanalugha hawa, ila tu Chimerah (1998), kuwa Kiswahili kifuate 'nyayo' za Kiingereza za ukopaji, manake 'hakuna haja ya kujisumbua.'

Mc Crum na wenzake (1986:19 katika Chimerah 1998) wanadai kwamba Kiingereza kina ukwasi mkubwa kutokana na uchukuaji wa istilahi mkopo kuzidi wa lugha zote 2,700 duniani. Kiingereza kimekopa istilahi nyingi kama mfano huu unavyodhihirisha:

(54)

(54a) Kutoka Kirusi - *glasnost* (uwazi), *perestroika* (upangaji upya).

(54b) Kutoka Kigiritini - *video, television* (runinga), na

nyingine nyingi.

Chimerah (1998), katika kitabu chake *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*, anadokeza kwamba Kiswahili kiendelezwe kileksikoni kwa mfanyiko wa ukopaji, na **harakati za kupata istilahi mkopo ziimarishwe.** Mtaalam huyu (1998:14) anadai kwamba:

> Lugha inapokuzwa mumo kwa mumo na bila ya kuruhusu athari zozote kutoka nje huwa **inajichimbia kaburi** lake yenyewe. Hivi ndivyo lugha ya Kilatini, ambayo kwa wakati mmoja ilikuwa na urasmi wa kisifabia wa kimaandishi na ya kuheshimiwa, ilivyodidimia.

Maoni haya ya Chimerah yanahitaji uchunguzi wa kina. Si kweli kwamba umaarufu wa Kilatini ulididimia kwa sababu haikuruhusu athari za nje. Sisi tunafahamu, kutokana na tajriba yetu, kwamba kati ya A.D. 550 na A.D. 700 Kilatini kilipoteza uasili wake, kutokana na kutawanyika, na ikawa lugha ya kimataifa hasa katika ufundishaji kote Barani Uropa. Lugha nyingine zilizofundishwa kama vile Kisanskrit (Daswani, 1989), Kiarabu asilia (Ibrahim, 1989), Kihebrania (Rabin, 1989), na Kijapani (Coulmas, 1989), pia kwa sababu za kisiasa na kijamii, zilipatwa na 'mkosi' huo wa Kilatini wa kufifia kimaandishi. Lugha haitambuliwi na kutazamwa kwa njia moja kwa wakati wote. Wakati hubadilisha kila kitu, lugha ikiwemo. Kwa hivyo, kutosambaa na kudidimia kimatumizi kwa Kilatini, kwa maoni yetu, huenda kulitokana na kukosekana kwa masimulizi ya kiutamaduni, yanayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, ambayo ni sifa za lugha asili yoyote. Kilatini kilizaa vilugha ambavyo vilikomaa vikawa lugha za kuheshimika kuliko lugha mama yenyewe. Inaelekea Chimerah (1998b) ana maoni

tofauti anapodai kuwa Kilatini kilikosa uwezo wa kubadilika na kukidhi matakwa na maendeleo ya mawasiliano katika nyanja ya teknolojia. Vilevile, anaonyesha bayana katika matini zake za juzi, mfano karatasi yake, "Kiswahili Through the Ages" (1999) kwamba, maendeleo ya kiutamaduni yalikuwa yanatokea nje ya lugha ya Kilatini na wala sio ndani.

Aidha, watetezi wa mfanyiko wa ukopaji wanadokeza kwamba kuwepo kwa wingi wa istilahi mkopo katika Kiswahili hakuwezi kuifanya ipoteze U-Afrika wake kwa sababu muundo wake wa Kibantu hautabadilika (Kitsao 1989). Sababu nyingine inayotolewa katika kutetea dhana ya ukopaji wa istilahi za kigeni ni kwamba, ukopaji huipa lugha pokezi nguvu za kiismu zinazohitajika katika mawasiliano ya kimataifa (Abdulaziz, 1989).

Hatukatai, wala si lengo letu kusema 'tusikope' istilahi za kigeni au 'tukwasishe' Kiswahili kutokana na istilahi mkopo. Lakini ieleweke kwamba 'upungufu' wa istilahi (iwapo upo) za Kiswahili, hautokani na kutopendelea kwa lugha hii kutazama au kuchunguza 'nje'. Kiswahili kina istilahi mkopo nyingi kama mifano hii (55) inavyothibitisha:

(55)

| (55a) | **Istilahi mkopo** | **Asili yake** |
|---|---|---|
| | wakati | '*waqt*' - Kiarabu |
| | anwani | '*anuan*' - Kiarabu |
| | habari | '*khabar*' - Kiarabu |
| | falaki | '*falak*' - Kiarabu |
| | mvinyo | '*vinho*' - Kireno |
| | bendera | '*bendeira*'- Kireno |
| | shule | '*schule*' - Kijerumani |
| | ngeli | '*ngeli*' - Kihaya |
| | soni | '*soni*' - Kibantu/Kiswahili |
| | duvai | '*duvin*' - Kifaransa |

| | |
|---|---|
| frikwensi | *'frequency'* - Kiingereza/Kilatini |
| fonimu | *'phoneme'* - Kiingereza/kilatini |
| fezi | *'phase'* - Kiingereza/Kilatini |
| bepari | *'beupar'* - Kihindi |
| chokora | *'chokra'* - Kihindi |
| pilau | *'pilaf'* - Kiajemi |
| dirisha | *'dirish'* - Kiajemi |
| daktari | *'docteur'* - Kifaransa |

Mifano iliyotolewa hapo juu ya istilahi mkopo, ni ushahidi kutosha kwamba hadi leo Kiswahili kinaendelea kuchukua maneno kutoka lugha za kigeni. Ukopaji huu unatokana pia na kutokuwepo kwa msamiati asili wa kurejelea dhana mpya inayoingia katika lugha pokezi.

Ukopaji wa istilahi za kuwakilisha dhana za kigeni hutumika kwenye lugha nyingi duniani. Kwa mfano, katika Runyankore-Rukiga na Luganda, dhana ya *"co-driver"* ni ngeni na haina istilahi asili. Lugha hizi zimelazimika kutoa maelezo marefu kuasilisha neno hili la kigeni:

"dereeva ow'oku bbali" - Runyankore-Rukiga

"dereeva ow'okubiri" - Luganda

"dereva-mwenza" - Kiswahili

Kadhalika, wanajamii hawa wamebadilisha neno *"co-driver"* ili lishabihi muundo wa lugha zao pokezi na kujenga **"kodereeva"**. Mifano zaidi:

| **Luganda** | **Kiingereza** |
|---|---|
| **sitensolo** | *'stencil'* |
| **emotoka** | *'motorcar'* (taz. Muranga 1992:11) |

Aidha, ukopaji wa istilahi za kigeni husababishwa na haja ya uangavu wa istilahi na iktisadi. Mathalani, kuna maneno ya Kiingereza yenye maelezo marefu katika Kiswahili:

*"co-heir"* - **arithiye pamoja na mwingine (mrithi-mwenza)**

*"adjective"* - **neno liongezalo maana ya jina**

(Madan/ F. Johnson, 1939).

Ili kutatua tatizo la urefu wa istilahi, hutokea azma ya ukopaji ama uundaji wa istilahi fupi (k.v. 'adjective' - **kivumishi**).

Uoneaji fahari wa lugha changizi ni sababu nyingine inayoufanya mfanyiko wa ukopaji kupewa umbele. Kuhusu swala hili, Ali (1966:16) anasema:

> Sehemu kubwa ya watu waliotia maneno ya Kiarabu katika Kiswahili ni watu wa Pwani ... kwa kuwa watu hawa waliwapenda Waarabu na ustaarabu wao, kama hivi leo watu wanavyopenda ustaarabu wa Wazungu ... wanaipenda lugha yao (Kiingereza). Kwa kupenda lugha yao waliyachukua maneno yao na kuyatia katika Kiswahili.

Naye Kihore (1983:170) anadai kuwa:

> ...litakuwa jambo la kufurahisha ikiwa uchunguzi utafanywa kuonesha ni vipi ~~na~~ kwa kiasi gani kuingizwa kwa maneno ya kigeni katika Kiswahili kunavyoendelezwa na mapenzi tuliyonayo kwa watu fulani na lugha zao.

(taz. pia Mazrui (1981) katika tasnifu yake ya uzamifu *"Acceptability in a Planned Standard"* kwa maelezo zaidi).

Sisi, ingawa tunafahamu kwamba ukopaji ni sifa ya lugha zote duniani, na kwamba kwa kawaida lugha hujikuta tu ikikopa kutoka kwa lugha zilizoiingilia mazingira yake, lakini hatuna budi pia kukubaliana na Ali (1966). Ukopaji mwingi wa istilahi za kigeni huenda ulitokana na wazungumzaji na wanalugha wa Kiswahili kuzionea fahari istilahi mkopo na lugha wanazokopa istilahi hizo. Kama anavyodokeza Kihore (1983) swala hili linahitaji uchunguzi

wa kina. Kwa hakika hapana sababu muhimu ya wataalam wa Kiswahili kuendelea kuonea fahari istilahi mkopo (badala ya msamiati asili) ambazo, kulingana na ulimwengu wa leo unaohitaji ubunifu, zinakimbiwa katika lugha nyingi. Kijerumani kwa sasa kinajirutubisha kiistilahi kwa kuhimiza matumizi ya maneno asili badala ya istilahi mkopo, kama mfano huu unavyodhihirisha:

(55b)

| **Istilahi asili zinazopendekezwa** | **Istilahi zilizoazimwa** |
|---|---|
| *dienslauf/stufenleiter* | *karriere* |
| *einhaftend* | *immanent* |
| *einrichtung, Leitlegung* | *installation* |
| *vermogen, Hauptgut* | *kapital* |
| *staatsmann* | *diplomat* |

(taz. Coulmas, 1989:191-2)

Nabhany (1978, 1982), baada ya kutambua umuhimu wa msamiati asili, anapendekeza msamiati ufuatao utumike (badala ya istilahi mkopo):

(55c)

| **Kiarabu** | **Istilahi Mkopo** | **Maneno Asili ya Kiswahili** |
|---|---|---|
| kaf | kofi | **ipi** |
| sahwi | sahau | **liwaa** |
| dam | damu | **ngeu, mweni, mazi** |
| faswahah | faswaha/fasaha | **bulibuli** |

Kwa hivyo Kiswahili, kama lugha nyingine za ulimwengu (k.v. Kijerumani), kitajitosheleza kwa upande wa istilahi iwapo kitafanyiwa uchunguzi wa kina katika msamiati asili. Mtindo wa wasomi na wataalam wa Kiswahili wa 'kuswahilisha' istilahi za

kigeni, pale ambapo pana msamiati asili, pia upo kwenye lugha nyingi duniani. Mifano ya istilahi za namna hii katika Luganda ni kama ifuatavyo:

(55d)

| **Istilahi asilia** | **Istilahi mkopo** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|
| e'so:nda | e'kko:na | (kona) - Kiingereza |
| amaa:nyi | e'fo:si | (nguvu) - Kiingereza |
| akalee:go | e'to:ni | (toni) - Kiingereza |

(Angalia Kiingi, 1989 na Mukama, 1992 kwa maelezo na mifano zaidi ya istilahi mkopo zilizo - "Gandaishwa" pale ambapo pana istilahi asili za kutumika).

### 4.8.3 Pingamizi Juu ya Ukopaji wa Istilahi za Kigeni

Pingamizi juu ya ukopaji wa istilahi za kigeni si swala geni duniani (Coulmas, 1989:187). Kuna wanalugha wanaopinga mfanyiko wa ukopaji, na wana sababu zao za kufanya hivyo. Katika kushikilia wazo kwamba Kiswahili kiendelezwe mumo kwa mumo, au kwa kutazama ndani ya lugha yenyewe, wanalugha wenye msimamo huu wanakanusha madai kuwa kila lugha hukopa na hakuna haja ya Kiswahili kujisumbua (taz. Mc Crum na wenzake, 1986).

Ingawa ni kweli kwamba 'lugha zote' duniani hukopa istilahi za kigeni ama hujiendeleza kileksikoni kwa utaratibu wa ukopaji, lakini ni utaratibu usio zalishi (rejelea 5.2.1.6, uk. 304). Kiarabu (Gallgher 1968:140), Kihebrania (Rabin 1989), Kijapani (Takada, 1989; Sugito 1989), Kijerumani (Coulmas, 1989:187) na Kichina (Pasierbsky, 1989; Ibrahim, 1989), ni lugha ambazo kwa

sasa hazionei fahari mfanyiko wa ukopaji na matumizi ya istilahi za kigeni. Kutoonea fahari ukopaji au istilahi mkopo si udhaifu kwa ulimwengu wa leo, bali ni ukomavu wa lugha husika (taz. Abdulaziz, 1989:43). Lugha ikijiendeleza kileksikoni pasi na ukopaji ni ishara ya ubunifu wa wataalam wanaohusika na shughuli za kukuza lugha, ubunifu ambao unahitajika sana na waundaji istilahi za isimu ya Kiswahili. Endapo tutakopa istilahi za kigeni kama vile *"predicate"* - kuwa ni **prediketa** (Massamba na Wenzake, 1999:18) basi na tuwe na uhakika wa kueleza; *"predicative nouns"*, *"predicative adjectives"*, *"adjective predicate"*, *"attributive adjectives"*, *"mass nouns"*, *"productive affix"* na *"pressupposition"*. Pana haja ya Kiswahili kufuata 'nyayo' za lugha zilizotajwa mbeleni, hususani Kichina, ambapo dhana za kigeni zinakopwa, lakini kabla ya dhana kuingizwa katika mfumo lugha, ugeni wake huondolewa na huasilishwa (hu-Chinaishwa). Huu ndio msimamo wa wahifadhina (Nabhany, 1982), msimamo ambao sisi pia tunauunga mkono. 'Kuboresha' na Kuswahilisha istilahi mkopo hupunguza uwezo wa ubunaji kwa upande wa wanalugha na wanaisimu wa Kiswahili. Imekuwa vigumu kwa mzungumzaji asiyefahamu lugha changizi kuelewa maana ya istilahi za isimu ya Kiswahili zinazoundwa kwa mfanyiko wa ukopaji (k.v. **leksisi**===*"lexis"*, **makroni**===*"macron"*, **umalapropu**===*"malapropism"*, n.k.). istilahi mkopo kama hizi, kwa bahati mbaya huonewa fahari na wanalugha wengi wa Kiswahili.

Pendekezo kwamba Kiswahili kiendelee kupata istilahi za kigeni, hususani za Kiingereza (Mwansoko, 1990), kwa maoni yetu halina mashiko. Mchango wa lugha za kigeni kileksikoni (Kiarabu,

Kiingereza, n.k.) katika maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia katika kikwi au mlenia huu utazidi kuwa mdogo sana. Lugha changizi zenyewe (rejelea **4.8.4**, uk. 170) zilikopa istilahi nyingi kutoka Kigiritini na lugha nyinginezo duniani. Lugha ya Kimalaysia, kwa mfano, ilikopa istilahi nyingi kutoka kwa Kiarabu (k.m. **iktisad, intikad**, n.k.) lakini haijakomaa kiistilahi. Kiarabu chenyewe kimesharabu istilahi nyingi zinazotokana na lugha Magharibi mwa Uropa, mno mno zile za kisayansi na kiteknolojia. Ukopaji wa istilahi za kigeni ni kujichimbia kaburi bure kileksikoni - manake kunawapunguzia wanalugha uwezo wao wa ubunaji. Lugha inapojiendeleza kiistilahi kwa mfanyiko wa ukopaji huonyesha uwezo wake wa kutojimudu. Ni maoni ya Chimerah (1989) kwamba Kimalaysia, Kiindonesia na Kifilipino lau zingepunguza ukopaji wa istilahi za kigeni zingeshinda mataifa ya Magharibi katika sayansi na teknolojia. Mataifa hayo yameegemea na kutegemea Kigiritini kileksia. Kijerumani, kwa kuhimiza matumizi ya maneno asili, kimepunguza matumizi ya istilahi mkopo (k.v. *'karotte'*, *'paket'*, *'papa'*, *'insekt'*, *'kilo'* n.k. Coulmas, 1989:187). Ubunaji unaohitajika zaidi kwa upande wa waundaji istilahi za Kiswahili lau ungepatikana ungesaidia sana katika kuimarisha na kufanikisha usambazaji wa maarifa ya kisasa ya kisayansi na kiteknolojia.

La muhimu ni uwezo wa wanaisimu wa Kiswahili kuwa wabunifu na wasijiingize katika 'mzozo' huu wenye historia ndefu. Uamuzi uachiwe watumiaji wa Kiswahili wenyewe (Mdee, 1980:59).

### 4.8.4 Uteuzi wa Lugha Changizi

Lugha changizi (L.C.) ni lugha ambayo, kutoka kwayo, dhana na istilahi mkopo huchukuliwa na kuingizwa katika lugha nyingine au lugha pokezi (L.P.). Suala la chanzo cha istilahi mkopo za Kiswahili limewachachafya wanalugha wengi (k.v. Temu, 1972; Mdee, 1980; Mwansoko, 1989; 1990; Tumbo na Mwansoko, 1992 na vyombo vya kukuza Kiswahili vya TUKI na BAKITA) kwa sababu ya umuhimu wake.

Wanalugha hawa inaelekea wametambua umuhimu wa chanzo au asili ya istilahi katika tathmini, na uteuzi wake, kinyume na Tauli (1968:70) anayedai kwamba asili ya neno haina umuhimu wo wote katika kutathmini neno. Vilevile, anadai kuwa ni ufaafu au ubora wa neno ambao unafaa kutiliwa maanani (taz. Ferguson, 1968:33). Kutotambua umuhimu wa chimbuko asili la istilahi, lugha maalum changizi, pamoja na **kuweka huru** sera ya lugha changizi katika shughuli za kukuza leksikoni ya Kiswahili, kumesababisha tatizo la wingi wa visawe vya istilahi za isimu ya Kiswahili (Mdee, 1983). Suala la 'usoko huria' wa lugha ambazo huchangia istilahi mkopo za Kiswahili halijatatuliwa hadi sasa. Mapendekezo yanayotolewa na vyombo vya kukuza lugha na wanaisimu wa Kiswahili yanakanganya watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Pendekezo la **BAKITA** (taz. *Kakulu No.3*, 1982:16) ni kwamba chimbuko la istilahi za Kiswahili liwe:

(1) Kiswahili chenyewe,

(2) Lugha za Kibantu,

(3) Lugha nyingine za Afrika,

(4) Lugha za kigeni.

Uchunguzi uliofanywa na Mwansoko (1989, 1990) unaonyesha kwamba walengwa wa Kiswahili wanapendelea istilahi za isimu na fasihi zitokane na:

(1) Kiswahili chenyewe na lahaja zake,

(2) Lugha za Kibantu,

(3) Kiingereza,

(4) Kiarabu,

(5) Kigiritini (Kigiriki na Kilatini) kwa mfuatano huo (1-5) (Pia rejelea 1.5, uk. 6).

#### 4.8.4.1 Ukopaji kutoka Kigiriki-Latini

**Kigiriki-Latini** ni chanzo kimojawapo cha istilahi mkopo za Kiswahili, hasa katika sayansi na teknolojia. Mbinu hii imeungwa mkono kwa sababu ni muhimu lugha ikope istilahi moja kwa moja kutoka "lugha azali changizi" (Kigiritini), badala ya kufanya hivyo kutoka lugha ambazo zenyewe zilikopa kutoka nyingine (Mdee, 1983; Mac William, 1985). Kadhalika, istilahi mkopo kutoka Kigiritini huwa na sifa ya umataifa. Msimamo wa Kiingi (1989), kuhusu jinsi ambavyo lugha ya Luganda na Kiswahili zinavyoweza kukuza istilahi zake, ni kwamba lugha hizi zipanue istilahi za kisayansi menyu kama vile bayolojia, fizikia, hesabu, na kemia, kwa kuazima mofimu moja kwa moja kutoka Kigiritini.

Msimamo wa Ohly (1977) na Kiingi (1981, 1989) wa uendelezaji wa istilahi za Luganda na Kiswahili kwa ukopaji kutoka Kigiriki-

Latini, umepingwa na Abdulaziz (1989:39). Abdulaziz anadai kuwa kufanya hivyo (kukopa mofimu moja kwa moja kutoka Kigiritini) kunahitaji mpango nyeti na fedha nyingi. Matokeo ya njia hii yatakuwa kuunda istilahi ambazo zitawakanganya walengwa.

Naye Mwansoko (1990:132) anapinga ukopaji kutoka Kigiriki-Latini kutokana na hofu yake kwamba wengi wa watumiaji wa Kiswahili hawaelewi lugha hiyo. Aidha, maandishi kuhusu Kigiriki-Latini ni haba mno. Ni ukweli usiopingika kwamba uchache wa istilahi mkopo kutoka Kigiriki-Latini (k.v. **video, televisheni**) unatokana na wataalam na walengwa wa Kiswahili kukosa elimu ya kimsingi katika Kigiriki-Latini. Inaelekea Kiingi (1992) amebadili msimamo wake. Anapendekeza kwamba Kiswahili kifuate mfano wa lugha za Kijerumani, Kichina, Kikorea, ambazo hazitegemei tena Kigiriki-Latini kiistilahi. Lugha hizo zinajiendeleza mumo kwa mumo katika taaluma za sayansi na teknolojia.

#### 4.8.4.2 Ukopaji kutoka Kiarabu

Hii ni mbinu ambayo imetetewa na wataalam wengi (k.v. Abdulaziz, 1985; Akida, 1977; Gibbe, 1981; Mbughuni, 1983) kwa sababu ni rahisi kuingiza istilahi mkopo za Kiarabu katika Kiswahili na kwamba zina ukubalifu mkubwa kwa walengwa. Abdulaziz (1985:195) anatoa utaratibu unaopaswa kuzingatiwa katika ukopaji. Anapendekeza chimbuko la istilahi mkopo za Kiswahili liwe:

(i) Lahaja za Kiswahili.

(ii) **Kiarabu.**

(iii) Lugha za Kibantu.

(iv) Kiingereza na Kigiritini.

Mwanalugha huyu anatetea ukopaji kutoka Kiarabu kwamba ni swala la kawaida mno linalotokana na maingiliano ya lugha hizi mbili ya muda mrefu. Abdulaziz (1989) anatufichulia kwamba:

> ... kutokana na maingiliano kati ya Waswahili na Waarabu kwa karne nyingi, Kiarabu ni changizi cha Kiswahili kama ilivyo Kigiritini kwa lugha za Ulaya. Ukopaji wa moja kwa moja kutoka Kiingereza aghalabu unaonekana kuwa si kawaida na hivyo haukubaliki. Jamii-wingi-lugha ya Kiswahili haitambui chanzo cha ukopaji kutoka Kiarabu kama 'ukopaji' ukilinganisha na ilivyo ukopaji kutoka Kiingereza. Wale tu ambao wanakijua Kiarabu ndio wawezao kujua kwamba ukopaji huo umetokea.
> (nukuu kutoka Kiingi, 1989:146)

Kutokana na dondoo hili, ni dhahiri kwamba Abdulaziz anachukulia ukopaji kutoka Kiarabu kuwa hautambuliki kwa urahisi, hivyo yapasa uendelezwe. Sisi hatuna sababu yoyote ya kuushuku msimamo wa mwanalugha huyu, wala kukanusha kwamba matumizi mapana ya istilahi mkopo za Kiarabu yametokana na kuathiriana kwa lugha hizi mbili. Kuna nyingi istilahi mkopo kutoka Kiarabu kwenye Kiswahili. Mifano:

**(56)**

(56a) **mguno**

(56b) **sarufi**

(56c) **sahili**

(56d) **irabu**

(56e) **shada**

(56f) **masurufu** (impresti)

(56g) **karadha** (advansi/mkopo)

(56h) **ankra** (invoisi)

Ukopaji wa istilahi kutoka Kiarabu haukosi kuwa na dosari zake. Mfanyiko huu ni zalishi tu katika sayansi ya jamii. Katika sayansi menyu, uteuzi wa Kiarabu kama lugha changizi haupendelewi (taz. Kiingi, 1981). Mathalani, tazama istilahi hizi na namna zinavyohusika na fani zifuatazo:

| **Fani** | **Idadi ya istilahi Mkopo kutoka Kiarabu** |
|---|---|
| Agronomia na ufugaji | 0 kwa 678 |
| Uhandisi kilimo | 0 kwa 285 |
| Kemia | 8 kwa 195 |
| Fizikia | 5 kwa 203 |

(ang. BAKITA, 1980, 1990:19; Irira, 1986:48)

Uhaba wa istilahi mkopo za isimu kutoka Kiarabu, umesababishwa na ukosefu wa ujuzi wa Kiarabu kwa walengwa na wataalam wa Kiswahili. Inaelekea walengwa wengi huzikataa istilahi mkopo za Kiarabu manake hawazielewi vizuri; yaani hawajui Kiarabu. Vilevile, hakuna makamusi ya Kiswahili-Kiarabu au Kiarabu-Kiswahili ya kurejelewa (Tumbo na Mwansoko, 1992:38). Ni kwa sababu hii ndipo Nabhany (1979), katika *Sambo ya Kiwandeo: The Ship of Lamu Island*, anapendekeza matumizi ya maneno ya asili yafuatayo badala ya ukopaji:

**utako** - mti wa mwanzo wa chini ya jahazi.

**turusi** - ubao ulio nyuma ya jahazi palipo na usukani.

**ushuba** - kikopo cha kutekea maji ya kutumiwa chooni.

(Kuhusu umuhimu wa arki za Kiarabu katika Kiswahili, tazama Akida, 1977).

#### 4.8.4.3 Ukopaji kutoka Kiingereza

Kiingereza, kwa muda mrefu sasa, kimetumiwa kama chanzo kikuu cha istilahi mkopo katika sayansi menyu, sayansi za jamii na teknolojia. Mukama (1989:6) anadokeza kwamba:

> ... Kiswahili kiko katika kilele cha kujikuza na kujipanua ili kumudu maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hivyo, sote bado tuko katikati ya harakati za kujiuliza maswala kama: **'Federal structure', anaphora, enzymology** ... ni nini kwa Kiswahili?

Ingawa hatuna uhakika kama utandaridhi (utandawazi) wa istilahi za isimu kupitia kwa ukopaji kutoka Kiingereza utatatua na kutoa jibu kamili la swala hili analouliza Mukama, ni vyema kukiri kwamba pana haja ya kuwekewa misingi na sera madhubuti lugha changizi zinazosharabisha istilahi lugha ya Kiswahili. Uteuzi wa Kiingereza, kama chanzo cha pekee au kikuu cha istilahi mkopo za Kiswahili (Mwansoko, 1989, 1990) una udhaifu. Kuna sababu nne kuu zinazofanya msimamo huu uwe dhaifu: Kwanza kabisa, mtaalam huyu hakueleza ni kwa sababu gani Kiswahili kikope istilahi kutoka kwa Kiingereza, lugha ambayo yenyewe imekopa istilahi zake kutoka lugha nyingine [k.m. Kilatini - chaire > **chair** (kiti), tabula > **table** (meza)]. Haieleweki ni kwa sababu gani ukopaji huo usitekelezwe moja kwa moja kutoka Kigiritini! (Kiingereza kimechota istilahi nyingi za Kigiritini - taz. Hall, 1964).

Tunachofahamishwa na Mwansoko (1990:134) ni kwamba ukopaji kutoka Kiingereza ni muhimu na umeendelezwa katika lugha kama vile Kisomali, Kihindi, Kiindonesia na Kimalaysia. Kadhalika, haieleweki bayana ni vigezo gani mwanalugha huyu amevitumia

katika kuteua Kiingereza. Suala la utengano wa kijamii halikuzingatiwa, manake kila jamii tumizi-lugha huwa tofauti, na tofauti hizo hujitokeza katika uteuzi wa lugha ya taifa na lugha rasmi kwa kutegemea sera ya lugha ya jamii husika.

Pili, hoja kwamba istilahi mkopo hutoka Kiingereza [angalia Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:26)] si ngeni kwa watumiaji wake wengi kutokana na 'elimu yao kwa Kiingereza' kwa maoni yetu inapotosha. Idadi kubwa ya istilahi mkopo za Kiingereza, hususani katika taaluma ya isimu, zina 'uvulivuli' kwa walengwa wengi wasio wasomi, na wazawa wa Kiswahili, ambao mara nyingi huzikataa istilahi hizo (taz. maelezo ya ukubalifu wa istilahi mkopo katika 6.1, uk. 318).

Tatu, kuwepo kwa vitabu vingi vya Kiingereza na makamusi ya Kiingereza-Kiswahili au Kiswahili-Kiingereza ya kurejelea si sababu tosha ya kufanya Kiingereza kiteuliwe kama 'chanzo kikuu' katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili (Khamisi, 1981:5). Kinachohitajika, kwa wataalamu na waundaji wa istilahi za Kiswahili, ni kuacha kuegemea sana kwenye lugha yoyote ya kigeni kiistilahi na kufikiria zaidi. "Usomi" wa wanaleksikografia wa Kiswahili unafaa kuwawezesha kuwa wabunifu (Kiingi, 1989). Utaratibu wa ubunifu unaopendekezwa na Temu (1972) na Kiingi (1989) utiliwe maanani katika shughuli za kukuza istilahi za isimu ya Kiswahili. Endapo ni lazima dhana na istilahi fulani za kigeni zikopwe na kuswahilishwa, basi, na ukopaji huo uwekewe mipaka au misingi ya kisayansi (Ohly, 1987).

Nne, uteuzi wa lugha moja ya kimataifa (Kiingereza), kama chanzo cha istilahi mkopo za Kiswahili (Mwansoko, 1990:134), utakwamisha juhudi za kuendeleza lugha hii. Vilevile, katika medani ya isimu, utazidisha tatizo la visawe vya kiistilahi. Makundi ya wataalamu (wasomi kwa wasio wasomi, wazawa kwa wasio wazawa wa Kiswahili), yataongezeka, na ushirikiano wao utakosekana katika kuunda, kusanifisha na kukubali istilahi mpya za Kiswahili. (Pia tazama matatizo ya ukopaji istilahi za Kiingereza katika **4.8.5**, uk. 182).

Hata hivyo, istilahi za isimu ya Kiswahili zilizokopwa kutoka Kiingereza ni nyingi sana, kama mfano unavyothibitisha:

**(57)**

(57a) **analojia**

(57b) **katafora**

(57c) **aloloki**

(57d) **alomofu**

(57e) **anteria**

(57f) **anthropofoniki**

(57g) **paleografia**

(57h) **stredenti**

(57i) **antroponemia**

**4.8.4.4 'Ukopaji' kutoka Lugha za Kibantu**

Hii ni mbinu mojawapo inayotumika katika kuendeleza istilahi za Kiswahili. Njia hii imetetewa sana na wataalam (k.v. Khamisi 1981, Nabhany 1982, Mdee 1986) ambao hawaoni haja ya kuchukulia

lugha za kigeni kama ghala la kuchota istilahi zinazohitajika katika Kiswahili. Hata hivyo, mfanyiko huu haujazalisha istilahi nyingi kwa sababu kadhaa: Kwanza, lugha za Kibantu ni nyingi sana (taz. Abdulaziz, 1972 na Waller Tabb, 1993). Wanalugha wa Kiswahili hushindwa kuteua lugha za kutumia kama vyanzo vya mikopo ya istilahi wanazohitaji. Ushindani wa lugha hizi na mvutano baina ya wazungumzaji wake, [nchini Uganda mvutano ni baina ya Kiswahili na Kiingereza; na lugha za kienyeji - Luganda na Runyakitara (Runyoro/Rutooro/Runyankore/Rukiga) (Ndoleriire 1996)] umesababisha kutoingizwa kwa istilahi za Kibantu katika makamusi na matumizi ya kila siku.

Istilahi chache zinazosanifishwa na kuingizwa kwenye kamusi za Kiswahili mara nyingi hutokana na misukumo, kutetewa na wazungumzaji wake wanaoshiriki katika semina na warsha za kuendeleza lugha hii. Baadhi ya mifano ya istilahi hizo ni:

(58)

| | | |
|---|---|---|
| (58a) | **bunge** | - Kinyamwezi/Luganda |
| | **ikulu** | - Kinyamwezi |
| | **juju** | - Kihausa |
| | **myuko** | - Kikaguru |
| | **nguka** | - Kinyakyusa |
| | **uga** | - Kizigua/Kiswahili |
| | **shuna** | - Kisumbwa/Kihaya |
| | **ngeli** | - Kihaya/Kiswahili |
| | **ngaha** | - Nyaturu. |

Pili, kuotozalisha istilahi nyingi kutoka lugha za Kibantu kunatokana na ukosefu wa makamusi ya lugha za Kibantu ambayo

yanaweza kurejelewa katika shughuli za kileksia (Tumbo na Mwansoko, 1992).

Kadhalika, utafiti wa kina katika istilahi mkopo za Kibantu na lugha nyinginezo zisizo za Kibantu unahitajika ili 'kubukua' istilahi zinazohitajika katika Kiswahili. Mfano zaidi wa istilahi za namna hii ni:

(58b) **itale** - Kisukuma

**fuwele** - Kizigua

**kola** - Kiibo

**ngalemo** - Kimaasai

**rara** - Kiyoruba

**mlulu** - Kipare

Tumbo na Mwansoko (1992:37) wanadai kuwa:

> ... **istilahi za Kibantu huepukwa kwa sababu ya uvulivuli wake kwa watumiaji wasio wazungumzaji wa lugha chasili za istilahi hizo.** Hii ni kwa sababu maumbo ya kimsingi ya maneno ya Kibantu-mamà yameshabadilika sana kiasi cha kwamba si rahisi tena kugundua ukaribiano wake.

Kauli ya wataalam hawa inahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina. Iwapo ukweli kwamba Kiswahili ni Kibantu haupingiki, ni vigumu kuelewa chanzo cha "**uvulivuli**" (ikiwa upo) wa istilahi za Kibantu, hasa 'uvulivuli' huo ukilinganishwa na istilahi mkopo za kigeni zinazopendelewa na wanaisimu hawa (ibid, 1992:26). **Uvulivuli** wa kuelewa istilahi si kigezo muhimu cha ufaafu wake. Muhimu ni "usayansi" wa istilahi na mbinu za uundaji istilahi zenye upeo wa juu wa ubora, suala ambalo wataalam hawa hawakulizingatia.

#### 4.8.4.5 Ukopaji kutoka Lahaja za Kiswahili

Hiki ni chanzo kingine cha istilahi za Kiswahili. Lahaja za Kiswahili (ni 15 au zaidi) hutoa mchango mkubwa katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili, kutokana na uelewano lugha, na ukaribiano mkubwa wa kimuundo baina yake na Kiswahili sanifu.

Kuhusu suala hili, Mukhwana (1988:61) yuasema:

> Kiswahili ni lugha na ikiwa haina msamiati wa kutajia kifaa jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua katika lahaja zote za lugha hii...ikiwa kwa bahati nzuri mojawapo ya lahaja za Kiswahili ina neno la kutajia kifaa hicho na lichukuliwe mara moja.

Naye Mdee (1986:125) anadai kwamba kuna istilahi za kilahaja ambazo zipo za kuweza kueleza dhana kadhaa, lakini watu wengi hawazijui kwa ajili ya athari ya istilahi za kigeni. Kauli za wataalam hawa zina mashiko. Kutopekuapekua miongoni mwa Waswahili wenyewe na kudurusi lahaja za Kiswahili kumewafanya wanalugha wa Kiswahili kuunda ama kukopa istilahi nyingi sana za kigeni pasipo na haja yoyote. Pale ambapo hatuwezi kupata istilahi faafu kutoka katika Kiswahili chenyewe na lugha za Kibantu, tunapendekeza 'tubuni' istilahi mpya kwa kuzingatia misingi ya kisayansi (rejelea 3.3.2, uk. 64).

Kama ilivyotajwa mbeleni (taz. 1.5, uk. 6), madai kwamba lahaja nyingi za Kiswahili bado hazijafanyiwa utafiti wa kutosha wa kileksikografia (Khamisi, 1986:5; Dunn, 1985:38; Mwansoko, 1989:163, 1990:96; Tumbo na Mwansoko, 1992:92), ambao ungeziwezesha kuchangia kikamilifu katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili, hayana uzito na yanapaswa kurekebishwa. Utafiti wa

kileksikografia uliofanywa na Nabhany (1978, 1982) katika lahaja za Kiamu, Kipate, Kisiu na Kitikuu "ambazo ndizo zilizokuwa na msamiati mkubwa kabla ya lugha za kigeni kukiathiri Kiswahili" ni wa kuridhisha kufikia sasa. Wanalugha wengine ambao utafiti wao katika istilahi za kilahaja za Kiswahili ni muhimu na haupaswi kupuuzwa ni Mdee (1980, 1986), Mukhwana (1988) na wa Mutiso (1992).

Nabhany, kwa wale wanaomfahamu, ni miongoni mwa wanalugha wa Kiswahili ambao msimamo wao unatetea uendelezaji wa Kiswahili kutokana na lahaja za Kiswahili. Mtaalam huyu amekusanya istilahi za kilahaja ambazo hazikufikiriwa katika Kiswahili sanifu.

Baadhi ya mifano ya istilahi za kilahaja ni:

**(59)**

| | | |
|---|---|---|
| (59a) | **uhumbe** | - bayolojia |
| | **mwao** | - oksijeni |
| | **uyoo** | - picha |
| | **fumo** | - mkuki |
| | **ngulizi** | - chifu. |

(taz. Nabhany, 1978 katika *Kandi ya Kiswahili*)

Ni kutokana na utafiti wa kileksikografia katika lahaja za Kiswahili ndipo wa Mutiso (1992) amekusanya msamiati wa kilahaja ufuatao:

| | | |
|---|---|---|
| (59b) | **sono** | - mapumziko |
| | **togo** | - sifa |
| | **nazaa** | - aibu |

**mwaro** - pwani

**sururi** - furaha

Mifano zaidi ya kilahaja:

(59c) **kidole** (Kiunguja)

**chanda** (Kimvita)

**kijaa** (Kiamu)

**kinwe** (Kitikuu)

(59d) **sinya** - neno la Kimijikenda

Haya ni maneno machache tu ya kilahaja. Yako mengi sana ambayo hayakufikiriwa katika Kiswahili sanifu, na kuyapata kwake ni kwa njia ya utafiti wa kina zaidi.

Sisi, ingawa tunaelewa kwamba watetezi wa ukopaji wa istilahi kutoka Kiingereza wana sababu zao za kushikilia msimamo wao, ni maoni yetu kwamba uendelezaji wa istilahi kutokana na lahaja za Kiswahili na lugha za Kibantu ni zalishi. Vilevile, utaratibu huu ndio unaofaa kuteuliwa pale ambapo hatuwezi kupata istilahi mwafaka katika lugha hii ya Kiswahili. Labda hoja hii itaeleweka zaidi tukijadili matatizo anuai ya ukopaji kutoka lugha ya Kiingereza.

### 4.8.5 Matatizo ya Ukopaji kutoka Kiingereza

Suala la matatizo ya istilahi mkopo kutoka Kiingereza limetajwa na wataalam wa awali (k.v. Tumbo-Masabo, 1990; Mdee, 1983; Kiingi, 1989, 1997; Chuwa, 1988; na Massamba, 1996) kwa juujuu, bila kujadili kwa kina chanzo na suluhisho la kudumu la matatizo hayo. Kama tulivyodokeza mwanzoni mwa tasnifu hii, chanzo cha

matatizo ya istilahi mkopo zilizokopwa kutoka sio tu Kiingereza, au Kigiritini, au Kiarabu, ni ukosefu wa misingi mahususi ya kisayansi ya kuundia na kusanifisha istilahi mkopo. Uchunguzi wa kina wa suala hili ni muhimu na utasaidia kuonyesha bayana hali halisi ya misingi iliyopo ya uasilishaji wa istilahi mkopo toka lugha za kigeni, hususani, ya Kiingereza. Misingi ya kisayansi inayotumiwa kwa sasa kuundia na kusanifisha istilahi mkopo toka Kiingereza zinakanganya, ni za jumlajumla. Labda hii ndio maana shughuli za kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili hazijakomaa, na istilahi nyingi mkopo zinazoundwa haziwaridhishi walengwa wake (Mdee, 1983; Kiingi, 1989).

Baadhi ya matatizo hayajapatiwa suluhisho la kudumu na BAKITA ama ufumbuzi. Mathalani:

(i) Je, istilahi mkopo zitamkwe vipi?

(ii) Je, istilahi mkopo kutoka Kiingereza ziandikwe vipi?

(iii) Je, mpangilio upi wa maneno ni sahihi kwa istilahi hizi?

(iv) Je, viambishi na maumbo unganifu ya kisayansi yashughulikiwe vipi?

Kabla ya kujadili matatizo haya kwa mapana na marefu yake, ni muhimu isisitizwe hapa kwamba maswala ya namna hii hayafungamani na Kiingereza tu bali pia yanajitokeza kwa istilahi mkopo kutoka lugha nyingine za kigeni. Kwa hivyo, kabla ya kuteua lugha changizi yoyote, ni vyema BAKITA kutafuta majibu thabiti ya masuala haya, la sivyo kiu ya watumiaji wa istilahi haitawaishia na usawazishaji wa kuridhisha wa istilahi mkopo hautapatikana.

#### 4.8.5.1 Usawazishaji Istilahi Mkopo Kimfumosauti

Suala la utamkaji wa istilahi mkopo toka Kiingereza limekuwa likiwakanganya wanalugha wa Kiswahili kwa muda mrefu. Je, istilahi mkopo zitamkwe kufuatana na matamshi ya Kiingereza sanifu, au kufuatana na matamshi ya Kiingereza kama walivyoyasikia na kuyamudu Waswahili?, au kufuatana na matamshi ya Kiswahli sanifu?

Yaelekea kwamba Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) (Tanzania), ambalo ndilo shirika linalounganisha mashirika mengine yanayojishughulisha na ustawishaji wa Kiswahili, limeshindwa kutoa agizo rasmi kwa waundaji istilahi wote wazingatie utamkaji upi wa istilahi. Ilivyo sasa ni mchanganyiko tu wa matamshi. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) yaonekana kwamba haisaidii kurekebisha hali hii. Hadi sasa, chombo hiki hakijakata shauri jinsi ya kutamka istilahi mkopo toka Kiingereza.

Kwa mfano, wapo wanaosema:

(60a) *"ion"* - **ayoni** (BAKITA)
- ioni (TUKI)

(60b) *"chamber"* - chamba (BAKITA)
- chemba (TUKI)

(60c) **ai sotupu** au **i sotupu**

(60d) **kosini** au **kosaini** (matamshi ya Kiingereza)

(60e) **jometri** au **jiometri**

(60f) **leksimi** au **leksimu**

Wakipendekeza suluhisho la tatizo hili, Tumbo-Masabo na Mwansoko

(1992:27) wamedahili kwamba istilahi zote kutoka Kiingereza sharti zisawazishwe kulingana na mfumo sauti wa Kiswahili kwa:

(1). Kuongeza vokali tamati kwenye istilahi zinazoishia na konsonanti k.m.

*"nominal"* - **nomino** (-irabu 'o' imeongezwa)

*"adverb"* - **advebo**

*"nasal:* - **nazali**

(2). Kuipangua mifuatano ya konsonati iliyo migumu kutamkika katika Kiswahili kwa kuigiza irabu kati yake k.m.

*"lexical"* - **leksika**

(3). Kuziwekea istilahi mkazo kwenye silabi zake za pili kutoka mwisho kila inapowezekana kufanya hivyo (au istilahi ziendelee kuwekewa mkazo kama ilivyo kwenye lugha chasili).

Tunakubaliana na wanalugha hawa kwamba iwapo konsonanti tamati ni /f/, /v/, /m/, /p/ au /b/, basi na ifuatiwe na irabu /u/ na konsonanti tamati zilizobakia zifuatiwe na irabu /i/, kwa sababu ya uwiano wa sauti au kuathiriana kwa konsonanti na irabu zilizo karibu yake. Mifano:

**alomofu**

**frikwensi**

4.8.5.2 Tahijia

Mtindo wa kuendeleza istilahi mkopo kwa kutumia herufi zinazowakilisha sauti zinazounda istilahi hizo (tahijia), ni suala lingine ambalo limewahangaisha na kuwakanganya waundaji istilahi za Kiswahili na halijatatuliwa bado (Kiango, 1996:78).

Katika **Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi** wa BAKITA (1990:9) inashauriwa kamba istilahi mkopo ziandikwe kwa namna tatu:

(1). Kufuatana na matamshi ya Kiingereza ya istilahi hizo kama yanavyosikika na mzungumzaji wa Kiswahili. Kwa mfano;

(61a) **alufabeti**

**thesaurusi**

**antroponimia**

(2). Kufuatana na maandishi ya Kiingereza ya istilahi hizo... Mathalani:

(61b) **alfabeti**

**fomula**

**tezauri**

**antoponemia** (BAKITA Tol.4.11)

(3). Kufuatana na matamshi na pia maandishi ya Kiingereza ya istilahi hiyo kama mfano huu unavyothibitisha:

(61c) **alufabiti** (matamshi ya Kiingereza ya /ph/ kama f katika Kiswahili).

**thesaurasi.**

**fomiula.**

**antoponimia.**

Ushauri huu wa BAKITA unakanganya. Haueleze ni lini istilahi mkopo toka Kiingereza zifuate matamshi ya Kiingereza au lini zifuate maandishi ya lugha hiyo, na lini ifuate mchanganyiko wa matamshi na maandishi ya lugha hiyo. Matokeo ni kwamba hapana usawazishji mzuri wa istilahi mkopo na, hivyo basi, sifa mojawapo muhimu ya istilahi faafu ya **utaratibu uliosawa** inaelekea kupuuzwa kutokana na mchanganyiko huu. Ndiposa Mbaabu (1991:119) haoni sababu ya kuazima neno **globe** la Kiingereza na kuliandika **glopu.**

Yafaa, kwa maoni ya Mbaabu, neno sanifu liwe **globu**. Uasilishaji wa "*phonology*" katika Kiswahili kama **fonologia** na/au **fonolojia** (Gibbe, 1981:4) unadhihirisha 'mchanganyiko maalum' uliopo, na unaopaswa kukomeshwa na chombo cha kusanifisha na kukuza istilahi cha BAKITA. Chombo hiki kinapaswa kutoa uamuzi wa kutumia mtindo mmoja wa kuziandika istilahi za namna hii (ni fonolojia, au fonologia, au ni sarufisauti/umbo-sauti!). Inapendekezwa hapa kuwa mtindo mmoja ukichaguliwa, basi ufuatwe huo huo tu.

Utafiti wa Mwansoko (1990) ulidhihirisha kupendelewa kwa istilahi mkopo za Kiingereza zilizoandikwa kufuatana na matamshi yake ya Kiingereza (mtindo wa 1), kama yanavyosikika na 'Waswahili' (taz. pia Mwansoko, 1989c:9-10 na 1992:29 kwa maelezo zaidi). Ukopaji istilahi wa namna hii tayari unafuatwa katika lugha nyingine zinazoendelea; mathalani, Kibahasa Malaysia na Kibahasa Indonesia (Omar na Noor, 1981:90), kama mfano huu hapa unavyotuonyesha:

"*gravity*"===**graviti**

"*hydrogeology*"===**hidrogeologi** (taz. Alisjahbana, 1976).

Pendekezo kwamba istilahi mkopo kutoka Kiingereza ziingizwe kwenye Kiswahili kufuatana na matamshi yake ya Kiingereza ni mwafaka. Endapo waundaji istilahi watazingatia mtindo huu mmoja (*data* = data na sio "deta" au "deita"), kama ni lazima ukopaji ufanywe katika uendelezaji wa istilahi, 'mkanganyiko' utapungua na istilahi zenyewe zitakuwa na ukubalifu mkubwa wa kimataifa kwa walengwa.

#### 4.8.5.3 Ukopaji wa Viambishi

Viambishi, kama mofimu ambazo hupachikwa kabla, katikati au baada ya mzizi, ni vijenzi muhimu vya istilahi. Viambishi vya kiistilahi hubeba maana maalum za kisemantiki. Katika Kiswahili, viambishi vya mkopo mara nyingi hutokana na Kigiritini. Suala hapa ni: Je, viambishi vya kisayansi ambavyo ni vingi sana katika Kiingereza vitoholewe, au vipewe visawe mahsusi vya Kiswahili? Baada ya kutambua kwamba hakuna utaratibu maalumu unaofuatwa, Kiingi (1989:173) anapendekeza kwamba viambishi vya kiistilahi vipewe visawe vya Kiswahili kutokana na lahaja za Kiswahili (ang. pia Zawawi, 1979:75-117).

Kiingi (1989:175) anadai kuwa unyumbuaji wa viambishi kutokana na lahaja za Kiswahili hautaruhusu ushindani wa mbinu zote mbili (utohoaji na visawe vya Kiswahili). Viambishi vya kilahaja vinavyofaa kutumika katika Kiswahili ni hivi vilivyo katika **(62)**:

(62a) **Ka**

(62b) **jiji-, m-, mji-, ba-, bam-, bamji-, kijiji-**

Kiambishi cha kilahaja katika (62a) **Ka-** kichukuliwe kutika lahaja ya **Kimvita** ilhali viambishi katika (62b) viasilishwe kutokana **Kiunguja**. Uimarishaji wa viambishi utasaidia katika kubuni viambishi faafu vya kimataifa. Viambishi vinavyofaa kutumiwa ni hivi vilivyo katika **(63)**:

**(63)**

| **Viwango vya Ukubwa/ Udogo** | **Ngazi za Kimatumizi** | **Viambishi** | **Mifano** |
|---|---|---|---|
| *exa* | $10^{18}$ | bamji- | **bamjifurushi** |
| *peta-* | $10^{15}$ | bam- | **bamfurushi** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *macromacro-* | *tera-* | $10^{12}$ | ba- | **basanduku** |
| *ultramacro-* | *giga-* | $10^{9}$ | mjiji- | **mjijisanduku** |
| *mega-* | *macro-mega* | $10^{6}$ | mji- | **mjitabu** |
| *maxi-* | *kilo* | $10^{3}$ | m- | **msanduku** |
| *hyper-* | *hecto-* | $10^{2}$ | ji- jiji- | **jijitu** |
| *super-* | *hyper-deca* | $10^{1}$ | ji | **jigoma** |
| *sub-* | *hypo-deci* | $10^{-1}$ | ki- kiji | **kijitabu** |
| *infra-* | *centi-* | $10^{-2}$ | ki- kijiji- | **kijijitabu** |
| *mini-* | *milli-* | $10^{-3}$ | ka- | **kageli** *(cohortus)* |
| | *micro-* | $10^{-6}$ | kaji- | **kajigeli** *(sub-cohortus)* |
| *ultramacro-* | *nano-* | $10^{-9}$ | kajiji- | **kajijigeli** *(infra-cohortus)* |

(taz. Kiingi, 1989:173-179).

Kwa msingi huu wa unyambuaji wa viambishi vya kilahaja, na vya lugha za Kibantu, Kiingi amependekeza chombo cha BAKITA kikubali matumizi ya **jiji-** ambapo kwa mfano:

*"superclassis"*===**geli**

*"subclassis"*===**kigeli**

*"infraclassis"*===**kijigeli**

*"supercohortus"*===**kijijigeli**

Mifano zaidi:

*genus*===**ndugu**

*subgenus*===**kidugu**

*infragenus*===**kijidugu**

*infratribus*===**kajijizazi**

(taz. pia Zawawi, 1979:75-117).

Maelezo haya ya Kiingi yana mashiko katika uundaji wa istilahi kwa sababu yanapelekea kwenye ulinganifu wa istilahi zinazowakilisha dhana zinazokaribiana kimaana, au zinazotokana na shina moja la neno. Istilahi mkopo zinapoundwa kwa mfungamano wa kidhana huleta usawazishaji mzuri unaowaridhisha walengwa wake (Tumbo, 1990).

Katika Kiswahili, baadhi ya viambishi mkopo vimepatikana visawe vyake mahsusi vya lugha hii. Kwa mfano:

(64)

| **Element ya kitajwa** | **Usanifishaji wa BAKITA** | **Usanifishaji wa TUKI** | **Mifano** |
|---|---|---|---|
| *-ium* | -iamu/ia | -i/-iumu | **americi/americium** |
| *-ate* | -eti | -ati/-ate | **kabohidrate** |
| *-one* | -oni | -oni | **toni** *(tone)* |
| *-ene* | -ini | -ene | **karotene** *(carotene)* |
| *-ose* | -osi | -ose/-osi | **maltosi** |
| *-ide* | -aidi | -idi | **nitridi** |
| *-ase* | -esi | -ase | **anafase/sukresi** |
| *-geo* | -jo | -jio | **jiografia/ jografia** |
| *-ism* | -u | -ua/zimu | **umalapropu/ sitoplazimu** |
| *-ics* | -ia | -ia/i | **fonetiki** |
| *-logy* | -jia | -jia/ia | **fonolojia** |
| *-ist* | -m-, mwana | -mwana | **mwanaisimu** |
| *-epi* | -nje | -nje ya | **ngozi ya nje** *(epidermis)* |
| *-dermis* | -ngozi | -ngozi | **ngozinje** *(epidermis)* |
| *-ecto* | -ekto | -nje | **eteseli nje** *(ectoplasm)* |

| | | | |
|---|---|---|---|
| *-derm* | -demi | -demi | **ektodemi** |
| *-u* | -yu | -u/yu | **nyutroni** *(neutron)* |
| *-eme* | -imu | -imu | **leksimu/glosimu** |

Ili ukopaji kutoka lugha za kigeni upunguzwe ama 'uishe kabisa' kuna haja ya waundaji istilahi kufikiria zaidi na kuwa wabunifu katika shughuli zao za kuendeleza viambishi vya Kiswahili. Ikiwa hapana tofauti za kidhana kati ya *-derm* na *-dermis*,

na *-dermis* ni **ngozi**

*-epidermis* ni **ngozi nje**

*-ectoplasm* ni **uteseli nje**, basi ukopaji wa viambishi katika Kiingereza na utohoaji wake umefanywa bila sababu maalum.

La muhimu ni viambishi vya kisayansi na vya kiisimu kutafutiwa visawe vyake vya Kiswahili. Pendekezo la Gibbe (1981) kwamba istilahi zote zinazobeba dhana ya "taaluma ya" (study of) au kiambishi **"ics"** ziandikwe kwa **"-ia"** (k.m. **fonetikia** 'phonetics', **akustikia** 'acoustics', **fonemikia** 'phonemics') linahitaji uchunguzi wa kina kabla ya kukataliwa na BAKITA na watumiaji wa Kiswahili. Huenda hii ni harakati ambayo itasaidia katika kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili kwa mwelekeo mmoja, kwa utaratibu ulio sawa, na kwa namna hii kutokomeza vurugu katika istilahi za isimu ya Kiswahili.

**(65)**

| | |
|---|---|
| *"catenation"* | **ukufu** |
| *"recursiveness"* | **uchamko** |
| *"bilingual"* | **wingilugha/ulumbi** |
| *"stops"* | **vikatizwaji/vizuiwa** |

*"glottal:* **nyuzi za glota/nyuzisauti**

ni jaribio zuri la iktisadi na upunguzaji wa ukopaji.

#### 4.8.5.4 Mpangilio wa Istilahi Mkopo Zenye Maneno Ambatani

Tatizo la mpangilio wa istilahi mkopo kutoka Kiingereza zenye maneno zaidi ya moja linaelekea kutatuliwa na BAKITA. Chombo hiki cha kuendeleza Kiswahili kimetoa agizo rasmi, kwa waundaji istilahi za Kiswahili, kwamba utohozi wa namna hii uzingatie mpangilio wa maneno **kulingana na sarufi ya Kiswahili**; yaani, vivumishi vifuate majina.

Kabla ya agizo hili rasmi kutolewa, watumiaji wa Kiswahili pamoja na wataalam wa lugha hii walitatizika katika upangaji wa istilahi mkopo kutoka Kiingereza (Tumbo na Mwansoko, 1992). Suala lililoshughulikiwa ni: Je, maneno yanayounda istilahi hizi yapangwe:

1. Kufuatana na sarufi ya Kiingereza, au
2. Kufuatana na sarufi ya Kiswahili?

Yaani istilahi iandikwe kama (66) inavyoonyesha:

**(66)**

**sodiamu kloraidi** *"sodium chloride"* au **natiri kloridi?**

Kifaransa *"chlorure de sodium"*?

Kijerumani *"Natriumchlorid"*?

Walengwa wa Kiswahili watapendelea istilahi hizi ziandikwe kama (67) badala ya (66).

**(67)**

(67a) **kloridi ya natiri** (**kloridi** ambayo ina **natiri** ndani

yake)

(67b) **asidi askobiki**

(67c) **oksidi nitrasi**

(67d) **kloridi ya ioni** (taz. Abdulaziz, 1985).

Kama tulivyofahamishwa na wataalam wa BAKITA wenyewe, kauli thabiti na agizo rasmi limetolewa tayari kwa waundaji istilahi, kwa hivyo, aina zote mbili za mpangilio wa maneno hazifai kuendelea kutumika kwenye Kiswahili cha kitaaluma.

Kuwepo kwa matatizo haya na mengine mengi katika ukopaji wa istilahi kutoka Kiingereza kunaupunguzia nguvu mfanyiko huu na kuweka wazi udhaifu wake. Massamba (1996:91-2) anapendekeza misingi ya uteuzi wa lugha changizi na uundaji istilahi ifuatayo:

1. Kiswahili chenyewe (lugha pokezi yenyewe)
2. Lugha za Kibantu (au lugha zinazokaribiana na lugha pokezi)
3. Lugha nyingine za Kiafrika na ambazo zinakaribiana na lugha za Kibantu.
4. Istilahi mwafaka zikikosekana katika 1-3 uasilishaji wa istilahi ufanywe kutoka lugha azali changizi.
5. Istilahi zilizoasilishwa sharti zizingatie mfumo wa kimofolojia na kifonolojia wa Kiswahili.

Misingi hii (1-3) inatumiwa na lugha nyingi duniani kuendeleza istilahi za sayansi na teknolojia. Mfano wa lugha hizi ni Kinyarwanda, Kichina (Pasierbsky 1989), Kimalagasy, Kiamhariki na Kihibrania (Rabin 1989). Ili kuepukana na 'uvulivuli' wa istilahi mkopo kwa walengwa wasioelewa lugha changizi za istilahi hizo, tunapendekeza kuwa ukopaji wa istilahi za kigeni utekelezwe

tu kama hatua ya mwisho (Ohly 1977). Misingi ya kisayansi ya uundaji istilahi zenye ukubalifu wa kimataifa iwaongoze waundaji binafsi na vyombo vya BAKITA, BAKIKE na TUKI katika harakati zao za kukuza lugha hii. Ni kwa kufanya hivyo ndipo maneno kama vile 'istilahi nguvu', 'visawe vya kiistilahi' au **"istilahi zenye uvulivuli"** yatasahaulika, na mahali pake kuchukuliwa na **istilahi faafu** na **zenye usayansi** za Kiswahili, hususani za isimu.

### 4.8.6 Taratibu za Ukopaji

Azma ya kipengele hiki ni kuonyesha taratibu zinazotumiwa katika ukopaji wa istilahi kutoka lugha za kigeni. Hii inatokana na ukweli kwamba lugha zinapokutana hukopeshana istilahi, hasa pale ambapo hapana neno mwafaka, au linaloweza kuundwa kwa urahisi la kuwakilisha dhana mpya. Mada hii imekwisha zungumziwa na wanaisimu na wanalugha wengi kama vile Zgusta (1971), Kitsao (1980), Irira (1982, 1990), Felber (1984), Temu (1984), Mdee (1986), na Kiingi (1989). Wako wataalam wengine ambao hawakutajwa hapa ambao wamechangia mada hii kwa namna moja au nyengine.

Tasnifu hii inajaribu kuelezea kwa kirefu na kwa njia nyepesi miongozo iliyotolewa kwenye kazi zilizotangulia, ili mifanyiko na taratibu za ukopaji zieleweke kwa urahisi. Felber (1984:176) anatambua kuweko kwa taratibu mbili kuu za ukopaji wa istilahi kutoka lugha za kigeni. Nazo ni:

1. Utohoaji.
2. Kaleki (tafsiri sisisi).

#### 4.8.6.1 Utohoaji

Mukhwana (1988:62) anaeleza utohoaji kama:

> namna ya kuunda majina hivi kwamba maneno ya lugha changizi yanafuata muundo wa lugha pokezi.

Katika kazi hii tunachukulia 'utohoaji' kama mfanyiko wa kuendeleza istilahi ambapo neno linachukuliwa kutoka lugha moja na kuingizwa katika lugha nyingine, **baada ya kufanyiwa marekebisho ili lilingane na tabia na muundo wa maneno ya lugha pokezi.** Ni aina na/au utaratibu wa ukopaji unaosisitiza **uswahilishaji wa istilahi mkopo ili uafikiane na muundo wa lugha pokezi (Kiswahili) kifonolojia na kimofolojia.**

Kuhusu suala hili, Temu (1984:117) anadokeza kuwa:

> Maneno yanapokopwa **yaswahilishwe** ili yafuate fonolojia ya Kiswahili lakini maana haina budi kubakia kama ilivyokuwa katika lugha changizi... utaratibu huu ndio kwa sasa **zalishi zaidi** hasa katika mwanda wa sayansi.

Iwapo ni kweli kwamba mbinu ya utohoaji ni "zalishi" katika kuunda istilahi za Kiswahili, kama anavyodai Temu, basi na utohoaji huo hauna budi kufanywa kwa mfumo maalum na sio kiholela. Ni vyema ukifanywa kwa utaratibu ambao utazifanya istilahi mkopo zenye ruwaza fulani kutoholewa kwa njia iliyo bayana. Hali halisi ilivyo kwa sasa ni kwamba wanalugha wa Kiswahili na chombo cha BAKITA wameshindwa kuunda sera ya utohoaji, hasa jinsi ya kutohoa (Mdee, 1986:119). Istilahi za isimu ya Kiswahili zinazoundwa kwa utohoaji hazina budi kufuata utaratibu maalum, ulio sawa na unaozingatia mwelekeo wa matamshi (taz. mfano wa 13, uk. 75).

Iwapo, kwa mfano, chombo cha TUKI (1990) wanakubaliana kuwa:

(68)

*epistemology* ni **epistemolojia**

*epigraphy* ni **epigrafia**

*epicene* ni **episini**

tunadadisi kuwa:

*epi*===epi

-*gy*===jia

-*phy*===fia

-*c*===s

-*ene*===ini (TUKI, 1990:24).

Basi itakuwaje,

(69)

*epithet*===**kivumishanomino**

*epiglotis*===**kidakatonge**?

Ile dhana ya *"epi"* ambayo inakaririwa katika (68) haipo katika seti ya (69). Wanaleksikografia wa Kiswahili watahitajika kuamua mfumo maalum wa kukabiliana na mbinu ya utohoaji iwapo ni 'zalishi' na ina umuhimu kwao, umuhimu ambao labda sisi hatuuoni.

Irira (1990:9), katika mada "Ubadilishaji maandishi," hakosei anapodokeza kuwa utohoaji wa maneno ya Kiingereza huzingatia mwelekeo wa matamshi "hivi kwamba katika Kiswahili matumizi ya herufi Q au q (kiu) na X au x (eksi) hayapo: Kwa hivyo **q** huwakilishwa na **k** na **x** huwakilishwa na eksi."

Katika istilahi za Kiingereza zilizowahi kutoholewa, kuna mwelekeo ufuatao:

**c-** kuwa **k** (*coronal*/korona, *calque*/kaleki)

**-ck-** kuwa **k** (*packet*/pakiti)

**-nce** kuwa **nsi** (*consonance*/konsonansi)

**-nt** kuwa **nti** (*consonant*/konsonanti)

**-g** kuwa **j** (*geography*/jiografia)

**ph-** kuwa **f** (*phonemic*/fonemiki)

**-ter** kuwa **ta** (*meter*/meta)

(taz. Irira, 1990:9)

Iwapo 'mwelekeo' huu kweli upo katika istilahi mkopo kutoka Kiingereza, basi istilahi za isimu ya Kiswahili zifuatazo (70) zinahitaji kufanyiwa usahihisho, kwa sababu utohoaji umefanywa usiohitajika:

**(70)**

*"glottis"*===**glota**

*"glottal"*===**glota**

*"glottopolitics"*===**siasalugha**

Utohoaji wa aina mbalimbali hutumika katika isimu ya Kiswahili. Kwa mfano kuna:

(a) **istilahi** kama ilivyofanywa kwa maneno ya Kiingereza: **hiponomi** *(hyponym)*, **homografu** *(homograph)*, **leksisi** *(lexis)*, **fezi** *(phase)*.

(b) **tafsiri maana** kama ilivyofanyika kwa istilahi kama: **kani** *(force)*, **nguvu** *(power)*, **ubuye** *(opacity)*, **buye** *(opaque)*.

(c) **shina la istilahi ya kigeni** na kuliongezea au kupunguza

viambishi vya Kiswahili au maumbo unganifu kama inavyothibitishwa na mfano (71) ufuatao:

**(71)**

**oks - oksidi, oksidisho, oksidishaji, n.k.**

**nitro - nitrisha, mnitrisho, unitrishaji, nitrifu, nitrati**

Minyambuliko hii imetokana na mashina husianifu ya maneno. Katika kutohoa istilahi ya kigeni, ni muhimu kuelewa etimolojia yake ili utohoaji sahihi ufanywe. Kwa mfano, neno **stesheni** la Kifaransa manake asili ilikuwa 'kituo cha meli,' ilhali sasa hutumika kwa maana ya 'kituo cha gari la moshi.' Kasoro na udhaifu wa utohoaji kutoka lugha kopaji (mtohoo wa mtohoo), ambapo hutokea hatari ya kuingiza ama kuondoa vipengele muhimu katika istilahi iliyotoholewa, zitafafanuliwa kwa mapana baadaye (tazama 5.2.1.6, uk. 304).

#### 4.8.6.2 Kaleki

Katika harakati zao za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, waundaji wa istilahi wamekuwa wakitumia pia utaratibu wa **'kaleki'** au tafsiri sisisi. **'Kaleki'** ni namna ya ukopaji ambapo neno au kirai kutoka lugha moja huhamishwa hadi lugha nyingine kisisisi au mofimu kwa mofimu (Muranga, 1992:11). Ni mfanyiko wa uundaji istilahi unaohusu tafsiri sisisi (tafsiri ya neno kwa neno ya istilahi ya lugha changizi), tafsiri ya wazo au ya maana, na tafsiri ya sauti. Wataalam walioshughulikia mbinu ya kaleki (k.v. Abdulaziz (1989), Mwansoko (1990), Mac William (1985), Catford (1965), Nida (1964), Crystal (1980), Muranga (1992) na Falk Julia

(1973)) wote wanaelekea kuafikiana kwamba mfanyiko huu wa kuendeleza istilahi ni **zalishi** na hutumika kwenye lugha nyingi duniani, k.v. Kirusi, Kijerumani (Falk Julia, 1973), (Kodukov, 1979), Kitaliano (Kramer, 1983), Kiingereza (Bauer, 1983), Luganda (Kiingi, 1989) na Runyankore-Rukiga (Muranga, 1992).

Kuhusu dhana ya kaleki, Falk Julia (1973:41) anasema:

> Kila lugha ina njia nyingi za kupanua au kubadili leksikoni yake. Huku ukopaji ukitawala lugha za Kiingereza na Kiswahili, kwa mfano, Kijerumani kimetumia sana mbinu ya kaleki au tafsiri mkopo-njia ya kuunda istilahi kwa neno linalokopwa kutafsiriwa mofimu kwa mofimu katika lugha linamoingizwa.

Ingawa inaelekea istilahi maalum zinazotokana na kaleki huwa 'faafu' na kwamba hapatokei utata zinapotumika, ni muhimu kukiri pia kwamba utaratibu huu **si zalishi** katika Kiswahili, na ndiyo maana hautumiwi sana (Falk Julia, 1973) na waundaji wa istilahi za lugha hii.

Baadhi ya mifano ya istilahi za kaleki, na lugha kopeshaji (<) ni:

**(72)**

(72a) **Kiingereza:**

*"masterpiece"* < Kijerumani *"meisterstueck"*

*"collaborator"* < Kifaransa *"collaborateur"*

*"adjective"* < Kilatini *"adjectivus"*

*"verb"* < Kilatini *"verbum"* / Kijerumani *"zeitwort"*

(Muranga, 1992:11-23).

(72b) **Kirusi:**

*'ubit Vyjemje'* < Kifaransa *'tuer le temps'* (pitisha muda) (Kodukov, 1979:223-224)

*'Ozivienie ekonomiki'* < Kigiriki *'ozivlenie ekonomika'* (ufufuaji wa uchumi) (Pasierbsky na Opalka, 1977:83).

(72c) **Kitaliano:**

*"luna di miele"* < Kiingereza *'honey moon'*

*'grattacielo'* < Kiingereza *'sky scraper'* (Kramer, 1983:313).

(72d) **Kiarabu:**

*"waqt"* < Kiindonesia *'waktu'* (wakati)

*"ilmu"* < Kiindonesia *'ilmu'* (elimu/sayansi)

*"sabab"* < Kiindonesia *'sebab'* (sababu)

(72e) **Kiindonesia:**

*'polisi'* < Kiholanzi *'politie'* (polisi)

*'sekerup'* < Kijerumani *'schroef'* (skrubu)

*'kartu'* < Kiholanzi *'kaart'* (kadi)

(Pasierbsky na Opalka, 1977:76).

Mbali na lugha hizi, kuna lugha za Kibantu ambazo pia zinaendeleza istilahi zao za isimu kwa mfanyiko wa kaleki au tafsiri mkopo katika kutaka kujieleza zenyewe, hususani katika isimu.

(72f) **Runyankore-Rukiga:**

**"enyaminwa"** < Kiingereza *"labial"*

< Kilatini *"labium"* (midomo)

**"enyankanka"** < Kiingereza *"palatais"* (kaakaa)

[palate===enkanka; **enya**===**ya** (Kiswahili)]

**"amaziina"** < Kiingereza *"nouns"* < Kilatini *"nomen"*

**"enyongyezi"** < Kiingereza *"adjective"*

< Kilatini *"adjectivus"* (kivumisho)

(72g) **Luganda:**

"erinnya erya lukale" < Kijerumani *"gattunsname"* (nomino kawaida)

"nakongezalinnya endazi" < Kijerumani *"hinweisendes Adjektiv"* (kivumishi onyeshi)

(taz. Muranga (1992) katika *Jarida la Idara ya Lugha na Isimu* - Makerere University, K'la uk. 3-23).

Istilahi nyingi za isimu ya Kiswahili zinazoundwa kutokana na mfanyiko wa kaleki hunyopolewa kutoka kwa ruwaza za istilahi za Kiingereza kama mfano (73) unavyodhihirisha:

**(73)**

(73a)

*"organs of speech"* < **ala za matamshi**

*"place of articulation"* < **mahala pa kutamkia**

*"root of tongue"* < **mzizi wa ulimi**

*"tip of tongue"* < **ncha ya ulimi**

*"semantic range"* < **mapana kisemantiki**

*"blade of tongue"* < **bapa la ulimi**

Mpangilio wa istilahi zinazotokana na kaleki huweza kubadilika ili ulingane na kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi. Mfano zaidi wa istilahi za namna hii ni kama ilivyo hapa:

(73b) *"fundamental frequency"* < **frikwensi msingi**

*"elastic limit"* < **ukomo mnyambuko**

(73c) *"horse power"* < **nguvu farasi**

(73d) *"sick leave"* < **likizo ya ugonjwa**

Ni ukweli usiopingika kwamba mbinu ya kaleki ina umuhimu mkubwa, umuhimu ambao umetambuliwa na lugha za Kibantu (k.v. Runyankore-Rukiga, Luganda, Runyakitara), ambazo zimo mbioni kujiendeleza kileksikoni pamoja na kutaka kujieleza zenyewe katika uwanja wa isimu. Hata hivyo, waundaji istilahi za Kiswahili watahitajika kutumia mfanyiko wa tafsiri sisisi kwa makini bila ya kutafsiri 'kiholela' istilahi hizo. Kutofanya hivyo kutakwamiza juhudi zao, na dhana za msingi zilizokuwa katika lugha changizi zitapotea ziingizwapo katika lugha pokezi. Tazama ilivyo 'vigumu' kutafsiri sisisi istilahi zifuatazo (74) hapa:

**(74)**

*"lexicography"*

*"infraphotodensitometer"*

*"hemochromatosis"*

*"bathythermograph"* (taz. Abdulaziz, 1989:40)

"Ugumu" huo huenda ukawaondokea wanalugha wa Kiswahili iwapo watazingatia anavyosema Ruo (1979) kwamba:

> Ndio, viko vitu vya kigeni ambavyo si vya asili ya nchi zetu hizi na hata si vya asili ya Afrika yote. Vitu hivyo hatuna majina yake na ni juu yetu kuvipa majina na kuvitumia kwa majina hayo. **Lakini ni wajibu wetu kuyatafuta kwanza maneno hayo ndani ya Kiswahili...**

Maoni yetu ni kwamba itakuwa vizuri iwapo anayoyasema Ruo yatafuatwa na jitihada zitafanywa kuimarisha mfanyiko wa kaleki unaohusu **tafsiri ya maana** (taz. k.m. *'dorsal'* - **nyuma**, *matrix* - solo) badala ya **tafsiri ya neno kwa neno** *"midwife"* - **mke wa kati** au **tafsiri ya sauti** *"horse power"* - **hosipawa**, *'stress'* - **sitresi**"

(mkazo), *"frequency"* - **frikwensi**, *"constituent"* - 'konstituenti') (TUKI, 1990).

Hadi wakati tulionao, mwelekeo umekuwa kutumia Kiingereza kupata istilahi mkopo zinazaoundwa kutokana na mfanyiko wa kaleki, kwa sababu ya **mazoea** kwa kuwa ndio lugha ya kigeni inayofahamika zaidi miongoni mwa waundaji wa istilahi za Kiswahili. Mtindo huu hauna budi kugeuzwa ili idadi ya istilahi za isimu ya Kiswahili iongezeke kama ilivyo katika lugha nyinginezo (taz. mfano wa 72), pasi na kujifungia kiistilahi katika lugha moja ya Kiingereza.

## 4.9 Muhtasari wa Sura ya Nne

Tumefafanua mbinu zinazotumiwa katika kuendeleza istilahi za Kiswahili. Tumeeleza kuwa mbinu za unyambuaji, uambatanishaji na ufufuaji ni zalishi na huunda istilahi angavu na zinazoeleweka kwa urahisi na walengwa.

Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba mifanyiko ya uradidi, upanuaji wa maana za maneno, na ufupishaji si zalishi, na hakuna taratibu au ruwaza madhubuti zinazofuatwa za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili kwa mbinu hizi. Aidha, katika sura hii, mna sababu za ukopaji wa istilahi za kigeni na pingamizi juu ya ukopaji wa istilahi. Tumedahili, katika tasnifu hii, kuwa uendelezaji wa istilahi za Kiswahili, kwa mfanyiko wa ukopaji, ni kujichimbia kaburi bure manake kunawapunguzia wanaistilahi uwezo wao wa ubunaji.

Kadhalika, kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba hapana dharura yo yote inayowashurutisha wanalugha wa Kiswahili kuunda istilahi mpya ama kutohoa na kukopa za kigeni pale ambapo hakuna istilahi makosa ama haja kuu ya matumizi. Wanahitajika tu kupekuapekua miongoni mwa Waswahili wenyewe na kupata istilahi faafu pale ambapo hapana neno mwafaka. Katika sura hii pia, tumeonyesha misingi ya uteuzi wa lugha changizi pamoja na matatizo ya ukopaji kutoka Kiingereza. Misingi inayotumiwa kuundia istilahi za mkopo kutoka lugha za kigeni imefafanuliwa katika sura hii.

Kwa kifupi, tunatarajia kuwa sura hii itawapa mwanga na kuwafaa watu wote watakaosoma kazi hii, hususani katika kuelewa mbinu za kisayansi za uundaji istilahi bila shida kubwa. Kadhalika, ni matumaini yetu kuwa uelewa wa wasomaji wa kazi hii juu ya uteuzi wa lugha changizi utapanuka zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Pia tunatumaini kuwa sura hii itakuwa mwongozo wa kufanyia utafiti wa baadaye kuhusu ukopaji wa istilahi za kigeni. Inawezekana pia watafiti wa vyombo mbalimbali, pamoja na waundaji istilahi binafsi, watanufaika na mawazo yaliyo katika sura hii. Endapo hoja kadhaa za kimsingi zilizojadiliwa katika sura hii zitazingatiwa na waundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, tunatumai kuwa malalamiko kuhusu 'udhaifu' na ukosefu wa 'usayansi' katika istilahi za isimu yatapungua au yatakwisha, na kazi ya wataalamu hao itakuwa na ufanisi wa kutosha.

Ni imani na matarajio yetu kuwa endapo yaliyojadiliwa katika sura hii yatarejelewa na wapenzi wa Kiswahili, kutakuwepo na mzunguko

mzuri wa istilahi za isimu katika kanda yetu utakaopelekea kwenye kiwango cha juu cha ulinganifu. Aidha, ni matarajio yetu kuwa sura hii itachangia, kwa kiwango fulani, katika kuimarisha istilahi za isimu ya Kiswahili na, hivyo, kuikomaza lugha hii katika medani ya taaluma.

# SURA YA TANO

## TATHMINI YA MBINU ZA KUUNDIA ISTILAHI ZA KISWAHILI

### 5.0 Utangulizi

Uundaji na usambazaji wa istilahi za Kiswahili kwa walengwa mbalimbali umewahi kufanywa na vyombo vya kukuza istilahi (BAKITA, BAKIKE, TUKI) pamwe na wataalamu binafsi (taz. 5.1, uk. 207). Mbinu za ubunaji zilizotumika hazina budi kufanyiwa tathmini ili kujua kama zinazingatia 'usayansi,' na kama mfumo wa sayansi unatumiwa katika ubunaji istilahi za isimu ya Kiswahili. Kulingana na Rubin (1971), tathmini husaidia katika kuchagua mbinu 'bora,' (faafu na ya kisayansi) zaidi kati ya nyingi zilizotumika katika ukuzaji wa lugha. Taarifa zitakazotokana na tathmini ya 'usayansi' katika mbinu za kuendeleza istilahi za Kiswahili, pamoja na kudhihirisha mfanyiko wenye upeo mkubwa wa ubora kati ya mifanyiko mingi inayotumika, pia itatusaidia katika kuonyesha kiwango cha ukubalifu wa istilahi zinazoundwa kwa walengwa (taz. sura ya 6). Mfanyiko bora na wa kisayansi katika uundaji wa istilahi utachukuliwa , kulingana na taarifa za tathmini, kama 'faafu' na ndio utakaopendekezwa utumike katika kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili zenye ukubalifu wa kimataifa.

Baada ya kuchunguza kwa jicho pevu kazi za wataalam mbalimbali walioshughulikia mbinu za ubunaji wa istilahi (taz. 1.1) imedhihirika wazi kwamba kuna usawa katika mitazamo yao, na hivyo kutuacha na mapendekezo **matatu** ya taratibu za kukuza Kiswahili.

Mapendekezo yenyewe yanajitokeza katika kazi na machapisho ya vyombo vya BAKITA, TUKI, BAKIKE, na ya watu binafsi kama vile Nabhany, Kapinga, Chimerah na Mbaabu. Kwa hivyo, katika sura hii, tathmini ya 'usayansi' katika mbinu za uundaji istilahi itafanywa, na tutajikita katika mbinu na mapendekezo ya vyombo hivi viwili, na aidha wataalam watatu tuliowataja. Mbinu ya Nabhany itajumlishwa pamoja na mtazamo wa Chimerah kwa sababu ya uwiano mkubwa uliopo. Vilevile wataalam hawa ni wana-CHAKITA (Chama cha Kiswahili cha Taifa, Kenya), hivyo basi, kuna usawa wa kimtazamo katika mifanyiko yao ya ubunaji istilahi za Kiswahili. Hali kadhalika, mbinu ya Kapinga itajumlishwa pamoja na mtazamo wa Mbaabu kwa sababu ya usawa katika fani ya isimu iliyoshughulikiwa na wanalugha hawa.

## 5.1 Tathmini ya Mbinu za Kuendeleza Istilahi za Kiswahili

Zipo kazi chache zilizoshughulikia tathmini ya mbinu za kuendeleza istilahi na ukubalifu wa istilahi. Mwansoko (1990, 1993) amefanya tathmini ya ukubalifu wa istilahi za isimu na fasihi miongoni mwa wanafunzi wa sekondari, vyuo vya elimu, Chuo Kikuu na walimu wa Chuo Kikuu. Katika utafiti huo, mtaalam huyu alichunguza mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa kubuni istilahi. Hizi ni pamoja na; 'njia zitokanazo na Kiswahili chenyewe,' kama vile:

- Uunganishaji na uambatanishaji wa maneno.
- Unyumbuaji wa maneno.
- Upanuzi wa maana za maneno.
- Uhulutishaji.

Ametathmini pia 'njia zitokanazo na ukopaji, k.v. ukopaji kutoka lahaja na lugha nyinginezo.

Mdee (1980) amefanya tathmini ya ukubalifu wa istilahi za biashara na ofisi katika mji wa Same, mkoani Kilimanjaro. Mbinu za uundaji wa istilahi zilizoshughulikiwa na Mdee (ibid) ni:

- Uasilishaji wa maneno mkopo na Uswahilishaji wake.
- Uasilishaji kutoka lugha za Kiafrika.
- Uundaji wa istilahi mpya kwa mfanyiko wa akronimu na ufupishaji.
- Unyambuaji.

Naye Sewangi (1996) amefanya tathmini ya ukubalifu wa istilahi za ufundi wa matrekta/magari zilizoundwa na TUKI mwaka wa 1986 katika kiwanda cha kuunganishia matrekta aina ya Valmet, kilichoko Kibaha (Pwani) na katika jiji la Dar es Salaam. Sewangi (ibid) alitumia mifanyiko mitatu ifuatayo:

- Ukopaji.
- Tafsiri.
- Ukopaji na tafsiri.

Kazi hii, kama tulivyodokeza mbeleni, inahusu tathmini ya 'usayansi' katika mbinu za ubunaji istilahi za isimu ya Kiswahili. Mbinu zitakazochunguzwa hapa ni pamoja na:

- Mbinu na vyombo vya BAKITA na TUKI,
- Mbinu za BAKIKE/Nabhany, CHAKITA/Chimerah, na
- Mbinu za Kapinga na Mbaabu.

### 5.1.1 Vyombo vya Ukuzaji wa Kiswahili

Kutokana na sera ya lugha ya nchi fulani, uendelezaji wa istilahi hupangwa na baraza la lugha au taasisi nyingine za serikali. Mojawapo ya kazi muhimu za kukuza lugha ambayo haijaendelea katika nyanja za kisayansi na kiteknolojia ni kuiundia istilahi mpya (taz. Tumbo, 1982). Wataalam wengine (Akida, 1983; Massamba 1986, 1989) wanaainisha uendelezaji wa istilahi za kisayansi na kiteknolojia za Kiswahili katika makundi mawili: **Njia rasmi** na **njia zisizo rasmi.** Katika kikundi cha **njia rasmi,** zimeainishwa harakati za mashirika tu ambayo yamepewa jukumu hili la ukuzaji wa istilahi na serikali, yaani kisheria. Nchini Tanzania, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limepewa jukumu kubwa la kukikuza na kukiimarisha Kiswahili kwa sheria za Bunge (kirasmi) za mwaka wa 1967. Vitendo vyote vingine kuhusu ukuzaji wa istilahi, mathalani vinavyotokana na Taasisi za Elimu au Idara za Vyuo Vikuu na wataalam binafsi wanaounda istilahi, vinaitwa **njia zisizo rasmi.**

Ni jambo lisilozusha ubishi kwamba si lazima taifa liwe na chombo rasmi cha kukuza istilahi ili istilahi zibuniwe. Nchi nyingi hazina chombo kama hicho, lakini bado zina vyombo vingine ambavyo vina mawiano thabiti ya kuendeleza lugha. Kwa mfano, katika Uganda hakuna chombo rasmi cha kukuza Kiswahili na, hivyo basi, kazi hiyo inaendelezwa na Chuo Kikuu cha Makerere, Chuo Kikuu cha Uisilamu cha Mbale, Baraza la Taifa la Mitihani, Redio na Runinga. Ndiposa Mukama (1989:11) hakosei anaposema:

> ...na tuna matumaini makubwa kwamba wapenzi wa uendelezaji na ukuzaji wa lugha za Kiafrika duniani watatuauni (kifedha) ili jitihadi zetu za kibinafsi mintarafu ya lugha ya Kiswahili zipate ufanisi.

Nchini Kenya, kuna chombo kisicho rasmi cha kukuza Kiswahili. Chombo hiki, Baraza la Kiswahili Kenya (BAKIKE), kama tutakavyoeleza baadaye, kinaelekea hakitekelezi wajibu wake wa kukuza Kiswahili kwa sababu ya ukosefu wa fedha na uongozi thabiti, hasa baada ya kifo cha aliyekuwa mwenyekiti, marehemu Abdalla Mohamed Lamy.

Hali iliyo nchini Kenya ni kwamba kuna ukuzaji 'huria' wa istilahi za Kiswahili; yaani hakuna mpango wa baraza la Kiswahili wala taasisi nyingine za serikali (au mpango wa 'kutoka juu'). Uchunguzi wa Krozewski na Wenzake (1986:46) unaunga mkono 'ukuzaji huria' wa lugha, kwamba ndio msingi wa kubuni istilahi za kitaaluma, mradi tu pawepo na data iliyoidhinishwa na kutathminiwa na taasisi rasmi.

Imefafanuliwa (Ohly, 1976) kuwa, katika Tanzania, wanaoshughulikia ukuzaji wa istilahi wanaweza kugawanywa katika vikundi vitatu: Kikundi kimoja ni kile kinachochukua mashina ya Kiswahili chenyewe kama msingi wa kujenga istilahi mpya; nacho kinaitwa 'Shule ya Tanga,' na kinawakilishwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). TUKI ni chombo kingine cha kuendeleza Kiswahili katika Tanzania, hasa katika mwanda wa kiakademia. Kingine, kinachojulikana kama 'Shule ya Zanzibar,' kinapendelea zaidi matumizi ya istilahi mkopo katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili. Kikundi cha tatu ni kile

kinachochanganya mitindo miwili hiyo ya Tanga na Zanzibar. Ohly hakueleza kwamba kuna na kikundi cha 'kinadharia' tu kinachokuza istilahi kwa kukopa maneno ya lugha nyingine za kienyeji zinazotumiwa Tanzania (Maina 1989:116). Kikundi cha tatu kinachochanganya mitindo miwili ni cha 'kinadharia' na kinawakilishwa na BAKITA.

#### 5.1.1.1 Chombo cha Kukuza Istilahi cha BAKITA

Historia, malengo, na kazi ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni masuala ambayo yamejadiliwa na wanaisimu na wanalugha wengi wanaotajika (Maina, 1977; Khamisi, 1980; Tumbo, 1982; Ridder, 1988; Massamba, 1989; Hamad, 1989; Mwansoko, 1991; Mbaabu, 1991). Hivyo basi hatuwajibiki kushughulikia kazi, mapisi, ama malengo ya BAKITA kwa undani, bali tutayagusia tu 'kijuujuu' kabla ya kutathmini, kama ilivyoelezwa mbeleni, 'usayansi' katika mbinu za kubuni istilahi za isimu ya Kiswahili.

Baada ya serikali ya Tanzania kukipatia Kiswahili kipaumbele na kuitangaza lugha hii kuwa lugha ya taifa (mwaka 1963), lugha rasmi (1967) na, kufuatia Wizara ya Elimu ya Taifa kutoa tamko kuwa Kiswahili kitakuwa lugha ya kufundishia masomo yote katika shule za msingi na Vyuo vya Elimu ya Taifa, kazi ya kuendeleza istilahi za lugha hii ilipamba moto katika jamii ya Tanzania. Hivyo ndivyo haja ya kuwa na chombo maalum cha kuendesha shughuli zote kuhusu Kiswahili ilivyozuka na kukua.

Mwaka wa 1967 ulikuwa ni 'mwanzo mpya' (Batibo, 1987) maanake Baraza la Kiswahili la Taifa liliundwa kwa ajili ya kuendesha shughuli zote zilizohusu lugha ya taifa, lugha rasmi, na lugha ya kufundishia. Baraza lenyewe lilipewa jukumu la mwisho la **uundaji** na **usanifishaji wa istilahi** zilizobuniwa ili zifuate muundo na sarufi ya Kiswahili. Baraza lina vitengo mbalimbali; usanifishaji, sarufi na maandishi, tafsiri, uchapishaji na utoaji, na aidha uendeshaji.

Ili kupata istilahi za isimu ya Kiswahili, BAKITA hutumia kamati yake maalum ya kusanifu lugha inayoitwa **Kamati ya Kusanifu Lugha (KAKULU)**. Mbali na kusanifisha istilahi, vile vile ni kazi ya KAKULU kuzisambaza istilahi zilizosanifishwa, kwa walengwa wa Kiswahili. Kazi ya Baraza kuhusu usanifishaji wa istilahi ni kuthibitisha tu mapendekezo yaliyoandaliwa na KAKULU. Kazi hiyo hufanywa katika Mkutano Mkuu wa BAKITA, na orodha ya istilahi zilizokubaliwa na Baraza husambazwa kwanza kama 'jaribio', na kisha nakala hupelekwa kwenye magazeti, redio, na vitabu vya *Tafsiri Sanifu* (Mdee, 1995).

Hata hivyo, uchunguzi wa wanaisimu wa Kiswahili (k.m. Mdee 1980, Khamisi 1986, Mkude 1985, Mac William 1985, Dunn 1985, Mwansoko 1989, Massamba 1989) kuhusu uundaji na usanifishaji wa istilahi za Kiswahili unaofanywa na BAKITA umeonyesha kutoridhishwa na 'matunda' ya Baraza kwa walengwa wengi.

Baadhi ya maswala yanayolalamikiwa, kutokana na dosari na udhaifu ulioko, ni pamoja na:

- Kukanganya kwa istilahi sanifu zinazoundwa.
- Kuwepo visawe vya kiistilahi vingi zaidi.
- Uholela katika matumizi ya viambishi vinavyozalisha istilahi.
- Usawazishaji mbaya wa istilahi mkopo kutoka lugha za kigeni ambao haulingani na sarufi ya Kiswahili.

(taz. Mwansoko, 1989c).

'Malalamiko' kuhusu mbinu za kuundia istilahi za Kiswahili za chombo cha BAKITA hayakuwahi kutolewa na wataalam wa awali. Labda ni kwa sababu eneo hili lilikuwa bado halijafanyiwa utafiti wa kutosha wa kileksikografia ambao ungewezesha 'mapengo' ama udhaifu wa mbinu zitumiwazo kubuni istilahi za kitaaluma kutambulikana na kuwekwa wazi. Istilahi 'zinabuniwa' kiholela na wale wanaozihitaji na halafu 'zinasanifishwa' na BAKITA pasi na mbinu zitumiwazo katika ubunaji istilahi zenyewe kuchunguzwa. Katika kutatua na kupunguza matatizo na udhaifu katika shughuli za ubunaji na usanifishaji wa istilahi, BAKITA (1990) limeandaa kiongozo madhubuti cha usanifishaji istilahi kinachoitwa "*Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi.*"

Mwongozo huu umenuiwa 'kuwasaidia wajumbe wa kamati ya kusanifu istilahi kufanya kazi yao kwa ufanisi zaidi mbali na kuwasaidia watu binafsi na asasi kuinua kiwango cha uundaji istilahi kwa mujibu wa kaida shurutishi na kanuni tama' (Akida 1990). Ingawa ukweli kwamba *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* ni mwanzo mzuri katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili haupingiki, lakini ni kweli pia kwamba madhumuni ya mwongozo yanakanganya na si wazi

(Mwansoko, 1990a). Mwongozo wa BAKITA (1990) haueleweki kama ni wa **USANIFISHAJI ISTILAHI** au ni wa **UUNDAJI ISTILAHI**, manake umeegemea sana katika uundaji istilahi. Msisitizo juu ya usanifishaji umejitokeza mara chache sana kwenye mwongozo. Hii ni kutokana na kutofahamu ama kutozingatia misingi ya usanifishaji.

**5.1.1.1.1 Usanifishaji wa Istilahi**

Kama ilivyotajwa mbeleni, miongoni mwa kamati za BAKITA, kuna **Kamati ya Kusanifu Lugha (KAKULU).** Kadhalika, imeelezwa hapo awali kwamba jukumu mojawapo la Baraza la Kiswahili la Taifa ni kusanifu lugha ama kusanifisha istilahi zinazoundwa na vyombo mbalimbali pamoja na wataalam binafsi. Kwa hivyo, kabla ya kutazama mbinu za kuundia istilahi za Baraza, ni muhimu kuweka wazi dhana ya usanifishaji, ambayo 'imechanganywa' na uundaji wa istilahi katika mwongozo wa BAKITA (1990). ((Tazama Mwansoko (1990) katika makala yake "Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi wa BAKITA (1990): Maoni na Mapendekezo," kwa maelezo zaidi juu ya udhaifu wa mwongozo huu)).

Aidha, ni muhimu tuifafanue na kuiweka wazi dhana ya usanifishaji kwa sababu istilahi zitakazotathminiwa katika kazi hii (taz. sura ya 5) ni istilahi za isimu ya Kiswahili 'zilizosanifishwa.' Ubunaji na usanifishaji wa istilahi ni maswala yanayoingiliana, na hatungeweza kuyatenganisha. Kitsao (1995:34), anadokeza kuwa "kusanifisha ni kuanzisha utaratibu unaonuiwa kusawazisha jambo. Ni kuweka kigezo kinachokubalika na kuzingatiwa kwa jumla."

Kusanifu lugha kuna azma ya kukuza **USAWA** wa lugha zinazohitajika katika mazingira mapana zaidi (taz. Mdee, 1986 na Mbaabu, 1991 kwa maelezo zaidi).

Kufuatana na nadharia ya Ray (1963), kila hatua ya usanifishaji inapaswa kutathminiwa kutokana na vigezo vitatu, navyo ni pamoja na:

- Ufaafu.
- Uaminifu au uaminikaji.
- Usawa au ulinganifu.

Kwa usemi mwingine, endapo kuna lazima uchanganuzi au uteuzi ufanywe kati ya istilahi mbili au zaidi, lazima maswali hayo yajibiwe kwanza.

Kutokana na nadharia hii, kwa mfano, kabla ya walengwa wa Kiswahili na wataalam wa isimu kukata shauri kati ya mapendekezo ya kusanifu istilahi za isimu: **shamirisho (1) na kikamilishi (2)** kwa '*complement*', wanabidika kujibu maswali yafuatayo;

- (1) ni rahisi zaidi kusoma, kuitumia kuliko (2)?
- (1) ni rahisi zaidi kuendelea kuitumia kuliko (2)?
- Umbo la (1) linatofautiana na (2) kwa namna gani?
- Kazi ya (1) inatofautiana na (2) kwa namna gani?
- Msemaji atajiheshimu akiweza kujipatia (1) rahisi kuliko (2)?
- Msemaji ataweza kujiheshimu akiweza kuendelea kutumia (1) rahisi zaidi kuliko (2)?

Huu ndio utaratibu ufaao wa kukuza lugha kwa maoni ya Ray, (1963).

Isisitizwe hapa kwamba umuhimu wa ushauri utategemea uzito wa kila kigezo pekee. Nao uzito huo unayategemea **maoni ya watu** wanaojaribu kuimarisha lugha sanifu katika jamii husika.

Kwa ufupi, usanifishaji ni majaribio yote ya kukabidhi na kukuza USAWA wa lugha katika jamii fulani. Majaribio hayo yanaweza kutoka 'juu' serikalini, ama kutoka 'chini' katika magazeti, vyombo vya habari, au watu binafsi ambao huathiri matumizi ya lugha na kusababisha usanifishaji. Usanifishaji wa istilahi ni mojawapo ya malengo ya ukuzaji wa lugha kwa jumla. Si lazima usanifishaji wa istilahi uwe kazi ya Baraza la lugha, manake unaweza kutoka katika sehemu nyingine za jamii.

Swala ambalo hadi sasa linaelekea halijatatuliwa ni, je, ni Kiswahili gani ambacho siku hizi kinaonekana 'sanifu'? Matumizi ya neno 'sanifu' kwa maana ya "standard" yamezua tatizo kama inavyodhihirika na wingi wa visawe vya kuirejelea dhana hii:

(i) **Lugha wastani** (Mbaabu, 1978)
(ii) **Kisanii** (Ohly, 1978)
(iii) **Kijingajinga** (Khalid, 1977)
(iv) **Ki-standard** (Bulletin, 1934)
(v) **Kizungu au kiserikali** (Whiteley, 1969)
(iv) **Kisanifu** (Mbaabu, 1991)
(vi) **kidaa** (hutumiwa sana Zanzibar)

Tazama kwa mfano:

*"Standard Translation"*===**Tafsiri sanifu.**

*"Standard drawing"*===**mchoro sanifu.**

*"Standard deviation"*===**mchuano wastani** ( Tol.4, 1980).

Kama ilivyo visawe vingi vya kuirejelea dhana ya "sanifu," ndivyo ilivyo na mitazamo inayotofautiana kuhusu hiyo *'standard;'* na kwa namna hii, kuongeza haja ya kufuata misingi ya usanifishaji. Katika kusanifu, hasa katika uundaji wa istilahi, wanalugha hawana budi kufuata misingi, miiko, tabia, na miundo ya lugha hiyo (Hamad, 1989:67).

Galinski (1982) ameieleza misingi ya usanifishaji. Nayo ni pamoja na:

- Usanifishaji wa istilahi unatangulia usanifishaji wa kiteknolojia.
- Lengo la usanifishaji wa istilahi ni iktisadi ya lugha.
- Matumizi yaliyopo yasibadilishwe bila sababu za maana.
- Kazi ya usanifishaji wa istilahi ni kazi ya kikundi cha watu.

Kuhusu misingi ya istilahi sanifu za BAKITA, Tumbo-Masabo (1982:406) anadai kuwa:

> Kuna pia makosa katika uundaji wa msamiati ambao unatekeleza kwa kutoelewa misingi ya kimataifa kuhusu uendelezaji wa istilahi. BAKITA mara nyingi husanifisha istilahi kwa kufuata matamshi ya Kiingereza, bila kufanya uchunguzi wa kietimolojia au kwa kuzingatia kanuni zinazoongoza uzalishaji wa istilahi za kisayansi kama zilivyoelezwa katika Stoberski (1974) ISO/R 843.

Dondoo hili linatuelekeza katika kutambua umuhimu wa usanifishaji wa kimataifa wa istilahi. Usanifishaji katika kiwango cha kimataifa ulifanywa mwaka 1931 na Wuster. Kitabu chake cha Usanifishaji wa Kimataifa wa lugha katika Uhandisi (*Die Internationale Sprachnormung in der Technik*) kiliweka msingi kwa

kamati maalum ya usanifishaji istilahi ya Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Usanifishaji vya Kitaifa [**International Federation of National Standardizing Associations**] (ISA) lililoundwa mwaka 1936. ISA ilitangulia ISO [International Organization Standardization]. Tangu wakati huo, kamati ya ISO, ambayo ilishughulikia usawazishaji wa kimataifa wa istilahi, TC 37, imetoa matoleo mengi yanayohusiana na ukuzaji na usanifishaji wa istilahi (taz. Ridder, 1988:28 kwa ufafanuzi zaidi).

La muhimu ni kwamba BAKITA na mashirika ya nchi nyingi, yawe ya kibinafsi au ya serikali, yanapaswa kushirikiana na kuzingatia misingi ya kimataifa ya usanifishaji wa istilahi. Irira (1990) anatufichulia umuhimu wa usanifishaji anapodokeza kwamba:

> Usanifishaji istilahi ni kimoja cha vipengee muhimu katika usanifishaji majumui wa lugha ambao hujumuisha; uteuzi wa lahaja au kigezo, uandikaji na ufafanuzi, uundaji wa istilahi, ukubalifu, uenezaji na matumizi rasmi.

Ili lugha ya Kiswahili ifaidi mawasiliano hakika na sahihi katika fikira pevu za kisayansi na kiteknolojia kama itarajiwavyo, inabidi Baraza la Kiswahili la Taifa liandae upya mwongozo wa usanifishaji istilahi. Mwongozo uliopo kwenye *KAKULU* Na.3, 1982, haujitoshelezi, na ni wa jumla mno, ilhali *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* wa BAKITA (1990) ulionuiwa kutoa 'maelezo muhimu yote kuhusu usanifishaji istilahi, hasa jinsi ya kuzisanifisha rasmi,' una matatizo mengi na ni finyu mno (Mwansoko, 1990b:10). Mathalani, kwenye sura 2.1.0. uk.2, tumeelezwa yafuatayo kuhusu lengo la mwongozo huu:

> ...kuchochea uenezaji wa taratibu, kanuni na kaida za usanifishaji ndani na nje ya Tanzania...kuwa na kaida asisika na shurutishi za kubuni, kusanifu na kuunda istilahi...

Kutokana na maelezo hayo, tungetarajia Mwongozo uweke wazi na ujadili kikamilifu 'kaida' za usanifishaji ambazo sharti zifuatwe na wasanifishaji ili kazi yao iwe na ufanisi wa kutosha. 'Kaida asisika na shurutishi' za usanifishaji wa istilahi hazijaelezwa kwa undani kwenye Mwongozo huu. Ndiyo maana hapajatokea mabadiliko yoyote licha ya kwamba 'malalamiko' mengi yamepelekewa Baraza na wataalam wa Kiswahili. Kwa mfano, Baraza lingali linafuata utaratibu wa zamani (Mwansoko, 1990). Istilahi zinaundwa moja kwa moja na kiholela, na badala ya kuwekwa tayari katika ufungamano wa kidhana ili zisanifishwe pamoja, zinapata ithibati ya Baraza hata kabla ya kuchunguza uwiano wa kimaana wa istilahi hizo.

Suala linalosisitizwa hapa, na ambalo ndilo la manufaa katika tasnifu hii, ni kwamba Baraza halina budi kuweka wazi misingi na kanuni za kimataifa za kusanifisha istilahi za Kiswahili, na kuwahimiza waundaji istilahi kufuata kanuni za uundaji wa istilahi. Kwa kufanya hivyo, nia ya kuboresha na kuzipa ufanisi wa kiwango cha juu shughuli za uundaji na usanifishaji istilahi itatimizwa na kuafikiwa (taz. pia Kitsao, 1989:57).

#### 4.1.1.1.2 Uundaji wa Istilahi: Mbinu za BAKITA

Mbinu ni mpango wa kutekeleza shughuli (za uundaji) kwenye vitendo au matukio ya kawaida. Tangu mwaka wa 1974 wakati

usanifishaji wa istilahi ulipoanza, kutokana na Agizo la Waziri Mkuu Nchini Tanzania, BAKITA imekuwa ikifuata kaida na utaratibu maalum katika kuzipata istilahi za kitaaluma. Sera imekuwa ni kutumia nyenzo za ndani na nje ya Kiswahili.

Utoaji wa kipaumbele kwa nyenzo hizo, kama inavyoelezwa kwenye Mwongozo wa BAKITA (1990:3) ni:

**Kiswahili Sanifu** kwa kutumia akiba ya msamiati iliyopo ili kupata visawe, minyambuliko, mifito, mirakabu, n.k.

**Lahaja za Kiswahili** zisizopungua 15 ambazo ni pamoja na Kipate Kiamu, Kimvita, Kiunguja, Kitikuu, Kivumba, Kipemba, Chi-chifundi, Kitumbatu, n.k.

**Lugha za Kiafrika** zinazojumlisha lugha za Kibantu na zisizo za Kibantu kama vile Kiluhya, Kikikuyu, Kiganda, Kimasai, Kihausa, Kindebele, Kizulu, Chichewa, Kisomali, Kifulani, Kimijikenda, Kipokomo, Kielwana, Kikomoro, n.k.

**Lugha za Kigeni** kama vile Kiarabu, Kiingereza, Kihindi, Kirusi, Kijerumani, Kigiriki, Kireno, Kihispanyola, Kituruki, Kitaliano, Kiswidi, n.k.

Katika jamii za Kitanzania, na hususani enzi hizi, mwelekeo umekuwa kutumia Kiingereza kupata istilahi mpya kwa sababu ya mazoea, kwa vile ni lugha iliyofahamika zaidi ikilinganishwa na Kiarabu. Ni maoni ya Tumbo na Mwansoko (1992:38) kuwa Kiarabu 'wakati wake umepita' na hakitoi mchango mkubwa wa kiistilahi (taz. 4.8.4.2, uk. 172). Kwa kifupi, BAKITA limeweka utaratibu wa kufuatwa kama mwongozo katika ubunaji wa istilahi za Kiswahili. Utaratibu huo ni:

(i) Istilahi mpya zinatakiwa ziundwe kutokana na Kiswahili chenyewe pamoja na lahaja zake. Kwa mfano, (75):

(75a) **Kiingereza** | **Kiswahili**

| | |
|---|---|
| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
| *'energy'* | **nguvu** |
| *'extract'* | **zidua** |
| *'tense'* | **njeo.** |

(taz. Besha, 1972)

(ii) Istilahi zitafutwe kutoka katika lugha za makabila ya Kibantu kama mfano huu unavyodhihirisha;

(72b)

| | |
|---|---|
| **Kingereza** | **Kiswahili** |
| *'fallow'* | **fuwele** (Kizigua) |
| *'affluent'* | **kipera** (Kingoni) |
| *'granite'* | **itale** (Kisukuma). |

(taz. Maina, 1989:115)

(iii) Istilahi zichunguzwe kutoka lugha zisizo za Kibantu. Mathalani:

(75c)

| | |
|---|---|
| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
| *'curving knife'* | **ngalemu** (Kimasai) |
| *'kola nuts'* | **kola** (Kiibo). |

(iv) Istilahi mpya kuundwa kwa kuunganisha silabi chache kutoka katika maelezo ya istilahi hiyo au sentensi. Kwa mfano:

(75d)

| | | |
|---|---|---|
| **Kiingereza** | **Kiswahili** | **Maelezo** |
| *'dawn food'* | **chakucha** | chakula cha kucha |
| *'lunch'* | **chakushindia** | chakula cha kushindia siku |

| | | |
|---|---|---|
| *'supper'* | **chajio** | chakula cha jioni au cha kuchwishia *(pass the evening with)* |

(taz. Chimerah, 1998).

(v) Istilahi mbili au tatu huunganishwa na kuunda istilahi moja, kama mfano huu unavyoonyesha:

(75e)

| **Kiingereza** | **Neno lililoundwa** | **Maneno mawili/matatu** |
|---|---|---|
| *'affricate'* | **kizuiwakwamizwa** | kizuiwa kwamizwa |
| *'apposition'* | **mrejeosawa** | mrejeo sawa |
| *'binarism'* | **uwiliwili** | uwili uwili. |

(taz. TUKI, 1990).

(vi) Istilahi za kigeni kutoholewa na kuandikwa kwa kufuata muundo na misingi ya lugha ya Kiswahili. Mathalani,

(75f)

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *'tone'* | toni |
| *'acronym'* | akronimu |
| *'morpheme'* | mofimu |
| *'typology'* | tipolojia. |

(taz. TUKI, 1990).

BAKITA huunda istilahi za isimu ya Kiswahili kwa kuazima istilahi za Kiingereza na kuzipa matamshi ya Kiswahili. Kuhusu mbinu hii ya utohoaji wa istilahi za kigeni, Mbaabu (1989:26) anasema:

> ...ni kosa kutegemea mifano ya Kiingereza pekee na kuazima muundo wa lugha hiyo katika kuunda msamiati wa kisayansi wa Kiswahili.

Naye Mwansoko (1990:113) hakosei anapodokeza kwamba, katika taaluma ya isimu, Baraza la Kiswahili la Taifa linaelekea kusisitiza umataifa wa istilahi za Kiswahili kwa kutumia mbinu ya ukopaji kutoka Kiingereza. Idadi ya istilahi za isimu ya Kiswahili zinaundwa kwa kutumia mbinu ya ukopaji na utohoaji inazidi kupanuka. Baraza hukataa istilahi za isimu zinazozalishwa na kupendekezwa na wataalam wa isimu na mahali pake huchukuliwa na istilahi mkopo zinazotoholewa za Kiingereza (taz. BAKITA, 1984).

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990) imekopa istilahi za Kiingereza kupindukia. Tazama mifano ifuatayo:

| (76) Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| '*alloloq*' | aloloki |
| '*allomorph*' | alomofu |
| '*allophone*' | alofoni |
| '*antonomasia*' | antonomasia |
| '*obstruent*' | obstruenti |

Asemavyo Mbaabu (1995:56) ni kwamba "kukopa kuna mipaka yake. Tukikopa bila mpango, itatubidi kulipa kwa kuipoteza lugha tuliyotarajia kuitajirisha kwa kukopa." Uchunguzi wa istilahi zilizoundwa na BAKITA pamoja na *Kamusi ya Istilahi za Sayansi na Teknolojia* ya BAKITA (1995) unadhihirisha kwamba chombo hiki hutumia mbinu za uundaji istilahi kama vile mnyambuliko (vitenguo), mifito, mirakabu (uambatanishaji), na ukopaji (uasilishaji na utohoaji).

#### 5.1.1.1.2.1 Minyambuliko ya Shina

**Minyambuliko** na **vitenguo** ni istilahi zinazotokana na shina moja. Mfanyiko wa unyambuaji wa shina hutekelezwa kwa kuongeza au kupunguza viambishi awali au tamati kwenye shina la istilahi. Unyambuaji wa shina katika kuunda istilahi huendelezwa kwa kutumia ruwaza mbalimbali (rejelea 3.4.2.1.1, uk. 118 kwa maelezo zaidi juu ya ruwaza ambazo hutumiwa na BAKITA).

Mifano ifuatayo ya istilahi zilizoundwa kwa mbinu ya unyambuaji inatoka katika *Kamusi ya Istilahi za Sayansi na Teknolojia* ya BAKITA (1995).

| | |
|---|---|
| (77) **choche.a** | **kichochezi** *(catalyst)* |
| **chubu.a** | **kichubuzi** *(abrasive)* |
| **rutub.u** | **kirutubisho** *(nutrient)* |
| **chachu** | **mchachuko** *(fermentation)* |
| **chepu.a** | **uchepukaji** *(refraction)* |
| **lahaja** | **ulahajishaji** *(dialectalization)* |

(taz. BAKITA, 1993).

#### 5.1.1.1.2.2 Mifito

**Mifito** ni mojawapo ya mbinu za kuendeleza istilahi inayohusu kufafanuliwa au kutoa maelezo sanifu ya dhana kwa istilahi zinazoundwa. Katika kubuni mifito, kuna udondoshaji wa vifungu au sehemu za kiisimu kutoka kwenye ufafanuzi au maelezo sanifu (Irira 1990:13). Udondoshaji hutokea wa:

(a) **Viunganishi** kama vile: na, ili, wa, madhali, angalau.

(b) **Vihusishi** kama: chini ya, juu ya, kwa sababu ya, kwa ajili ya, kutokana na.

(c) **Vivumishi** kama: dogo, kubwa, finye, zuri, baya, tata, chache, sahili.

(d) **Viambishi** awali na tamati (ambapo shina la neno huongezwa).

Hata hivyo, mbinu ya mifito si zalishi na haitumiki sana katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili. Mfano wa mifito iliyotokana na ufafanuzi au maelezo sanifu ni pamoja na:

**UKIMWI** (Ukosefu wa Kinga **Mwilini** - '*Aids*')

(taz. BAKITA, 1990:14).

#### 5.1.1.1.2.3 Mirakabu

**Mirakabu** ni miungano ya maneno, au mofimu, ama maumbo unganifu ili kupata istilahi mpya kwa ajili ya dhana mpya. Mfanyiko huu ni zalishi na hutumika sana katika kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili, pamoja na istilahi za sayansi na teknolojia.

Mifano ifuatayo ni ya mirakabu ya neno na neno, au neno na umbo, n.k.

**(78)** (Istilahi za kisayansi na teknolojia)

(78a) **fundibomba** (fundi + bomba) = '*plumber*'

(78b) **nyonyochupa** (nyonyo + chupa) = '*formula feeding*'

(78c) **nyonyotiti** (nyonyo + titi) = '*breastfeeding*'

(78d) **myeyungano** (myeyuko + muungano) = '*fusion.*'

Mbinu hii pia imetumika kupata istilahi za isimu ya Kiswahili kama mfano **(79)** huu unavyothibitisha:

(79a) **kizuiwakwamizwa** (kizuiwa + kwamizwa)

(79b) **mkondohewa** (mkondo + hewa)

(79c) **mshukohatua** (mshuko + hatua).

(Maelezo kuhusu udhaifu wa mbinu ya mirakabu taz. 5.2.1, uk. 298)

Viambishi vyenye 'thamani maalum' au maumbo unganifu hutumiwa katika kuunda istilahi ambatano. Baadhi ya mifano ni kama vile:

**(80)** bio = hudokeza maisha au kiumbehai

bayo

-lojia *(-logy)* = hudokeza sayansi au mtaala

jio- *(geo-)* = hudokeza ardhi au dunia

-grafia *(-graphy)* = hudokeza namna ya kuandika, kuwakilisha, n.k.

meta- *(meter-)* = kipimio

heksa- *(hexa-)* = sita

hidro- *(hydro-)* = humaanisha maji

oksi- *(oxy-)* = yenye au itumiayo oksijeni

themo- *(thermo-)* = huhusiana na joto

foto- *(photo-)* = inahusika na nuru na pia inadokeza dhana ya kifotografia

(taz. BAKITA, 1990:11).

Kutokana na matumizi ya viambishi au maumbo unganifu, tunapata istilahi za Kiswahili kama mfano huu **(81)** unavyoonyesha;

(81a) biolojia (au bayolojia)

(81b) hidrolojia (au haidrolojia)

(81c) jiografia

(81d) fotografia

Katika isimu ya Kiswahili, mfano wa istilahi zilizoundwa kwa mfanyiko huu wa maumbo unganifu ni kama vile **(82)**:

(82a) **ethnolojia**

(82b) **etimolojia**

(82c) **glotokronolojia**

(82d) (uanishaji) **kijiografia**

(82e) **demografia**

Ipo haja ya kutambua na kutumia viambishi na maumbo ya istilahi za kigeni kwa **mfumo uliosawa** kwa ajili ya kuendeleza istilahi za Kiswahili, hususani za isimu. Iwapo Baraza linatambua umuhimu wa 'viambishi vyenye thamani maalum' au maumbo unganifu, basi istilahi katika mfano huu ziliundwa kiholela;

**(83)** **sayansimelea** = "*parasitology*" (badala ya **parasitolojia**)

**pimamchepuko** = "*refractometer*" (badala ya **refrakitometa**)

(BAKITA, 1995)

**5.1.1.1.2.4 Ukopaji wa Istilahi za Kigeni**

Katika lugha nyingi, uundaji wa istilahi umeathiriwa na matumizi ya mbinu ya ukopaji kwa sababu ya umuhimu wa mbinu yenyewe. Hata hivyo, kwa vipimio vya manufaa, si muhimu kwamba istilahi mpya imekopwa au la. Kuhusu suala la ukopaji, Ferguson (1968:38) anasema:

> Msamiati maalum unaweza kuwa faafu kwa njia sawa ikiwa umeundwa kutokana na mfanyiko wa uundaji wa mumo kwa mumo au kutokana na ukopaji wa lugha nyingine. Masuala ya

> wahafidhina yanaweza kuwa ya kukosoana kiasi kwamba hisia nzito na kutoelewana huibuka lakini hayafai kwa mafanikio ya mwisho ya... kukuza leksikoni ya lugha.

Istilahi ngeni aghalabu hukopwa na huingizwa kwenye mfumo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili **baada** ya kukosekana kwa istilahi ya asili na kisha hupewa umbo na tabia ya Kiswahili. Baraza la Kiswahili la Taifa hufuata aina mbili za ukopaji: Uasilishaji na Utohoaji.

Katika **uasilishaji**, istilahi hutwaliwa na huingizwa kwenye matumizi na mfumo wa istilahi za Kiswahili kama ilivyo kimaandishi na kimatamshi pasi na kufanyiwa mageuzi ya umbo. Kwa mfano:

| **(84)** | **Kilatini** | | **Kiarabu** | | **Kireno** |
|---|---|---|---|---|---|
| (84a) | ***data*** | (84b) | **kitabu** | (84c) | **machela** |
| | ***video*** | | **safari** | | **bendera** |
| | ***anemia*** | | **adabu** | | **bomba** |

Mbinu ya **utohoaji** inayohusu upatiaji wa istilahi mkopo muundo na tabia ya Kiswahili ili iafikiane na iwiane na istilahi katika mfumo wa matumizi ya Kiswahili, ndiyo itumikayo sana na Baraza katika kuunda istilahi za kitaaluma, hususani za isimu. Mfano ni kama kwenye istilahi zifuatazo:

| **(85)** | **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| (85a) | *atom* | atomu |
| (85b) | *bacteria* | bakteria |
| (85c) | *iodine* | iodini |
| (85d) | *fuse* | fyuzi |
| (85e) | *fuel* | fueli |
| (85f) | *rozine* | rozini |

| | |
|---|---|
| (85g) *tray* | trei. |

(taz. katika BAKITA, 1995).

Mifano zaidi ya utohoaji katika taaluma ya isimu ya Kiswahili:

| **(86) Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| (86a) *polysemy* | **polisemia** |
| (86b) *polyphony* | **polifonia** |
| (86c) *phase* | **fezi** |
| (86d) *ontogeny* | **ontojenia** |
| (86e) *nominal* | **nomino** |
| (86f) *cenemetics* | **senematiki** |
| (86g) *intonation* | **intonesheni** |

(taz. katika BAKITA, 1995).

Katika taaluma ya sayansi, istilahi zifuatazo **(87)** zimeundwa kwa mbinu ya **utohoaji** na BAKITA:

| **(87) Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| (87a) *gas* | **gesi** |
| (87b) *matter* | **mata** |
| (87c) *hormone* | **homoni.** |

Ili kupata istilahi bora na zinazokubalika kwa walengwa, tunapendekeza kwamba BAKITA iboreshe mbinu za uundaji istilahi za Kiswahili. Mbinu za kubuni istilahi, kama ilivyo na istilahi zenyewe, zinapaswa kutandawazishwa. **Kutandaridhishwa kwa mbinu** za kuundia istilahi na **usanifishaji wa istilahi**, kama vitendo maalum vinavyohusu sehemu ya lugha, havipaswi kutenganishwa katika uendelezaji na ukuzaji wa lugha. Utandaridhi wa mbinu za kuundia istilahi vilevile utaleta **usawa** wa kimataifa katika mbinu zitumiwazo na vyombo mbalimbali pamoja na wataalam binafsi

wanaounda istilahi; na kwa namna hii, utapunguza **ukuzaji huria** wa istilahi za Kiswahili, hususani za isimu. Ili kupunguza tatizo la wingi wa **visawe** vya istilahi za isimu ya Kiswahili, mbinu zitakazotandaridhishwa zitapaswa kutumiwa kama dira ya kuamulia 'usayansi' katika istilahi, na mifanyiko iliyotumika katika uundaji wake. Aidha, ili kupata mbinu ya kisayansi katika kuundia istilahi za Kiswahili zenye ukubalifu kwa walengwa, BAKITA haina budi kuandaa misingi ya kisayansi ya kuundia na kusanifisha istilahi. Misingi hiyo ikitwe katika nadharia za kiistilahi (taz. 2.1 kwa maelezo zaidi juu ya nadharia za uundaji wa istilahi).

### 5.1.1.2. Chombo cha Kukuza Istilahi cha TUKI

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilianzishwa baada ya kuvunjika kwa Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki mwaka 1964 (Mbaabu, 1991). Lengo kuu la TUKI ni 'kukuza Kiswahili na kueneza matumizi yake katika viwango vyote nchini Tanzania, Afrika Mashariki, na katika sehemu zingine za ulimwengu' (Mhina, 1980:359).

Baadhi ya madhumuni ya TUKI ni:

i) Kuendesha uchunguzi wa lugha kwa madhumuni ya kukikuza na kukistawisha Kiswahili katika nyanja zote.

ii) Kushughulikia ukuzaji wa istilahi za Kiswahili na utengenezaji wa kamusi ya Kiswahili.

iii) Utoaji wa jarida; *"Kiswahili."*

Kwa muda mrefu tangu mwaka 1970, wakati wa kutambuliwa rasmi kwa

TUKI na sheria ya Bunge, jukumu lake limekuwa ni kuandaa miradi ya utafiti juu ya istilahi na uundaji wa makamusi, lugha na fasihi. Kuhusu shughuli ya kamusi, uandishi na uchapishaji wa kamusi za Kiswahili-Kiingereza, Kiingereza-Kiswahili, na Kiswahili-Kiswahili ndiyo miradi mikubwa ya TUKI. Kufikia sasa, Taasisi imefanikiwa katika kuchapisha kamusi ya *Kiswahili-Kiswahili* (1981), *Kiingereza-Kiswahili* (1996) pamoja na kamusi za kitaaluma kama vile *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990), *Istilahi: Fizikia, Kemia, Biolojia* (1987). Maswala ya kitaaluma ya isimu, leksikografia na fasihi huchapishwa na Taasisi katika jarida la *Kiswahili* na *Mulika*.

Isisitizwe hapa kwamba Taasisi hutekeleza kazi zake za kuendeleza Kiswahili kwa ushirikiano na idara na asisi zingine za kuendeleza Kiswahili kama vile Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Taasisi ya Elimu ya Taifa; na BAKITA (taz. Chimerah 1998:7 kuhusu taasisi za Afrika Mashariki za uchunguzi wa Kiswahili). Kati ya Mashirika haya, BAKITA ndilo shirika la umma lenye mamlaka ya juu (ya kisiasa) zaidi kuhusu Kiswahili ((taz. pia Massamba, 1985 na Mhina, 1980) kwa maelezo zaidi juu ya mamlaka ya Baraza)).

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili hukusanya istilahi na kisha huzipeleka kwa BAKITA ili ziidhinishwe, zisanifishwe, na kusambazwa. Vyombo vya kukuza lugha vya BAKITA na TUKI vina uhusiano mzuri katika utekelezaji wa kazi zao. Kwa mfano, vyombo hivi hujishughulisha na UUNDAJI WA ISTILAHI na uandishi wa kamusi za kitaaluma pasi na mizozo wala migongano (Mwansoko, 1991).

Hata hivyo, uundaji wa istilahi katika TUKI ni shughuli ambayo **imelalamikiwa** na watumiaji istilahi na wataalam wengi (taz. Massamba, 1989; Mbaabu, 1991). Hususani, malalamiko haya yamehusu:

- Udhaifu wa istilahi zinazoundwa ambazo hazipigi ndipo.
- Kukosekana kwa mbinu mwafaka na za kisayansi za kuundia istilahi.
- Usawazishaji mbaya wa istilahi mkopo na mapendeleo ya tafsiri sisisi katika istilahi zinazoundwa za kitaaluma, hususani, za isimu ya Kiswahili, na
- Mwelekeo wa Taasisi kuwa ni wa kitaifa zaidi kuliko kimataifa.

Kwa jumla, tunaazimia hapa kuchunguza mbinu za TUKI za uendelezaji wa istilahi za isimu ili kuziweka wazi pamoja na kutathmini 'usayansi' katika mbinu hizo.

Kabla ya wataalamu na wanaisimu wengi kuanza kujishughulisha na uundaji wa istilahi za kisayansi, kazi hii ilipewa Sheikh Hamisi Akida na TUKI. Sheikh Akida aliajiriwa mwaka wa 1970 na alishughulikia uundaji wa istilahi za bayolojia na za aina nyingine. Kazi ya mtaalam huyu iliwasisimua wanaisimu na waundaji istilahi wengi ambao walipata hamu na ghamu ya kuunda na kubuni istilahi zilizohitajika. Kuhusu suala la ubunaji wa istilahi, Chimerah (1998b:11) katika makala yake "Kiswahili Jana na Leo na Kesho: Swala la Msamiati," anasema:

> ...ili neno libunike na kushika, ni sharti kwanza pawe na haja kuu kimuktadha wa matumizi. Aidha, ili mbunaji wa neno apate msukumo mkuu wa kubuni istilahi...mada husika humjia kwa lugha ngeni ambayo haina tafsiri ya moja kwa moja katika lugha yake.

Tunachosisitiza hapa ni kwamba kukosekana kwa istilahi

zilizokubalika na kuidhinishwa kimataifa kulileta 'msukumo' mkuu wa kubuni istilahi za kisayansi katika TUKI.

#### 5.1.1.2.1 Uundaji wa Istilahi/Mbinu za TUKI

Ili kuleta ufanisi katika shughuli ya kuendeleza na kukuza Kiswahili kileksikoni, mbinu ambazo hutumiwa na Taasisi ni pamoja na:

- **Ukopaji** (tafsiri ya moja kwa moja, utohoaji, na tafsiri ya maana)
- **Uambatanishaji**
- **Ufupishaji** (akronimu, uhulutishaji)
- **Unyumbuaji na uambishaji**
- **Upanuzi wa maana** za maneno n.k.

Mbinu hizi hutumika kwa kufuata misingi na kanuni zifuatazo:

- **Umbo la kitu**
- **Utendaji kazi wa kitu**
- **Hali ya kitu chenyewe**, na
- **Athari ya kitu.**

**Umbo la kitu:** TUKI imezipata istilahi nyingi kwa kuangalia na kuchunguza **umbo** la kitu chenyewe na kulifananisha na kitu kingine ambacho kinafahamika katika Kiswahili cha kawaida. Kwa mfano;

**kidoletumbo** - *appendix* (kitu mfano wa kidole kinachoning'inia kwenye utumbo mpana)

(taz. pia misingi ya BAKIKE/Nabhany katika 5.1.1.3, uk. 248).

**Utendaji kazi wa kitu:** Kazi ya kuwakilisha kitu pia hutumika kama msingi mmojawapo wa kuundia istilahi. Dhana inayojitokeza kutokana na kazi ya kitu fulani huchunguzwa kwa makini kabla ya kuundiwa neno la Kiswahili (Yambi, 1988:155). Mathalani:

**kiribahewa** - *airsac* (kazi ya kuhifadhi akiba ya hewa na kuufanya mwili uwe mwepesi wakati wa kuruka. Kiriba - ni mfuko wa ngozi).

**kitambaza** - *lateral* - ni istilahi ambayo pia imeundwa kwa msingi wa utendaji kazi wa kitu.

**Hali ya kitu chenyewe:** Baadhi ya istilahi zimeundwa kwa kudadisi jinsi kitu chenyewe kilivyo na kupata istilahi ya kuelezea hali ya kitu hicho. Mfano mzuri ni:

**msago** - *digestion* (hali itokeayo chakula kifikapo tumboni na **kusagwa**) (taz. pia istilahi kama vile **mpumuo** - *aspiration*, na **manenohisia** - *bias words*).

**Athari ya kitu** kitafsiriwacho ni msingi mmojawapo pia unaotumiwa na Taasisi katika kuunda istilahi za Kisayansi. Kwa mfano:
**kiviza** - *inhibitor* (kemikali inayofanya mgeuzo wa kuvizia).

Massamba (1989:74-76) anaziita kanuni hizi kwamba ni 'mbinu' za kuundia istilahi, hoja ambayo hatukubaliani nayo. Maoni yetu ni kwamba hizi si mbinu za kuundia istilahi bali ni misingi ya uundaji wa istilahi zinazotumiwa na TUKI katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili (Kuhusu tofauti ya dhana hizi, taz. 3.3, uk. 60).

Wataalamu wa awali walioshughulikia mbinu za kuundia istilahi za Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (k.v. Yambi, 1988; Massamba, 1989) wanaelekea kutambua mbinu za **unyambuaji, muungano wa maneno, utohoaji**, na **kaleki** (tafsiri ya moja kwa moja) kwamba ni 'zalishi,' na ndizo zinazotumika sana katika kuendeleza istilahi za Kiswahili. Uchunguzi wetu wa machapisho mbalimbali ya TUKI, hususani *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu* (1990) unaonyesha kuwa Taasisi huegemea kwenye mbinu za **ukopaji, utohoaji, kaleki, kufasiri maana** kutoka lugha nyingine kwa Kiingereza, **uambatanishaji, unyumbuaji, uambishaji, upanuzi wa maana za maneno**, na **ufupishaji**, kwa mfuatano huo, katika kukwasisha lugha ya Kiswahili kileksikoni (taz. 5.2, uk. 289). Katika uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, mbinu hizi hutumika. Hapa tutafafanua kwa mapana kwa sababu ya umuhimu wa suala hili.

### 5.1.1.2.1.1 Ukopaji

**Ukopaji** wa istilahi ni mojawapo wa mbinu 'rahisi' za kuendeleza leksikoni ya lugha. Katika kusisitiza umuhimu wa mbinu ya ukopaji, Chimerah (1998a:46) anadokeza kwamba ukopaji au 'uvamizi' wa lugha nyingine katika Kiswahili ulitokana na sababu kwamba 'hakuna lugha hata moja yenye uwezo wa kueleza kila kitu na kila dhana ulimwenguni. Dhana ngeni kwa waneni wa lugha yo yote huwa ni nadra sana kupata tafsiri ya moja kwa moja. Hivyo mapengo muhimu ya kiistilahi hujazwa kwa ukopaji na kwa namna hii lugha za kimataifa hupata kupanuka.'

Kiingereza ni mojawapo ya lugha za ulimwenguni ambayo imejirutubisha kiistilahi kwa mbinu ya ukopaji. Asilimia themanini ya istilahi za Kiingereza cha siku hizi zimekopwa kutoka lugha nyingine, Kiswahili kikiwemo (McCrum, Cran, McNeil, 1985, katika Chimerah, 1998). Mathalani, Kiingereza kimekopa (na hadi sasa kinaendelea kukopa) istilahi na maneno yafuatayo kutoka lugha nyinginezo; *pyjamas* kutoka Kihindi, *tomato* kutoka KiAzteki, *coffee* kutoka Kituruki au Kiarabu, *tea* kutoka Kichina au Kiarabu, na mengine mengi. Lugha hii imeendelea kukopa istilahi/maneno yanayohusiana na sanaa (*critique, connoisseur, pointillism*), maswala ya kijamii (*etiquette, parvenu, elite*), masuala kuhusu vyombo vya kusafiria (*garage, hangar, chauffeur, fuselage*). Kutoka Kiholanzi, Kiingereza kimekopa istilahi *taffrail, schooner* na kutoka Kilatini maneno maelfu, yakiwa ni pamoja na ya sanaa (*studio, replica, fiasco, scenario*). Kutoka Kijerumani, Kiingereza kimepata kwa njia ya ukopaji istilahi nyingi za kisayansi, hususani za kemia, kama *paraffin, cobalt* na *quartz* (Barber 1964:215).

Kutoka lugha nyingine, maneno yamekopwa na Kiingereza kulipotokea haja na sababu maalum - kama "Kiafrikana" *apartheid* na kutoka Kirusi *perestroika* (upangaji upya), *glasnost* (uwazi) (Chimerah 1998:37), na mengine kama *sputnik* na *lunik*. Kigiriki-Latini kimechangia Kiingereza istilahi na maneno mengi (*video, television, synthesizer*) (McCrum, Cran, McNeil, katika Chimerah, 1998). Kiingereza, kwa njia ya ukopaji, kimekwasishwa na maneno ya Kiswahili kama **Bwana** na **safari**.

Katika kufuata 'nyayo' za Kiingereza, ni bayana basi kwamba chombo cha kukuza lugha ya Kiswahili cha TUKI, kimeipa umbele mbinu hii ya ukopaji ambayo kwayo lugha ya kisasa iliyoendelea inaweza kupata sifa ya 'umataifa' (Chimerah 1998:9). TUKI, katika kuendeleza istilahi za Kiswahili, hutumia taratibu mbili za ukopaji; **utohoaji** na **kaleki** (tafsiri ya moja kwa moja), pamoja na **tafsiri ya maana** (taz. **4.8.6**, uk. 194).

Mbinu ya **utohoaji** imetumika na Taasisi katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili. Kwa mfano **(88)**:

| (88a) | (88b) | (88c) |
|---|---|---|
| **polisemia** | **ontojenia** | **kategoria** |
| **filolojia** | **osiloskopu** | **sedila** |
| **filojinia** | **palatografia** | **konsonansi** |
| **othografia** | **tagmetiki** | **kakolojia** |
| **elementi** | **umalapropu** | **bisemia.** |

Uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili kwa mbinu ya tafsiri ya moja kwa moja (tafsiri sisisi) au kaleki pia ni mbinu inayotumiwa sana na TUKI, kama mfano huu **(89)** unavyodhihirisha;

| | **Kiswahili** | **Kiingereza** |
|---|---|---|
| (89a) | **video** | *video* |
| (89b) | **isopoda** | *isopoda* |
| (89c) | **aljebra** | *algebra* |
| (89d) | **sandhi** | *sandhi* |
| (89e) | **tagma** | *tagma* |
| (89f) | **tagmeme** | *tagmeme.* |

Mbinu hii ya uhamishaji istilahi hutumiwa sana katika Bahasa, Malaysia (Omar, 1981). Mwansoko (1990b:9) anapendekeza kwamba istilahi za Kiswahili zipanuliwe kwa njia ya kaleki ambayo 'inapaswa kuungwa mkono na wanaleksikografia wanaoshughulikia

lugha za Kiafrika,' kwa sababu huleta 'usawazishaji mzuri wa istilahi za mkopo.' Katika kutetea pendekezo lake kwamba istilahi mkopo kutoka Kiingereza ziingizwe kwenye Kiswahili kufuatana na matamshi yake ya Kiingereza, Mwansoko (1990) anasisitiza kwamba kwa kufanya hivyo, 'mkanganyiko katika utohozi wa istilahi hizo utapungua na kuisha kabisa, na istilahi zenyewe zitakuwa na ulinganifu unaokubalika'; suala ambalo linahitaji uchunguzi wa kina.

Mbinu ya **kufasiri au kutafsiri maana** kutoka lugha nyingine hadi Kiswahili vile vile hutumiwa na TUKI katika uendelezaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Mbinu hii imetumika kwa manufaa makubwa katika kuunda istilahi za isimu kama mfano huu **(90)** unavyodhihirisha:

(90a) **kifyonzo** - *sibilant*

(90b) **ubadili** - *complimentarity*

(90c) **usilasila** - *syntagmatic*

(90d) **msuguano** - *friction*

(90e) **nenopotofu** - *ghostform*

(90f) **uonyeshibainishi** - *deixis*

(90g) **kishazi bebwa** - *embedded clause.*

Mifano zaidi ya istilahi zilizoundwa kutokana na kutafsiri maana ni **(100)**:

(100a) **neno halafa** - *ambivalent word*

(100b) **uchopekaji** - *anaptyxis*

(100c) **mujarabu** - *attested*

(100d) **upenyu** - *aperture*

(100e) **alama mpaka** - *boundary marker.*

(taz. tathmini ya usayansi katika istilahi za TUKI katika 5.1.1, uk. 209).

Kwa jumla, ingawa mbinu ya ukopaji inatiliwa uzito sana na kupendelewa katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili, istilahi nyingi zinazotokana na mbinu hii hazina uangavu, kama mifano **(99)** na **(100)** hapa inavyoonyesha. Kadhalika, elementi za Kigiriki ambazo zimetumiwa sana katika kuunda maneno ya Kiingereza hazikuendelezwa wala hazikusawazishwa vizuri zilipokopwa na kuingizwa katika Kiswahili. Elementi hizo ni kama *bio* (uhai), *graph* (andika, chora), *photo* (mwangaza), *phone*(sauti), *morph* (umbo) na nyingine kama vile *hypo, nym,* au *nymy, gram,* na *logy* (lojia, elimu). Kwa mfano, iwapo

*-graph* ni **grafu**

*graphy* ni **grafia** kama ilivyo katika

*homograph*===**homografu**,

*homography*===**homografia**,

*palatography*===**palatografia**,

*idiography*===**idiografia**.

basi hapakuwa na haja ya TUKI (1990) kuunda istilahi **herufijozi** kwa maana ya *diagraph* (badala ya **diagrafu**), au **pichataarifa** (badala ya **pikitogramu**). Hii ni dalili tosha kuwa ukopaji unafanywa bila sababu maalum.

Kadhalika, mbinu ya **kufasiri maana** haitumiwi na TUKI kwa kufuata mantiki sawa kama mfano huu **(101)** unavyothibitisha:

(101a) *lingua franca*===**lugha mawasiliano** (badala ya **lugha sambazi**)

(101b) *linguistic taboo*===**adabu ya lugha** (badala ya **kaida za kiisimu**)

(101c) *mutual intelligibility*===**kusikilizana** (badala ya **uelewanolugha**)

(101d) *mutual exclusive*===**kutoana (uelewanosauti)**

(101e) *nomenclature*===**istilahi sanifu (taaluma sanifu)**

(101f) *psychological subject*===**kiima mantiki (kiima kisaikolojia).**

Istilahi zinazopendekezwa hapo juu (kwenye mabano) tumezibuni sisi na ni maoni yetu kwamba zinaweza kufikia kiwango kikubwa cha ubora, uangavu, na ukubalifu mkubwa kwa walengwa wa Kiswahili. Hivyo basi, si jambo la busara kwa wataalamu wa isimu ya Kiswahili na vyombo vya kukuza lugha hii kuzipinga kwa kisingizio chochote kile kabla ya kuzifanyia tathmini ya 'ufaafu' na 'usayansi' wake. Mbinu ya ukopaji, licha ya kuwa ina wafuasi wengi wanaoiunga mkono katika kukuza lugha, inapaswa kutumiwa kama hatua ya mwisho baada ya kukosekana kwa njia mwafaka za kuendeleza lugha kileksikoni. Ubunaji wa istilahi kutoka lahaja za Kiswahili na lugha za Kibantu haujazalisha istilahi nyingi za isimu (Istilahi chache zilizopo ni kama vile **njeo, ngeli** (Mac William, 1986)).

### 5.1.1.2.1.2 Uambatishaji na Uunganishaji

Uambatishaji na uunganishaji pia hutumika sana na TUKI katika kuunda istilahi za Kiswahili. Mbinu hii ya kuzalisha neno

kutokana na istilahi mbili huru zinazojitegemea hutumiwa katika lugha nyingi duniani (Marchand, 1969).

Wapanuzi wa Kiingereza, kwa mfano, wametumia mbinu ya uambatishaji na uunganishaji katika kuendeleza leksikoni ya lugha hiyo. Kupitia kwayo, maneno yafuatayo yamepatikana:

**Kiingereza:** *airscrew, bandmaster, childlike, graveyard, nosedive, oatcake, outcry, pigtail, n.k.*

Maneno mengine ya Kiingereza ni muhimu sana katika kuunda istilahi ambatani; mathalani maneno yenye viishio vya *man* (kama *postman, frogman, businessman, barman*) na viishio vya *wise* (kama *discussionwise, examinationwise*).

Katika taaluma ya isimu ya Kiswahili, TUKI imetumia mbinu ya uambatanishaji katika kuunda istilahi nyingi za isimu. Mifano **(102)**:

(102a) **uwiliwili**

(102b) **taathiralugha**

(102c) **kiambishindani**

(102d) **kizingamsamiati**

(102e) **kiolezafaridi**.

Istilahi ambatani huchukuliwa kama istilahi moja ikiwa:

(a) Maana yake haiwezi kutambulikana kutokana na upekee wa sehemu zake kama ilivyo katika **lugha-ghaibu**, (au katika Kiingereza, mfano *air-umbrella* na *bubble-car*, au

(b) Istilahi hizo zina ruwaza yenye mkazo wa neno moja, kama ilivyo katika (irabu) **unganifukati** (*centring dipthongs*), au katika Kiingereza, mfano *redbrick* na *paperback*.

Umuhimu wa mkazo na wa kiimbo kinachoshirikishwa unaweza kutambulikana unapolinganisha **kiinitete** na **kiini tete**; **kizingatoni** na **kizinga toni**; au **mrejeosawa** na **mrejeo sawa** (au Kiingereza, *a blackbird* na *a black bird* au *the greenhouse* na *the green house* (Barber, 1964:217). Istilahi ambatani inapopata mashiko baada ya mpito wa kiwakati, mabadiliko ya kifonetiki huifanya itofautiane kabisa na maneno asilia yaliyoizalisha. Elementi ambazo hazipewi mkazo aghalabu hubadilika. Kwa mfano, **elimu** (Tazama, kwa mfano, istilahi **elimumaana** (semantiki), **elimumuundo** (sintaksia)).

Wakati mwingine matamshi ya elementi zote zinazojenga neno ambatani hubadilika na hutofautiana na elementi zake asilia. Mabadiliko ya matamshi ya aina hii yanapotokea, elementi za neno lenye matamshi mapya zinaweza kutumika katika kuunda neno ambatani jipya. Mfano mzuri ni neno ambatani la Kiingereza *nobleman*. Kiunganishi *man* katika *nobleman* kimetumika katika kubuni na kuunda maneno mapya kama vile *postman* na *frogman* ambapo viishio havipewi matamshi sawa na ya neno huru *man* (Barber, 1964:218). Kuhusu hoja hii, Mbaabu (1995:55) anauliza: "Ikiwa tutakopa **steshenimasta** mbona tusikope **piimasta** (*P.E. Master*), **domitorimasta, sabjektimasta,** n.k.?" (taz. 4.2, uk. 133, kwa ufafanuzi juu ya hoja hii).

### 5.1.1.2.1.3 Unyambuaji na Uambishaji

Mbinu za unyambuaji na uambishaji vile vile hutumika sana na TUKI katika kuunda istilahi za Kiswahili. Vitenzi na vivumishi vya

Kiswahili hunyambuliwa kwa kuambishwa, na hivyo hupelekea kwenye uzalishaji wa istilahi mpya. Viambishi awali na viambishi tamati huongezwa kwenye neno la Kiswahili lililopo au kwenye shina la neno katika kuunda istilahi mpya (Abdulaziz 1989:41). Katika Kiingereza, istilahi ambazo zimeundwa namna hii ni kama zifuatazo:

Kiambishi awali *un-* *unconditional, unlucky, untie* na *de-* (kwa kuongezwa kwenye kitenzi) *decontrol, denationalize*

Viambishi awali kama *dis-, pre-, anti-, mis- na pro-* pia hutumika katika kuunda maneno ya Kiingereza. Mfano wa kiambishi tamati ni *ize* ambacho kinaweza kuongezwa kwenye kivumishi (*national, tender, miniature*) au kwa nomino (*carbon, vapour, vitamin*) katika kuunda vitenzi vipya (*nationalize, carbonize*).

Katika Kiingereza cha kisasa, viambishi tamati vinavyotumika sana katika kuunda istilahi mpya ni pamoja na: k.m. *-er bumper, walker, talker, eater; -ist (capitalist, stockist)*, na *-y* ama *-ie (goalie* na *nappy)*. Viambishi vya kiistilahi katika Kiingereza, havitokani na lugha yenyewe asilia, bali vimekopwa na vinatokana na Kigiriki-Latini. ((Tazama Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:30-31) kwa maelezo zaidi juu ya viambishi vinavyounda istilahi za Kiswahili)).

Katika isimu ya Kiswahili, kiambishi cha kiistilahi ambacho kimetumika katika kuundia istilahi nyingi za taaluma hii ni **u-**. Kiambishi awali **u** + shina la jina/kitenzi/kivumishi. Mifano **(103)**:

(103a) **urekibishaji** < rekebisha

(103b) **uleksishaji** < leksia

(103c) **udhahania** < dhahania

(103d) **uradidiaji** < radidi

(103e) **unong'oni** < nong'ona.

(taz. pia Mdee, 1985:134 na Khamisi, 1989:121).

Viambishi vingi vya kiistilahi bado havijapewa visawe vya Kiswahili, na hutoholewa kiholela. Kwa mfano, *ety* = **eti-**: *de-ety* = ?

*ety/etymology*===**etimolojia**

*de-etymologisation*===**uyeyukaji kimofimu**

Kiambishi *iso-* hakijapatiwa kisawe mahsusi cha Kiswahili. Tazama, kwa mfano, iwapo, *iso* ni **kizinga**;

*isogloss*===**kizingasifa** na

*isomorph*===**kizingaumbo**; sasa basi inakuwaje

*isomorphism* ikawa ni **ushabahimiundo?**

Utohoaji wa viambishi kama *idio*===**idio**, *tics*===**tiksi**, *iso*===**kizinga**, n.k. hauna budi kufuata mfumo uliosawa na kuandikwa kwa njia ambayo haitatanishi walengwa wake (taz. *idio*===**idio**).

*idiophone*===**idiofoni**

*idiography*===**idiografia**

*idiolect*===**mtindopeke** (TUKI, 1990).

Kati ya *accent* na *idiolect*, istilahi ipi ni **lafudhi** au ipi ni **mtindopeke?** Uundaji wa istilahi kwa kutumia viambishi vya kiistilahi unapaswa kufanywa na TUKI kwa kuzingatia mantiki na misingi ya kisayansi, na wala siyo kiholela (taz Kiingi, 1989:162 kwa ufafanuzi zaidi wa 'uholela' katika viambishi vilivyosanifishwa na vinavyotumiwa na BAKITA na TUKI katika

taaluma ya sayansi).

#### 5.1.1.2.1.4 Upanuzi wa Maana za Maneno

Mbinu ya kuyapa maneno yaliyopo kwenye lugha maana pana zaidi ya ile yake ya awali hutumika katika lugha nyingi ulimwenguni, ingawa haitumiwi sana na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili katika kuendeleza istilahi za Kiswahili. Umuhimu wa mbinu hii katika kuendeleza istilahi za Kiingereza ni swala ambalo limeshughulikiwa na wataalamu wengi (k.v. Ayto, 1983:96-97; Barber, 1964:219-220).

Barber (1964) anaitambua mbinu ya upanuzi wa maana za maneno kwamba ni mfanyiko unaohusu uhamishaji wa neno kutoka kategoria moja ya kisarufi hadi nyingine; mathalani, kutoka kwa nomino hadi kwa kitenzi, au kutoka kwa kivumishi hadi nomino. Kwa mfano, neno la Kiingereza *market* (soko) lilikopwa kutoka Kifaransa katika karne ya kumi na saba na awali lilitumiwa kama nomino (kama usemi "*a market is held here every Saturday*") (Ridder, 1988). Ingawa hivyo, kwa sasa neno hili limepanuliwa kimaana na linatumika kama kitenzi (kama usemi "*this soap is marketed by E.A.I.*") (taz. Stern, 1931).

Mfanyiko wa upanuzi wa maana za maneno hautumiki sana katika kuunda istilahi za isimu na TUKI, kwa sababu imekuwa vigumu kutofautisha maana mahsusi ya istilahi kutoka kwa maana zake za kawaida. Hata hivyo, mbinu hii imetumiwa sana na Waarabu katika kuendeleza leksikoni yao (Chimerah, 1998). Mifano ya Kiswahili

ya istilahi za namna hii ni kama vile **ubuye** ambalo hapo awali lilitumiwa kwa maana ya **kujificha** kwa watoto wanapocheza, lakini limeongezewa maana katika istilahi za isimu na kuwa ni 'hali ya neno kuwa na umbo ambalo halidokezi maana' (Massamba, 1988:143).

Istilahi **kifulizwa** (*continuant*) pia imeundwa kwa namna hii. Kitenzi **fuliza** maanake asilia ni kutenda jambo bila kupumzika. Kutokana na kitenzi hiki kukapatikana nomino **kifulizwa** (kwa kupanua maana ya neno hili) ambayo imeongezewa maana na kuwa ni 'sauti zinazotamkwa kwa mwendelezo' (taz. TUKI, 1990).

Kama ilivyotajwa mbeleni (3.3.3, uk. 80) mbinu ya kupanua maana ya maneno yaliyopo katika lugha inafaa kuepukwa na vyombo vya kukuza Kiswahili, kwa sababu istilahi zinazopanuliwa maana huwatatiza walengwa wake katika kutofautisha maana zake mbalimbali, hasa kwa nyanja zinazokaribiana na zinazotumia istilahi hizo.

5.1.1.2.1.5 **Ufupishaji**

Kufikia hapa, tumeweza kuonyesha mbinu kuu zinazotumiwa na chombo cha kukuza Kiswahili cha TUKI katika kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili; hata hivyo, ziko pia mbinu ndogo ndogo ambazo kwazo maneno mapya yamepatikana, na hatuna budi kuzichunguza. Mojawapo ya mbinu hizo ni **ufupishaji**.

Aghalabu ufupishaji hutokea kwa kudondosha au kuondoa **sehemu za mwisho wa maneno**, au za **kirai kizima**, au hata silabi ya **kwanza**

ya neno pekee, kama mfano huu **(104)** unavyodhihirisha:

(104a) **faridipekee** kuwa **faridipeke** (*particle*)

(104b) **alatulii** kuwa **alatuli** (*passive articulator*)

(104c) **sifabia sarufi** kuwa **sarufibia** (*universal grammar*)

(104d) **lugha iliyoundwa** kuwa **lughaunde** (*artificial language*).

Mbinu ya ufupishaji imetumika sana katika Kiingereza. Kwa mfano, udondoshaji wa sehemu za mwisho wa neno kama *photograph* kuwa ni *photo*, au udondoshi wa sehemu ya mwisho wa kirai kizima, kama *public house* kuwa ni *pub*, ama *permanent house* kuwa *perm*. Wakati mwingine silabi za **kwanza** ya neno ndizo hudondoshwa, kama *aeroplane* kuwa *plane* (Barber, 1964:220).

Istilahi chache za isimu ya Kiswahili huundwa kwa mbinu ya **uhulutishaji**. Uhulutishaji ni aina moja ya ufupishaji (rejelea **4.3**, uk. 139) ambapo istilahi moja huundwa kutokana na istilahi mbili zenye maana mbili tofauti ili istilahi hiyo mseto iwe na maana changamano (Irira, 1990:13). Mara nyingi silabi moja au mbili za istilahi mbili za awali hudondoshwa ili istilahi mpya ikidhi sifa muhimu ya iktisadi na itamkike kwa urahisi. (Tazama istilahi hizi ndefu: **pembetatu ya kisemantiki** *(semantic triangle)*, **sifa muhimu za lugha** *(intra-linguistic features)*, **elimuugonjwawanawake**/elimuzazi *(gynaecology)* (Kiingi, 1989)).

Katika Kiingereza, maneno kama vile ***brunch*** *(breakfast + lunch)*, ***subtopia*** *(suburban +utopia)*, ***fantabulous*** *(fantastic + fabulous)*, ***infortainment*** *(information + entertainment)*, ***chunnel*** *(channel + tunnel*, na mengineyo yaliundwa kwa namna hii ((taz. pia (**5.1.1.3**,

uk. 248 na 5.1.2.1, uk. 274) mbinu za uundaji istilahi za Nabhany na Chimerah kwa maelezo zaidi juu ya istilahi mahuluti za Kiswahili)).

Kama mifano ya hapo juu inavyoonyesha, mfanyiko wa ufupishaji hutumika sana na TUKI, na ni njia mojawapo maarufu katika kuendeleza leksikoni za lugha nyingi. Mbinu zilizojadiliwa hapo juu ni muhimu na zinatumiwa na TUKI katika kuunda istilahi za isimu. Hii inadhihirisha kwamba kazi ya chombo hiki ya kukuza na kuendeleza Kiswahili haifanywi shelabela, bali inafanywa kwa kufuata misingi maalum ya mbinu za kuundia istilahi za lugha hii ya Kiswahili. 'Usayansi' na 'ufaafu' wa istilahi zinazoundwa na TUKI ni suala ambalo litafafanuliwa baadaye (taz. Sura ya Sita).

### 5.1.1.3 Chombo cha Kukuza Istilahi cha BAKIKE

Kukosekana kwa mwongozo kuhusu ukuzaji wa istilahi za Kiswahili kulisababisha hali ya kutaka kuwepo Baraza la Kitaifa za Kiswahili au Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili nchini Kenya. Mwaka wa 1987 **Baraza la Kiswahili Kenya** (BAKIKE) lilianzishwa kwa minajili ya kuikuza lugha ya Kiswahili na kuisambaza kila pembe nchini na baina ya nchi. (Hivi sasa pia kuna BALUTA - Baraza la Lugha la Taifa, ambalo limepitishwa na bunge).

Kwenye jarida moja la *Mwangaza wa Lugha*, ambalo ni chombo kinachotumiwa na Baraza hili kusambaza lugha, tunasoma:

> ...Kenya ndipo mahala palipozaliwa lugha ya Kiswahili, lakini...leo nchi ya Kenya imeachwa nyuma katika harakati za kukuza lugha hii...shabaha yetu ya kubuni shirika

hili ni kutaka kuiondolea nchi yetu fedheha hiyo...na kuikuza lugha hii ya taifa.
(Maoni ya Mhariri, Jan-Feb 1988:3)

Kutokana na dondoo hili, ni dhahiri kwamba Baraza lina lengo kuu la kuendesha uchunguzi wa lugha kwa madhumuni ya kukikuza na kukistawisha Kiswahili. Shughuli za Baraza hili, ambazo ni za kitaifa zaidi kuliko kimataifa, haziendelei sana kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kutosha, kutoungwa mkono na serikali, na aidha ukosefu wa wanaistilahi bingwa ndani ya Baraza. Tatizo hili limeleta wasiwasi mkubwa juu ya uwezo wa BAKIKE wa kuendeleza Kiswahili kileksikoni kwa ufanisi. Ndiposa si ajabu kwamba hadi sasa, Baraza limechapisha majarida **manne** tu yenye mada *Mwangaza wa Lugha* na *Lugha na Utamaduni*. Toleo la mwisho lilichapishwa mwaka wa 1990. (Tulifahamishwa na Said Karama, mweka hazina wa BAKIKE, kwamba ombi la Baraza la msaada wa kifedha kutoka kwa serikali ya Kenya na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's) halijapata mafanikio yoyote).

Tatizo la kifedha (na la uongozi) litakapotatuliwa, Baraza, ambalo linaelekea kufifia na halitambulikani kwa Wakenya wengi, litapanua shughuli zake ili ziwe za upeo wa kimataifa na wala si kitaifa tu. Jukumu la kukikuza Kiswahili kiistilahi lilipewa Ahmed Sheikh Nabhany, ambaye pia ni Mdhamini wa Baraza la Kiswahili Kenya na mwandishi wa makala ya 'ISTILAHI ZA LUGHA.'

Kama ilivyotajwa katika utangulizi wetu wa sura hii, mbinu za uundaji wa istilahi za BAKIKE haziwezi kutofautishwa na mbinu za A.S. Nabhany za kukuza na kuendeleza Kiswahili, kwa sababu ni yeye (Nabhany) aliyepewa jukumu hili kulitekeleza kwa niaba ya

Baraza. Kwa hivyo, mbinu za BAKIKE na za Nabhany za kuundia istilahi za Kiswahili ni suala ambalo litashughulikiwa hapa kama suala moja lisilopaswa kutenganishwa.

#### 5.1.1.3.1 Uundaji wa Istilahi: Mbinu za Nabhany

Mbinu za uundaji wa istilahi zinazotumiwa na BAKIKE/Nabhany ni pamoja na;

**Ufupishaji** (uunganishaji, uhulutishaji, na ukatizaji).

**Ufufuaji** na upanuaji wa maana za msamiati asilia na wa kilahaja.

**Ubunaji**, kwa maana ya kutafsiri au kufasiri maana za maneno.

Wataalamu walioshughulikia kazi za Nabhany za kukuza Kiswahili (k.v. Ridder, 1988; Mbaabu, 1989; Mwaro, 1993; Chimerah, 1998) wanaelekea kukubaliana kwamba mbinu ya Nabhany ya kukikuza Kiswahili kileksikoni kwa **kurejea-nyuma-hadi-kwenye-mizizi-ya lugha yenyewe** ni mwafaka na inafaa kutumiwa na wataalamu na waundaji istilahi za lugha hii iwapo lengo la kukitanua Kiswahili litafanikiwa.

A.S. Nabhany, mzaliwa wa Lamu anayeishi Mombasa, ni mtaalamu mtajika katika Kiswahili. Msimamo wake, ambao hauelekei kupwayapwaya, unatetea ukale wa Kiswahili na lahaja zake. Katika 'kupigania' ukale wa lugha hii ya Kiswahili, na kama jaribio muhimu la kukiendeleza Kiswahili, amekusanya istilahi za kale ambazo zimefunua utajiri wa kiistilahi wa Kiswahili katika fani mbalimbali zikiwemo za kisayansi na kiteknolojia. Maneno aliyoyabuni, na aliyokusanya, yanapatikana katika machapisho na tungo zake mbalimbali kama vile, *Utenzi wa Sambo ya Kiwandeo/ The*

*Ship of Lamu-Island* (1979), *Kandi ya Kiswahili* (1978), *Umbuji wa Kiwandeo* (1985), shairi la "Umbuji wa Mnazi" (1985) na makala: "Kiswahili Chajitosha" (TUKI, 1976), "Uundaji wa Istilahi katika Kiswahili" (1998) na makala mengineyo ya istilahi za lugha.

Katika "Umbuji wa Mnazi," Nabhany (1985:xxviii) anatufichulia madhumuni ya kuunda istilahi za mambo ya kale na anasema:

> Madhumuni ya mtunzi yalikuwa mawili: Kwanza, kuudhibiti msamiati na utamaduni wa lugha juu ya mambo yanayohusiana na mnazi kwa ajili watu wa siku zijazo wanufaike. Pili, kutaka kuwafunza wenziwe faida za mnazi kwa ajili ya kuwatia hima katika ukulima wao.

Mbali na kutaka kuelimisha vizazi vijavyo juu ya 'ukwasi' wa Kiswahili, ilhamu ya mtaalamu huyu ya kubuni maneno ilitokana na kutoridhika kwake na maneno mapya yaliyoundwa na 'mabingwa wa lugha' walioko Tanzania. Nabhany (1998:2) anatudokezea kuwa:

> Niliona kwamba watu walibuni neno la kuwakilisha *television* wakaliita **kisanduku cha sanamu** au **kiona mbali** ndipo nikaona umuhimu wa mimi nichangiye katika jambo hili kwa sababu mimi mwenyewe ni Mswahili na nina haki ya kubuni na nina ujuzi wa lugha ya Kiswahili...

Ni muhimu isisitizwe hapa kwamba, Kiswahili ni mojawapo wa lugha zinazokua kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa hivyo, ili kukidhi maendeleo ya taaluma hizi, uundaji wa istilahi mpya ni suala ambalo haliwezi kuepukwa. Istilahi mpya, kwa mujimbu wa Nabhany (1982), huundwa baada ya kukosekana kwake katika lahaja (ndimi) kumi na tano (15) za Kiswahili kwa kufuata misingi na kanuni maalum. Misingi inayofuatwa na BAKIKE/Nabhany ni pamoja na kubuni istilahi kwa kuzingatia:

i) Umbo la kitu

ii) Utendajikazi wa kitu; na

iii) Sauti au mlio wa kitu.

(linganisha pia na misingi ya TUKI katika 5.1.1.2, uk. 230).

Upo utaratibu na kaida zinazofuatwa na jopo la istilahi la BAKIKE la kukuza Kiswahili katika kuzipata istilahi za taaluma. Baraza limeweka utaratibu huu ambao ulianza kutumika tangu mwaka wa 1987 wakati Baraza lilipoanza kushughulikia ukusanyaji wa istilahi za Kiswahili. Ufuatao ndio mwongozo wa utaratibu uliowekwa na unaofuatwa na BAKIKE katika uundaji wa istilahi:

i) Istilahi mpya zinatakiwa zibuniwe baada ya kuhakikisha kuwa hazimo kabisa katika Kiswahili chenyewe.

ii) Kukosekana kwa istilahi hizi kutoka Kiswahili chenyewe humlazimu muundaji istilahi kutazama katika lahaja zote za Kiswahili istilahi nyingine yo yote ambayo maana yake inaelekea kukaribiana na hiyo istilahi anayotaka kubuni.

iii) Ukosefu wa istilahi ya aina hiyo katika lahaja zote za Kiswahili, huzua haja ya kutazamwa katika lugha za makabila ya Kibantu ambayo yana uhusiano wa karibu wa Waswahili.

iv) Kama pia katika makabila hayo istilahi imekosekana, hapo ndipo muundaji istilahi atakapotumia **mbinu ya kuunganisha vipande viwili au vitatu vya maneno ya Kiswahili na kuunda neno moja.** Istilahi hiyo inayobuniwa iwe ni rahisi katika kutamkika na kuandikwa. Isiwe ni kavu yenye kukwaruza-kwaruza umbuji wa ufasaha wa ulimi wa Kiswahili (Nabhany, 1988:5).

v) Utaratibu wa tano wa kubuni istilahi ni kufuata taratibu za asili (zilizokuwa zikifuatwa na Waswahili wa kale) za kuchagua istilahi yo yote ya kubuni kutoka katika wazo la

mwenye kubuni, ikibandikwa juu ya kitu hicho kilichokosa jina kiitwe kwa jina hilo. ((Taratibu za BAKIKE hazijishughulishi na utohoaji ama ukopaji kutoka lugha za kigeni (Kiarabu, Kiingereza, n.k.) kwa sababu ya imani nyeti kwamba maneno mengi ya mkopo yana visawe vyake vya Kibantu na Kilahaja za Kiswahili)). Mbinu za uundaji istilahi zifuatazo zitafafanua hoja zilizotolewa hapo juu.

### 5.1.1.3.1.1 Ufupishaji: Uunganishaji na Uhulutishaji

Mbinu mojawapo muhimu inayotumiwa na BAKIKE/Nabhany katika kuunda istilahi za Kiswahili ni **ufupishaji**. Ufupishaji, kama ulivyotajwa mbeleni (rejelea 5.1.1.2.1.5, uk. 246), ni mfanyiko wa kupunguza urefu wa istilahi za kawaida kwa kudondosha sehemu fulani za istilahi hizo. Ni muhimu kuzingatia kuwa ufupishaji wa istilahi haufanywi mbagambaga bali kwa kufuata mantiki na misingi ya kisayansi ya uundaji istilahi. Kuna aina nne (4) za ufupishaji. Hizo ni:

- Uunganishaji
- Uhulutishaji
- Akronimu, na
- Ukatizaji.

Mifanyiko ya **uunganishaji** na **uhulutishaji** ndiyo hutumiwa zaidi na BAKIKE/Nabhany. Mifanyiko ya ufupishaji inaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

**Uunganishaji** - ni mbinu ya kuunda istilahi/neno moja kutokana na kuunganisha maneno mawili, au matatu. Mbinu hii imetumiwa sana na Nabhany katika kuunda istilahi nyingi za Kiswahili kama mfano

huu **(105)** unavyodhihirisha:

(105a) **runinga** (*television*)

Asili na usuli wa neno **runinga**, ambalo limeshika sana kote kuzungumzwako Kiswahili (Chimerah 1998b:10), ni kuwa neno hili linatokana na maneno mawili yaliyofinyangwa kitaalamu na kuundwa neno moja. Maneno hayo hayo ni:

**rununu** (sauti kutoka mbali) + **maninga** macho yaonayo mbali (rununu ya 'kuenga'/kutazama kwa macho/'maninga').

(Kwa maoni ya mbunaji, awali, Watanzania walikiita chombo cha **televisheni** 'kisanduku cha masanamu,' na baadaye wakakiita 'kiona mbali.').

(105b) **ulimbe** (sayansi)

Neno **ulimbe**, lenye umbo la Kibantu, limeundwa kwa kutumia muunganisho wa maneno matano yaani:

**Utaalamu** wa **uchunguzi** wa **ulimwengu**, **uundaji**, na **viumbe**

Herufi [u] inawakilisha maneno: **utaalamu** na **uchunguzi**, [li] inawakilisha neno **ulimwengu** (na **uundaji**) na **mbe** inawakilisha neno **viumbe**.

Kwa msingi wa **utendajikazi wa kitu** na kwa mbinu ya uunganishaji, Nabhany pia ameunda maneno yafuatayo;

(105c) **barua pepe** - *e-mail* (**barua** ya kupeperushwa)

(105d) **pataninga** - *video* (pacha/**pata** ya runinga)

(105e) **mwengoya** - *radio* (**mwengo**-sauti kutoka mbali - ya kuya/ kuja)

(105f) **uyoka** - *x-ray* (uyoo = picha, nyuka = rays; picha

inayotolewa na nyuka)

(105g) **wewindu** - *focus* (**weu** - mwangaza, **windu** - kungu).

(taz. *Kandi ya Kiswahili*, 1978)

Inaelekea Nabhany (1978, 1998) na Chimerah (1998:11-14) hawatofautishi mbinu za kuunda istilahi za **uunganishaji** na **uhulutishaji**. Ingawa wataalamu hawa wanatueleza kwamba neno **runinga** (na mengineyo yaliyomo kwenye mfano wa **105**) liliundwa katika "mkombo/utaratibu wa nne" wa kuunganisha maneno mawili au matatu, ilivyo ni kwamba mbinu ya uhulutishaji ndiyo iliyotumika. Istilahi **runinga**, **ulimbe**, n.k. ni istilahi mahuluti na ziliundwa kwa mfanyiko wa uhulutishaji (taz. **4.3.2**, uk. 143) na wala siyo uunganishaji pekee.

**5.1.1.3.1.2 Ufufuaji na Upanuaji wa Maana za Msamiati Asilia**

Mfanyiko wa ufufuaji na upanuaji wa maana za msamiati asilia na wa kilahaja pia umepewa uzito sana na BAKIKE/Nabhany. Ufufuaji na urudishaji katika matumizi kwa msamiati asilia ambao haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu, unajikita katika misingi kwamba kuijenga lugha ndani ya lugha ndiko kuiendeleza lugha (rejelea pia **4.6**, uk. 150).

Baraza la Kiswahili Kenya (BAKIKE)/Nabhany, katika harakati za kuipunguzia lugha ya Kiswahili istilahi mkopo (hasa maneno ya Kiarabu na Kiingereza) limeona ni aula kuingiza istilahi zaidi za Kibantu na za Kilahaja katika Kiswahili kwa kutumia mbinu ya ufufuaji. Ukuzaji wa istilahi za lugha kwa mfanyiko wa ufufuaji umetumika katika lugha nyingi. Kwa mfano, Kiingereza kilijipatia

istilahi za kilahaja kama vile *bogie, flange, trolley* (Barber, 1964:221). Kwa njia hii, istilahi nyingi za lugha ya Kiingereza, kama ilivyo Kiswahili, pia 'zilikufa' na nyingine faafu kuzuliwa. Katika Kiingereza, maneno yaliyokufa ni, kwa mfano, *sweg* (makelele), na *wered* (umati wa watu) (Aitchison, 1981 na Barber, 1964:222-224). Katika kusisitiza matumizi ya maneno asilia ya Kiswahili/Kingozi badala ya maneno mkopo, Nabhany anaweza kulinganishwa na Eliezer Ben-Yehuda (1857-1922) ambaye anatambuliwa kama mwasisi wa 'ufufuaji wa Kihebrania/Kiyahudi.' Ben-Yehuda alitetea sana mbinu ya ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo wa istilahi za kisayansi na kiteknolojia za Kihebrania. Istilahi asilia zilizofufuliwa zilitumiwa katika maandishi, maongezi na mawasiliano ya kila siku katika jamii ya Wayahudi, na kwa namna hii, kuipunguzia lugha ya Kihebrania U-Arabu mwingi kileksikoni (Rabin, 1989:26-37).

Mifano ifuatayo **(106)** inafafanua hoja iliyotolewa hapo juu kuhusu istilahi zilizohuishwa kimaana:

(106a) **mangala** - *microscope* (taz. katika *Kamusi ya Visawe*, 1998:130)

**Mangala** ni istilahi iliyopewa muktadha mpya wa matumizi kutokana na methali. Kulingana na fikira za Waswahili, **mangala** ni chombo ambacho hufanya samaki mdogo (k.v. mtumbuu) kuonekana na umbo kubwa sana (umbo la papa). Ndipo Waswahili wakasema, "Usiku ni mangala, dagona huona papa."

(taz. pia **hadubini** kwa maana ya *"microscope"* lililoundwa na Sheikh Jamil Rafiq mwaka wa 1977 na kukubalika na BAKITA)

(106b) **mapisi** - historia

(106c) **ngosi** - *energy* (taz. pia **kawi/nishati/ngondo**)

(106d) **mwai** - *oxygen*

(106e) **tungondo** - *hygiene*

Mifano zaidi **(107)** ya maneno asilia ya Kiswahili/Kingozi ni:

| | Kiswahili Asilia | Kiarabu |
|---|---|---|
| (107a) | **darasoo** | lazima |
| | **ndeo** | kiburi |
| | **mize/miche** | malikia |
| | **jagina** | shujaa |
| | **kievu** | dhaifu |
| | **kiyandipota** | risasi |

Mbinu hii ya kuendeleza istilahi mumo kwa mumo inaungwa mkono na wataalamu wengi (k.v. Mdee, 1980; 1981; na Akida, 1977).

#### 5.1.1.3.1.3 Ubunaji: Kufasiri Maana za Maneno

Ubunaji ni uwezo wa kujitokeza na fikira za kiisimu zinazomwezesha mwanalugha kuimarisha istilahi zilizopo kwa kuzipa sura nyingine, au muktadha mwingine wa utumizi (Mwaro, 1993:88). Mbinu ya ubunaji na kufasiri maana za maneno pia inatiliwa uzito na BAKIKE/Nabhany katika kukuza Kiswahili. Mbinu hii pia imetumiwa sana na Waarabu katika kuipanua lugha yao kiistilahi (Temu, 1972; Chimerah, 1998).

Katika Kiswahili, mbinu ya ubunaji na kufasiri maana za maneno kutoka lugha za kigeni (hasa Kiingereza) imetumika katika kuunda istilahi za lugha hii na BAKIKE/Nabhany "kwa minajili ya kukitia

ulimbwende uhitajikao Kiswahili" (Chimerah, 1998b:10). Mifano ya istilahi zilizoundwa kwa misingi ya maana ya neno na utendajikazi wa kitu na kwa kutumia mbinu hii ni **(108)**:

(108a) **ngamiza** - *computer* (kompyuta)

(108b) **pepesi** - *fax* (faksi)

(108c) **fumano** - *reflection* (nunuriko)

(108d) **vuguto** - *heater*

(108e) **kwezo** - *lift*

(108f) **mshabeko** - *jeck*

(108g) **koto** - *overtime* (ajari) (taz. Mdee, 1980)

(108h) **mfumbati** - *secretary* (katibu).

Maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu ya ubunaji na kufasiri maana ya maneno ni mengi. Haya ni **baadhi** tu ya meneno hayo, (mengine ni kama **mtuso** (*bump*), **uka** (*ray*), **upili** (*secondary*), **keteo** (*roundabout*), **mpeki** (*driver*), n.k.). Jopo la istilahi la Baraza la Kiswahili Kenya linaendelea kukikuza Kiswahili kwa kuibunia lugha hii istilahi ambazo zina "Ubantu zaidi na wala si Uzungu" (Nabhany, 1978). (Taz. pia neno **funditi** - *geography* lililoundwa na Sheikh Said Mohammed Sharrif Saidi na Nabhany).

Hadi sasa wanalugha binafsi ambao wamejitokeza na mbinu tofauti za kuendeleza istilahi za Kiswahili mbali na Nabhany (1982), ni Chimerah (1998), Mbaabu (1985), Kapinga (1983), S.A.Mohamed (1995), miongoni mwa wengine. Hapa tutaeleza njia zao za kukuza Kiswahili.

### 5.1.1.4 Ukuzaji wa Kiswahili: Chombo cha CHAKITA

Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA) ni chombo kimojawapo muhimu katika taifa la Kenya kinachoshughulikia ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili. Mwaka wa 1997 ulikuwa ni 'mwanzo mpya' kwa wapenzi na wanalugha wa Kiswahili, kwani chama cha CHAKITA kiliundwa kwa ajili ya kupanua lugha hii katika uwanja wa mawasiliano na taaluma za elimu. Tangu mwaka huo, CHAKITA huandaa makongamano ya kimataifa, na makala yanayowasilishwa baadaye huchapishwa katika jarida linaloitwa *TAALUMA*. Hadi sasa, wanachama wa CHAKITA ambao inaelekea wamepata kariha ya kuzalisha istilahi za Kiswahili ni Kimani Njogu, Chimerah na Mbaabu. Huku Kimani akishughulikia fasihi, na Mbaabu akielemea uwanja wa isimu, Chimerah ameelemea zaidi upande wa vitumeme (elektroniki) ambao unapanuka kila uchao. Ukweli ni kwamba upanuzi wa Kiswahili kiistilahi unahitajika katika kila uwanja (taz. Mukama, 1989), na hata zaidi katika uwanja wa mawasiliano ambapo kuna mazoea ya kutumia maneno mkopo ya Kiingereza hata pasipo na lazima yoyote (Massamba, 1989:66).

Chimerah, baada ya kugundua kuwa kuna istilahi makosa zilizoingizwa katika KIswahili (kama vile **mazingara, uana, nasibu, msaada** *(Aids)*), amependekeza kuwa istilahi za kisayansi zinazoundwa zisiwe kakamavu bali ziweze kunyambulika ikilazimu. Kutokana na msimamo huu, mwanalugha huyu ameweza kubuni istilahi za Kiswahili kama vile **tarakilishi** (taz. mfano wa **109b**). Neno la Kiingereza *"computer"* lenyewe ni la mnyambuliko. Ni nomino inayotokana na kitenzi cha Kiingereza *"compute."* Neno

**tarakilishi** limebuniwa kutokana na sababu kwamba neno mkopo tulilonalo **kompyuta** halituelekezi moja kwa moja katika maana ya chombo hicho (taz. pia 6.0, uk. 315). Si tu, kitenzi cha Kiingereza, *"compute,"* ambacho ndicho kilichozaa neno kompyuta, kimepuuzwa kabisa katika Kiswahili. Kulingana na Chimerah, wabunaji wangebuni istilahi ya neno *"compute"* kwanza, kabla ya kupendekeza neno 'kimelea kompyuta.' Huku ni kupuuza mizizi, na badala yake kung'ang'ania matawi. Hapa tutatoa maelezo ya jinsi mwanalugha huyu anavyozalisha istilahi za Kiswahili.

**5.1.1.4.1 Njia ya Chimerah ya Kuendeleza Istilahi za Kiswahili**

R.M. Chimerah, kama ilivyotajwa hapo awali, ni mmoja wa wataalamu binafsi ambao wamepata kariha ya kubuni istilahi mpya za Kiswahili. Kutokana na maelezo ya Chimerah (1998b:12) mwenyewe katika makala: "Kiswahili Jana na Leo na Kesho, Swāla la Msamiati" amebuni maneno kwa 'kufuata nyayo' au misingi ya mbinu alizozitumia Nabhany. Njia za uundaji istilahi zinazotumiwa na mwanaistilahi huyu ni **unyambuaji, upanuzi wa maana za maneno, kufasiri maana za maneno, uhulutishaji, akronimu, upanuaji wa maana za maneno asilia ya Kibantu, kaleki na ukopaji** (kutoka Kiarabu na Kiingereza). Hapa tutaeleza.

**5.1.1.4.1.1 Uhulutishaji na Akronimu**

Njia hii ya uundaji istilahi, kwa ufupisho wa maneno yanayotumiwa kwa pamoja, kwa kuchukua sehemu fulani za neno ili kuunda neno jipya, imetumika sana na Chimerah (1998) katika kuzalisha

istilahi za Kiswahili. Kuna istilahi nyingi zilizobuniwa kwa kufuata mbinu ya uhulutishaji na akronimu kama mfano huu **(109)** unavyoonyesha:

(109a) **zutafindaki** limeunganishwa kutokana na maneno **zuo** + utafiti + kinda**kindaki** (mahali panaposhughulikiwa vyuo na utafiti kwa ukamilifu)

(109b) **tarakilishi** - (kompyuta)

Neno mahuluti **tarakilishi** limeundwa kutokana na **tarakimu** + **akili** + **mashine** (yaani) 'mashine inayoparanya tarakimu kama akili.' Chimerah amependekeza kuwa neno **tarakilishi** linaweza kuwa na kisawe **tarabongo** ambapo **ubongo** ni neno asilia la Kiswahili ilhali akili ni neno ambalo asili yake ni Kiarabu. Matumizi ya **tarabongo** ni hatua muhimu ya kukipunguzia Kiswahili maneno mkopo ili lugha hii ibakie, kama anavyopendekeza Nabhany (1982), katika U-bantu. Hata hivyo, neno **tarabongo** lina udhaifu namna mbili kulingana na Chimerah: Kwanza, dhana ya mashine inakosekana katika neno hili. Pili, halinyambuliki, na huu ni udhaifu mkubwa kwa kuwa kuna dhana nyingi changizi ambazo zinaweza kuibuliwa na dhana kuu ya *'computer,'* kama tutakavyoonyesha hapo chini.

Neno **tarakilishi** linaponyambuliwa, linazalisha maneno kadhaa mengine kama **nitarakilishie, kutarakilisha, utarakilishaji, tarakilishika, tarakilikika,** n.k. Kwa kutumia ujuzi huuhuu, Chimerah ameunda maneno zaidi.

Mifano:

(109c) **vitumeme** *(electronics)* - **vitu** + **umeme** (ambapo u hiyo hiyo moja ipo kwa maneno yote mawili).

(109d) **kitumeme** *(electronic device)* - **kitu** + **umeme** .

(109e) **ochoma** *(navigate)* kutokana na uhulutishaji wa ongoza + chombo + majini.

Mfano zaidi wa maneno yaliyoundwa kwa njia hii ni **umenke/menke** (*genderhood/ gender*), **tarifalishi** (*e-mail*), na neno **tanuvuguti** pamoja na kitenzi chake **tanuvuguta**. Aidha amependekeza **warakameme** au **baruameme** kama visawe vya **tarifalishi**, japo anaona ya kwamba tatizo la visawe hivyo ni kwamba yameganda; yaani hayanyambuliki kama **tarifalishi** linavyoweza kunyambulika kwa urahisi: mfano **tarifalisha**, **nitarifalishie**, n.k. Kulingana na Chimerah, maneno yaliyobuniwa na wataalam wengine kurejelea dhana ya *"e-mail,"* yamezingatia *"mail"* nomino tu, na kupuuza *"mail"* kitenzi (yaani *"mailing"*). Chimerah anaona hili pia ndilo tatizo la maneno **baruameme** na **warakameme**.

Chimerah na Nabhany sio wanalugha peke yao wa Kiswahili wanaotumia mbinu ya uhulutishaji na akronimu katika kuendeleza leksikoni za lugha hii ya Kiswahili. Neno **UKIMWI**, lilibuniwa kutokana na maneno **U**kosefu wa **KI**nga **MWI**lini, na limepata mashiko ya kimataifa. Wanajopo wa kipindi cha redio ya Kenya, "Lugha Yetu," wakiongozwa na marehemu Profesa Jay Kitsao, ndio walioubuni neno hili **UKIMWI** wakitumia pia mbinu ya akronimu na uhulutishaji.

#### 5.1.1.4.1.2 Ubunaji: Fasiri ya Dhana za Kigeni

Njia ya ubunaji kwa kutafsiri au kufasiri dhana za kigeni kutoka lugha changizi hadi kwa lugha pokezi pia imetumiwa sana na Chimerah katika kuendeleza istilahi za Kiswahili. Watetezi wa

mbinu hii ya kuunda istilahi, baada ya kutambua dhana na mfumo wake (Tumbo 1982, Nabhany 1982, Marshad 1984), wanadai kwamba ni mfanyiko zalishi na umetumiwa katika kuendeleza leksikoni ya lugha nyingi ulimwenguni, hususan Kiarabu.

Kupitia kwa njia ya kufasiri na kupanua maana ya maneno kutoka lugha nyingine hadi Kiswahili, Chimerah amebuni istilahi nyingi, kama inavyodhihirishwa katika mfano **(110)** huu:

(110a) **vutoti** - *gravity* (nguvu kuu zinazovuta chini)

(110b) **ripukochi** - (**volkeno**) (mripuko kutoka chini, ardhini)

(110c) **vitumeme** - *electronics*

(110d) **kipanya** - *computer mouse*

(110e) **kiwaa** - *screen*, **kuwiza/kung'aza/kuwisha** (*to screen*)

(110f) **shemeretua/shemereshi/kidhibiti** - *remote control*

(shemeretua ndilo linalopendelewa na mbunaji mwenyewe)

(110g) i) **wazogande/dhanagande** - *stereotype*

ii) **nyazogande/dhanagande** - *stereotypes*

(110h) i) **kutumbisha** - *cloning*

ii) **kitumbi** - *clone*

Haya ni baadhi ndogo tu ya maneno yaliyobuniwa na msomi huyu kwa 'kufuata nyayo' za Nabhany, kama anavyodai yeye. (Tathmini ya usayansi katika mbinu hii ya uundaji istilahi na istilahi zilizoundwa tazama 5.2.1.2, uk. 300).

#### 5.1.1.4.1.3 Ufufuaji na Upanuaji wa Maana za Msamiati Asili wa Kibantu

Katika harakati zake za kuiendeleza lugha ya Kiswahili kileksikoni, mbunaji istilahi Chimerah amekuwa akitumia vile vile

njia ya ufufuaji na upanuaji wa maana za maneno asili ya Kibantu na ya kilahaja. Ni muhimu kuzingatia kuwa juhudi ya kukuza lugha hii, hasa kiistilahi, zinahitajika kwa haraka sana na kama anavyodokeza Chimerah (1998:46); wala hazipaswi kuachiwa 'mabingwa' wa lugha peke yao.

Mifano ya istilahi ambazo zimeundwa kwa njia hii ni kama ifuatayo **(111)**:

(111a) **kiyuweo** - *(laptop)* kutokana na neno **kiweo** *(lap)* na **iyu** *(top)*.

(111b) **kiwaa** - *(screen)* kutokana na **waa** (angaza), **kuwiza** *(to screen)* kutokana na **kuwaa** (kung'ara).

(111c) **sakima** - *memory*; **sakimu** - *memorise* (katika tarakilishi).

(111d) **kikumbi** - *computer disk*.

(111e) **thakala** - *hard disk* (kutokana na Kiarabu.

(111f) i) **ndiakuu ya mawasiliano** - *information highway*.

ii) **ndiakuu shadidi ya mawasiliano** - *information superhighway*.

(111g) **tondomiza** (au ngoimiza) - *compact disk* (kifaa kinachoshika maongezi au nyimbo bila ukingo).

Ni muhimu isisitizwe hapa kwamba ingawa Chimerah (1998:47) ni mtetezi wa mbinu ya kuundia istilahi ya **ukopaji**, na anapendekeza kwamba kuikuza lugha kwa kutazama **nje ya lugha** (na wala siyo mumo kwa mumo) ndiyo njia ya kimapinduzi zaidi, yeye mwenyewe haitumii sana mbinu hii, tofauti na wataalamu wa TUKI na BAKITA. Labda ni kwa sababu, kama Nabhany, maneno ya lahaja za Kiswahili za mwambao wa Kenya, pamoja na yale ya lugha jirani za Kibantu zinazohusiana kwa ukuruba zaidi na Kiswahili yanamjia kwa wepesi

zaidi akilini mwake. Vilevile, ni azma ya Chimerah kubuni maneno ya lugha za Kibantu mahali ambapo katika eneo zima la msamiati, maneno yanayotumika ni ya kigeni tu ilhali Kiswahili kinaweza kubeba dhana zozote, za kisayansi zikiwemo, vizuri sana kama mifano hii inavyodhihirisha:

**Majina ya Sayari**

| **Asili ya Kibantu** | **Kiarabu** | **Kiingereza/ Kigiriki-Latini** |
|---|---|---|
| **yeyuzi** | zaibaki (au zebaki) | *mercury* |
| **kombezi** (lenye kung'ara kama kombe *(shell)* **-zi**=ukubwa) | zuhura | *venus* |
| **ntizi/tiatizi** (mama wa udongo au nchi) | ardhi/dunia | *earth* |
| **ngeuzi** (nyekundu) | mirithi | *mars* |
| **pwagizi** (kubwa na inayotisha) | mushtarii | *jupiter* |
| **viringizi** (ya miviringo) | saratani | *saturn* |
| **nilizi/mbingizi** (ya buluu kama mbingu) | utaridi | *neptune* |
| **janizi** (ya kijani kibichi) | zohali | *uranus* |
| **upezi** (iliyo katika upeo wa mbali zaidi) | kausi | *pluto* |

Maneno yote katika eneo hili ni ya Kiarabu. Kinachodhihirishwa katika uundaji huu wa maneno ni kwamba Kiswahili kina uwezo wa kujiendeleza mumo kwa mumo. Ni jukumu la waundaji istilahi, wasomi, na wanalugha kuwa wabunifu zaidi ili kuipunguzia lugha hii istilahi mkopo zisizo na ulazima wowote.

#### 5.1.1.4.1.4 Unyambuaji

Mbinu ya unyambuaji pia imetumiwa na Chimerah katika kubuni istilahi nyingi za Kiswahili. Mbinu hii ya ubunaji istilahi imetumika sana na mwanalugha huyu kutokana na azma yake kwamba maneno yanayoundwa yasiwe makakamavu bali yaweze kunyambulika. Istilahi za Kiswahili ambazo zimeundwa na Chimerah kwa njia hii ni:

**utandaridhi** - *globalisation*

Neno **utandaridhi** ni mnyambuliko unaotokana na unganisho la maneno mawili: **kutanda** *(to spread)* + **aridhi** *(the globe)*. Mfanyiko huu zalishi umetumika na msomi huyu katika kubuni, kwa njia ya unyambuzi, maneno yafuatayo:

**utandaridhi** - *globalism*

**kitandaridhi** - *global*

**mtandaridhi** - *globalist*

**tandaridhisha** - *globalize*

**kiutandaridhi** - *globally*

**kijiji kitandaridhi** - *global village* (taz. usemi: Ulimwengu ni kijiji kitandaridhi tu *(the world is just a global village)* (taz. pia maneno **utandawazi**===*"globalization"* lililopendekezwa na Mwaro, 2000, kutokana na maneno mawili **kutanda** + **uwazi** (u inadondoshwa) na pia **zingiro** (mzunguko/duwara, neno lililopendekezwa na Nabhany (1998)).

Neno **kutandaridhi** limebuniwa kutokana na msingi kwamba visawe vyake vya kiistilahi vilivyobuniwa na wanaistilahi wengine, vilivyoko, havinyambuliki. Mbali na kuwa hayanyambuliki, neno

linalopendekezwa **umataifa** (taz. pia Kapinga, 1996:47) linawahangaisha walengwa wake manake '**umataifa**' ni *international*. Katika maendeleo mengine, kutokana na neno la Kiingereza *"code,"* Chimerah (1999:19) amependekeza **koda**, ambalo analinyambua jinsi ifuatavyo: **kukoda** *(to code)*, **kukodua** *(to decode)*, **kukodesha** *(to codify)*, **kukodewa** *(to be coded for)*, **kukodea** *(to code for)*, **kikodua** *(decoder)* au **kikodushi** (*decoder*, kifaa), **mkodua** *(decoder*, mtu*)* au **mkodushi** (*decoder*, mtu), **toboa koda** *(break the code)*. Pia **fichua koda** *(break the code)*, **nambakoda** *(code number)*.

Katika kuzingatia mfanyiko wa unyambuaji wa kileksia, Chimerah pia huendeleza istilahi kwa kuyachunguza na **kuyanyambua maneno yaliyobuniwa na watu wengine**, kama mifano hii inavyodhihirisha:

| **Maneno Yaliyobuniwa na Nabhany** | **Maneno Mnyambuliko ya Chimerah** |
|---|---|
| **runinga** (televisheni) | **runingisha** *(to televise)*.<br>**runingishwa** *(to be televised)*. |
| **rununu** (simu) | **nukununu** *(fax message)* kutokana na uunganishaji wa **rununu** (ujumbe uletwao kwa simu) + **nukuu** *(copy)*.<br>**nukununishi** *(fax machine)* yaani kitu ambacho hunakili ujumbe yuletwao kwa simu.<br>**nukununisha** *(fax)* - kitenzi kutokana na **nukununishi**. |
| **mangala** (taz. mfano 106a) | **ningala** *(telescope)* - uunganishaji wa **runinga** + mangala. |

**uka** *(ray)* **uka-mraba** *(x-ray)*.

**5.1.1.4.1.5 Uendelezaji wa Maneno 'faafu' Yaliyoundwa na Watu Wengine**

Kutokana na sababu kwamba Chimerah hajaunda istilahi maalum kwa kila dhana (na hili hakuna awezaye abadani), mwanaistilahi huyu amependekeza pia **maneno yaliyobuniwa na watu wengine.** Pale ambapo tayari ameunda istilahi nyingine mwafaka, Chimerah anapendekeza istilahi 'faafu' zaidi zitumike. Kwa mfano:

**msukanishi/wavukazi** *(network)* kitu ambacho kinaunganisha; au patumike neno la Nabhany **UNGAMANISHI.** Angependelea hili kuliko yake mwenyewe.

**kusukanisha/wavukaza** *(networking)*; ama patumike neno la Nabhany **KUUNGAMANISHA**, ambalo analipendelea zaidi.

**mdahalishi/mdahilishi** *(internet)*, yaani kitu ambacho huruhusu mawasiliano kupitia kwa kompyuta; ama pia neno la Nabhany **UNGAMANISHO** litumike, japo halipendelei sana katika muktadha huu.

Hali kadhalika, pale ambapo istilahi zilizobuniwa na watu binafsi wa awali hazikuzingatia 'uangavu,' Chimerah **anapendekeza istilahi pendezi zaidi**, kama mifano hii ifuatayo inavyoonyesha:

**kazama** - fokasi *(focus)* (kitenzi); kazamo (nomino); kazamisha (kitenzi) badala ya 'wewindu' (taz. mfano **105g**). Pia mkazamo *(a person's focus)*.

**daro** - vitisho vikubwa (kutokana na neno **dara**/jaribu=*challenge*).

**ndaro** - vitisho vya kawaida.

**kidaro** - vitisho vidogo badala ya '**changamoto**' ambalo linatumika kimakosa mahali ambapo maana yake hasa ni **kutia motisha** (kumotisha) au kutia hamu (taz. Mohamed na Mohamed, 1998). Fauka ya hayo, neno **changamoto** halinyambuliki. Tazama pia, **mdaraji** *(the challenger)*, **mdarwaji** *(the challenged)*, **ku(dariza)** *(challenging,* kama katika tatizo au kazi).

Mifano zaidi ya istilahi faafu zinazopendekezwa na Chimerah ni:

**bwame** - *cyber*.

**ubwamelifu** - *cybercrime*.

**ubwakameme** - *cyberspace* (yaani hali ya nafasi kuu ya vitumeme).

**bwakameluma** - *cybernetics* (yaani utaalamu katika utendajikazi wa teknolojia ya ubwakameme).

**bwakamemudu** - *cybernate* (yaani uwezo wa kumiliki kupitia kwa ujuzi wa teknolojia ya ubwakameme).

**bwakametu** - *cyborg* (yaani mtu-mtambo aliyeundwa kwa sayansi ya ubwakameme).

(**Bwaka** ni neno lililopendekezwa na Nabhany kwa maana ya ombwe *vacuum*. Nabhany pia anapendekeza maneno mengine kwa maana ya *"vacuum."* Hata hivyo, Chimerah anadahili kuwa **ombwe** ndio *"vacuum,"* na **bwaka** ni **"anga kuu"**).

Uundaji wa istilahi aghalabu hutokana na msukumo fulani. Kuhusu jambo hili Said A. Mohamed, *Tata za Asumini* (uk. 15) anatueleza:

> lakini kwa kani na nia, alipeleka mkono wake wa kushoto na kuushika mkono wa kulia wa Asumini. Viganja vilikutana na kuumana. Kwa mbali, kila mmoja wao alianza kusikia hisia ngeni - **ujotojoto si ujotojoto, mnyongeresho si mnyongeresho na msisimko si msisimko. Labda mchanganyiko wa yote hayo;** mchanganyiko ambao labda ungeitwa, **ujomnyosisi.**
>
> (Taz. katika Mohamed, 1995:42).

Ukosefu wa dhana na hisia inayotaka kuwasilishwa katika dondoo hili ndio uliokuwa msukumo katika uundaji wa neno **ujomnyosisi;** na ionekanavyo ni kwamba Chimerah amechukua msimamo huo huo katika ubunaji wa istilahi za Kiswahili.

**5.1.1.4.1.6 Ukopaji**

Mbinu ya ukopaji, ingawa haitumiwi sana na Chimerah kama tulivyotaja hapo awali, ni mojawapo ya njia ya ubunaji wa istilahi za Kiswahili. Uchunguzi wa maneno yanayozalishwa na mwanaistilahi huyu unaonyesha maneno kadhaa yenye asili ya Kiarabu na ya Kiingereza pia, au mseto wa Kiarabu, Kiingereza na Kibantu. Mathalani, neno la awali kulibuni, **tarakilishi** - ni mseto wa maneno ya Kiswahili ambayo asili yake ni Kiarabu na Kiingereza. Tazama vijenzi vyake hapa:

**tarakimu** - asili ni Kiarabu.

**akili** - asili ni Kiarabu.

**mashine** - asili ni Kiingereza.

(Taz. pia **alamachuo** - *bookmark* (nomino), **alamachuosha** - *bookmark* (kitenzi) ambapo **alama** ni Kiarabu na **chuo** ni Kibantu).

Aidha kuna istilahi alizozipendekeza ambazo ni za **Kiarabu** moja kwa moja, kama mifano hii inavyodhihirisha:

**shamsa** - *solar* (neno la Kiarabu lenye maana ya jua).

**kawi ya shamsa** - *solar energy* (**kawi** na **shamsa** yatokana na Kiarabu).

**kamara** - *lunar* (kutokana na neno la Kiarabu *kamar*, yaani mwezi).

**mvuto wa kamara** - *lunar pull*.

**barisi** - *orbit* (kitenzi, asili ni Kiarabu).

**mstarini** - *on line*. (Mstari asili yake ni Kiarabu, ilhali mofu "-ni," ni Kibantu).

Chimerah pia anatumia maneno mkopo ya Kiswahili yanayofanana na menziyao ya Kiingereza kwa sadfa, kama haya yafuatayo:

**wavulishi** - *web* (wavu-*net;* yaani wavu wa tarakilishi).

**wavuti** - *website* (yaani kiini cha wavulishi).

**wavulisha** - pitisha ujumbe kwa njia ya wavulishi.

**wavulishwa** - (ujumbe) kupitishwa kwa njia ya wavulishi.

**wavu ulimwengu wote (wuw)** - *World Wide Web (www)*, yaani wavulishi ulimwenguni kote.

**kialiki** - *click* (Kibantu kutokana na sauti ya **kualika**, kama **mbegu kavu**).

**tovuti** - *site* (kutokana na kit**ovu+uti**; yaani **"kati ya kati"**).

Anapendekeza kwamba maneno ya lugha mbili (haya asili yake) yakifanana kwa sadfa, basi kwa vyovyote vile, yapewe kipaumbele katika kuendelezwa.

Kiingereza vilevile kimetumiwa na Chimerah kama chanzo kikuu cha istilahi mkopo za Kiswahili. Maneno ambayo yamependekezwa na mwanalugha huyu ambayo asili yake ni Kiingereza ni, mfano:

**modemu** - *modem* (ya tarakilishi).

**nambakoda** - *code number*.

**lainini** - *on line* (Kiingereza-Kibantu).

**laini** - *line* (katika tarakilishi).

**progiramu** - *programme*.

**televizisha** - *to televise*.

**televizishwa** - *to be televised*.

##### 5.1.1.4.1.7 Tafsiri Sisisi

Mbinu ya Tafsiri sisisi (kaleki) vilevile imetumiwa na Chimerah kuundia istilahi za Kiswahili. Kwa mfano:

**vuna data** - *harvest data*.

**msafara data** - *data traffic*.

**singidata** - *database*.

**nenopishi/nenopisi** - *password*.

**fumandipo** - *direct hit* (kitenzi), au **ufumi ndipo** (nomino).

**kavazi ya singidata ya virusi** - *virus database archive*.

##### 5.1.1.4.1.8 Uwekaji wa Maneno katika Muktadha Mpya wa Utumizi

Aidha, kuna maneno aliyoyatoa katika kamusi zilizochapishwa. Maneno hayo ameyatia katika **muktadha mpya wa utumizi**, moja kwa moja, na/au akayahuluti, kama mifano hii inavyoonyesha:

**duma/gwia** - (kamata au nasa kitu, au data kitu) *(Kamusi ya Visawe, 1998)*.

**dowea** (umelea), **sakasaka** (rejelea *Kamusi ya Visawe, 1998*).

**taarasha** - *bulletin* (taarifa rasmi ya habari) (TUKI - *English -Swahili Dictionary)*

**ochoma** - *navigate* (ongoza **chombo majini** (TUKI - *English -Swahili Dictionary)*).

##### 5.1.1.4.1.9 Matumizi ya Visawe

Uchunguzi uliofanywa na Mdee (1980) na MacWilliam (1985) kuhusu mikabala ya walengwa wa Kiswahili juu ya istilahi mpya

zinazoundwa, unaonyesha kwamba wengi wao hawakupendezwa na istilahi zilizoundwa pale ambapo tayari kuna nyingine mwafaka na zilizopata mashiko na ukubalifu wa kimataifa. Ingawa istilahi hizo zilikataliwa kwa sababu ya **mazoea** ya istilahi zilizoko katika lugha (taz. Gibbe, 1978; Hamad, 1989:70; na Massamba, 1989:79), ni maoni yetu kuwa huu ni msimamo mpotofu hasa tukizingatia istilahi makosa zilizoingizwa katika Kiswahili kama vile **mazingara** *(environmental surroundings)*, **msaada** *(AIDS)*, na mengineyo. Uundaji istilahi unapaswa kuendelezwa iwapo pana haja kuu kimuktadha wa utumizi. Kama Chimerah (1998b:11) mwenyewe anavyotueleza, muktadha wa utumizi ni muhimu; ndio maana Kimani Njogu darasani, katika kutafuta istilahi mwafaka za kurejelea *absurd*, *dialogism* na *deconstruction* alijikuta akitumia neno **ubwege** badala ya *absurd*, **usemezo** badala ya *dialogism* na **udenguzi** badala ya *deconstruction*.

Uundaji istilahi ni jukumu la mbunaji, lakini uamuzi unaohitajika juu ya istilahi 'mwafaka' zinazoundwa, na uteuzi wa matumizi, ni wa jopo na watumizi wenyewe. Kazi ya kutunga istilahi 'faafu' si rahisi, kwa vile mtu hajui ugumu wa istilahi anazozitunga kwa watumizi-lengwa. Ndiposa Chimerah, mara kadhaa, akapendekeza zaidi ya istilahi moja ili kuwapa watumiaji haki ya uchaguzi (rejelea 5.1.1.4.1.5, uk. 268). Misingi ya kisayansi ya uundaji istilahi (Picht na Draskau, 1985), na vigezo vya ufaafu wa istilahi vya PEGITOSCA (taz. Kiingi, 1989) ndio mwongozo utakaowasaidia wanalugha na watumiaji wa Kiswahili katika kuamua patumike istilahi zilizopendekezwa za Nabhany ama za Chimerah, kwa mfano, ama maneno yote mawili yatumike kama visawe. Tazama

jedwali hili kwa mfano:

| Istilahi za Nabhany | Istilahi za Chimerah | Kiingereza |
| --- | --- | --- |
| **barua pepe** (barua ya kupeperushwa huku wapiga kule yatoka) | **tarifalishi** (rejelea maelezo awali ya mbunaji | *e-mail* |
| **ngamiza** (asili yake ni Kiamu kwa maana ya shimo linalomeza maji bila kujaa | **tarakilishi** (taz. mfano 109b) | *computer* |
| **pepesi** (neno lenye asili ya Kibantu) | **nukununu** (nukuu+rununu) | *fax* |
| **ndaki** (chuo ambacho chasomesha elimu ya juu kindakindaki) | **zutafindaki** (taz. mfano 109a) | *university* |
| **uyoka** (uyoo (picha) +**uka** (mwali) neno **uyoka** ni la kilahaja) | **uka-mraba** | *x-ray* |
| **zingiro** (mzunguko/duwara) | **kitandaridhi** | *global* |

(Kwa maelezo zaidi juu ya jinsi istilahi hizi zilivyoundwa na maana yake rejelea 5.1.1.3.1, uk. 250 na 5.1.1.4.1.3, uk. 263).

### 5.1.2 Ukuzaji wa Istilahi za Isimu: Mbinu za Mbaabu na Kapinga

Mbaabu na Kapinga ni miongoni mwa wanaistilahi walioshughulikia na kuelemea upande wa isimu ya Kiswahili. Ni muhimu kuchunguza mbinu zao za uundaji istilahi kwa minajili ya kuibua 'usayansi' wa mifanyiko waliyoitumia.

#### 5.1.2.1 Njia ya Mbaabu ya Kuundia Istilahi za Isimu ya Kiswahili

Isimu ya Kiswahili ni taaluma maalum ambayo inaendelea kukuzwa kiistilahi na wanalugha wa Kiswahili. Mbaabu, kama ilivyotajwa

hapo mbeleni, ni mmoja wa wataalamu binafsi ambao wamejitolea kuendeleza leksikoni ya lugha hii kwa kuundia istilahi kwa mbinu mbalimbali. Kulingana na Mbaabu (1989:27) azma yake ya kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili ilitokana na kukosekana kwa "msamiati uliokubalika na kuidhinishwa na mataifa (kimataifa)." Ni katika misingi hii ndipo ni muhimu kutathmini 'usayansi' katika mbinu za uundaji istilahi zinazotumiwa na mtaalamu huyu kwa minajili ya kuibua sababu za kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi zilizozalishwa kwa walengwa wa Kiswahili (taz. 6.2.1). Mbinu anazozitumia Mbaabu (1992) ni unyambuaji na uambishaji, na kufasiri kwa dhana zilizomo katika lugha za kigeni.

#### 5.1.2.2 Unyambuaji na Uambishaji

Unyambuaji na uambishaji ni uundaji wa istilahi kwa kuongeza viambishi vifuatilizi na viambishi awali kwenye mzizi wa neno ili kujenga istilahi mpya au ya kategoria ile ile (rejelea 4.1, uk. 118-132).

Katika kusisitiza umuhimu wa mbinu hii, Mbaabu (1992) anajadili ruwaza zifuatazo:
- Uundaji nomino kutokana na maneno mengine.
- Uundaji nomino kutokana na vitenzi.
- Nomino kuundwa na vitenzi vingine (mnyambuliko wa vitenzi).
- Nomino kuundwa kutokana na vivumshi.

Nomino nyingi za Kiswahili huundwa kutokana na maneno mengine kwa kufuata taratibu mbalimbali; mathalani, matumizi ya kiambishi /ana/, ambacho kimetumiwa katika kuunda nomino kama vile

**mwanaistilahi, mwanaleksikografia, mwanasarufi** (taz. Mutahi, 1986).

Njia nyingine anayoitumia Mbaabu katika kubuni nomino au istilahi za Kiswahili, ni **nomino kutokana na vitenzi** kwa kutumia viishio i,e,o, na u. Kuhusu utaratibu huu, Mbaabu (1992:109) anasema:

> Nomino kadhaa zaweza kutokana na vitenzi visivyofanyiwa mabadiliko yoyote. Vitenzi hivyo huwa na muundo wa mzizi ulioongezwa kiishio a... Nomino kama vile **mpiga, pigo,** na **mlo** zimeundwa kutokana na vitenzi ambavyo havijafanyiwa mabadiliko yoyote...

Ni maoni yetu kwamba nomino hizo zimeundwa kutokana na mizizi ya vitenzi pamoja na viambishi vifuatilizi, ambavyo ni mofimu maalum za kubadilisha vitenzi kuwa nomino. Hata hivyo, hatuna ubishi wowote kuhusu uainishaji wa Mbaabu wa nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi au vitenzi vingine; yaani kuwepo kwa:

- Vitenzi vyenye asili ya Kibantu, na
- Vitenzi vilivyokopwa.

**Vitenzi vyenye asili ya Kibantu** huishia kwenye irabu a, na **vitenzi vilivyokopwa** kutokana na lugha za kigeni kama vile Kihindi, Kiajemi, Kiarabu, huishia kwa irabu a, i, u, na e. Mfano wa nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi ni **(112)**:

| | Kitenzi | Nomino |
|---|---|---|
| (112a) | ambisha | **kiambisho** |
| (112b) | iga | **kiigo** |
| (112c) | ingiza | **kiingizi** |

Istilahi kadhaa za isimu ya Kiswahili zimeundwa na Mbaabu (1992) kwa kuongeza kiambishi awali **ki-** na kiambishi tamati au kiishio

o, kama mfano (113) huu unavyodhihirisha:

(113a) **kielezo**

(113b) **kitendo**

(113c) **kihusiano**

(113d) **kishangao**

Istilahi zinazoundwa kwa kutumia kiambishi tamati **o** huwa na maana ya matokeo ya tendo (matokeo ya vitenzi vilivyotumiwa kuziunda) na maana ya kitu kinachotumiwa kutenda kitendo (k.m. **kiishirio, kifanano,** n.k.). Nomino nyingine zinazoundwa kutokana na kiambisho awali **ki-** hudokeza maana ya kitu kinachotenda au cha kufanyia jambo fulani (k.m. **kijalizo**). (taz. pia Polome 1967:78). (Kwa maelezo zaidi na mifano kuhusu uundaji wa istilahi kutokana na mnyambuliko wa vitenzi na vivumishi, rejelea **4.1.1**, uk. 118).

### 5.1.2.3 Kufasiri kwa Dhana

Mwanaisimu Mbaabu, baada ya kutambua kwamba Kiswahili, kama lugha nyingine duniani, ina uwezo wa kueleza dhana zilizomo katika lugha nyingine, ameitumia mbinu ya kufasiri maana za maneno kwa kutazama mfumo wa dhana. Kuhusu suala hili, Ruo (1989:99) hakosei anaposema:

> ...Ikiwa lugha za Ulaya zimeweza kufasiri dhana ambazo hazimo katika lugha hizo, kwa nini Kiswahili kishindwe kueleza dhana hizo? Istilahi nyingi za Kiyunani, Kilatini, n.k. zimewahi kutafsiriwa na kutajirisha Kiingereza. Hii imewezesha lugha ya Kiingereza kujitosheleza.

Katika kutafsiri na kufasiri dhana, njia inayotumiwa sana ni

kupambanua kwanza sifa bainifu za dhana ya istilahi na kutumia sifa hizo kuzalisha istilahi. Mathalani, *onomatopoeia* (**anomatopia**) limefasiriwa kuwa **kiigo**. Msingi wa tafsiri hii ni sifa bainifu ya **anomatopia**, yaani, neno linaloiga.

Istilahi zilizopatikana kwa njia hii ni nyingi, kama inavyothibitishwa na mapendekezo ya Mbaabu katika mfano **(114)** huu:

| | Kiswahili | Kiingereza |
|---|---|---|
| (114a) | **kiini** | *root* |
| (114b) | **sauti** | *phoneme* |
| (114c) | **mizani** | *syllable* |
| (114d) | **sifa** | *adjective.* |

Ingawa Mbaabu (1992) alifanikiwa mara nyingi kupambanua sifa bainifu na kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili kwa utaratibu wa kupanua/kufinya (mfinyo) maana ya asili ya istilahi, ni maoni yetu kwamba istilahi nyingine zilizoundwa kwa mbinu hii hazisadifu kwa walengwa wake (taz. 6.1, uk. 318). Kwa mfano, **kijina** badala ya **kiwakilishi**, **kiini** badala ya **mzizi**, na kadhalika. Hata hivyo, maneno haya yanatokana na azma ya mwanalugha huyu kwamba maneno yanayoundwa yasiwe na utata bali yaweze kuangaza maana (uangavu).

#### 5.1.2.4 Maneno 'Pendezi' Yaliyobuniwa na Watu Wengine

Kadhalika pale ambapo waandishi na wataalamu wengi wa isimu ya Kiswahili (k.v. Abdulla 1988; Nkwera 1978; Kapinga 1983)

wanaelekea kukubali na kuridhishwa na istilahi za TUKI (1990) ambazo hazikuzingatia uangavu Mbaabu (1992), anapendekeza istilahi 'pendezi' zaidi. Tazama kwa mfano **(115)**:

| | **Mbaabu (1992)** | **Kapinga (1983)** | **TUKI (1990)** |
|---|---|---|---|
| (115a) | jina/**nauni** | nomino | **nomino** |
| (115b) | **kielezo** | kielezi | **kielezi** |
| (115c) | **vitendo** | vitendo | **vitenzi** |
| (115d) | **vihusiano** | vihusishi | **vihusishi** |
| (115e) | **kiambisho** | kiambishi/o | **kiambishi** |
| (115f) | **kiishirio** | kiishiria | **kiishiria** |
| (115g) | sifa | kivumishi | **kivumishi** (kutokana na vumisha) |
| (115h) | shadda | mkazo/shadda | **mkazo** |
| (115i) | sauti | fonimu | **fonimu** |
| (115j) | kiigo | kifanano | **kifanano** (onamatopoea) |
| (115k) | mizani | silabi | **silabi** |

Kutokana na mifano hii **(115)** (ila tu 115c), ni dhahiri kwamba madai ya Mbaabu (1989:27) kwamba "ninandelea kutumia msamiati wangu katika kuwafunza walimu wa Kiswahili nchini Kenya kwa kuwa kwa maoni yangu **unatoa ufafanuzi zaidi wa mnyambuliko wa vitendo vya Kiswahili**. Ninafanya **hivyo kwa kukosa msamiati uliokubalika na kuidhinishwa kimataifa**" - yana umuhimu wake (taz. Habwe, 1995:20).

Kama anavyokiri Mbaabu (1989:27) mwenyewe; "kuwapo kwa istilahi nyingi tofauti zenye kuwakilisha dhana ileile ni tatizo kubwa katika ufundishaji wa sarufi na muundo wa Kiswahili" (taz. pia Gibbe, 1981:4-5). Aghalabu hutokea **utata** katika uteuzi wa

istilahi bora ambapo kuna visawe vingi vya kiistilahi, kama ilivyo hapa:

- Kielezi/kisifa/ziada ya kitendo/kiongozo cha kitendo /kielezo/kijalizo.
- Kiima/mtendaji/kitendaji/faali.
- Kipua/nazali/king'ong'o, n.k.

Matokeo ya hali hii ya wingi wa visawe vya kiistilahi ni kwamba imekuwa vigumu katika mataifa ya Afrika Mashariki kufundisha somo la isimu ya Kiswahili katika vyuo vikuu, ambapo kila mwanalugha hujikuta katika hali ya kutatizika asijue ipi ndiyo istilahi faafu na bora ya kutumiwa anapofundisha somo hili. Pendekezo la Mbaabu (1989:26) na Mukama (1989) kwamba tuwe na kamati ya kimataifa ya kutoa mwongozo thabiti wa kuidhinisha istilahi mpya za isimu ya Kiswahili zinazoundwa lina mashiko na vilevile udhaifu wake. Lina mashiko kwa sababu itakuwa ni hatua moja muhimu yenye kuzipa istilahi mpya ukubalifu kwa walengwa. Hata hivyo, katika hatua ya utekelezaji, huenda jambo hili lina udhaifu na lisiwezekane. Kwanza panahitajika mifumo ya kiserikali ya lugha ambayo itaruhusu jambo hili kutekelezeka. Pili, fedha nyingi zinahitajika ili kuufanikisha mradi huu. Tatu, lugha haziendelezwi jinsi hii. Wanalugha Waingereza, Waamerika, Waostralia na Wa-Newzealand hawakukutana wala kuunda kamati ya kimataifa ya kuunda istilahi pamoja (taz. Chimerah, 1998). Istilahi za lugha zote ziliundwa na watu binafsi "vivi hivi" tu bila mpango mahsusi na wanaleksikografia (wanamakamusi) na wanaisimu.

Mbaabu hajatunga istilahi maalum kwa kila dhana. Kwa hivyo, hata baada ya madai kwamba 'anaendelea kutumia msamiati wake kwa sababu unatoa ufafanuzi zaidi,' mwanalugha huyu amependekeza pia istilahi zilizobuniwa na watu wengine. Pale ambapo tayari ameunda istilahi mpya, ilhali kuna istilahi nyingine mwafaka, Mbaabu 'anazitambulisha' istilahi zake, zaidi kwa kutumia pia istilahi ambazo zimeundwa na wataalam wengine. Kwa mfano, Mbaabu (1992):

- **jina** (nauni) uk.19
- **menoni** (ufizi) uk.6
- **shadda** (mkazo) uk.35.

Mbaabu ameunda istilahi zinazopatikana katika mfano (116a) lakini ametumia sana istilahi za (116b). Tazama mfano huu **(116)**:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (116a) | **vitendo** | (116b) | **vitenzi**, uk.39 |
| | **vielezo** | | **vielezi**, uk.49 |
| | **viambisho** | | **viambishi** uk.76 |
| | **uradufu** | | **uradidi**, uk.65 |
| | **jina** | | **nomino**, uk.66 |
| | **kiini** | | **mzizi**, uk.133 (mzizi wa kitenzi, n.k.) |

Matumizi haya ya istilahi za (116b) kama visawe vya (116a) yanadhihirisha kukosekana kwa istilahi zilizokubalika na kuidhinishwa Tanzania. Kwa hivyo, Mbaabu (1989:27) ana sababu tosha za kuendelea kudai kuwa "mimi hutumia neno **kiambisho** badala ya **kiambishi** na **kiini** badala ya **mizizi**" (taz. pia Massamba na Wenzake, 1999). Ni muhimu lugha ya Kiswahili ikuzwe kwa kuizidishia visawe vya kiistilahi, lakini sio katika taaluma ya

isimu, na kwa kujaza mapengo ya kiistilahi yaliyopo. Mapengo yanayotokana na kuingizwa kwa dhana za kigeni ama istilahi kubuniwa kimakosa, au kufa kwa istilahi fulani fulani katika lugha pokezi yajazwe kwa kuzingatia misingi ya ubunaji istilahi. Kwa ujumla, njia za Mbaabu za kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili, ambazo ni mbinu za **unyambuaji** na **kufasiri kwa dhana** zilizomo katika lugha za kigeni, zinahusiana kimsingi na "uangavu" wa istilahi.

### 5.1.2.2 Njia ya Kapinga ya Kuundia Istilahi za Isimu ya Kiswahili

Katika harakati zake za kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili, Fr. C. Kapinga amekuwa akitumia mbinu mbalimbali ambazo hutumika pia katika lugha nyinginezo. Nazo ni pamoja na njia ya istilahi **mnyambuliko, mwambatano wa maneno**, kutafsiri au **kufasiri maana** ya dhana za kigeni na njia ya **ukopaji** wa istilahi kutoka lugha nyinginezo za kigeni. Katika kuzijadili mbinu hizi za uundaji istilahi, tutazingatia zaidi 'usayansi' katika mbinu zinazotumiwa na mtaalamu huyu kuzalisha istilahi za isimu ya Kiswahili.

#### 5.1.2.2.1 Unyambulishaji

Kwa mujibu wa maelezo ya Kapinga (1983:26) **mnyambuliko** ni ile hali ya kulipa neno maana nyingine kwa kuongeza viambishi fulani fulani, au kwa kuambatisha kiambisho kwenye mzizi ama mashina ya maneno ili kupata neno jingine lenye maana. Istilahi za isimu ya Kiswahili zilizopatikana kwa njia ya mnyambuliko ni za aina ya majina, vivumishi, vielezi, na vitendo (taz. pia Kapinga,

1996:47-50).

Istilahi nyingi sana za taaluma ya isimu zimetungwa kwa kunyambua matendo (mnyambuliko wa vitenzi). Katika kutofautisha 'kitendo' na 'kitenzi', Kapinga (1983:55) anadai kuwa "...neno 'kitenzi' ndilo jina la utendaji na 'kitendo' ndilo jina la matokeo ya utendaji. Yaelekea kitenzi ni mama na kitendo ni mwana. Kitenzi ni kifanyaji kitendo na tukio ni kifanywaji." Sisi tunachukulia "kitenzi" kwa maana ya aina ya neno ambalo hueleza namna tendo linavyotendeka. Ni muhimu isisitizwe hapa kwamba viambisho **i, ji, u, o, e** na **a** ndivyo vitumikavyo katika kuunda istilahi za vitendo. Viambisho hivyo huambatanishwa mwishoni mwa mzizi au shina la kitendo, ilhali mwanzoni mwa mzizi huwekwa kiambisho cha ngeli inayohusika, kama tuonavyo katika mifano **(117)** ifuatayo:

(117a) m-sem-i = **msemi.**

(117b) mw-unda-ji = **mwundaji.**

(117c) u-fasaha = **ufasaha.**

(117d) u-taratibu = **utaratibu.**

(117e) m-kaz-o = **mkazo.**

(117f) m-kop-o = **mkopo.**

(117g) ki-imb-o = **kiimbo.**

Mifano zaidi ya istilahi za isimu zilizoundwa kutokana na mbinu ya unyambulishaji ni kama **(118)** ifuatavyo:

(118a) {-tamk-} = **tamk-o, ki-tamk-wa** (fonimu).

(118b) {-tend-} = **ki-tend-o, ki-tend-wa** (yambwa), **kitenzi.**

(118c) {-elez-} = **ki-elez-i,** (taz. pia **kiingizi, kivumishi,** n.k.).

#### 5.1.2.2.2 Mwambatano wa Maneno

Uambatanishaji wa maneno ni mbinu nyingine ambayo imetumika sana na TUKI/Kapinga (1983) katika kuzalisha istilahi za isimu ya Kiswahili. Istilahi ambatani, ambazo aghalabu huwakilishwa kimaandishi na maneno mawili, au zaidi, yaliyo huru, hupatikana kwa kuyaunganisha na kuunda neno moja, kama inavyothibitishwa katika mifano **(119)** ifuatayo:

| | **Maneno Mawili/Matatu** | **Neno Moja Lililobuniwa** |
|---|---|---|
| (119a) | nyakati sahihi | **nyakatisahihi.** |
| (119b) | viambishi vya kivina | **viambishikivina.** |
| (119c) | vielezi miigo | **vielezimiigo.** |
| (119d) | vielezi idadi | **vieleziidadi.** |
| (119e) | mafungutenzi sambamba | **mafungutenzisambamba.** |
| (119f) | usawazisho wa matamshi | **usawazishomatamshi.** |

#### 5.1.2.2.3 Kufasiri kwa Maana ya Dhana

Njia ya tatu ya kubuni istilahi mpya za isimu ya Kiswahili ni kufasiri dhana za kigeni. Mbinu hii inasisitiza kwamba kabla ya kubuni istilahi, ni muhimu kutambua dhana na mfumo wa dhana ili istilahi mpya iwiane na maana ya dhana asili katika lugha changizi. Mifano **(120)** ifuatayo inathibitisha hilo:

| | **Kapinga (1983)** | **TUKI (1990)** |
|---|---|---|
| (120a) | **vitamkwa** | **fonimu.** |
| (120b) | **mwambatanisho** | **uambishaji.** |
| (120c) | **viigizi** | **onamatopia.** |
| (120d) | **vielezimiigo** | **idiofoni.** |

(120e) **maandishi** othografia.

(120f) **viingizi/vijazio** kihisishi.

(120g) **mwendesho wa vitenzi** uainishaji vitenzi kiuambishi.

(120h) **ving'ong'o** nazali.

(120i) **viini** (undani mwa kitu) mizizi.

### 5.1.2.2.4 Ukopaji

Katika harakati za kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili, njia ya kukopa na kutohoa istilahi za kigeni na kuziandika kwa kufuata muundo na misingi ya lugha ya Kiswahili, imetumiwa vile vile na Kapinga (1983).

Istilahi za isimu ya Kiswahili zilizopatikana kwa kutohoa na kuswahilisha istilahi mkopo ni nyingi. Kwa mfano **(121)**:

| | **Kiswahili** | **Kiingereza** |
|---|---|---|
| (121a) | **sentensi** | *sentence* |
| (121b) | **alofoni** | *allophone(s)* |
| (121c) | **konsonanti** | *consonant* |
| (121d) | **silabi** | *syllable* |
| (121e) | **alfabeti** | *alphabet* |
| (121f) | **Othografia** | *orthography* |

(taz. pia **shadda**, istilahi mkopo kutoka Kiarabu, uk. 6).

Katika mbinu hizo nne zilizotajwa hapo juu, mbinu ya tatu, ambayo ni **kufasiri maana** ya dhana kutoka lugha nyingine kuingia Kiswahili, ndiyo iliyotumiwa sana na Kapinga (1983) katika kuendeleza istilahi za Kiswahili, hususani, za isimu. Mbinu ya

kufasiri maana ni zalishi, na tunapendekeza itumiwe na wanaleksikografia na waundaji istilahi za Kiswahili iwapo azma ya kuitanua lugha hii itafanikiwa.

Uamuzi wa Kapinga (1983) wa kuegemea kwenye njia ya "kufasiri maana" una misingi katika kutaka kukipunguzia "ugeni" Kiswahili, na kurahisisha istilahi za lugha hii (taz. mfano wa **120**). Juhudi na mwelekeo huo unahitaji kuimarishwa kwa vile njia hii hurahisisha uundaji wa istilahi zenye ukubalifu kwa walengwa (taz. 5.1, uk. 207). Hata hivyo, ingawa istilahi nyingi zilizopendekezwa na Kapinga (1983:205-207) zinaonyesha kiwango cha juu cha 'uangavu,' kuna dosari katika baadhi ya istilahi zake:

Kwanza, kuna uundaji kivoloya wa istilahi kwa kutafsiri maana. Tazama **upogoupogo** katika mfano huu **(122)** ufuatao:

| | **Kiswahili** | **Kiingereza** |
|---|---|---|
| (122a) | **vitenzi vya mizizi mifupi** | *monosyllabic verbal stem, root.* |
| (122b) | **vitenzi visaidizi** | *auxillary verb.* |
| (122c) | **vishirikishi vipungufu** | *defective auxillary verb.* |
| (122d) | **vishirikishi viambishi** | *copulative verbal, class concords.* |
| (122e) | **mfumo wa lugha** | *structure of a language.* |
| (122f) | **utaratibu wa viambishi** | *order of affixes.* |
| (122g) | **usawazisho wa matamshi** | *coalescence of vowels.* |

Inaelekea Kapinga (1983) hakuzingatia misingi ya uundaji wa istilahi (Picht na Draskau, 1985) na mbinu za kisayansi za kuendeleza leksikoni ya lugha. Ni maoni yetu kwamba, watumiaji

wa Kiswahili wataona fahari kutumia istilahi za **(123)** badala ya/mahali pa **(122)** ambazo zinaweza kuzusha shaka (ila tu 122b):

(123a) **vitenzi vyenye mzizi wa silabi moja.**

(123b) **vitenzi visaidizi.**

(123c) **vitenzi visaidizi vipungufu.**

(123d) **vitenzi vishirikishi.**

(123e) **muundo wa lugha.**

(123f) **mpangilio wa viambishi**, na

(123g) **uwiano wa vokali.**

Pili, ingawa Kapinga (1983, 1986) aliazimia kuipunguzia "ugeni" lugha ya Kiswahili, uundaji wake wa istilahi mpya 'unahalalishwa' na kuboreshwa kwa kuongeza visawe vya istilahi mkopo za Kiingereza katika mabano { }. Kwa mfano, **mwambatanisho** (*agglutination*) uk.46, **vitamkwa** (fonimu) uk.46, **shadda** (mkazo) uk.6, **viini** (mizizi) uk.27, **kitendwa** (*object*) uk.16, **ving'ong'o** (nazali) uk.23.

Matumizi haya ya istilahi mpya na visawe vyake kwenye mabano, katika fani ya isimu, tofauti na katika fani anuai za sanaa na sayansi za jamii, yanaonyesha hali ya kukosa uamuzi. Kama tulivyotaja mbeleni, kuendeleza leksikoni ya lugha katika taaluma ya isimu ni kutoa uamuzi unaohitajika, pamoja na kuunda na kuteua istilahi moja kwa dhana moja inayoiwakilisha. Ni maoni yetu kuwa imani kwamba istilahi mbili, tatu, au zaidi zinapoundwa za kuwakilisha dhana moja huwapa walengwa nafasi ya kuteua istilahi bora, na ndiko kuikuza lugha (Besha, 1986), huenda ina mashiko tu katika fani za sanaa na sayansi za jamii, lakini sio katika

fani za sayansi menyu na isimu. Hii ni kwa sababu taaluma hizi huhitaji zaidi istilahi zinazogonga kwa udhahiri pale ambapo zimelengwa. Vile vile, ni kutokana na sababu kwamba katika fani fulani fulani (kama vile isimu na sayansi menyu), haisaidii chochote kuwa na visawe. Taaluma zenyewe ni za kigeni, zilianzia Marekani peke yake, na wenyeji wenyewe wanatumia istilahi moja kwa dhana moja, hivyo hakuna ulazima wa kuwa na visawe katika lugha pokezi (Kiswahili).

Tatu, utohozi wa viambishi vya kiistilahi wa Kapinga (ibid) haufuati misingi iliyokwishapendekezwa hapa (taz. 3.3.2, uk. 64) hasa ya kuziandika istilahi kulingana na matamshi yake katika lugha changizi. Kwa mfano, matumizi ya **otografia** (taz. Massamba na Wenzake, 1999:19), **ortografia** badala ya **othografia** (TUKI, 1990) kwa maana ya *orthography* yanakanganya; yaani kiambishi *ortho* ni **oto, orto** au ni **otho**? (Kwa maelezo kuhusu viambishi vya kiistilahi, rejelea 6.3.1.4, uk. 367). Ni muhimu, kutokana na sababu zilizotajwa hapo awali, istilahi za isimu ya Kiswahili ziepuke wingi wa visawe. Kwa jinsi hii, vyombo vya BAKITA, BAKIKE, TUKI havina budi kuunda istilahi ambazo zitakidhi matakwa ya walengwa wa istilahi za taaluma hii pasi na kujali tofauti ziwazo zozote; mathalani, viwango vya elimu, mazingira yao, n.k. (Felber, 1984). Kwa hivyo, imani nyingine kuwa istilahi ziundwe kufuatana na viwango vya elimu vya walengwa wake (Mwansoko, 1990) pia inafaa ichunguzwe kwa mapana. Ni maoni yetu kuwa kuwepo kwa makundi mawili ya kiistilahi katika fani ya isimu: Istilahi za wasomi na istilahi za watu wasio wasomi, ama za wazawa na wasio wazawa, kutawakanganya watumiaji wake, na kutaizorotesha lugha

hii ya Kiswahili. Ni maoni yetu kwamba uundaji wa istilahi moja kwa dhana moja (taz. Yambi, 1988:157), katika taaluma ya isimu ya Kiswahili, kwa kutumia mbinu na misingi ya uundaji istilahi, ndiyo njia ya pekee ya kuinua upeo wa ubora wa istilahi za taaluma hii zinazoundwa na watu binafsi, ama vyombo vya kukuza lugha ya Kiswahili.

**5.2 Usawa katika Mbinu za Uundaji wa Istilahi za Kiswahili**

Kiswahili, kama lugha nyingine yoyote ile, hutumia mbinu za kisifabia zilizoko katika kuendeleza leksikoni yake kama vile; unyambuaji, uunganishaji, uambatanishaji, ufupishaji, upanuzi wa maana za maneno, na ukopaji. Hata hivyo, inaelekea kuwa kuna mbinu ambazo hutumika sana na waundaji istilahi na vyombo vya kukuza lugha ya Kiswahili vya BAKITA, BAKIKE, TUKI, kuliko mbinu nyinginezo. Hali hii ya kuzipendelea na kuzipatia mbinu fulani za uundaji istilahi kipaumbele dhidi ya nyingine ina umuhimu wake, na ndio msingi wa uchunguzi wa suala hili la usawa katika mbinu za uundaji istilahi za Kiswahili.

Uchunguzi wa usawa katika mbinu zitumikazo kuunda istilahi za Kiswahili ni hatua mojawapo muhimu katika jaribio la kukuza istilahi za lugha hii, hususani istilahi za isimu. Ili istilahi za isimu ya Kiswahili zitokane na mfumo wa kimantiki, hatuna budi kushughulikia kipengele cha usawa katika mbinu za kuundia istilahi. Isitoshe, dhana ya usawa katika mbinu za uundaji wa istilahi, mbali na kuwa mwongozo katika uundaji wa istilahi 'faafu' na zinazokidhi haja ya malengo yake, pia ni kizuizi cha

'ukuzaji huria' wa istilahi. Usawa katika mbinu ni dhana ambayo itatambulisha mbinu bora katika kutunga istilahi zenye kufuata ruwaza inayokubalika kulingana na sarufi ya Kiswahili. Tazama jedwali (1) kwa maelezo zaidi:

**Jedwali 1: Usawa katika Mbinu za Uundaji Istilahi**

| NA | BAKITA | TUKI | BAKIKE/ Nabhany | CHIMERAH | MBAABU | FR. KAPINGA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ukopaji na utohoaji | Ukopaji na utohoaji | uunganishaji na uambatanishaji | uunganishaji | upanuzi wa maana za maneno | unyambuaji na uambishaji |
| 2. | mirakabu/ uambatanishaji | uambatanishaji | ubunaji/kufasiri maana | ubunaji/kufasiri maana | uasilishaji wa maneno kutoka Kiswahili chenyewe | ukopaji na utohoaji |
| 3. | mifito/ uhulutishaji | unyambuaji | uhulutishaji | uhulutishaji | unyambuaji | uunganishaji |
| 4. | ubunaji | ubunaji | ufufuaji na upanuzi wa maana za maneno asilia | unyambuaji | ubunaji | upanuzi wa maana za maneno |
| 5. | unyambuaji | upanuzi wa maana za maneno | unyambuaji | upanuzi wa maana za maneno asilia ya Kibantu | uunganishaji | ubunaji |
| 6. | kaleki | kaleki | akronimu na ukopaji kutoka Kiarabu | akronimu na ukopaji kutoka Kiarabu/ Kiingereza | ukopaji na utohoaji | uasilishaji wa maneno kutoka Kiswa-hili chenyewe |
| 7. | finyazo | uradidi | uradidi | utohoaji | uradidi na kaleki | uradidi |

Mpangilio huu kinambari (NA) unatokana na upambanuzi wa istilahi zilizoko na zilizoundwa kupitia vyombo vya kukuza Kiswahili, na aidha wataalam binafsi. Vigezo vya umbo la istilahi, na aina ya mfanyiko uliotumika kuundia istilahi mbalimbali vimetumika hapa. Kutokana na jedwali (1), ni jambo lisilozusha ubishi kwamba mbinu inayotumiwa sana na waundaji istilahi binafsi, na vilevile kupitia vyombo vya BAKITA, BAKIKE na TUKI, ni ile ya **uunganishaji** wa maneno mawili au zaidi. Mbinu hii inafuatiwa na **ubunaji** au tafsiri ya maana za maneno, **mnyambuliko**, **ufufuaji** wa maneno asilia ya Kiswahili, na **ukopaji** (utohoaji na kaleki) kwa mfuatano huo. (Hapa tunachukulia mbinu ya uunganishaji kwa maana sawa na uambatanishaji, ingawa tunafahamu kuwa istilahi muungano kimaandishi huwakilishwa kama neno moja ilhali istilahi ambatano

huwakilishwa kama maneno mawili yanayojitegemea).

Aidha, kutokana na jedwali (1), tunaona kwamba vyombo vya BAKITA na TUKI vinapendelea zaidi matumizi ya mbinu ya ukopaji na utohoaji katika kuzalisha istilahi za Kiswahili. Sababu za kuzalisha istilahi kwa kutegemea kukopa sana kutoka kwenye lugha zilizoendelea zimejadiliwa na wataalam wengi (k.v. Abdulaziz, 1989; Mwansoko, 1990; Chimerah, 1998a).

Upendeleo wa Watanzania wa kutumia mbinu ya ukopaji kutoka lugha za kigeni, hususani ya Kiingereza una historia ndefu. Vyombo hivi vya kukuza Kiswahili, TUKI na BAKITA na wataalam binafsi Watanzania (k.v. Kapinga, 1983; Besha, 1994; Massamba na Wenzake, 1999) sana sana hutohoa na huswahilisha istilahi mkopo. Hali hii huenda ni kwa sababu hawana lahaja ya Kiswahili asilia jirani (Kiunguja asilia kiko Visiwani (Whiteley, 1969)). Waundaji istilahi Wakenya (taz. mbinu za Nabhany, Chimerah, na Mbaabu), pamoja na kwamba huchukua mashina ya Kiswahili chenyewe kama msingi wa uundaji istilahi mpya, pia wanategemea mno mno maneno asilia na lahaja za Kiswahili hususani ya Kimvita, Kiamu, na hata Kiunguja (rejelea 5.1.1.3.1.2, uk. 254).

Kutoka kuundwa kwa Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (1930) iliyoazimia kufanikisha shughuli za kuendeleza Kiswahili (Mbaabu, 1991), hadi kubuniwa kwa mrithi wake, *Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili* (TUKI), na baadaye kuundwa kwa *Baraza la Kiswahili la Taifa* (BAKITA) mwaka wa 1967, mbinu tatu (3) zimetumika kukuza Kiswahili. Mbinu hizo ni pamoja na:

i) Kuchukua neno geni bila mabadiliko yoyote.

ii) Utohozi wa neno geni (mitohoo ya maneno).

iii) Upanuzi wa maana ya neno lililoko.

Aghalabu kila mbinu (i-iii) imekuwa ikitumika, kama mfano huu **(124)** unavyoonyesha:

| | i) | ii) | iii |
|---|---|---|---|
| 124a | *intonation* | intonesheni | **kiimbo/lafidhi** |
| 124b | *predicate* | prediketa | **kiarifu** |
| 142c | *presupposition* | prisapozisheni | **kiashiria** |

Mifano zaidi:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 125a | *greese* | grisi | **mafuta** |
| 125b | *energy* | enaji | **nguvu/kawi/nishati** |
| 125c | *accelerator* | ekselereta | **kichapuzi** |
| 125d | *parasitology* | parasitolojia | **sayansimelea** |

(taz. BAKITA, 1995)

Kwa hakika, vyombo vya BAKITA na TUKI, pamoja na wanalugha Watanzania, sio wataalam pekee wa Kiswahili wanaotumia mbinu hizi (i-iii) mintarafu ya kuendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili. Tuzingatie, kwa mfano, Bloomfield aliyeandika *Sarufi ya Kiswahili* (1931) na kujaribu 'kukuza' istilahi za isimu ya Kiswahili kwa misingi ya ukopaji. Bloomfield alibuni, kwa mfano, kitenzi cha =**vota** (*voter*) kwa maana ya =**piga kura**. Kutokana na kitenzi =**vota** aliunda istilahi nyingi, kama mfano **(126)** unavyodhihirisha:

| **(126)** | **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| (126a) | *voter* | **mvota** |
| (126b) | *pollingbox* | **kivoto** |
| (126c) | *election* | **uvoto** |

(126d) *to electioneer* **-votesha**

(126e) *to be a candidate* **-voteka**

(126f) *ballot box* **kivoteo**

(taz. Ridder, 1988:31)

Kuhusu uundaji huu na 'ufaafu' wa istilahi zilizobuniwa na Bloomfield, Whiteley (1967:247) anadokeza kuwa "...ni muhimu ifahamike hata hivyo, kwamba istilahi hizo hazikupata mashiko na hazikuingizwa katika matumizi ya kila siku, ingawa kwa wakati ule istilahi hizo zilifanikiwa." Hata hivyo, Whiteley hakutoa sababu za 'kufanikiwa' kwa istilahi hizo za Bloomfield wakati zilipoundwa, na kisha kukataliwa baada ya muda.

Akitathmini kazi ya BAKITA, na kama ilivyotajwa hapo awali, Tumbo (1982) hakosei anapodokeza kwamba kuna makosa yanayofanywa katika uundaji wa istilahi mpya ambayo hutokea kwa sababu ya kutoelewa misingi ya kimataifa ya kuendeleza istilahi (rejelea 3.3.2, uk. 64). Istilahi nyingi zilizobuniwa na kusanifishwa na BAKITA hufuata matamshi ya Kiingereza pasi na kufanya uchunguzi wa kietimolojia, au kuzingatia miongozo katika uzalishaji wa istilahi 'faafu' za kisayansi, kama ilivyowekwa katika Stobeski (1979) na ISO/R. 843 (taz. k.m. **malathioni** - *malathion*, katika BAKITA, 1995).

Tukirejelea jedwali (1) tunaona pia kwamba mbinu ya ubunaji, au tafsiri ya maana za maneno pia inatumiwa sana na vyombo vya kukuza Kiswahili na watu binafsi kuundia istilahi za lugha hii. Mbinu ya ubunaji inapewa kipaumbele katika harakati za kukuza istilahi kuhusiana na hududi pana ya mawasiliano kitaaluma, kwa

sababu huzalisha istilahi mpya lakini ambazo si 'mpya' hata kidogo kwa walengwa wake. Asili ya istilahi buniwa ni Kiswahili chenyewe. Ndiposa, kwa mfano, watumiaji wa Kiswahili hawapati shida kukubali istilahi k.v. **tarakilishi** ingawa kuna **kompyuta**. Neno **kompyuta** litapotea ama kufa siku zijazo kwa sababu halizingatii sifa muhimu za uzalishaji na unyambulikaji. Ni vigumu, kwa mfano, kufasiri kitenzi *"to compute"* ama kishazi *"Compute for me this,"* katika Kiswahili (taz. Chimerah, 1998a). Hali hii imeleta "mwanya" unaohitaji kuzibwa kwa/na istilahi nyingine 'faafu' zaidi (kama **tarakilishi** ambayo inaendelea kupata mashiko imara) zinazoibuka mahali pake. Hali kadhalika, watumiaji wa Kiswahili hawaoni ugumu wowote wanapotumia neno **runinga** badala ya **televisheni**. Ingawa **televisheni** limetumiwa kwa muda mrefu, lakini linaendelea kufifia kutokana na kiwango chake cha chini cha uangavu. Massamba (1996:96) anadai kwamba **runinga** lina 'ugeni' zaidi kwa walengwa wake kuliko **televisheni**. Katika maoni yetu, ingekuwa kwamba **televisheni** ndilo neno lenye 'ugeni' zaidi kuliko **runinga**. Neno **runinga** linaendelea kupata mashiko imara ya kimataifa.

Kadhalika, wataalamu wengi (k.v. Temu, 1972; Ohly, 1982; Krozewski na Steger, 1986) wanafahamu kwamba mbinu ya ubunaji au tafsiri ya maana za maneno ilitumika sana katika Kiingereza (taz. pia Barber, 1964). Kwa mfano, William Shakespeare aliitumia mbinu hii pale, alipounda neno *assasination* kutokana na neno *assasin* (taz. katika Chimerah, 1998). Shakespeare baadaye alibuni maneno mengi sana jinsi hii. Wataalamu wa Kiswahili waliopata 'kariha' ya kubuni istilahi kwa kutumia mbinu ya

ubunaji ni wengi. Kwa mfano, S.A. Mohamed (1990:15) kama ilivyotajwa mbeleni, alibuni neno **ujomnyosisi**. Neno hili linatokana na uhulutishaji na, akronimu. Ni mianzio ya maneno **ujotojoto**, + **mnyongeresho** + msisimko (taz. katika Mohamed, 1995:42). M.S. Abdullah (1976:7) katika *Mwana wa Yungi Hulewa* anasema:

> ...na 'kupeleleza ni **kuduhusi** na **kudukiza** jambo kwa **kulidunzi** pamoja na kulipekua na kulichakura...

Maneno yaliyozalishwa kwa ubunaji na mwandishi huyu ni **kuduhusi**, **kudukiza** na **kulidunzi**. Naye Shaaban Robert (1956:57) katika *Wasifu wa Siti Binti Saad* alibuni maneno mengi jinsi hii. Robert anasema:

> kujikimu ni **kujiruzuku**. Kujiruzuku ni kujitegemea kwa chakula, nguo, na **masurufu** mengi katika maisha.

Mbinu za ubunaji na unyambuaji hutumika katika lugha nyingi zinazoendelea duniani (k.v. Kihebrania (Rabin, 1989), Kichina (Pasierbsky, 1989). Lugha hizo hazitegemei sana lugha za kigeni kiistilahi. Hivyo, ni muhimu wataalam wa Kiswahili wawe wabunifu na wasiegemee kwenye ukopaji na utohoaji. Kukopa kuna mipaka yake. Ukopaji wa istilahi za kigeni wa kupindukia utatubidi 'kulipa' kwa kuipotezea lugha hii U-Afrika wake kama asemavyo Mbaabu (1995:56). Mbinu nyingine kama vile **upanuzi wa maana za maneno**, uhulutishaji, kaleki, uradidi, ufupishaji (akronimu) inaelekea zinatumika kinadra sana katika ukuzaji wa Kiswahili wa BAKITA, TUKI, BAKIKE na waundaji istilahi binafsi. Hata hivyo, katika harakati za kusasaisha Kiswahili, itakuwa bora kwa wanaleksikografia, waundaji istilahi, na vyombo vya ukuzaji lugha vya BAKITA, BAKIKE na TUKI kuzingatia na kuzipatia kipaumbele

mbinu zalishi, za 'kisayansi', na zenye usifabia. Mbinu hizi, kama ilivyotajwa mbeleni ni: Uunganishaji na uambatanishaji, ubunaji, unyambuaji, ufufuaji na ukopaji - hasa kutoka lugha za Kibantu na lugha nyingine za Afrika.

Ilivyo kwa sasa ni kwamba chombo cha kuendeleza Kiswahili cha BAKITA huzipatia nafasi sawa mbinu zote za uundaji wa istilahi za Kiswahili pasi na kujali uzalishaji na usayansi wa mbinu zenyewe katika lugha husika. Inaelekea pia, chombo cha BAKITA huchukulia kwamba hakuna mbinu ya uundaji istilahi iliyo bora zaidi ya nyingine katika uendelezaji na ukuzaji wa Kiswahili (Kiango 1984). Sisi hatukubaliani na mtazamo huu kwa sababu hauzingatii tofauti za kifonolojia, kisarufi, na matamshi ya lugha zinazohusika. Ndiposa katika tasnifu hii imependekezwa kuwa mbinu zalishi na za kisayansi za kuundia istilahi (kama vile **uunganishaji/uambatanishaji, ubunaji, unyambuaji, ufufuaji** na kwa kiwango fulani **ukopaji**) zikipewa kipaumbele katika ujenzi wa istilahi mpya, zitachangia katika ukubalifu wa istilahi zinazoundwa, kwa watumiaji wake (taz. 6.2.4). Aidha, ni matumaini yetu kuwa uzingativu wa mifanyiko hii utarahisisha kazi ya uundaji istilahi za Kiswahili.

Ni muhimu tukumbushane hapa kwamba mbinu za uundaji istilahi ni za upekee-lugha na utekelezaji; na hivyo basi mfululizo wa matumizi yake hutofautiana kwa kutegemea muundo wa kifonolojia na kisarufi wa kila lugha. Hata hivyo, ujenzi wa istilahi mpya za isimu ya Kiswahili kwa mbinu zalishi, na za kisayansi zilizotajwa hapo juu, ndio msingi wenyewe wa ukuzaji wa lugha.

Na kama alivyosema Chimerah (1998a:40) matumizi ya Kiswahili chenyewe katika kuunda istilahi mpya za Kiswahili yanaonyesha ukomavu wa lugha hii. Hii yaelekea kweli, hususani katika medani ya isimu. Ni uthibitisho pia kwamba mbinu ya ufufuaji na upanuzi wa maana za msamiati asilia (taz. 5.1.1.3.1.2, uk. 254) inayotumiwa sana na BAKIKE/Nabhany, ikirekebishwa na kuimarishwa kwa ujuzi wa isimu ya lugha, ingefaa sana kutumiwa katika fani anuai za sanaa, sayansi za jamii, na teknolojia (Mbaabu, 1989:25). Aidha, ujenzi wa msamiati wa mumo kwa mumo ni uthibitisho kwamba Kiswahili kina uwezo wa kuzalisha istilahi mwafaka bila kutegemea kukopa sana kutoka kwenye lugha nyingine. Kwa mfano, katika orodha ya istilahi za hisabati 708, ni istilahi 36 pekee ambazo zimekopwa kutoka Kiingereza; vilevile, miongoni mwa istilahi za jiografia 629, ni istilahi 38 pekee ambazo zimekopwa kutoka Kiingereza (Irira, 1986:48).

Iwapo wanaleksikografia wa Kiswahili watazingatia kwa kadri inavyowezekana mfanyiko wa uasilishaji/ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo wa istilahi za isimu ya Kiswahili, lugha hii, kama tulivyotaja mbeleni, itabuniwa msamiati maridhawa na itakuwa na istilahi 'faafu' zaidi. Istilahi 'hafifu' zilizoundwa kimakosa (k.v. **mazingara, nasibu,** (taz. Besha, 1994:86)) kwa sababu ya haraka ya kujaza mapengo katika dhana za kigeni, zitakufa zenyewe. Labda ni muhimu, kwa misingi ya yale yaliyojadiliwa kufikia sasa kuhusu mbinu za uundaji istilahi, kuchunguza na kufanya mapitio ya kila mojawapo ya mbinu hizo kwa minajili ya kuibua dosari na upana wake wa kimatumizi katika viwango vya kimataifa.

### 5.2.1 Mapitio ya Mbinu za Uundaji Istilahi

Mifanyiko iliyojadiliwa hapo juu ni mbinu za kisifabia zinazotumiwa katika lugha nyingi kuendeleza leksikoni zao, na wakuzaji wa Kiswahili wamekuwa wakitumia mbinu hizo katika harakati zao za kuunda istilahi. Ishadaiwa, katika tasnifu hii, kwamba mfululizo wa matumizi ya mbinu za kuundia istilahi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine (upekee-lugha) kwa kutegemea muundo wa kifonolojia na kisarufi wa kila lugha husika. Hapa tutachunguza ruwaza za kisayansi na zalishi katika ukuzaji wa lugha kiistilahi.

#### 5.2.1.1 Uunganishaji/Uambatanishaji

Mbinu ya uunaganishaji/uambatanishaji ambayo kwayo maneno mawili au zaidi huunganishwa na kuwa neno moja huru au la kujitenga, ni zalishi katika lugha nyingi za Kijerumani, Kirusi (Kodukov, 1976), Kipoli na Kiindonesia (Alisjahbana, 1976). Hata hivyo, lugha nyingine kama vile Kihebrania na Kichina hazitumii sana mfanyiko wa uunganishaji katika kuunda istilahi (Pasierbsky, 1989:90-103). Kadhalika, lugha ya Kitaliano, kama ilivyo lugha zote za Kiromania, pia hutumia kwa nadra sana mbinu ya uunganishaji/uambatanishaji katika kuendeleza leksikoni (Kramer, 1983:311). Na, kama anavyosema Mwansoko (1990:65), Kifaransa, ingawa kina uwezo wa kutumia mbinu ya uunganishaji, hutumia sana ruwaza za istilahi ungani za aina ya kihusishi "*de*" na "*a*" pekee.

Abdulaziz (1989:37) anasema kwamba lugha ya Kiswahili haiambatanishiki kwa urahisi. Dhana "ambatani" mara nyingi huwakilishwa kimaandishi kwa ujenzi endelezi. Kwa mfano, Kiswahili hukopa istilahi kama *"sodium"* na *"chloride"* pamoja na umbo lake ambatani, kama **sodiamukloraidi.** Abdulaziz (ibid) anatoa mfano ufuatao katika kuonyesha ukosefu wa ulinganifu wa mtiririko:

| | |
|---|---|
| *sodium nitrate* | **nitratisodio** |
| *iron chloride* | **kloridichuma** |
| *hydrochloric acid* | **asidi hidrokloriki** |
| *sodium hydrogen sulphate* | **kiberitihidrojeni-sodio.** |

Mtaalam huyu (ibid:38) anapendekeza, na sisi tunakubaliana naye, kuwa wakuzaji wa Kiswahili wanahitajika kutoa uamuzi kuhusu njia yenye ulinganifu wa mtiririko. Aidha, pana haja ya kuimarisha njia ya kuendeleza mbinu ya uunganishaji, ya kuundia istilahi za Kiswahili ili istilahi ambatani zinazoundwa zisiwatatanishe walengwa wake.

Aidha, si rahisi kuelewa moja kwa moja maana katika istilahi ambatani ambapo zaidi ya mzizi mmoja hutumika kuzalisha neno moja. Kwa mfano:

**(127)**

(127a) *mycology* **elimuuyoga** (BAKITA, 1995).

(127b) *gynaecology* (i) **elimuuzazi** (TUKI, 1990), au

(ii) **elimugonjwamke** (Kiingi, 1989)

(Elimu ya ugonjwa wa mwanamke).

(127c) *appendix* **kidoletumbo.**

Istilahi ambatani katika **(127)**, zinakosa sifa za udhahiri na uangavu za PEGITOSCA. Mtumiaji wa Kiswahili wa kawaida atatatizika kufasiri maana katika (127a) iwapo hajui maana ya mzizi **uyoga**. Istilahi ambatani **elimuuzazi** (127b,i) na **kidoletumbo** (127c) hazina udhahiri kwa sababu hazilengi kinachomaanishwa bayana (taz. pia Falk Julia, 1973). Mfano wa (127b,ii), ingawa una sifa za udhahiri, hauna sifa muhimu ya iktisadi katika istilahi. Kutokana na sababu kwamba maana ya istilahi ambatani haiendi kila mara na maana ya sehemu zake (k.m. *blackbox* yaweza kuwa nyeupe au manjano), ni vigumu kufasiri maana inayowakilishwa katika istilahi ambatani. Kwa hivyo, ni muhimu, kama anavyodai Abdulaziz (1989:38) kuwepo na njia ya ulinganifu wa mtiririko katika mbinu ya uunganishaji ili istilahi 'faafu' za Kiswahili, hususani za isimu, zizalishwe kwa wingi kama ilivyo katika mfano huu **(128)**:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (128a) | *affricate* | **kilegezapumzi** | legeza + pumzi |
| (128b) | *flap* | **kigongaufizi** | -gonga + ufizi |
| (128c) | *segment* | **kipandesauti** | -kipande + sauti |
| (128d) | *retroflex* | **kibinuaulimi** | -kibinua + ulimi. |

### 5.2.1.2 Ubunaji/Fasiri ya Maana za Maneno

Ingawa uendelezaji wa istilahi kwa mbinu ya ubunaji hutumika katika lugha nyingi duniani, k.v. Kiingereza (Barber, 1964), Kipoli (Cienkowski, 1983), Kijerumani (Ehlich, 1989), na Kiindonesia (Alisjahbana, 1976), haijatiliwa uzito ipasavyo katika Kiswahili. Uzingativu wa ruwaza hii na wanaleksikografia wa Kiswahili utarahisisha na kuchapusha kazi ya uundaji istilahi

za isimu ya Kiswahili (taz. pia Muranga, 1992). Ubunaji ni mfanyiko bora zaidi katika uendelezaji wa lugha kiistilahi, na hakuna dosari au udhaifu wowote ambao tungeweza kuutoa. Ni mbinu muhimu sana ya uendelezaji istilahi katika fani anuai za sanaa, sayansi menyu, sayansi za kijamii, isimu, teknolojia na fani nyinginezo zinazodhaniwa kuwa ni vigumu kuwakilishwa kwa Kiswahili (taz. Besha, 1972).

#### 5.2.1.3 Unyambuaji

Uundaji wa istilahi kwa mbinu ya unyambuaji si suala geni. Unyambuaji ni mfanyiko zalishi ambao hutumika sana kwenye lugha za Kijerumani, Kitamili (Zvelebil, 1983), lugha za Kislovoniki (Fodor, 1983/4), Kiingereza (Barber, 1964; Bauer, 1983), Kiindonesia (Alisjahbana, 1976), Kitaliano (Kramer, 1983), na pia Kiswahili (Tumbo na Mwansoko, 1992). Hata hivyo, mbinu hii si zalishi katika lugha nyingine. Kihebrania, kwa mfano, kina idadi ndogo sana ya viambishi mnyambuliko. Kichina hakina kabisa viambishi mnyambuliko.

Katika Kiswahili, istilahi zinazozalishwa kutokana na mbinu ya unyambuaji, hususani ya isimu ya Kiswahili, hueleweka kwa urahisi sana na walengwa wake, kwa sababu hubuniwa kutokana na mizizi ya kawaida ya lugha hii. Tazama kwa mfano,

| | | |
|---|---|---|
| *adjective* | **kivumishi** | < -vumisha |
| *inversion* | **mpinduo** | < -pindua |

#### 5.2.1.4 Ufufuaji na Uasilishaji wa Msamiati Asilia

**Ufufuaji** wa msamiati asilia na ujenzi wa mumo kwa mumo wa istilahi ni mfanyiko wa kuendeleza lekskoni ambao umewahi kutumika kwenye lugha nyingi duniani. Utaratibu wa ufufuaji wa maneno asilia hutumika katika Kihebrania (Rabin, 1989), Kijapani, Kikorea (Takada, 1989), Kichina (Pasierbsky, 1989), na pia katika Kiswahili (Mwaro, 1993). Ufufuaji wa msamiati wa zamani katika Kiswahili, ingawa ni ruwaza ambayo haitumiki katika 'kuunda' msamiati mpya, lakini ni muhimu katika ukuzaji wa lugha. Msamiati asilia uliosahaulika katika *Standard Swahili*, mbali na kwamba unairudishia lugha hii ukale wake na kuiondolea ugeni mwingi kimsamiati (taz. Whiteley, 1969:79-96), pia unaweza kutumika pale ambapo hapana msamiati mwafaka (taz. Mdee, 1981; 1986). Tazama kwa mfano:

**mbolezi** (Kimvita) 'Ushairi wa makiwa' (*elegiac poetry*)
**njeo** (Kiamu) *tense*
**ng'ozi** (Kimtang'ata) *leafcurl* (taz. pia Mukhwana, 1988).

Msamiati asilia na wa kilahaja uhuishwe na kupewa matumizi mapya. Kwa mfano, asili ya maneno **mangala** - *microscope* (Nabhany, 1982) na **ningala** - *telescope* (Chimerah, 1998a) (**runinga** + **mangala**) ni Kiswahili chenyewe, na ni upanuzi wa matumizi yake katika muktadha mwingine.

Utaratibu wa uasilishaji au ufufuaji wa msamiati asilia na ujenzi wa mumo kwa mumo ni muhimu, na unazalisha istilahi zinazoeleweka (zenye ubuye) kwa urahisi, na dhahiri kwa walengwa wake. Mfanyiko huu unafaa kutiliwa manani na wabunaji istilahi za

Kiswahili katika fani za sanaa, sayansi za jamii, na teknolojia (taz. pia Besha, 1972; na Mutahi, 1986; kwa ufafanuzi zaidi juu ya uendelezaji wa lugha kiistilahi mumo kwa mumo). Na kama anavyosema Mdee (1986:125) "Kiswahili kina maneno mengi asilia ya kuweza kueleza dhana kadhaa, lakini kutoyajua kwetu kumefanya kuunda au kutohoa maneno kwa dhana hizo." Pale ambapo hatuwezi kupata istilahi mwafaka katika Kiswahili chenyewe au kwa ruwaza ya ufufuaji wa msamiati asilia basi natuunde. (Kuhusu uzalishaji wa istilahi za isimu kwa mfanyiko huu katika lugha za Uganda, tazama Muranga, 1992:3-23).

#### 5.2.1.5 Uhulutishaji

Mbinu ya uhulutishaji hutumika pia kwenye lugha nyingi ulimwenguni kama vile Kiingereza (Barber, 1964) na Kirusi (Kodukov, 1979). Utaratibu wa uhulutishaji (ambapo mofimu huru mbili au zaidi huchanganywa ili kuunda neno jipya, ambalo hubeba kwa pamoja maana zote za mofimu huru husika), unakaribiana sana na uunganishaji/uambatanishaji, na si rahisi kuzitenganisha ruwaza hizi mbili za kuundia istilahi (rejelea 4.2, uk. 133). (Taz. kwa mfano, neno la Kiingereza *sub topia* < ***suburban utopia****)*. Mbinu za uhulutishaji na ubunaji ndizo zinazotumiwa sana na Chimerah (1998a, 1998b) na Nabhany (1982, 1998) katika uendelezaji na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili (rejelea jedwali la 1).

Hata hivyo, hakuna utaratibu madhubuti unaofuatwa katika kujenga istilahi mahuluti, na, kwa jinsi hiyo, baadhi ya istilahi

zinazozalishwa kupitia mbinu hii hazina uangavu, ulinganifu wa mtiririko, na, hivyo basi, hazieleweki kwa urahisi kwa walengwa wake (k.m. **wewindu, kanieneo, kizigeu**). Nyingi za istilahi mahuluti huungwaungwa kiholela kufuatana na mapenzi ya wale wanaoziunda (Tumbo na Mwansoko, 1992:36).

### 5.2.1.6 Ukopaji na Utohoaji

Ukopaji, hasa kutoka lugha zilizoendelea, ni mbinu inayotumika katika karibu lugha zote duniani (Abdulaziz, 1989; McCrum, Cran na McNeil, 1986). Temu (1984:117) anadai kuwa hakuna lugha ambayo inaweza kujiendeleza bila kukopa istilahi kutoka lugha nyingine, na kwamba juhudi za wapangaji lugha wengi (taz. Zvelebil, 1983; kuhusu Kitamili) za kukwepa ukopaji hazikufaulu. Mtaalam huyu anatazama lugha za kigeni, hususani Kiingereza, kama ndilo kapu au ghala mnamofaa kuchotwa istilahi zinazohitajika katika Kiswahili. Sisi, ingawa tunaelewa kuwa 'hakuna lugha duniani isiyokopa' na kwamba ukopaji ni mbinu mojawapo ya kupanua lugha kiistilahi (taz. Chimerah, 1998a:38). Hata hivyo, kama ilivyoelezwa mbeleni, tunapendekeza kuwa mbinu ya ukopaji itumiwe tu iwapo hapana njia nyingine ya kukuza lugha ya Kiswahili. Iwapo ipo, njia hiyo itumike.

Kihore (1983:170) anadokeza kuwa "hadi leo Kiswahili bado kinaendelea kuchukua maneno toka lugha za kigeni...uchunguzi ufanywe kuonyesha ni vipi na kwa kiasi gani kuingizwa kwa maneno ya kigeni katika Kiswahili kunavyoendelezwa na mapenzi tuliyo nayo kwa watu fulani na lugha zao..." Tunakubaliana na Kihore

kwamba ukopaji mwingi wa istilahi, hasa za isimu ya Kiswahili, kutoka lugha za kigeni (Kiingereza, Kiarabu na nyinginezo) huenda ulitokana na waundaji istilahi hizo kuonea fahari istilahi mkopo na lugha wanazozikopa istilahi hizo (taz. k.m. matumizi ya **fonimu** badala ya **kitamkwa**, **idiofoni** badala ya **kielezimiigo**, **glota** badala ya **sauti ya kikoo**). Ingawa Kiingereza kinaendelea kujirutubisha kiistilahi kwa kukopa istilahi kutoka lugha nyingine za kigeni, hii si sababu tosha ya Kiswahili pia kufanya hivyo. Suala la 'upekee-lugha' halina budi kuzingatiwa. Ni muhimu kueleza hapa kwamba mfululizo wa kutumia mbinu fulani ya kuundia istilahi, mbali na kwamba unategemea 'upekee-lugha' na muundo wa kifonolojia na kisarufi wa kila lugha husika, pia unaweza kubadilika kiwakati. Katika Kihangari, kwa mfano, mbinu ya uambishaji ndiyo iliyotumika sana katika karne ya 19 kuendeleza leksikoni ya lugha hiyo; lakini kwa wakati huu, mbinu ya uunganishaji ndiyo inayotumika sana (Fodor, 1983/4:448). Mabadiliko kama haya ya mbinu kiwakati hayana budi kuzingatiwa, na huenda mbinu zisizotumika sana katika kuundia istilahi za Kiswahili (k.v. uhulutishaji, kaleki, uradidi, akronimu) zikawa ndizo zenye kutumika sana karne ya 21.

### 5.2.1.7 Kaleki

Mbinu ya kaleki (au ukopaji sisisi) pia imekuwa ikitumika kuundia istilahi katika lugha nyingi duniani kama vile; Luganda, Runyankore-Rukiga (Muranga, 1992), Kijerumani (Falk, 1973), Kiingereza (Barber, 1964) na Kiswahili. Istilahi nyingi za isimu ya Kiswahili zinazoundwa kwa ruwaza ya kaleki, kama ilivyotajwa

hapo awali, huhamishwa kutoka kwa Kiingereza kama mfano huu **(129)** unavyoonyesha:

(129a) **lugha toni** *tone language*

(129b) **kushusha daraja** *rank shift*

(129c) **fonetiki maabara** *laboratory phonetics.*

(taz.pia mfano wa 73)

Kutokana na mfano huu **(129)** ni dhahiri kwamba istilahi za isimu zinazojengwa kwa mfanyiko wa kaleki zina kiwango cha juu cha 'ufaafu' na uangavu, na haziwakanganyi walengwa wake. Hata hivyo, katika utaratibu huu, pana hatari kubwa ya waundaji istilahi kushindwa kusawiri dhana zilizokusudiwa kama ilivyokuwa katika lugha ya chasili. Ili maana katika dhana ya msingi iliyokuwa katika lugha chasili (changizi) isipotoke, ni muhimu wanalugha watumie mbinu ya kaleki kwa makini katika kukuza lugha ya Kiswahili.

#### 5.2.1.8 Upanuzi wa Maana za Maneno

Mbinu ya upanuzi wa maana za maneno pia hutumika katika lugha nyingi, ingawa hutumiwa sana kuundia istilahi za Kiingereza (Barber, 1964:219). Kuhusu mfano wa istilahi za Kiingereza zilizoundwa kwa mfanyiko huu, rejelea **4.5**, uk. 148, na **5.1.1.2.4**, uk. 227. Kama tulivyotaja hapo awali (taz. **4.5**), istilahi zinazoundwa kwa mfanyiko huu zinaweza kutatanisha walengwa wake, hasa kutokana na ugumu wa kutofautisha maana mahsusi ya istilahi kutoka kwa maana zake za kawaida (taz. maelezo zaidi katika 3.3.3, uk. 80).

#### 5.2.1.9 Uradidi

Uradidi, kama tendo la kukariri au urudiaji wa mofimu nzima, ama sehemu ya mofimu, au mfuatano katika neno (Batibo & Rottland, 1992:89), ni mbinu inayotumika katika Kihehe (Odden & Odden, 1985), Kihausa (Newman, 1986), Kiingereza (Bauer, 1983), Kijerumani (Coulmas, 1989), lakini si zalishi katika lugha nyingine. Kiswahili, kwa mfano, hakitumii sana mbinu ya uradidi kuzalisha istilahi za isimu (Ashton, 1944:316). Katika Kiindonesia, ingawa uradidi huweza kutumika, lakini baadhi tu ya mofimu ndizo huwekwa katikati ya mzizi, kwa vile lugha hii inaruhusu kutenganishwa kwa mzizi. Kwa mfano:

**Kiindonesia**

| **Umoja** | **Wingi** |
| --- | --- |
| *Kursi* (kiti) | *kursikursi* (viti) |
| *lalat* (nzi) | *lalatlalat* (nzi - wengi) |

Uradidi nusu (uradidi wa sehemu tu za mofimu) ni nadra sana kutumika katika lugha hii ya Kiindonesia (taz. Rubanza, 1996:54).

Katika lugha ya Ilakano katika Ufilipino, uradidi kamili (urudiaji wa mofimu ile ile au zile zile mara mbili) hutumika sana. Mofimu ya hali (umoja/wingi) huwekwa mwanzoni mwa mofimu mzizi, au shina, au hata neno zima, kama mfano huu **(130)** unavyodhihirisha:

**Kifilipino**

| | **Umoja** | **Wingi** |
| --- | --- | --- |
| (130a) | *ulo* (kichwa) | *ululo* (vichwa) |
| (130b) | *talon* (uwanja) | *taltalon* (nyanja/viwanja). |

Katika (130a) mofimu ya hali ya wingi *ul* imeongezwa mwanzoni mwa shina *ulo*. Katika mfano wa (130b), sehemu ya neno *tal* imeongezwa mwanzoni mwa shina *talon* (taz. pia Kapinga, 1983:180).

Ingawa lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kutumia aina zote mbili za uradidi, yaani uradidi kamili na uradidi nusu (k.v. katika **barabara, kizunguzungu** na **unyevunyevu**, (taz. Polome, 1967:104-5), utaratibu huu haujengi istilahi angavu, na, kwa ajili hiyo, etimolojia ya baadhi ya maneno yanayobuniwa haieleweki wazi. Kwa mfano, si wazi kuwa maneno **barabara,** na **kizunguzungu** yanatokana na **-bara** au **-zungu** yanajirudia. Na anavyosema Rubanza (1996:55), ili maneno kama haya yawe na sifa ya uradidi, yapaswa kuwa ama:
**barabarabarabara** >*barabara> *barabarara,
**kizunguzunguzunguzungu**> *kizunguzungukizunguzungu.

Ili mfanyiko wa uradidi utumike sana katika uzalishaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, pana haja ya kutoa fasili mufidi ya uradidi inayoafiki na kulandana kikamilifu na mifano, au (na) matumizi halisi. Kwa kufanya hivyo, tofauti baina ya mfanyiko wa uradidi (upachikaji wa mofimu katika mzizi au shina ambalo linarudiwa) na wa unyambuaji (upachikaji wa mofimu katika mzizi), itabainika wazi. Aidha, umuhimu wa kubainisha mzizi au shina la neno linalorudiwa utazingatiwa, sio tu na waundaji istilahi, bali pia na walengwa wake.

Kutotumika sana kwa mbinu ya uradidi kunatokana pia na ukosefu wa udhahiri katika istilahi radidi. Maana zinazojitokeza katika istilahi radidi hutegemea muktadha na wala sio umbo la neno.

Wanaleksikografia wa Kiswahili wanahitajika kubuni istilahi radidi kwa mujibu wa misingi ya uundaji wa istilahi (taz. Picht & Draskau, 1985). Kwa hivyo, itakuwa vyema iwapo vyombo vya BAKITA, TUKI, BAKIKE na waundaji binafsi wa istilahi za Kiswahili watatambua kuwa si kila istilahi yenye kuonyesha kukariri inaafiki fasiri ya uradidi (taz. Marvesik, 1978:299-334) kwa maelezo ya kina juu ya mfanyiko wa uradidi)).

### 5.2.1.10 Finyazo (Akronimu na Ukatizaji)

Mbinu za akronimu na ukatizaji (finyazo) hutumika pia katika lugha nyingi, ingawa katika Kiingereza inaelekea ni mifanyiko inayofahamika sana ya kuundia istilahi (Barber 1964:221). Mfano wa finyazo katika Kiingereza ni:

| | |
|---|---|
| *telly* | *television* |
| *cab* | *cabriolet* |
| *photo* | *photograph* (mwisho wa neno unadondoshwa) |
| *prefab* | *prefabricated house* |
| *perm* | *permanent wave* |
| *pub* | *public house* (kishazi kizima kinadondoshwa). |

Katika Kiswahili, mfanyiko wa finyazo hautumiki sana katika kujenga istilahi, hususani za isimu, kutokana na sababu mbili kuu: Kwanza kabisa, hakuna mantiki ama mfumo ulio wazi wa kufuatwa katika uundaji wa istilahi finyazo. Kwa mfano, ni kwa nini **NINGALA** lisiwe **RUNINGALA** (runinga+mangala) - *telescope?* Labda ni kwa sababu katika '*telescope*' simu haimo. Pili, istilahi nyingi zinazoundwa kwa utaratibu wa finyazo ni za muda tu, 'hufa' kwa urahisi mno. Hata hivyo, baadhi ya finyazo -

akronimu, huwa ni za kudumu katika leksikoni ya lugha (k.m. **UKIMWI** - ni neno ambalo limepata mashiko imara).

Ili mbinu za ufupishaji (finyazo) za akronimu na ukatizaji ziepuke matatizo haya na zitumike sana katika uundaji wa istilahi za Kiswahili, ni muhimu waundaji istilahi wafuate mantiki fulani yanayoeleweka. Vilevile, wafuate mfumo ulio bayana wa kuteua silabi za maneno katika kuzalisha neno jipya. Kufikia sasa, inaelekea, kama anavyosema Mdee (1986:123), uteuzi wa silabi za kuundia istilahi finyazo unafanywa kwa sibu. Uundaji istilahi kwa kufuata mfumo wa kimantiki ipasavyo utaziwezesha istilahi finyazo nyingi zinazozalishwa kuwa na upeo wa juu wa ubora, ufaafu, na usawazisho mzuri. Vilevile, zitaeleweka kwa urahisi kwa watumiaji wake na, kwa namna hii, kuimarisha mawasiliano ya kitaaluma.

Kwa ujumla, ili kuepuka udhaifu na dosari zilizojadiliwa katika mbinu mbalimbali za kuundia istilahi, tunapendekeza vyombo vya ukuzaji lugha na waundaji istilahi, wanapounda istilahi mpya, wafikirie mfumo wa lugha yote. Istilahi zinazoundwa moja kwa moja na bila kuzingatia ufungamano wa kidhana zapasa zinyimwe ithibati ya BAKITA na BAKIKE.

## 5.3 Muhtasari wa Sura ya Tano

Katika sura hii, tumejadili mbinu za kisifabia zinazotumika katika uendelezaji na ukuzaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili. Pia tumetathmini 'usayansi' katika mbinu za uundaji wa istilahi

za vyombo vya BAKITA, BAKIKE, TUKI na za wataalam weledi binafsi kama vile Kapinga, Chimerah, Mbaabu na Nabhany. Kutokana na tathmini hii, imedhihirika kwamba kuna usawa au usifabia katika mbinu za uundaji istilahi za Kiswahili. Kadhalika, kutokana na tathmini hii, imebainika kwamba mbinu za uendelezaji wa istilahi za Kiswahili zinazotumika sana ni ile ya uunganishaji, ikifuatiwa na ubunaji, unyambuaji, ufufuaji na upanuzi wa maana za maneno asilia, na ukopaji, kwa mfuatano huo.

Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba vyombo vya ukuzaji wa Kiswahili vya BAKITA na TUKI, na waundaji istilahi binafsi Watanzania (k.v. Kapinga) sana sana hutumia mbinu ya utohoaji na uswahilishaji wa istilahi mkopo. Kwa upande mwingine, imedhihirishwa kwamba chombo cha BAKIKE (Baraza la Kiswahili la Kenya) na waundaji istilahi binafsi Wakenya (k.v. Nabhany, Mbaabu na Chimerah) huchukua mashina ya Kiswahili chenyewe kama msingi wa uundaji istilahi mpya. Pia imeelezwa kuwa wanaleksikografia na wataalam Wakenya hutegemea mno maneno asilia na lahaja za Kiswahili, sana sana Kimvita na Kiamu, katika uendelezaji wa leksikoni ya lugha hii ya Kiswahili. Vile vile imebainika kwamba pale ambapo wanalugha Wakenya wameunda istilahi mpya ilhali kuna istilahi nyingine mwafaka iliyobuniwa na watu wengine, wamependekeza istilahi pendezi zaidi itumike.

Aidha, katika sura hii tumeonyesha kwamba mbinu ya ubunaji maneno ya Kibantu, mahali ambapo katika eneo zima maneno yanayotumika ni ya kigeni tu, hutumiwa sana na waundaji istilahi Wakenya katika ukuzaji wa istilahi, kuhusiana na hududi pana ya

mawasiliano kitaaluma. Imefafanuliwa kuwa mbinu ya ubunaji huzalisha istilahi mpya lakini zisizo 'mpya' hata kidogo kwa walengwa wake, maanake asili ya istilahi buniwa huwa ni Kiswahili chenyewe. Hali kadhalika, tumeeleza kuwa mbinu za uundaji istilahi, kama vile upanuzi wa maana za maneno, uhulutishaji, kaleki, uradidi, na ufupishaji, ingawa zinatumika katika lugha nyinginezo duniani, sio zalishi, na hazitumiwi sana katika uzalishaji wa istilahi 'faafu' za Kiswahili. Mapitio na tathmini ya mbinu za uundaji istilahi zinazotumiwa na vyombo vya BAKITA, TUKI, BAKIKE na watu binafsi walioteuliwa, yamebainisha udhaifu, na dosari. Aidha yamebainisha na sababu za kupendelewa kwa mbinu fulani ya ukuzaji istilahi kuliko nyingine. Tumeonyesha pia kuwa maana zinazojitokeza kutokana na istilahi mahuluti (mifito), istilahi mkopo, finyazo, na istilahi zinazoradidiwa si bayana, na, kwa hivyo, fahiwati zingine zinashindwa kujichomoza kidhahiri.

Isitoshe, katika sura hii, tumeonyesha kuwa mbinu ya ufufuaji na upanuzi wa maana za msamiati asilia ikirekebishwa na kuimarishwa kwa ujuzi wa isimu ya lugha, ingefaa sana kutumiwa katika uendelezaji wa leksikoni katika medani za sanaa, sayansi za jamii, na teknolojia. Tumeeleza kuwa mtindo na imani ya kutazama lugha za kimagharibi, hasa Kiingereza, kama ndilo kapu au ghala mnamofaa kuchotwa istilahi zinazohitajika katika Kiswahili, unafaa uchunguzwe upya, manake ukopaji si ubunaji. Aidha, tumesisitiza kuwa mfululizo wa matumizi ya mbinu za uundaji istilahi hutegemea 'upekee-lugha,' na hutofautiana kwa kutegemea muundo wa kifonolojia na kisarufi wa kila lugha. Vilevile,

imesisitizwa kuwa mfululizo wa kutumia mbinu fulani za kuundia istilahi hubadilika kiwakati.

Fauka ya hayo, katika sura hii, mna dhana ya usanifishaji wa istilahi kama kitendo maalum kinachohusu sehemu ya lugha. Tumeonyesha kuwa mbinu za kuundia istilahi, jumla na istilahi zenyewe, zinapaswa 'kutandawazwa' ili kupunguza ukuzaji na **uundaji huria.** Imefafanuliwa pia kwamba mbinu za kisayansi zitakazotandaridhishwa zitumiwe kama dira ya kuamulia 'usayansi' katika istilahi mpya zinazozalishwa na vyombo vya ukuzaji lugha, na wataalam binafsi wanaobuni istilahi za lugha hii.

Aidha, katika sura hii, tumechochea utafiti zaidi juu ya manufaa ya visawe katika ukuzaji wa istilahi na lugha kwa jumla. Mintarafu ya ukweli kwamba visawe huondoa uchapwa wa lugha, imesisitizwa kuwa kuna njia mbili za kukuza lugha kiistilahi, nazo ni: Kwa kuizidishia visawe vya kiistilahi, na kwa kujaza mapengo ya kiistilahi yaliyopo na yatokanayo na aidha kufa kwa istilahi fulani, ama uingizwaji wa dhana za kigeni katika lugha pokezi. Imesisitizwa, vile vile, kwamba manufaa ya visawe vya kiistilahi hutegemea fani au taaluma yenyewe. Mathalani, katika taaluma ya isimu na sayansi menyu (tofauti na katika fani za sanaa, sayansi ya jamii na teknolojia) kuweko kwa visawe vingi vya kiistilahi vyenye kurejelea dhana moja huleta utata na ugumu katika ufundishaji, na huwakanganya walengwa wake.

Tunatarajia kuwa sura hii itawapa mwanga na kuwaelekeza wachapishaji, waandishi, walimu, wanafunzi, watangazaji,

wanaleksikografia, waundaji istilahi binafsi na wapenzi wa Kiswahili, kuhusu nyenzo na mbinu za kisayansi za uundaji wa istilahi. Tunatumaini kuwa sura hii itakuwa mwongozo utakaoelekeza fikra za wabunaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, na juhudi zao kwenye mwelekeo tama wa kubuni istilahi 'faafu' zinazohitajika ili lugha hii iweze kujieleza kikamilifu katika isimu.

Pia, tunatumaini kuwa sura hii itawafaa wapenzi wa Kiswahili wote popote walipo, katika kuelewa mbinu zalishi na za kisayansi za uundaji istilahi bila shida kubwa. Kadhalika, ni matarajio yetu kuwa kazi hii itawaelekeza na kuhusianisha wabunaji istilahi binafsi na vyombo vya ukuzaji Kiswahili vya BAKITA, BAKIKE na TUKI, ilimradi waweze kukamilishana kifikira na kiutekelezaji katika juhudi zao za kuendeleza lugha ya Kiswahili. Mwisho, tunatumaini kwamba sura hii imemulika na kushughulikia baadhi ya maswala 'yanayolalamikiwa' ipasavyo, hususani, suala la 'upungufu' wa istilahi za isimu, linalowasumbua sana walimu, wanafunzi, wafasiri, na waandishi wa matini za isimu.

# SURA YA SITA

## TATHMINI YA USAYANSI KATIKA ISTILAHI ZA ISIMU

### 6.0 Utangulizi

Hadi sasa vyombo vya kukuza istilahi za Kiswahili vya BAKITA na TUKI na wanalugha binafsi wanaendelea kuundia istilahi lugha hii, zikiwemo istilahi za isimu. Tathmini ya istilahi za isimu zinazobuniwa haina budi kufanywa ili kuona kama istilahi hizo zinazingatia 'usayansi.'

'Usayansi' katika istilahi, kama ilivyoelezwa hapo awali, ni uwezo wa istilahi kufanyiwa majaribio au utafiti na kuweza kuelezwa kutokana na utafiti. Kadhalika, 'usayansi' katika istilahi ni uwezo wa istilahi kuweza kuelezwa kimantiki, ili 'ufaafu' wake ueleweke, kwa kufuata na kuzingatia vigezo na kanuni maalum za uundaji wa istilahi (rejelea 3.3.2, uk. 64).

Kama tulivyotaja mbeleni, katika tathmini ya istilahi za isimu ya Kiswahili, kitakachosisitizwa ni vigezo vya kisayansi vya ufaafu wa istilahi na misingi ya uundaji wa istilahi. Ni muhimu ieleweke, kutokana na utangulizi huu, kwamba katika matumizi ya lugha, wasemaji hutofautiana sana. Ziko tofauti za aina nyingi, kama vile za kijamii, kihistoria, kimasafa, kiutamaduni, na kisiasa. Tofauti hizi huleta 'ugumu' katika maelekeo ya kufikia kiwango cha usawa (umataifa) ambao unahitajika, kwa upande wa mtumizi na wala sio mbunaji, wa kuteua istilahi faafu za isimu.

Kwa hivyo, taarifa zitakazotokana na tathmini ya istilahi za isimu ya Kiswahili itakuwa na manufaa mengi: Kwanza kabisa, tathmini ya istilahi za isimu itaonyesha istilahi zenye upeo mkubwa wa ubora na ukubalifu kwa walengwa. Pili, tathmini ya istilahi za isimu itawasaidia watumiaji wa Kiswahili katika uteuzi wa istilahi 'faafu' zaidi panapotokea haja ya kuchagua kati ya istilahi mbili, tatu au zaidi zenye kurejelea dhana moja. Tatu, tathmini hii itasaidia katika kuteua mfanyiko zalishi na wenye 'usayansi' kati ya mifanyiko mingi inayotumika katika kuunda istilahi. Kwa kigezo cha 'usayansi', mbinu bora katika uundaji wa istilahi za isimu itakuwa ile ambayo, kulingana na taarifa za tathmini, istilahi zake zitakuwa na kiwango cha juu cha 'usayansi'. Aidha, kwa kigezo cha 'usayansi', istilahi bora itakuwa ile ambayo itapata alama za juu kutokana na jaribio la PEGITOSCA (rejelea 1.6, uk. 11).

Uteuzi wa istilahi 70 za isimu ya Kiswahili kutoka katika orodha kuu ya istilahi 859 (taz. takwimu za istilahi katika Irira (1990:19) ulifanywa kwa kutumia vigezo vya **umbo la istilahi** na **mbinu za uundaji** wa kila mojawapo wa istilahi hizo. Pia, uteuzi wa istilahi ulizingatia kigezo cha matumizi; yaani historia pana ya kimatumizi ya istilahi katika taaluma ya isimu.

Kwa kutumia kigezo cha umbo la istilahi pekee, istilahi zote za isimu ziliainishwa katika makundi mawili (2). Makundi hayo ni:

(i) Istilahi zenye umbo sahili.

(ii) Istilahi zenye umboambatano la:

a) Maneno mawili au zaidi yasiyo na kihusishi (k.v. **vielezimiigo**)

b) Maneno mawili au zaidi yaliyoambatanishwa kwa vihusishi (k.v. **usawazisho wa matamshi**).

Kwa kutumia kigezo cha aina ya mfanyiko (mbinu za uundaji) istilahi za isimu ziliainishwa katika makundi sita (6) yafuatayo:

(i) Istilahi zinazotokana na uunganishaji/uambatanishaji.

(ii) Istilahi zinazotokana na ubunaji (tafsiri ya maana za maneno.

(iii) Istilahi zinazotokana na mnyambuliko (unyambuaji).

(iv) Istilahi zinazotokana na ukopaji (utohoaji na kaleki).

(v) Istilahi zinazotokana na upanuzi wa maana za maneno.

(vi) Istilahi zinazotokana na ufupishaji (uhulutishaji na akronimu).

Kwa kutumia vigezo vya umbo la istilahi pamoja na mifanyiko, istilahi za isimu ya Kiswahili ziliainishwa katika makundi kumi (10) yafuatayo:

(i) Istilahi sahihi zilizobuniwa, kwa mfano, **umezwaji** (*absorption*).

(ii) Istilahi sahihi zilizokopwa, kwa mfano, **leksisi** (*lexis*).

(iii) Istilahi sahihi zilizonyambuliwa, kwa mfano, **ubanaji** (*bracketing*).

(iv) Istilahi ambatani bila kihusishi zenye maneno mawili au zaidi yaliyotafsiriwa maana, kwa mfano, **kishazi sababu** (*causal clause*).

(v) Istilahi ambatani bila kihusishi ambazo neno moja kuu limetoholewa na neno la kijalizo limebuniwa, kwa mfano,

**sentensi funge** (*bound sentence*).

(vi) Istilahi ambatani bila kihusishi ambazo neno kuu limebuniwa na neno la kijalizo limekopwa, kwa mfano, **badiliko kianolojia.**

(vii) Istilahi ambatani bila kihusishi zilizokopwa, kwa mfano **fonetiki akustika.**

(viii) Istilahi ambatani zenye kihusishi ambazo neno kuu limebuniwa na neno la kijalizo limekopwa, kwa mfano, **uyeyukaji wa kifonimu.**

(ix) Istilahi ambatani zenye kihusishi ambazo neno kuu limekopwa na neno la kijalizo limebuniwa, kwa mfano, **anthropolojia ya ulughai** (Sengo, 1997).

(x) Istilahi ambatani zenye kihusishi na maneno mawili au zaidi yaliyotafsiriwa maana, kwa mfano, **mabadiliko sauti kimazingira.**

Kutokana na uainishaji huu, katika tathmini, kila kundi litawakilishwa na istilahi saba (7). Vigezo vya umbo la istilahi na mbinu za uundaji istilahi ndivyo vilikavyotumiwa katika kutathmini istilahi za isimu zilizoundwa na vyombo vya kukuza lugha na watu binafsi walioteuliwa.

## 6.1 Misingi ya Kutathmini Istilahi za Isimu ya Kiswahili

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni chombo kimojawapo muhimu katika ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili nchini Tanzania. Chombo cha BAKITA hurasimisha na husanifisha istilahi zinazobuniwa na kupendekezwa na chombo cha Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baada

ya kukubali na kusanifisha istilahi za isimu zinazopendekezwa na TUKI, BAKITA huzichapisha katika kijitabu cha *Tafsiri Sanifu* (taz. Toleo 2, 1976). Katika sura hii, tutajaribu kutathmini istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoundwa na TUKI (1990), bila (au na) uhusishwaji wa BAKITA na, aidha, istilahi zinazoundwa na wataalam binafsi wa isimu ya Kiswahili. Tathmini ya istilahi za isimu itasaidia, kama ilivyoelezwa hapo awali, katika uteuzi wa mifanyiko bora kati ya nyingi zinazotumika katika uendelezaji wa leksikoni ya lugha hii (taz. pia Rubin, 1971). Kadhalika, tathmini ya istilahi itasaidia katika kuchagua na kuunda istilahi 'faafu' za isimu ya Kiswahili na, kwa namna hii, kuiwezesha lugha hii kujieleza yenyewe kikamilifu katika taaluma ya isimu.

Kabla ya kuzama katika tathmini ya istilahi inayopendekezwa, huenda ni muhimu kuchunguza misingi ya kutathmini istilahi. Uchunguzi wa wanaisimu na wataalam wengi (k.v. Mdee, 1980; Kiingi, 1989; Mwansoko, 1990; na Sewangi, 1996) kuhusu suala la ufaafu na ukubalifu wa istilahi katika fani anuai za sanaa, sayansi na teknolojia, umeonyesha umuhimu wa kuegemeza tathmini ya istilahi kwenye kanuni ya kisayansi (taz. pia Picht na Draskau, 1985).

Hadi sasa, uchunguzi wa Kiingi (1989), na tathmini yake ya istilahi za kisayansi za Luganda na Kiswahili, ni wenye kuridhisha na ni muhimu kwetu. Katika kutathmini 'usayansi' katika istilahi za Luganda na Kiswahili, Kiingi (ibid:78-144) alitumia misingi ya ufaafu wa istilahi vya PEGITOSCA (rejelea 3.3.2.4, uk. 71). Vigezo vya PEGITOSCA, kama vipimo vya istilahi

bora, vinasaidia katika:

(i) Uteuzi wa istilahi 'faafu' kati ya istilahi mbili au zaidi zenye kurejelea dhana moja; yaani ikiwa kuna neno **x** ambalo linatakikana lichaguliwe kati ya maneno 1, 2, 3 jaribio la PEGITOSCA linaweza kutumika. Istilahi 'faafu' na inayokidhi mahitaji ya PEGITOSCA sharti ipate alama kati ya 12 na 20.

$x$ ---- $x^{-1}$, $x^{-2}$, $x^{-3}$

(ii) Kupendekeza neno linaloundwa kupewa hadhi ya istilahi;

$(x')$, $x$, $x^{i}$, $x^{ii}$ - ni maneno.

$R$ - ni kifaa cha kiwango cha upendekezaji wa neno kupata hadhi ya istilahi.

(iii) Kutambua sababu za kukubalika ama kukataliwa kwa istilahi. Dhana ya ukubalifu huambatana na maswala ya kiisimunafsia, utamaduni na hadhi ya jamii-tumizi-lugha (Chomsky, 1965:11) na haielezeki 'vivi hivi tu' (Mdee, 1980:51).

Ili waundaji istilahi wajitokeze na mtindo sawa wa kuundia istilahi, ni muhimu wafuate na wazingatie vigezo maalum. Vigezo vya ufaafu wa istilahi vinavyopaswa kuzingatiwa vinajitokeza katika PEGITOSCA.

Viwango vya upendekezaji wa neno $(x'_i)$ kupata hadhi ya istilahi $(R)$ vinadhihirisha kutokana na alama (P) zinatolewa kwa **kila kigezo** cha ufaafu wa istilahi (taz. Kiingi 1989:34-7). Hapa tutaeleza:

Kuhusu udhahiri, inasisitizwa kuwa:

$Rp(x'_i) = 6$ iwapo $(x'_i === x)$ kuna udhahiri (usawa wa neno na dhana kimaana

$Rp(x'_i) = 0$ iwapo $(x'_i === x)$ hakuna udhahiri katika

neno.

Kuhusu iktisadi, inasisitizwa kuwa:

$Re(x'_i)$ = 4 ikiwa kuna idadi ndogo ya silabi katika neno.

$Re(x'_i)$ = 1 ikiwa kuna idadi kubwa ya silabi lakini si kubwa sana (wastani).

$Re(x'_i)$ = 0 ikiwa kuna idadi kubwa sana ya silabi katika neno (katika Kiswahili istilahi ndefu sana huwa na silabi zaidi ya sita (Mwaro, 1998:25).

Neno lililo na silabi moja, mbili, au tatu, linapata alama 4 kutokana na sifa ya iktisadi.

Kuhusu uzalishaji, inasisitizwa kuwa:

$Rg(x'_i)$ = 3 ikiwa msingi wa ubunaji wa neno ni kitenzi.

$Rg(x'_i)$ = 2 ikiwa msingi wa ubunaji wa neno ni kielezi.

$Rg(x'_i)$ = 1 ikiwa msingi wa ubunaji wa neno ni nomino.

$Rg(x'_i)$ = 0 ikiwa ni vinginevyo.

Kuhusu umataifa, inasisitizwa kuwa:

$Ri(x'_i)$ = 1 ikiwa neno lina mashiko ya kimataifa.

$Ri(x'_i)$ = 0.5 ikiwa neno lina mashiko ya kitaifa lakini yasiyo ya kimataifa.

$Ri(x'_i)$ = 0 ikiwa ni vinginevyo.

Kuhusu uangavu, inasisitizwa kuwa:

$Rt(x'_i)$ = 2 ikiwa neno ni asilia, mnyambuliko au limebuniwa.

$Rt(x'_i)$ = 1 ikiwa neno ni mahuluti.

$Rt(x'_i)$ = 0 ikiwa neno ni mkopo.

Kuhusu utusani, inasisitizwa kuwa:

$Ro(x'_i)$ = 0 ikiwa neno lina sitara.

$Ro(x'_i)$ = -1 ikiwa neno lina matusi au ni mwiko.

Kuhusu utaratibu maalum, inasisitizwa:

$Rs(x'_i)$ = 0 ikiwa neno lina utaratibu maalum unaokubalika.

$Rs(x'_i)$ = -4 ikiwa neno, kulingana na kanuni za kimataifa,

lina uholela.

Kuhusu utaratibu ulio sawa, inasisitizwa kuwa:

$Rc(x'_i) = 0$ ikiwa neno lina utaratibu uliosawa unaokubalika kimataifa.

$Rc(x'_i) = -1$ ikiwa neno linafuata, kulingana na kanuni za kimataifa, utaratibu thabiti.

Kuhusu ukubalifu na ufaafu, inasisitizwa kuwa:

$Ra(x'_i) = 0$ ikiwa neno lina ukubalifu katika lugha.

$Ra(x'_i) = -1$ ikiwa ni vinginevyo.

Kwa utumikaji:

$Rp(x'_i) = P$, $Re(x'_i) = E$, $Rg(x'_i) = G$, $Ri(x'_i) = I$, $Rt(x'_i) = T$, $Ro(x'_i) = O$, $Rs(x'_i) = S$, $Rc(x'_i) = C$, $Ra(x'_i) = A$, na $R(x') = P$ ni alama muhimu katika tathmini ya istilahi za isimu ya Kiswahili. Tuchukue kwa mfano:

| | **1a) Prediketa** | **1b) Kiarifu** | **2a) Jinsiakike** | **2b) Menke kike** *(feminine gender)* |
|---|---|---|---|---|
| **P** | 1 | 6 | 2 | 6 |
| **E** | 4 | 4 | 4 | 3 |
| **G** | 1 | 2 | 1 | 1 |
| **I** | 0.5 | 0.5 | 1 | 0.5 |
| **T** | 0 | 1 | 2 | 2 |
| **O** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **S** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **C** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **A** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **P =** | 6.5 | 13.5 | 10 | 12.5 |

Maneno ya (**1b**) na (**2b**) yamefaulu jaribio la neno kupendekezwa kupata hadhi ya istilahi wakati ambapo maneno ya (**1a**) na (**2a**) yanaonyesha kutofaulu mahitaji ya jaribio la PEGITOSCA. Maneno ya (**1a**) na (**2a**) tunaweza kusema kuwa hayakidhi mahitaji ya jaribio hili kutokana na alama zake za chini, hasa katika sifa za udhahiri na uangavu wa istilahi.

Ni muhimu ieleweke kwamba misingi hii ya kutathmini istilahi sio taratibu za 'kisheria' ambazo lazima zifumbatwe na kila istilahi inayoundwa. Na kama wanavyodokeza Tumbo na Mwansoko (1992:32) kuna istilahi chache za isimu ya Kiswahili ambazo hazielezeki kutokana na mantiki yoyote au utafiti, na hukiuka taratibu zilizopendekezwa hapo juu. Hili ni jambo la kawaida, na hutokea kwenye lugha zote duniani. Hata hivyo, mantiki ya kuchunguza misingi ya kutathmini istilahi ya PEGITOSCA (taz. Kiingi, 1989) ni kwamba endapo misingi hiyo itafuatwa ipasavyo na wanaleksikografia na waundaji istilahi, basi nyingi ya istilahi za isimu zinazobuniwa zitakuwa na upeo wa juu wa ubora, na zitaeleweka kwa urahisi kwa walengwa wake. Kadhalika, kanuni za PEGITOSCA zinaweka msingi thabiti wa kutathmini istilahi za fani anuai za sanaa, sayansi za jamii, sayansi menyu, teknolojia na isimu, msingi ambao tunanuia kujenga. Tutaujenga msingi huu kwa kutathmini 'usayansi' katika istilahi za isimu zinazozalishwa na kusambazwa na TUKI (na baadaye kutathmini istilahi za wataalam binafsi), ambayo ndiyo mada inayofuatia.

### 6.1.1 Tathmini ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili za TUKI

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), katika juhudi zake za kuendeleza na kukuza istilahi, imeunda na kusambaza istilahi kwa walengwa mbalimbali, zikiwemo za isimu. Hapa, tunaazimia kuchunguza na kutathmini istilahi za isimu zilizochapishwa katika *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990) ili kuona kama istilahi hizo zina 'usayansi', na kama vigezo vya ufaafu wa istilahi vya PEGITOSCA vinazingatiwa.

Ziko kazi chache zilizoshughulikia tathmini ya istilahi zinazoundwa na kusambazwa na TUKI za Fasihi (*Kiswahili* 52/1&2, 1988), za Sayansi (*Kamusi ya Fizikia, Kemia na Biolojia*, 1990), Ufundi wa Matrekta/Magari (Ripoti ya Valmet 1986) na za Lugha na Isimu (Kamusi ya Isimu, 1987). Katika kazi yake "Probleme des Sprachausbaus in Entwicklungslandern, Terminologiepragung im Swahili" katika Finke (1983:77-118) Werner Krummer amewasilisha matokeo ya uchunguzi wake wa kimajaribio alioufanya kwa usaidizi wa TUKI mwaka wa 1975/76. Uchunguzi wa Krummer (1983) uliazimia kutathmini sifa za kiisimu katika istilahi mpya zilizoundwa na TUKI kuanzia mwaka wa 1964-1977 na ukubalifu wa istilahi hizo kwa walengwa. Uchunguzi huo ulionyesha kutoridhika kwa walengwa na udhahiri wa istilahi mpya zilizoundwa, hususani katika fani za sayansi. Hali ya kutoridhika (au kutokubalika) kwa walengwa, kwa maoni ya mtaalam huyu, inasababishwa na waundaji wa istilahi hizo kusisitiza sifa ya uangavu wa istilahi, huku wakipuuza vigezo vingine vya ufaafu wa istilahi. Krummer hakuona 'ufaafu' wowote katika maneno yaliyopendekezwa na TUKI (1987) na hakuona ni kwa jinsi gani yatapatiwa hadhi ya istilahi siku zijazo.

Vipengele vyote vya (a)- katika jedwali la (2) hapa chini vimechambuliwa kwa kina na Krummer mwenyewe. Hapa, kwa kifupi, jukumu letu linajikita katika kuchunguza iwapo mapendekezo ya TUKI, vipengele vyote vya (b)-, yanakidhi mahitaji ya vigezo vya ufaafu wa istilahi; uchunguzi ambao utatupatia mwongozo katika tathmini ya baadaye ya istilahi za isimu.

Jedwali 2: Ufaafu wa Istilahi

| | P | E | G | I | T | O | S | C | A | Alama |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (1a) uzoasafu | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | -2 | 0 | 0 | 2 |
| (1b) **spishi** | 6 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| (2a) insekta | 0 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| (2b) **mdudu** | 6 | 4 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (3a) chembe | 6 | 4 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| (3b) **seli** | 4 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 |
| (4a) elimumwili | 6 | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| (4b) **anatomia** | 3 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | -1 | 0 | 0 | 8 |
| (5a) nguvu | 0 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| (5b) **nishati** | 4 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | -1 | 0 | 0 | 8 |

(taz. pia Kiingi, 1989:170-172)

Vipengele au vitamkwa vyote (a-) vinavyopendekezwa na Krummer (1983), ila tu **elimumwili** na **chembe**, havikidhi jaribio la PEGITOSCA la 'ufaafu' wa istilahi. Katika istilahi zilizoundwa na TUKI (1987) (b-), maneno **seli**, **anatomia**, na **nishati** hayakufaulu jaribio hili kwa sababu ya kukosa sifa za udhahiri na utaratibu maalum.

Naye Kiingi (1989) amefanya tathmini ya 'ufaafu' wa istilahi za sayansi zilizoundwa na kuchapishwa na TUKI mwaka wa 1987 na kusanifishwa na BAKITA. Uchunguzi wa mtaalamu huyu ulikusudia, miongoni mwa masuala mengine, kuona kama istilahi zilizoundwa na chombo hiki cha kukuza Kiswahili zinakidhi kanuni za ufaafu wa istilahi za PEGITOSCA zilizojadiliwa katika sura ya pili. Akiwa na madhumuni hayo hayo, Kiingi (1997) ametathmini, kwa kutumia vigezo vya PEGITOSCA, *Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia* ya TUKI (1990). Kazi hii, kama tulivyotaja hapo awali, inahusu

tathmini ya istilahi za isimu zilizochapishwa kwenye *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (KSIL) na TUKI, 1990. Kabla ya tathmini ya istilahi za isimu, huenda ni muhimu tueleze, japo kwa kifupi, usuli wa istilahi zitakazotathminiwa. Istilahi za isimu za TUKI (1990) zilitokana na semina na makongamano mawili ya kitaifa yaliyoandaliwa na TUKI katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka wa 1986 na 1987. Lengo kuu katika makongamano hayo lilikuwa ni utayarishaji, usanifishaji na usambazaji wa istilahi za kitaaluma katika fizikia, kemia, biolojia, lugha na isimu. Zaidi ya istilahi maalum 5,000 zilizalishwa na kusanifishwa.

Katika utangulizi wa Ripoti ya TUKI wa jopo la isimu katika kongamano hilo, tunaelezwa kuwa katika harakati za uundaji istilahi, sarufi ya Kiswahili ilizingatiwa na kwamba:

> ...ukopaji wa maneno ya kigeni ulikataliwa na kamati, kwa hivyo istilahi nyingi zilizalishwa kwa mfanyiko wa **unyambuaji**, ila tu kulipotokea ulazima wa kukopa neno la kigeni.
> (taz. pia Kiingi, 1989:162 kwa maelezo zaidi).

Jopo la isimu halikujitokeza au halikuweza kujitokeza na utaratibu maalum na uliosawa na kutatua tatizo la usasaishaji wa istilahi. Katika jopo hilo la isimu (vile vile katika jopo la fizikia), sehemu ya Ripoti inatufichulia kuwa:

> Suala la misingi/kanuni zinazohusu **viambishi** halijatatuliwa kabisa. Kamati kwa hivyo inashikilia yaliyoafikiwa katika makongamano ya awali lakini ilipewa jukumu la kurekebisha na kuimarisha misingi kuhusu viambishi vya kiistilahi mradi tu kanuni za kisarufi zisikiukwe. Kwa hivyo, misingi inazidi kuwekwa huku kazi ikiendelea na uamuzi wa mwisho unasubiriwa baada ya kukamilika kwa shughuli hii.
> (Nukuu katika Kiingi, 1989:163)

Inaelekea wanajopo, wakiwemo wataalam wa Kiswahili, na wanaisimu

walitegemea tajriba, hisia, na uelewa wao katika uzalishaji wa istilahi mpya. Hapakutokea uchambuzi wa kina wa maneno kabla ya kupewa hadhi ya istilahi kama ilivyopendekezwa na kujadiliwa katika **6.1** (uk. 318). Hili linadhihirika kutokana na jinsi wanajopo walivyotohoa na kusanifisha viambishi vya kiistilahi vinavyotokana na Kiingereza. Baadhi ya viambishi vya mkopo havikupewa na havijapewa visawe mahususi vinavyobeba maana maalum za kisemantiki vya lugha ya Kiswahili, hususani katika taaluma ya isimu.

#### 6.1.1.1 Utaratibu Maalum na Uzalishaji katika Istilahi

Katika *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, ya TUKI (1990), kuna istilahi za isimu zilizosanifishwa pasi na kuzingatia sifa ya utaratibu maalum na uzalishaji. Iwapo mfano huu ni sahihi:

(1) *epicene*===**episini**

(2) *epistemology*===**epistemolojia**

(3) *epigraphy*===**epigrafia**

tunadadisi kuwa viambishi mkopo vimeswahilishwa kwa utaratibu maalum, yaani:

*epi*===**epi**, *-logy*===**-lojia**, na *-graphy*===**-grafia**

Hata hivyo, katika sehemu hii, kwa kutaka kupunguza ukopaji, pia tunapata:

(4) *epithet*===**kivumishanomino**

*epiglotis*===**kidakatonge**

*epidermis*===**ngozi nje** (*epi*===**nje**)

Kutokana na mifano hii (1-4) ile dhana ya *epi-* hairejelewi kwa utaratibu maalum. Jambo hili pia halitiliwi manani na TUKI

(1990:28) katika istilahi zifuatazo:

(5) *glosseme*===**glosimu**

*glossematics*===**glosematiki**

*gloss*===**kifasiri**

Ikiwa hakuna tofauti za kidhana kati ya *"gloss"* na *"glosse-"*, basi ukopaji umefanyika usiohitajika.

Katika Kiswahili, mojawapo wa mofimu zalishi na zinazonyambulika ni **"-sha."** Katika kuweka ukopaji na utohoaji wa istilahi mkopo katika hali ya chini, sifa ya uzalishaji wa istilahi imezingatiwa, kama mfano wa (6-10) unavyoonyesha, na ni hatua nzuri inayoelekea kwenye unyambuaji wa kileksia wa mofolojia za Kiswahili:

(6) *natural*===**asilia**

*naturalism*===**uasilia**

*naturalise*===**asilisha.**

(7) *grammar*===**sarufi**

*grammatise*===**sarufisha**

*grammaticalisation*===**usarufishaji.**

(8) *brackets*===**mabano**

*bracketing*===**ubanaji**

*bracketise*===**banisha.**

(9) *palatal*===**kaakaa**

*palatalize*===**kaakaisha**

*palatalization*===**ukaakaishaji.**

(10) *affix*===**kiambishi**

*affixing*===**ambisha**

*affixation*===**uambishaji.**

Kutokana na mifano hii, inaelekea kwamba unyambuaji wa kileksia, hususani, katika taaluma ya isimu, umezingatiwa na TUKI (1990). Kadhalika, uzalishaji wa istilahi kutokana na utaratibu maalum pia umezingatiwa.

#### 6.1.1.2 Matumizi Kimataifa

Umataifa wa istilahi hautokani tu na uswahilishaji wa istilahi mkopo za Kiingereza zilizozalishwa kutokana na Kigrikolatini, lakini ni uasilishaji wa ishara na finyazo kwa kufuata kaida shurutishi za kimataifa, kama katika mifano ifuatayo:

(11) *noun (N)*===**nomino (N)**

(12) *morphophoneme* {T}===**mofofonimu {T}**.

Matumizi ya "N" na "T" yanazingatia kaida za kimataifa zinazoongoza uzalishaji wa ishara. Ingawa kuna:

(13) *morphology*===**mofolojia**

(14) *phonology*===**fonolojia**

(15) *acronym*===**akronimi**.

hakuna sababu maalum ya kuchukua finyazo ya jina la Kiingereza na kuiweka finyazo hiyo na jina la Kiswahili. Ili kuepukana na upotoshaji wa dhamira ya ukweli, ni bora na sahihi kuambatisha finyazo na ishara ya Kiswahili na jina la Kiswahili, au finyazo ya Kiingereza na jina la Kiingereza. Kiswahili kina uwezo wa kuwa na ishara na finyazo zake sahihi na hakika, (kwa mfano, *verb*===kitenzi (t), *fonol.*===fonolojia) mradi tu zifuate kaida shurutishi zinazotumika kimataifa.

#### 6.1.1.3 Udhahiri Kiistilahi

(16) *negative particle*===**kikanushi**

*particle*===**faridipeke**

*negate*===**kanusha (kukanusha)**

*negation*===**kanusho**

*contrapositive*===**kikanusho.**

(BAKITA, Tol.2:15)

Ile dhana ya **faridipeke** (*particle*) haijitokezi katika **kikanushi** (*negative particle*). Iwapo kiambishi kitangulizi **ki-** kinaashiria udogo, basi madhumuni ya kutofautisha **faridipeke** na dhana ya msingi, *negative* (hasi), hayajatimizwa. Ikiwa, hata hivyo, kiambishi kitangulizi **ki-** hakidokezi udogo hapa, basi istilahi **kikanushi** ina utata na hailengi maana ya dhana ya *negative particle* kwa uwazi.

Mifano zaidi ya istilahi za isimu zinazokosa sifa ya udhahiri ni:

(17) *complementarity*===**utoano**

*mutual exclusive*===**kutoana**

*mutual intelligibility*===**kusikilizana**

*mutual knowledge*===**elimu shirikishi.**

Maarubu yanafaa yawe ni kutofautisha kati ya *mutual exclusive* (**kutoana**) na *complementarity* (**utoano**). Ingawa kiambishi **ku-** kina uwezo wa kubadili kitenzi cha aina yoyote na kukifanya nomino (Khamisi, 1989), hapa kiambishi hiki hakitimizi lengo la kutofautisha dhana zinazohusika. Aidha, dhana ya *mutual*, ambayo inakaririwa katika kila istilahi iliyo katika seti hii (*mutual intelligibility, mutual knowledge* ila tu katika *complementarity*)

haijitokezi katika istilahi za Kiswahili. Isitoshe, hakuna uhusiano wowote unaoonyeshwa kati ya istilahi zilizobuniwa za Kiswahili na istilahi mkopo za Kiingereza. Kila istilahi ni tofauti kabisa na nyingine. Kwa vile **kutoana** na **utoano** ni istilahi ambazo zimetumiwa kwa maana ya kuathiriana kwa sauti, tunaweza kuchukulia istilahi zifuatazo, kwa mfano:

*mutual*===**uelewano**

*mutual exclusive*===**uelewano utoano**

*mutual intelligibility*===**uelewano kusikilizana**

*mutual knowledge*===**uelewano elimu**

kama mapendekezo ya mtafiti ya istilahi dhahiri. Istilahi za TUKI, katika mfano huu (17) huenda zikahitaji usahihisho siku za usoni ili ziakisi vilivyo sifa za dhana zinazowakilisha. Tazama mfano zaidi:

(18) *breathed segment*===**kinong'onwa**

Ikiwa tunakubaliana na TUKI kuwa:

*breath*===**mpumuo**

*segment*===**kipandesauti**

*breathy voice*===**sauti mpumuo**,

itakuwaje basi *breathed segment* iwe **kinong'oni** badala ya **kipandesautimpumuo** (taz. pia *breathy phonation*===**unong'oni**, ilhali *phonation*===**utamkaji**).

Aidha, katika (19), sifa ya udhahiri wa istilahi haikutimizwa:

(19) *adaptation*===**utohozi**.

**Utohozi** ni uswahilishaji wa istilahi na hauwezi kuwa na maana sawa na '*adaptation.*' Kwa vile **utohozi** ni uswahilishaji wa istilahi zitokanazo na lugha za kigeni, hususani Kiingereza, ili

zifuate fonolojia ya Kiswahili (k.m. *register*===**rejista**, *lexis*===**leksisi**), mtafiti anapendekeza kuwa:

*adaptation*===**uasilishaji**

Hii inatokana na sababu kwamba istilahi **uasilishaji** inagonga kwa uwazi pale ambapo imelengwa. (**Uasilishaji** ni kuchukua neno lilivyo kimaandishi na/au kimatamshi bila kubadilisha umbo, k.m. **tagmeme, mora, tagma, sandhi,** na **tempo**).

Katika (20), sifa ya udhahiri wa istilahi pia haikuzingatiwa:

(20) *coalescence*===**muungano**

*convergence*===**muungano**

*co-occurence*===**muoano**

*cohesion*===**mshikamano**

Istilahi **muungano** haionyeshi bayana tofauti iliyopo kati ya dhana ya *"coalescence"* na *"convergence,"* wala haigongi kwa udhahiri pale ambapo imelengwa. Si ajabu, kwa hivyo, kuwa dhana ya *"coalescence"* katika isimu ya Kiswahili ina visawe vingi mno vya kiistilahi vifuatavyo:

(i) **muoano** (ii) **muumano** (iii) **uwiano** (Mbaabu, 1992),

(iv) **muungano** (v) **usawazisho** (Kapinga, 1983),

(vi) **mwingiliano**, (vii) **mshikamano** (Mdee, 1981),

(viii) **mkamatano**.

Tatizo hili huenda linatokana na uundaji wa istilahi moja moja za isimu bila kuzingatia ufungamano wa kidhana. Hali hii, mbali na kuwakanganya walengwa wake, pia, ni mzigo usiohitajika katika ukumbuko wao (taz. Gibbe, 1981).

### 6.1.1.4 Utaratibu Uliosawa Kifonolojia katika Istilahi

(21) Ikiwa: *double consonant*===**konsonanti maradufu**

*double comparison*===**ulinganishi maradufu**

*double negative*===**ukanushi maradufu**

*double articulation*===**utamkaji sawia**

*generous plural*===**wingi maradufu**

*generalised transformation*===**ugeuzi maradufu**,

basi tunadadisi uafaka wa *"double"*===**maradufu**, *"double"*===**sawia**, *"generous"*===**maradufu**, na *"generalised"*===**maradufu**, ambazo kwa yakini zinakanganya.

Kwanza, **maradufu** (au uradufu) ni istilahi makosa. Hakuna uhusiano wowote wa kimaana kati ya *"double", "generous"* na *"generalised"*. Kila moja ya istilahi hizi ni tofauti kabisa na nyingine, na hazifai kuwakilishwa na neno **maradufu**. Haieleweki ni lini neno **sawia** linastahiki kutumiwa kwa maana ya *"double"*. Katika jaribio la kusisitiza uangavu, wanaleksikografia wa *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, kutokana na mfano huu, inaelekea hawakuzingatia utaratibu uliosawa wa istilahi. Ile dhana ya *"double"* ya mwanzo hairejelewi katika istilahi zote zenye kiambisho hicho katika mfano uliotolewa hapo juu. Haieleweki ni kwa nini *"double articulation"*===**utamkaji sawia**, isiwe **utamkaji maradufu** iwapo mfumo uliosawa unafuatwa katika uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Aidha, iwapo tunakubali kuwa:

*generalise*===**jumuisha**, na tunafahamu kuwa

*generous*===**maradufu**

basi inadhihirika bayana kuwa

*generalised transformation*=== ni **ugeuzi jumuishi** na wala siyo **ugeuzi maradufu.**

(22) *isomorphism*===**ushabihimiundo**

*isophone*===**kizingamatamshi**

*isomorph*===**kizingaumbo**

*isotone*===**kizingatoni**

*isolex*===**kizingamsamiati**

*isograph*===**kizingasifa**

*isogloss*===**kizingasifa**

*isosyntagm*===**kizingamuundo**

Kutokana na istilahi hizi, tunadahili kuwa *"iso-"*===**kizinga**, *"phone"*===**matamshi**, *"-tone"*===**toni**, *"-lex"*===**msamiati**, *"-graph"* na *"-gloss"*===**sifa**, na *"-syntagm"*===**muundo.** Matumizi ya mofimu *"iso-"*===**kizinga** katika uzalishi wa istilahi ni jaribio bora katika uzingatiaji wa utaratibu uliosawa. Hata hivyo, haieleweki na hakuna sababu maalum za kuwepo kwa *"isomorphism"*===**ushabihimiundo.** Vilevile, dhana ya **"uzinga"** haieleweki inatokana na nini. Mifano zaidi:

(23) *idiophone*===**idiofoni**

*idiography*===**idiografia**

*ideogram*===**idiogramu.**

Tungetarajia, kwa hivyo, *"idio-"* au *"ideo-"* kuswahilishwa kwa utaratibu uliosawa kama **idio-**; ndiposa uswahilishaji wa *"idiolect"*===**mtindopekee**, una ufefe usiohitajika. Katika (24), pia ukosefu wa sifa ya ulinganifu wa mtiririko unadhihirishwa;

(24) Ikiwa tunakubaliana na TUKI kuwa:

*hyponym*===**hiponimi**

*hyponymy*===**hiponimia**

*hypo*===**hipo**

*nym*===**nimi**

*nymy*===**nimia**

basi itakuwaje

*hypotaxis*===**utegemezi**

*hypotactic clause*===**kishazi tegemezi**?

Mfano huu pia ni dhihirisho la kutozingatiwa kwa utaratibu uliosawa katika baadhi ya istilahi zilizoswahilishwa na TUKI kwa mfanyiko wa ubunaji au tafsiri ya maana za maneno (taz. pia MacWilliam 1985). Hapa kuna mfano zaidi:

(25) *syntax*===**sintaksia**

*syntactic*===**kisintaksi**

Mtu anaweza kuielewa barabara mifanyiko hii, lakini kwa vile,

*syntactic order*===**mpangilio kisintaksi**

*syntactic category*===**kategoria kisintaksi**

ziko jinsi zilivyo, ni dhahiri kuwa

*"synta-"*===**sinta-**.

Kwa hivyo, uswahilishaji wa *"syntagmatic"* kama **usilisila**, ingawa ni jaribio la kupunguza ukopaji kutoka Kiingereza, hauzingatii sifa ya ulinganifu wa mtiririko katika istilahi za isimu ya Kiswahili. Aidha, neno **usilisila** lenyewe limekopwa kutoka Kiarabu, **silsil**===minyororo *(chains)*.

### 6.1.1.5 Iktisadi katika Istilahi

(26) *ecology*===**ekolojia** (elimu ya mazingira)

*ecology of language*===**ekolojia lugha**

(27) *dialectology*===**elimulahaja**

(28) *gynaecology*===**elimuuzazi** (jinakolojia)

Hapa tunaona ya kwamba mofimu *"-logy"* inaashiriwa kama **-lojia** na **elimu-** katika fani ya isimu ya Kiswahili. Iwapo *"-logy"* inachukuliwa kwa maana ya **elimu-** mtindo upi unatarajiwa kutumika?

elimu ya x?

elimu x?

au

elimux?

Tazama kwa mfano, neno *"gynaecology"* katika Kijerumani linafasiriwa kwa maneno mawili, yaani: *"gyna"kologie"*===**jinakolo**jia (Kiswahili), na *"Frauenheilkunde"*===elimu ya magonjwa ya wanawake.

Kwa hivyo, katika mfano **(28)**, tunapendekeza matumizi ya maneno yafuatayo:

*gynaecology*===**elimutibanke** au tibake (elimu inayohusu matibabu ya wanawake)

*gynaecologist*===**mtibanke** (au tabibunke)

kwa sababu ni mwafaka na yanaeleweka.

Hata hivyo, ni muhimu ieleweke kuwa mofimu *"-logy"* inapofasiriwa kama **elimu-**, katika mtindo wowote ule, aghalabu hupoteza msingi wa iktisadi wa lugha. Tazama kwa mfano:

*meteorologist*===**mwanaelimuhewa** (mwanamitorolojia)

*ecologist*===**mwanaelimumazingira** (mwanaikolojia)

*dialectologist*===**mwanaelimulahaja** (mwanalahaja)

Kwa usemi mwingine, suala nyeti hapa ni, kwa jinsi gani sifa za iktisadi, uzalishaji na uangavu zitaoanishwa na kuendelezwa katika istilahi za isimu ya Kiswahili?

(29a) *morphology*===**mofolojia**

*phonology*===**fonolojia**

lakini pia kuna istilahi

(29b) *morphology*===**mofoloji**

*phonology*===**fonoloji** (taz. S.A. Mohamed, 1995:36)

ambazo bila shaka zinazingatia zaidi sifa na msingi wa iktisadi. Mfano huu wa (29b) unaonyesha kuwa **-a** inaweza, kwa mujibu wa iktisadi, kuondolewa na kudondoshwa katika Kiswahili pasi na kupoteza maana na utamkaji wa istilahi (taz. mfano **hisia===hisi, jinsia===jinsi**).

(30) **'sarufi ya kisifabia'===sarufibia**

**'isiyo na kisarufi'===isokisarufi**

**'neno lililoundwa'===nenounde**

ni jaribio bora la kiiktisadi na la kupunguza istilahi mkopo za kigeni. Hapa "kigeni" ina maana ya zile istilahi za Kibantu moja kwa moja, au za Kiarabu, Kiingereza, na nyinginezo ambazo zimekopwa kabla ya kuandikwa kwa tasnifu hii. Kwa mfano, **sarufi, mashine**, n.k. Ni maoni yetu kuwa hakuna sababu ya kimsingi katika taaluma ya isimu kuwa na **-lojia** na **elimu-** kama virejelea vya dhana ya *"-logy"*, (au **-ia** na **-i**). Mfumo mmoja utumike kimantiki katika uzalishaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili.

#### 6.1.1.6 Uangavu Kiistilahi

Inaelekea kwamba chombo cha ukuzaji lugha cha TUKI, katika kung'ang'ania uangavu wa kileksia, hakifuati ulinganifu wa mtiririko unaokubalika, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha: Mantiki inaelekeza kuwa ikiwa

(31) *linguistic philosophy*===**falsafa ya lugha**

*linguistic relativity*===**taathira lugha**

*linguistic taboo*===**adabu ya lugha**

*linguistic norm*===**kaida ya lugha**

*linguistic typology*===**uainishaji lugha kimuundo**

*linguistic circle*===**wataalamili isimu**

basi,

*linguistic(s)*===**lugha**

*linguistic(s)*===**isimu** (linganisha na usemi **lugha wiyati**, Sengo, 1997).

Katika jaribio hili la uangavu kiistilahi, tofauti kati ya **isimu** na **lugha** haijitokezi. Istilahi zilizopendekezwa si mwafaka kwa sababu ya kutozingatiwa kwa sifa ya uangavu na ya utaratibu uliosawa katika uundaji wa istilahi 'faafu' za Kiswahili. Hapa kuna mifano zaidi:

(32) Ikiwa

*geographical classification*===**uainishaji kijiografia**

*geographical dialect*===**kitarafa**

*geographical linguistics*===**isimulahaja**

*linguistics geography*===**jiografia ya isimu**

basi tunadadisi ni vipi

*"geographical"*===**kijiografia**, *"geographical"*===**lahaja** ilhali dhana ya '*geography*' haipo.

Tazama pia mifano hii:

(33) *phonological item*===**faridi kifonolojia**

*phonometrics*===**fonometriki**

*phonostylistics*===**sauti mitindo**

ikidhihirisha *"phono"*===**fono**, *"phono"*===**sauti**.

(34) *phonemic contrast*===**mlingano kifonimu**

*phonemic notation*===**mabano mkwaju**

*phonemic overlapping*===**usawazishano**

*phonemic transcription*===**unukuzi mpana**.

Hapa, jaribio la kung'ang'ania uangavu wa istilahi linapuuza sifa muhimu ya uangavu wa kiistilahi na ulinganifu wa mtiririko kwa kutorejelea ile dhana ya *"phonemic"*. (Taz. pia *"systematic transcription"*===**unukuzi sisisi**).

Aidha, ikiwa

(35) *analogy*===**analojia**

*analogism*===**uanalojia**

*anaphora*===**mrejeosabiki**

*anaphoric word*===**umbo mrejeosabiki**

*anaphoric substitute*===**umbo mrejeosabiki**,

basi *"ana-"*===**ana-**, *"ana-"*===**sabiki**, *"-phora"*===**mrejeo**, na *"anaphoric"*===**mrejeosabiki**.

Kwa hivyo, uswahilishaji wa *"apposition"*===**mrejeosawa**, ingawa unazingatia uangavu wa kiistilahi, si mwafaka kwa sababu istilahi hii haiakisi vilivyo sifa ya dhana inayowakilisha. Mifano zaidi, ni kama ifuatavyo. Ikiwa

(36) *inter-language*===**lugha unde**

*artificial language*===**lugha unde**

*coined word*===**neno unde**

*artificial speech*===**matamshi unde**

basi

*"artificial"*===**unde**, *"inter-"*===**unde**, *"coined"*===**unde**. Ingawa hili ni jaribio moja muhimu lenye kuzingatia msingi wa iktisadi katika istilahi, na istilahi hizi ni angavu na zinaeleweka,

lakini hakuna ruwaza maalum, na utaratibu uliosawa wa dhana ya **'unde'** haukutiliwa maanani. Kwa mfano:

(37) *bound accent*===**shadda funge**

*bound morpheme*===**mofimu funge**

*bound sentence*===**sentensi funge**

*matrix sentence*===**sentensi solo**

*kernel sentence*===**sentensi msingi.**

Ingawa hii ni hatua muhimu sana katika uzalishaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili zinazoonyesha uangavu, lakini papo hapo kuna ukanganyifu. Kwa mfano, dhana ya *matrix*===**solo.** Haieleweki neno **solo** linatokana na neno gani la Kiswahili. Ni kutokana na kutozingatiwa kwa vigezo vya PEGITOSCA ndipo watumiaji wa istilahi za isimu wakapata shida katika kukubali istilahi zifuatazo:

(38) *nominalize*===**kujinisha (nominisha)**

(39) *nominalization*===**ujinishaji (unominishaji)**

(40) *adverb*===**advabo** (kielezi) (taz. Mdee, 1980).

Istilahi hizi, licha ya kwamba zinazingatia msingi wa iktisadi wa lugha, si toshelevu na angavu na zinawakanganya walengwa wake.

### 6.1.1.7 Ufaafu, Ukubalifu katika Lugha na Utusani

(41) *arbitrariness*===**unasibu**

*nominalism*===**unasibu**

Neno **unasibu** ni mnyambuliko wa **"nasibu"** ambalo ni neno makosa kabisa na lilitiwa katika Kiswahili na TUKI kutokana na kutojua kuwa hayo ni maneno mawili yanayotokana na usemi **"bahati na sibu".** **Kusibu** ni kutendeka sawasawa bila kupangwa. Iwapo neno

**"nasibu"** limetoholewa kutokana na neno **"nasaba,"** basi haya pia ni makosa, sababu nasaba maana yake ni uhusiano wa karibu sana, au tabaka *(caste)* (Chimerah katika mazungumzo yetu, 1999). Labda baada ya kugundua udhaifu katika neno **nasibu**, na kwamba halitofautishi vilivyo dhana ya *"arbitrariness"* na *"nominalism"*, chombo cha TUKI kimeswahilisha *"nominalism"*===**unominishaji** (Rejelea mfano wa 38 na 39).

Ikiwa

(42) *pedagogical linguistics*===**isimu shule**

*pedagogical grammar*===**sarufi shule**

*pedagogical*===**shule**

hatutarajii kupata fasiri ya:

*pedagogical linguistics*===**isimu kipedagojia**

*pedagogical grammar*===**sarufi kipedagojia.**

Kuna uwezekano wa walengwa kukanganyika kutokana na matumizi ya **shule**, "mahali ambapo watoto hufundishwa elimu", na **shule**, kama **kipedagojia.** Mfano zaidi:

(43) *content*===**umbo maana**

*content word*===**neno la kileksia**

*cluster*===**mlolongo**

*consonant cluster*===**mlolongo konsonanti.**

Ikiwa haikutarajiwa kwamba **umbo maana** (*'content'*) ni istilahi inayoweza kukanganyika na **yaliyomo**, vivyo hivyo, hatutarajii **mlolongo**, mfululizo wa utamkaji, kukanganywa na **mlolongo**, mstari, kikundi, au mfuatano wa watu au vitu. Neno **mlolongo===mstari** ndilo linalofahamika sana katika jumuiya ya wazungumzaji wa Kiswahili.

(44) *classical*===**ukale/kimapokeo**

*classical language*===**lugha bora**

(*classical*===**bora**, *classical*===**ukale**)

Fasiri ya istilahi *"classical language"* kwa maana ya **lugha bora**, haizingatii sifa ya udhahiri; na hivyo basi si faafu, na kwa ajili hiyo, haikubaliki. Aidha, ikiwa:

(45) *frequency*===**kasimawimbi**

*frequency count*===**uchanganuzi maneno kiidadi**

basi, *frequency*===**kasimawimbi**, na aidha **uchanganuzi**, ilhali

*count*===**maneno kiidadi, hesabu**

Kwa watumiaji wa lugha wasio wasomi, **kasimawimbi** haiwezi kuwa *"frequency"*. Watu hawa watatarajia

*frequency*===**mfululizo**

*frequency*===**mawimbi ya sauti**

*count*===**hesabu**

*frequency count*===**hesabu kimfululizo.**

Huenda wasomi, kutokana na mfumo wa kijamii, wasipate taabu kutumia

*frequency*===**frikwensi.**

Suala muhimu, na linalosisitizwa hapa, ni kwamba chombo cha TUKI kinafaa kuzalisha istilahi faafu za isimu zisizokanganya walengwa.

(46) *deixis*===**usonde**

*opacity*===**ubuye**

*opaque*===**buye**

Istilahi hizi, pamoja na kwamba si angavu, haieleweki zinatoka wapi.

Vilevile, pale ambapo tungetarajia

(47a) *back of the tongue*===**nyuma ya ulimi**

(48a) *basic vocabulary*===**msamiati wa kimsingi**

(49a) *manner of discourse*===**namna ya hali za usemi/matumizi lugha**

(50a) *generalised phrase structure grammar*===**sarufi miundo virai jumuishi**

tunapata

(47a) *back of the tongue*===**shina ulimi**

(48a) *basic vocabulary*===**msamiati msingi**

(49a) *manner of discourse*===**kidato cha mazungumzo**

(50a) *generalised phrase structure grammar*===**sarufi miundo virai changamani.**

Tatizo hili la mpangilio wa istilahi za isimu zinazotoholewa kutoka lugha za kigeni haliwezi kutatuliwa pasi na kuzingatia sarufi na sintaksia ya Kiswahili; yaani, vivumishi vifuate nomino.

Kutokana na tathmini ya istilahi za isimu zilizozalishwa na TUKI (1990), ni jambo lisilozusha ubishi kuwa utohoaji na uzalishaji wa kupindukia wa istilahi mkopo kutoka Kiingereza umezingatia misingi ya **udhahiri, iktisadi, umataifa** na **utaratibu maalum.** Wakati huo huo, uegemeaji katika uswahilishaji na utohoaji umeonyesha kutozingatia kwa vigezo vya **uzalishaji, uangavu, utusani, ulinganifu wa mtiririko**, na **ufaafu** pamwe na **ukubalifu** wa istilahi katika mfumo wa kiutamaduni au jamii ya watumiaji wa Kiswahili.

Kwa jumla, tathmini hii imeonyesha kuwa baadhi ya istilahi za isimu zilizoundwa na TUKI mwaka 1990 hazina 'usayansi' na hazizingatii misingi ya 'ufaafu' wa istilahi (taz. Picht & Draskau, 1985). Kwa vile hali hii pia imethibitishwa na kiwango cha chini cha ukubalifu wa istilahi za Kiswahili kwa walengwa (taz. Mdee, 1980; Mwansoko, 1993; na Sewangi, 1996), hatuwezi kukwepa kutoa pendekezo kwamba *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990), inahitaji kurekebishwa na kuandikwa upya. Urekebishaji wa kamusi hii unahitaji kuzingatia viambishi vya kiistilahi vilivyobuniwa na kuasilishwa kutokana na baadhi ya lahaja za Kiswahili. (Taz. Kiingi, 1989:175 kwa maelezo zaidi kuhusu viambishi awali vinavyofaa kuchukuliwa kutoka lahaja za Kimvita na Kiunguja). Ndiposa huenda ni muhimu tutathmini istilahi za watu binafsi ili kuona kama zinazingatia 'usayansi'.

### 6.1.2 Tathmini ya Istilahi za Isimu za Wataalam Binafsi

Wanaisimu na wataalam binafsi wengi (kama vile, Nkwera, 1978; Maganga, 1979; Akida, 1983; Kapinga, 1983; Abdulla, 1988; Khamisi, 1988; Mbaabu, 1992; na Besha, 1994) wameunda istilahi mpya za isimu ya Kiswahili baada ya kutambua kwamba istilahi zilizopo hazitoshi na hazitoshelezi mahitaji ya walengwa wake. Hata hivyo, ni muhimu ieleweke kwamba chombo maalum cha BAKITA cha kuendesha shughuli zote kuhusu lugha ya Kiswahili, pamoja na usanifishaji, kimeachia watu binafsi na *Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili* (TUKI) mamlaka na dhima ya uundaji na usanifishaji wa istilahi, (Mwansoko, 1990). Ndiposa si ajabu kupata baadhi ya istilahi mpya za isimu zimeundwa na wataalam binafsi, na

kuingizwa katika machapisho yao na katika matumizi ya kila siku. (Mdee, 1995; anapendekeza kipindi cha 'majaribio' ya ubora wa istilahi kiwe miaka mitano hadi kumi).

Ingawa sisi tunafahamu kuwa istilahi fulani kuwa 'sanifu' si kwamba ni bora zaidi kuliko nyingine, lakini umuhimu wa usanifishaji haupaswi kupuuzwa katika harakati za kuendeleza leksikoni ya lugha. Kusanifu istilahi kuna madhumuni ya kukuza upatanisho, usasa na usawa wa lugha unaohitajika katika mazingira mapana zaidi (taz. Ferguson, 1968). Kutozingatiwa kwa suala la usanifishaji na misingi ya uundaji wa istilahi na waundaji istilahi binafsi, kumesababisha uundaji wa istilahi mpya zisizo na mantiki sahihi, na 'ukuzaji huria' wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Ilivyo ni kwamba watumiaji wa istilahi za isimu zinazozalishwa hukanganyika panapotokea haja ya kuchagua kati ya istilahi mbili, tatu au zaidi zilizoundwa na wataalam tofauti zenye kurejelea dhana moja (taz. Jedwali la 3). Tathmini ya usayansi wa istilahi za isimu, kwa hivyo, inaazimia kukomesha vurugu kwa kutatua tatizo hili na kuleta nidhamu na upatanisho katika istilahi za isimu ya Kiswahili.

Kazi yetu hapa ni kutathmini 'usayansi' katika istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoundwa na wataalam binafsi, ambazo tayari zimekwisha 'kusanifishwa', ili kuthibitisha iwapo zinakidhi misingi ya ufaafu wa istilahi au la. Istilahi za isimu zilizobuniwa na kupendekezwa na Kapinga (1983) vipengele (a)-, Mbaabu (1992) vipengele (b)-, na Besha (1994) vipengele (c)-, ndizo zilizotathminiwa katika sehemu inayofuata ili kubainasha

usayansi uliopo. Aidha, tulichunguza ni mbinu ipi (au zipi) inayounda (au zinazounda) istilahi zenye 'usayansi' na ukubalifu wa kimataifa miongoni mwa hadhira lengwa. Tazama jedwali hili la (3) kwa maelezo zaidi:

**Jedwali 3: Usayansi katika Istilahi za Isimu**

| Istilahi | Chimbuko la Istilahi (Aina ya Mfanyiko) | Usayansi katika Istilahi (Vigezo vya Istilahi 'faafu') | | | | | | | | | Alama |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | P | E | G | I | T | O | S | C | A | |
| (1a) vimadende (trills) | uasilishaji wa neno la Kiswahili | 4 | 4 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (1b) vitambaza | tafsiri ya maana za maneno (ubunaji) | 5 | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | -2 | 0 | 0 | 11 |
| (1c) vilainisho | upanuaji maana; unyambuaji <lainisha | 2 | 3 | 3 | 0 | 1 | 0 | -2 | 0 | 0 | 7 |
| (2a) kitendwa (object) | tafsiri ya maana za maneno; unyambuaji <tenda | 5 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| (2b) yambwa | uasilishaji wa neno la Kiswahili | 4 | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| (2c) kishamirishi | unyambuaji <shamiri | 3 | 2 | 2 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8.5 |
| (3a) kijalizo (complement) | unyambuaji <jaliza | 5 | 4 | 2 | 0.5 | 2 | 0 | -1 | 0 | 0 | 12.5 |
| (3b) kielezo | unyambuaji <eleza; tafsiri ya maana ya neno | 3 | 4 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | -1 | 0 | 0 | 11.5 |
| (3c) kikamilishi | kufasiri maana; unyambuaji <kamilisha | 6 | 3 | 2 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13.5 |
| (4a) usawazisho wa matamshi (vowel harmony) | uambatanishaji; kufasiri maana | 2 | 1 | 2 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6.5 |
| (4b) uwiano wa irabu | uasilishaji; uambatanisho | 6 | 3 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 |
| (4c) upatanisho wa irabu | tafsiri ya maana za maneno; uambatanisho (<upatanisho+irabu) 'irabu'-neno mkopo kutoka Kiarabu | 6 | 2 | 2 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (5a) kiwakilishi pronoun | unyambuaji <akilisha | 4 | 3 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (5b) kijina | upanuaji wa maana wa jina | 3 | 4 | 1 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (5c) kibadala/ pronomino | uasilishaji <badala ukopaji kutoka Kiingereza | 4 | 4 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6.5 |
| (6a) kitamkwa phoneme | unyumbuaji <tamko; tafsiri ya maana za maneno | 6 | 4 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15.5 |
| (6b) sauti | upanuaji wa kimaana wa sauti | 4 | 4 | 0 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9.5 |
| (6c) fonimu | utohoaji-neno mkopo kutoka Kiingereza | 2 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| (7a) majina noun | upanuzi wa kimaana wa jina | 6 | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 |
| (7b) nauni | tafsiri mkopo | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | -1 | -1 | 0 | 5 |
| (7c) nomino | utohoaji-neno mkopo kutoka Kiingereza | 3 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 |
| (8a) mchakato process | ubunaji (kufasiri maana) | 1 | 4 | 0 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5.5 |
| (8b) mfanyiko | uasilishaji; ubunaji | 4 | 4 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 |
| (8c) mnyumbusho | unyambuaji<nyumbua; kutafsiri maana (taz. pia Mukama 1989:7) | 2 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| (9a) kidaka tonge epiglottis | uambatanishaji <-daka+tonge | 6 | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| (9b) epiglotisi | utohoaji-neno mkopo kutoka Kiingereza | 1 | 3 | 0 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4.5 |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (10a) kiingizi<br>interjection | unyambuaji <ingiza; kufasiri maana | 3 | 4 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (10b) kishangao | upanuaji wa kimaana wa <mshangao | 3 | 4 | 3 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11.5 |
| (10c) kihisishi | uasilishaji; upanuzi wa kimaana <hisi | 4 | 4 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 |
| (11a) silabi<br>syllable | utohoaji-neno mkopo kutoka Kiingereza | 3 | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 |
| (11b) mizani | upanuzi wa kimaana za maneno <mizani ubunaji | 6 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| (12a) viigizi<br>idiophone | unyambuaji <igiza; kufasiri maana | 3 | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| (12b) vielezi miigo | kufasiri maana (ubunaji); uambatanishaji <vielezi+miigo | 6 | 3 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (12c) idiofoni | utohoaji na ukopaji | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| (13a) umaizilugha<br>competence | uambatanishaji/uunganishaji <umaizi+ lugha (taz. pia Mwansoko 1990:174) | 4 | 2 | 2 | 0.5 | 1 | 0 | -1 | -1 | 0 | 7.5 |
| (13b) uwezolugha | uunganishaji <uwezo+lugha | 6 | 3 | 2 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (13c) umilisi lugha | (ubunaji) kufasiri maana za maneno uunganishaji <umilisi+lugha | 5 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| (14a) kihusishi<br>conjunction | unyambuaji <husisha | 3 | 4 | 3 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11.5 |
| (14b) kihusiano | upanuzi wa kimaana wa <uhusiano | 4 | 4 | 3 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (14c) kiunganishi | unyambuaji <uunganishaji; upanuzi wa maana za maneno | 6 | 3 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 |
| (15a) nazali<br>nasal | utohoaji-neno mkopo kutoka Kiingereza | 2 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| (15b) kipua | upanuaji wa kimaana wa <pua; uasilishaji | 5 | 4 | 1 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11.5 |
| (15c) king'ong'o | uasilishaji (neno asilia) | 6 | 4 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 |
| (16a) kiima<br>subject | upanuzi wa kimaana wa <ima | 3 | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| (16b) kitendaji | unyambuaji <tenda | 3 | 4 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | -1 | 0 | 0 | 11.5 |
| (16c) faali | ubunaji (kufasiri maana za maneno) | 3 | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9.5 |
| (17a) kiarifu<br>predicate | unyumbuaji <arifu; ubunaji | 6 | 4 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 |
| (17b) kifungu Kitenzi | tafsiri ya maana za maneno <fungu, tenda | 3 | 1 | 3 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8.5 |
| (17c) prediketa | utohoaji, neno mkopo kutoka Kiingereza | 2 | 4 | 0 | 0.5 | 0 | 0 | -1 | -1 | 0 | 4.5 |
| (18a) ubebwaji<br>embedding | unyambuaji <bebwa | 3 | 4 | 3 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11.5 |
| (18b) uchopekaji | ubunaji (kufasiri maana) | 4 | 3 | 3 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (18c) umezaji | upanuzi wa kimaana wa <meza | 0 | 4 | 3 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8.5 |
| (19a) mkazo<br>stress | unyambuaji <kaza; na upanuzi wa kimaana | 5 | 4 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 |
| (19b) shadda | ukopaji, neno mkopo kutoka Kiarabu | 2 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| (20a) vijenzi<br>constituents | upanuzi wa kimaana wa <jenga; unyambuaji | 6 | 4 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 |
| (20b) viambajengo sisisi | uunganishaji<viambajengo+sisisi | 5 | 2 | 3 | 1 | 2 | 0 | -1 | 0 | 0 | 12 |
| (21a) Jozi bainifu<br>minimal pairs | uunganishaji/uambatanishaji <jozi+bainifu | 2 | 2 | 2 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7.5 |
| (21b) Jozi za sauti | uambatanishaji; tafsiri ya maana | 6 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (21c) Jozi za nitoe nikutoe | upanuzi wa kimaana wa <toa; uambatanishaji | 2 | 1 | 2 | 0.5 | 0 | 0 | -1 | 0 | 0 | 4.5 |
| (22a) sintaksia<br>syntax | utohoaji-ukopaji kutoka Kiingereza | 3 | 4 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 |
| (22b) sarufi miundo | uunganishaji/uambatanishaji <sarufi+miundo; 'sarufi' -neno mkopo kutoka Kiarabu | 6 | 2 | 2 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |
| (23a) mzizi<br>root | uasilishaji wa neno | 6 | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 |
| (23b) kiini | upanuzi wa kimaana wa <kiini; msingi wa tukio/kitendo | 3 | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| (24a) abjadi<br>alphabet | ukopaji, neno mkopo kutoka Kiarabu (taz. pia Gibbe 1981:11) | 5 | 4 | 1 | 0.5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11.5 |
| (24b) alfabeti | utohoaji, ukopaji kutoka Kiingereza | 4 | 4 | 1 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9.5 |
| (25a) nyakati sahihi<br>simple tense | uunganishaji <nyakati+sahihi, 'sahihi' neno mkopo kutoka Kiarabu | 5 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (25b) njeo sahihi | uasilishaji, 'njeo' neno asilia la Kiswahili; uunganishaji <njeo+sahihi | 6 | 4 | 2 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14.5 |
| (26a) intonesheni<br>intonation | utohoaji, neno mkopo kutoka Kiingereza | 2 | 3 | 0 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5.5 |
| (26b) kiimbo | unyambuaji <-imba | 4 | 4 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| (26c) mkokotoo | unyambuaji <-kokotoa ambalo ni mnyambuliko wa <kokoto aina ya mawe (calculus) yanayotumiwa katika kuhesabu | 4 | 4 | 2 | 0.5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12.5 |

Katika kupima 'usayansi' wa istilahi, kama ilivyoelezwa hapo awali, istilahi iliyopata alama 12 (ambayo ni sawa na asilimia 50 na kuendelea) inakidhi mahitaji ya PEGITOSCA ya kupendekeza neno kupewa hadhi ya istilahi, ilhali ile iliyopata chini ya

alama 12 haina 'usayansi' na haikubaliki. Aidha, mfanyiko wa kuundia istilahi uliopata asilimia 50, istilahi zake zina usayansi na zinakubalika, mahali ambapo ule uliopata chini ya 50 hauna usayansi na haukubaliki (yaani $12 < Rx'_i < 20$).

Jedwali lifuatalo linatoa picha ya jumla ya kiwango cha 'usayansi' kulingana na uchanganuzi wa data iliyotokana na majibu na hoja za wasailiwa (rejelea Kiambatisho cha 2 na 3).

**Jedwali 4: Kiwango cha 'Usayansi' Kulingana na Data**

| AINA YA MBINU AU MFANYIKO ULIOTUMIKA KUUNDIA | JUMLA YA ISTILAHI ZILIZO-TATHMINIWA | ISTILAHI ZENYE USAYANSI | | ISTILAHI ZISIZO NA USAYANSI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | IDADI | % | IDADI | % |
| UASILISHAJI KUTOKA KISWAHILI CHENYEWE | 9 | 9 | 100 | 0 | 0 |
| UBUNAJI (Kufasiri maana za maneno | 9 | 5 | 55.6 | 4 | 44.4 |
| UUNGANISHAJI/ Uambatanishaji | 10 | 6 | 60 | 4 | 40 |
| UNYAMBUAJI | 16 | 9 | 56.25 | 7 | 43.75 |
| UPANUZI WA KIMAANA WA ISTILAHI | 13 | 3 | 23.1 | 10 | 76.9 |
| UKOPAJI na UTOHOAJI | 13 | 0 | 0 | 13 | 100 |
| **JUMLA** | **70** | **32** | **45.7** | **38** | **54.3** |

Kutokana na jedwali 4, inabainika kwamba katika jumla ya istilahi za isimu ya Kiswahili 70 zilizofanyiwa tathmini, zilizo na usayansi ni 32 tu ambazo ni sawa na asilimia 45.7 ya istilahi zote zilizoundwa na wataalam binafsi. Kiwango hiki cha

'usayansi' katika istilahi ni cha chini ya asilimia 50, ambayo katika tathmini, hiki ndicho kiwango cha chini cha usayansi. Katika istilahi za isimu ya Kiswahili zilizofanyiwa tathmini, zisizo na usayansi ni 38; kwa hivyo, si faafu kwa watumiaji kwa kiwango cha asilimia 54.3.

Uchambuzi wa 'usayansi' katika mbinu za uundaji istilahi, kutokana na jedwali 4, unaonyesha pia kwamba istilahi za isimu zilizoundwa kwa mfanyiko au mbinu ya **uasilishaji wa maneno kutoka Kiswahili chenyewe** zina 'usayansi' kwa asilimia 100. Kwa upande mwingine, istilahi zilizozalishwa na mfanyiko wa **kufasiri maana za maneno (ubunaji)** zina usayansi kwa asilimia 55.6. Aidha, istilahi za isimu zilizotokana na mbinu ya **uunganishaji na uambatanishaji** zina usayansi kwa asilimia 60. Istilahi zenye 'usayansi' zilizoundwa kwa mfanyiko wa **unyambuaji** zina asilimia 56.25, mahali ambapo istilahi zilizobuniwa kwa njia ya **upanuzi wa maana za maneno** zina usayansi kwa asilimia 23.1 (kiwango ambacho ni chini ya asilimia 50). Hali kadhalika, istilahi za isimu zilizoundwa na wataalam binafsi walioteuliwa kwa mbinu ya uundaji istilahi, ya **ukopaji** na **utohoaji**, hazina 'usayansi' kabisa (asilimia 00), na hivyo basi si 'faafu' kwa walengwa wake. Inaelekea mbinu za uundaji istilahi za **uradidi, uhulutishaji** na **ufupishaji** (akronimu na ukatizaji) hazitumiki sana na waundaji istilahi binafsi katika kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili (taz. pia Mwansoko, 1990; kuhusu sababu za kutotumika kwa mifanyiko hii, taz. pia 3.3.3, uk. 80).

Aidha, uchambuzi wa usayansi wa istilahi za isimu (tazama jedwali 3) unaonyesha kuwa baadhi ya istilahi zilizopendekezwa na wataalam hawa, mathalani, **mizani, kitendaji, faali, abjadi,** na **alfabeti,** hazina usayansi na hazikidhi mahitaji ya **PEGITOSCA** kutokana na kiwango cha chini kilizopata (kiwango ambacho ni chini ya alama 12). Hali hii inazua haja ya waundaji istilahi kuunda istilahi nyingine mpya, zenye usayansi, na zitakazovumiliwa zaidi, na ambazo, kama visawe faafu vya istilahi zilizotajwa, zitafaa kupewa ithibati ya wasanifishaji kwa matumizi mapana ya kitaaluma.

Istilahi za isimu zenye usayansi, kwa mfano, **kikamilishi, kibadala, kiunganishi, king'ong'o,** zinafaa zaidi kwa watumiaji wa istilahi wa viwango vyote vya elimu, yaani wenye kisomo cha 'chini' na wenye kisomo cha juu. Basi istilahi za isimu zinazodaiwa kuwa za 'kimataifa', ilhali hazina 'usayansi' (tazama Mwansoko, 1989a:164), mathalani, **nazali, idiofoni, intonesheni, pronomino,** na nyingine nyingi zilizokopwa kutoka lugha za kigeni (k.v. Kiingereza), hazifai kuvumiliwa zaidi. Utaratibu wa kuzingatia 'usayansi' wa istilahi, utawezesha uundaji na usanifishaji istilahi kwa manufaa ya watu wa aina zote. Hali ilivyo sasa ni kuwa istilahi zinabuniwa na kusanifishwa kwa kufuata viwango vya elimu vya watumiaji istilahi (taz, **Kakulu,** Na.3, 1982; na Besha, 1986:3).

Kwa jumla, tathmini hii imeonyesha kuwa istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoundwa na wataalam binafsi, Kapinga (1983), Mbaabu (1992), na Besha (1994) hazina 'usayansi' kwa asilimia 54.3.

Hali hii inathibitishwa na ukweli kwamba, katika jumla ya istilahi 25 zilizoundwa na Kapinga (1983), zilizo na 'usayansi' ni 11 tu, ambazo ni sawa na asilimia 44 ya istilahi zake zote 25 zilizofanyiwa tathmini (kiwango ambacho ni chini ya asilia 50). Vile vile, katika jumla ya istilahi 22 zilizoundwa ama zilizopendekezwa na Besha (1994) ni 9 tu ambazo zina 'usayansi,' hii ikiwa ni sawa na asilimia 40.

Istilahi za isimu zilizopendekezwa ama zilizobuniwa na Mbaabu (1992) zinadhihirisha kiwango cha juu cha ufaafu na 'usayansi.' Ndiposa katika jumla ya istilahi za isimu 23 zilizozalishwa na mtaalam huyu, 12 zina 'usayansi', ambazo ni sawa na asilimia 52 (taz. jedwali la 5). Kiwango hiki kwenye tasnifu hii kilichukuliwa kuwa cha juu katika kuonyesha 'usayansi' wa istilahi. Ukosefu wa 'usayansi' katika baadhi ya istilahi za isimu ya Kiswahili zilizopendekezwa na Mbaabu (k.v. **kishangao, vitambaza, kiini**), na zilizobuniwa na Kapinga na Besha (taz. jedwali 5) unatokana na mbinu zilizotumiwa kuendeleza istilahi hizo. Suala hili huenda likathibitika na kueleweka zaidi tunapotazama kwa undani nafasi ya istilahi za isimu za kila mtaalam kati ya hawa (taz. 6.2, uk. 355) watatu. Hata hivyo, jedwali lifuatalo linatoa picha kamili ya mbinu za uundaji istilahi zinazopendelewa na wataalam binafsi walioteuliwa, kulingana na uchambuzi wa data.

**Jedwali 5: Mbinu za Uundaji Istilahi za Isimu Kulingana na Data**

| Mbinu za Uundaji Istilahi Zilizotumika | WAUNDAJI ISTILAHI BINAFSI | | | | | | Jumla ya Istilahi Zilizotathminiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kapinga | | Mbaabu | | Besha | | |
| | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | |
| UASILISHAJI KUTOKA KISWAHILI CHENYEWE | 2 | 22.2 | 4 | 44.5 | 3 | 33.3 | 9 |
| UBUNAJI (KUFASIRI MAANA ZA MANENO) | 2 | 22.2 | 3 | 33.3 | 4 | 44.5 | 9 |
| UUNGANISHAJI/ UAMBATANISHAJI | 5 | 50 | 3 | 30 | 2 | 20 | 10 |
| UNYAMBUAJI | 8 | **50** | 4 | 25 | 2 | 25 | 16 |
| UPANUZI WA MAANA ZA ISTILAHI | 3 | 23.1 | 7 | **53.8** | 3 | 23.1 | 13 |
| UTOHOAJI/UKOPAJI | 5 | 38.5 | 2 | 15.3 | 6 | 46.2 | 13 |
| **JUMLA** | **25** | | **23** | | **22** | | **70** |

Kutokana na Jedwali 5, tunaona kwamba, katika uendelezaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili, mbinu tofauti tofauti zinapendelewa na wabunaji istilahi mbalimbali. Inabainika pia kuwa Kapinga (1983), kwa mfano, anapendelea mbinu za ubunaji istilahi za isimu zifuatazo (kwa mfuatano wa 1,2, hadi 6):

1. Unyambuaji na uambishaji.
2. Uunganishaji na uambatanishaji.
3. Ukopaji na utohoaji wa istilahi mkopo.
4. Upanuzi wa istilahi kimaana.
5. Ubunaji na tafsiri ya maana za maneno.
6. **Uasilishaji** wa maneno yaliyopo na yanayotumika kutokana na

Kiswahili chenyewe, kurejelea dhana/istilahi za kigeni.

Naye Besha (1994) anapendelea mbinu za ubunaji istilahi za isimu kwa mfuatano ufuatao (1,2, hadi 6):

1. Ukopaji na utohoaji.
2. Unyambuaji na uambishaji
3. Ubunaji - kufasiri maana za maneno.
4. Upanuzi wa istilahi kimaana.
5. Uasilishaji kutoka Kiswahili chenyewe.
6. Uunganishaji na uambatanishaji.

Mbinu za kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili zinazotumiwa na Mbaabu (1992), kutokana na uchambuzi wa data, zinafuata mpangilio ufuatao (1,2,3, hadi 6):

1. Upanuzi wa maana za maneno.
2. Uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe.
3. Unyambuaji na uambishaji.
4. Ubunaji - kufasiri maana za maneno.
5. Uunganishaji na uambatanishaji.
6. Ukopaji na utohoaji (rejelea pia 3.2, uk. 55 na Jedwali 4).

Katika jumla ya istilahi za isimu 16 zilizobuniwa na wataalam hawa kwa kutumia mbinu ya unyambuaji, istilahi 8 (asilimia 50) zilibuniwa na Kapinga. Hali kadhalika, katika jumla ya istilahi za isimu 13 zilizozalishwa na wataalam hawa kwa mfanyiko wa upanuzi wa maana za maneno, istilahi 7, ambazo ni sawa na asilimia 53.8 zilibuniwa na Mbaabu. Na katika jumla ya istilahi 13 zilizofanyiwa tathmini na ambazo zilibuniwa na wabunaji

istilahi walioteuliwa kwa mfanyiko wa ukopaji na utohoaji, istilahi 6 (asilimia 46.2) zilibuniwa na Besha, istilahi 5 (asilimia 38.5) zilibuniwa na Kapinga na idadi ya istilahi 2 (asilimia 15.3) zilibuniwa na Mbaabu.

Hali hii inadhihirisha kuwa Besha na Kapinga wanaendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili sana sana kwa mfanyiko wa **utohoaji,** tofauti na Mbaabu ambaye anachukua, kwa kiwango kikubwa, mashina ya Kiswahili chenyewe kama msingi wa kubuni istilahi mpya za lugha hii. Ndiposa katika jumla ya istilahi 9 zilizobuniwa na wataalam hawa kwa mfanyiko wa uasilishaji wa maneno kutoka Kiswahili chenyewe, istilahi 4 (asilimia 44.5) zilibuniwa na Mbaabu, istilahi 3 (asilimia 33.3) zilibuniwa na Besha na ni istilahi 2 tu (asilimia 22.2) ambazo zilibuniwa na Kapinga kwa kutumia mbinu hii.

Kutokana na tathmini ya msingi wa 'usayansi' katika istilahi na mbinu za uendelezaji istilahi (rejelea Jedwali 4) na matokeo yake, inadhihirika kwamba mfanyiko au mbinu inayozalisha istilahi za isimu ya Kiswahili zenye 'usayansi' ni ile ya **uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe** kurejelea dhana/istilahi za kigeni. Mbinu hii ya uasilishaji wa maneno kutoka Kiswahili chenyewe inafuatwa na mbinu ya **uunganishaji na uambatanishaji, unyambuaji, ubunaji, upanuzi wa maana za maneno,** na **ukopaji** na **utohoaji,** kwa mfuatano huo huo. Kwa hivyo, uzingativu wa mifanyiko ya **uasilishaji, ubunaji, uunganishaji** na **unyambuaji** itarahisisha na kuchapusha kazi ya ubunaji istilahi za isimu zenye usayansi na ukubalifu kwa walengwa. Mbinu ya **upanuzi wa**

**maana za maneno yaliyopo**, licha ya kwamba ina kiwango cha chini cha 'usayansi' (haina usayansi kwa asilimia 76.9), kama mfanyiko wa ufupishaji, inafaa kuepukwa kulingana na misingi ya uundaji wa istilahi (rejelea 3.3.3, uk. 80) ili kuepusha utatanishi (taz. Picht na Draskau 1985). Uepukaji wa mbinu hii ya upanuzi wa maana za maneno vile vile utapunguza malalamiko juu ya udhaifu wa istilahi zinazozalishwa kwa ruwaza hii. Malalamiko kama hayo huenda yakadhihirika kutokana na uchunguzi wa nafasi ya istilahi za isimu zinazobuniwa na wanaistilahi binafsi walioteuliwa.

## 6.2 Nafasi ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili Zilizobuniwa na Watu Binafsi

### 6.2.1 Nafasi ya Istilahi za Isimu za Mbaabu

Mbaabu (1992) ni mmoja wa wataalam binafsi wa Kiswahili ambao wameiundia lugha hii istilahi ambazo zina nafasi kubwa kutokana na kiwango chake cha juu cha ufaafu na usayansi (rejelea 5.1.2, uk. 344). 'Usayansi' katika istilahi zilizobuniwa na Mbaabu kwa kiwango cha asilimia 52 (rejelea Jedwali 4) unaweza kuelezwa kwa njia mbili:

Kwanza, 'usayansi' wa istilahi za isimu za mtaalam huyu umesababishwa na mbinu zalishi na za kisayansi anazozitumia katika ubunaji wa istilahi. Matumizi, kwa mfano, ya mfanyiko wa uasilishaji wa maneno kutoka Kiswahili chenyewe yana umuhimu wake. Uundaji wa istilahi za isimu kwa mbinu ya uasilishaji wa istilahi za Kiswahili chenyewe, mbali na kwamba hudhihirisha kuwa Kiswahili kina uwezo wa kujiendeleza mumo kwa mumo, pia huzalisha istilahi zinazoeleweka kwa walengwa (taz. Mdee, 1980).

Aidha, istilahi zinazoasilishwa kutoka Kiswahili chenyewe zina nafasi kubwa katika uendelezaji wa leksikoni ya lugha hii kwa sababu zina "uwenyeji" kwa watumiaji (Nabhany, 1982). Na asemavyo Mkude (1983), istilahi zenye uwenyeji na umbo lililozoeleka, huwa ni nyepesi kujifunza na kutumika. Hivyo basi, 'usayansi' wa istilahi za isimu zilizozalishwa kutokana na mfanyiko wa uasilishaji wa maneno kutoka kwa Kiswahili, umetokana na 'uwenyeji' wa umbo la istilahi mpya zilizoundwa na kueleweka kwa urahisi kwa istilahi hizo. Ndiposa Mdee (1986:125) hakosei anapodokeza kuwa "waunda maneno hawana budi kudurusu Kamusi za Kiswahili (za zamani) ili wayafahamu maneno mengi ya Kiswahili wasiyoyajua ambayo wangeweza kuyatumia kueleza dhana mpya badala ya kutohoa au kuunda neno jipya." Hata hivyo, matumizi ya mbinu ya upanuzi wa maana za maneno yamesababisha ukosefu wa 'usayansi' katika baadhi ya istilahi zilizobuniwa na Mbaabu.

Pili, 'usayansi' wa istilahi za isimu zilizoundwa na Mbaabu umesababishwa na uzingativu wa misingi na vigezo vya uundaji wa istilahi 'faafu'. Kipengele cha uwezo wa istilahi kulenga maana ya dhana inayotumiwa kwa udhahiri kimezingatiwa sana na Mbaabu (rejelea Jedwali la 3). Istilahi isiyobeba dhana husika kama inavyoeleweka kwa walengwa hutatanisha, hukosa usayansi na hukataliwa (Sewangi, 1996:18). Tatizo hili halijidhihirishi katika istilahi kadhaa za Mbaabu zilizotathminiwa (taz. 5.1.2, uk. 344; tazama pia istilahi k.v. **miigo, kipua, kihusiano**). Kuhusu kipengele cha uangavu na ukubalifu, Mbaabu (1992:24) anasema:

> ...ukubalifu wa msamiati unategemea aina ya msamiati...na taratibu zilizotumiwa kuunda msamiati huo. Msamiati wa mila na utamaduni, kwa mfano, yafaa ubuniwe na baraza la wazee likiongozwa na taratibu maalum...

Maoni ya aina hii yamewahi kutolewa na wataalam wengi (k.v. Kihore, 1983; Khamisi, 1985) lakini, kwa bahati mbaya, hayajapewa uzito unaohitajika. Kutokana na umuhimu wa misingi ya uundaji istilahi, tunapendekeza kwamba istilahi zenye usayansi za Mbaabu zipewe nafasi kupitia kwa vikao mbalimbali vya kitaifa na kimataifa, kwenye maandishi, na aidha katika ufundishaji wa mafunzo ya isimu ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, istilahi ambazo hazina usayansi (k.v. **mizani, kielezo, kijina, nauni**) hazipasi kuidhinishwa kimataifa.

Tukizingatia nafasi ndogo iliyopewa istilahi zenye usayansi zilizobuniwa na Mbaabu, tunaweza kusema kuwa tatizo la wanalugha wa Kiswahili kuzipinga istilahi zilizopendekezwa na wataalam wengine kwa sababu 'hazina ladha' linadunisha maendeleo katika uwanja huu bure bilashi (taz. 6.3, uk. 361). Yatubidi tukubali au tukatae istilahi fulani kutokana na misingi ya kisayansi, na sababu zinazodhihirika, na wala sio kwa visingizio na visababu. Istilahi 'bora' ni ile iliyofuata nidhamu au mantiki fulani katika uundwaji wake. Kuwepo (au kutokuwepo) kwa "mwonjo" katika istilahi, kwa maoni yetu, ni kigezo hafifu cha kupimia 'ufaafu' wa istilahi kwa vile si rahisi kueleza dhana ya 'mwonjo' au 'ladha' katika istilahi. Tunafahamu kuwa maoni yetu ya kutaka istilahi 'faafu' za isimu zenye 'usayansi,' kama vile za Mbaabu kupewa nafasi kubwa, huenda yasifanikiwe kukwepa pingamizi. Tatizo la ukubalifu lipo (taz. Massamba, 1996). Hata hivyo,

itakuwa vizuri wanaleksikografia wa Kiswahili wakiziidhinisha na kuzipatia istilahi za isimu zenye 'usayansi' nafasi katika maandishi ya kila siku kwa ajili ya maendeleo ya lugha hii.

### 6.2.2 Nafasi ya Istilahi za Isimu za Kapinga

Istilahi za isimu ya Kiswahili zilizobuniwa na Kapinga (1983) zina nafasi ndogo katika uendelezaji wa leksikoni ya lugha hii kutokana na kiwango chake cha chini cha 'usayansi' (taz 5.1.2, uk. 274). Inabainika kuwa (taz. Jedwali 3), katika jumla ya istilahi 25 zilizoundwa na Kapinga, zisizo na 'usayansi' ni 14 ambazo ni sawa na asilimia 56. Istilahi hizo zinajidhihirisha kama zinavyoonyeshwa kwenye Jedwali 6.

**Jedwali 6: Istilahi za Isimu Zisizo na Usayansi Ikilinganishwa na Zile Zilizopendekezwa na Walengwa**

| NA | Kiingereza | ISTILAHI ZISIZO na usayansi | ISTILAHI Zilizopendekezwa |
|---|---|---|---|
| 1 | *vowel harmony* | usawazisho wa matamshi | uwiano wa irabu |
| 2 | *process* | mchakato | mfanyiko |
| 3 | *object* | kitendwa | yambwa |
| 4 | *interjection* | vijazio (viingizi) | kihisishi |
| 5 | *idiophone* | viigizi | miigo (vielezi miigo) |
| 6 | *competence* | umaizilugha | umilisilugha |
| 7 | *conjunction* | kihusishi | kiunganishi |
| 8 | *nasal stop* | nazali | king'ng'o |
| 9 | *subject* | kiima | kitendaji |
| 10 | *embedding* | ubebwaji | uchopekaji |
| 11 | *syntax* | sintaksia | sarufi miundo |
| 12 | *minimal pairs* | jozi bainifu | jozi za sauti |
| 13 | *alphabet* | alfabeti | abjadi? |
| 14 | *intonation* | intonesheni | mkokotoo |

Uamuzi wa Kapinga (1983) wa kuegemea kwenye mbinu za uundaji istilahi za unyambuaji, uunganishaji, ubunaji, au kufasiri maana za maneno umemwezesha kuzalisha istilahi za isimu zenye 'usayansi' kwa asilimia 44 tu. Hata hivyo, azma ya mtaalam huyu ya kuitanua lugha ya Kiswahili kiistilahi inaelekea haikufanikiwa kutokana na kutozingatia kwa mfanyiko zalishi na wenye 'usayansi' wa uasilishaji wa maneno kutoka Kiswahili chenyewe (taz. Jedwali 5). Istilahi asilia zilizohuishwa na kupanuliwa kimaana zimepewa nafasi ndogo katika maandishi ya Kapinga. Kwa hakika hakuna sababu muhimu ya kutoendeleza leksikoni ya Kiswahili kwa mfanyiko wa uasilishaji au ujenzi wa mumo kwa mumo. Sisi, ijapokuwa tunafahamu kuwa kila lugha hukopa, na ukopaji ni sifa ya lugha zote, ukosefu wa 'usayansi' katika baadhi ya istilahi za isimu za Kapinga (na pia Besha, 1994) unatokana na ukopaji na utohoaji mwingi wa istilahi kutoka lugha za kigeni, hususani Kiingereza (taz. mfano wa 121). Mfanyiko wa ukopaji na utohoaji, ingawa hutumika katika kuundia istilahi za isimu, hauna 'usayansi,' na istilahi mkopo aghalabu hazikubaliki kwa walengwa wake (Mdee, 1980:52). (k.m. *"object"*===**yambwa**, badala ya **kitendwa**; *"subject"*===**kiima** badala ya **kitendaji** - rejelea Jedwali 6, NA. 3, na 9 ambapo ruwaza maalum haifuatwi).

Aidha, ukosefu wa usayansi katika istilahi za isimu zilizozalishwa na Kapinga (1983) unatokana na kutozingatiwa kwa misingi ya ubunaji istilahi 'faafu' za Kiswahili (taz. Kiingi, 1989). Huku akizingatia vigezo vya uangavu wa istilahi na udhahiri, mtaalam huyu inaelekea hakutilia maanani vigezo muhimu kama vile uzalishaji wa istilahi, umataifa, na utaratibu ulio

sawa (rejelea Jedwali 3). Hata hivyo, istilahi zilizopendekezwa na zenye usayansi zilizobuniwa na mtaalam huyu (k.v. **majina, viwakilishi, kijalizo, kitamkwa, mkazo**, na nyinginezo kama vile **viyeyusho** (nusu irabu), **vikariri** (viradufu), **mwendesho wa vitenzi** (*conjugation of verbs*) zikipewa nafasi katika maandishi ya kila siku, zitasaidia kuziba mapengo ya istilahi za isimu ya Kiswahili. Uzingativu wa istilahi zenye 'usayansi' utaviwezesha vyombo vya kukuza Kiswahili vya TUKI, BAKITA na BAKIKE, na watu binafsi kuepuka kuunda istilahi kiholela na kwa dhana ambazo tayari zina istilahi 'faafu' zenye kuziwakilisha. Kufanya hivyo kutaipanua lugha hii ya Kiswahili kileksia.

Kadhalika, tunaweza kusema kuwa taadhima, hadhi, na nafasi ya chini iliyopewa istilahi za isimu za Kapinga (1983) na walengwa na waundaji istilahi wa baadaye (k.v. Mbaabu, 1992; Besha, 1994) inatokana na kutoridhika kwao na njia alizozitumia katika kueleza dhana za kigeni (Mbaabu, mawasiliano binafsi 1998). Ndiposa Mbaabu (1989:99) anajitapa, kama tulivyotaja hapo awali kuwa, "...ninaendelea kutumia msamiati wangu ... kwa kuwa unatoa ufafanuzi zaidi wa mnyambuliko wa vitendo vya Kiswahili." Kwa usemi mwingine, Mbaabu anazingatia kigezo cha 'ufaafu' wa istilahi cha uzalishaji. Mbinu za uundaji istilahi zinazo-pendekezwa na Kapinga hazitilii manani sifa ya mnyambuliko wa vitendo vya Kiswahili ama uwezo wa istilahi wa kuzalisha maneno zaidi kwa mnyambuliko. Kwa mfano, ikiwa:

*phrases* === **vifungu** (uk.43)

*adjective* === **kivumishi** (uk.91)

*participle* === **kitenzi vumishi** (uk.91) (taz. pia TUKI,

1990:14)

*modifier* === **kivumishi** (TUKI, 1990)

inatokeaje basi kuwa *participle phrase* iwe **virai vitenzivumishi** badala ya **vifungu vitenzivumishi?** Kwa maoni yetu, **vifungu** (au virai) **vitenzivumishi** havipo katika isimu ya Kiswahili manake *participle* huvumisha vifungu nomino. Kadhalika, istilahi hii haikidhi mahitaji ya sifa za iktisadi na utaratibu uliosawa kama vigezo muhimu vya ufaafu na usayansi wa istilahi. Tazama pia kutozingatiwa kwa vigezo vya uzalishaji na utaratibu maalum katika mfano huu: Ikiwa, *nouns* === **majina** (uk.68); inatokeaje kuwa *nominalisation* === **unominishaji** (utaratibu wa kuunda majina) na *nominalism* === **unasibu?** (taz. pia TUKI, 1990).

Ni kutokana na umuhimu wa misingi na vigezo vya uundaji wa istilahi 'faafu' ndipo tunasisitiza kwamba 'usayansi' katika istilahi za isimu utumiwe na wabunaji istilahi wote, pamoja na vyombo vya TUKI, BAKITA na BAKIKE, kama msingi wa kuona istilahi zipi zipewe nafasi katika Kiswahili. Mifanyiko bora ya kubuni istilahi hizo iwekewe uzito mkubwa. Kufanya hivyo kutaiwezesha lugha hii kujieleza kikamilifu, hususani katika isimu. Labda suala hili litaeleweka zaidi tukifafanua matatizo ya ukuzaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili.

## 6.3 Matatizo katika Ukuzaji wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili

Wataalam na wanaisimu wanaelekea kukubaliana kwamba lugha ni kitu chenye uhai, inakua, haidumai. Misingi ya uundaji istilahi, kama njia mojawapo ya kukuza lugha, ni muhimu iwe katika hali ambayo

haitapotosha ukuaji huo (Heine, 1981). Lugha yoyote ile hukua kutokana na mahitaji ya wale waitumiayo lugha hiyo (Ferguson, 1968). Ukuaji huo wa lugha hutokana na sababu kwamba jamii inaendelea kuwa na vipengele maalum zaidi ambavyo havikuwepo hapo awali. Hali hii ndiyo inayowakumba waundaji istilahi binafsi na vyombo vya kukuza Kiswahili vya TUKI, BAKIKE na BAKITA katika harakati za kuendeleza leksikoni ya lugha hii ya Kiswahili.

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, kumekuwa pia na matatizo maridhawa katika ukuzaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Suala la matatizo katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili limewavutia na limeshughulikiwa na wataalam wa Kiswahili wengi, mathalani Ohly (1977), Temu (1984), Mac William (1985), Hamad (1989), Mwansoko (1996), Massamba (1996), miongoni mwa wengine. Hapa labda itafaa lau tukitoa ufafanuzi mdawari wa matatizo hayo, hususani yanayohusu taaluma ya isimu ya Kiswahili. Baadhi ya matatizo, kama yatakavyoonyeshwa hapa chini, ni ya kiisimu, kisiasa, na kijamii. Matatizo yatakayojadiliwa huathiri sio tu ukuzaji, bali pia usasaishaji na usawazishaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili.

### 6.3.1 Matatizo ya Kiisimu

Ingawa ni kweli kwamba istilahi mkopo na arki za kileksia za kigeni hutumiwa katika lugha fulani ili kuikuza lugha pokezi (Ferguson, 1971:227), wanaistilahi wengi wa Kiswahili (k.v. Mdee, 1980; Nabhany, 1982) wanaelekea kukataa kwamba kutumia istilahi mkopo nyingi kupindukia ni kukuza lugha ya Kiswahili. Kutumia

istilahi mkopo (k.v. **wakati sahihi**===*simple tense*) pale ambapo pana istilahi asili za Kiswahili ama za Kibantu (k.v. **njeo sahihi**) si kukuza lugha, bali ni kuizorotesha (taz. pia Opalka na Pasierbsky, 1977:85).

Kuna sababu mbalimbali za kiisimu zinazofanya kuwepo kwa istilahi mkopo nyingi mno na viambajengo vya kiistilahi mkopo za kigeni visipendelewe katika ukuzaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Hapa tutazifafanua.

#### 6.3.1.1 Uwezo wa Kuleta Mabadiliko katika Muundo wa Kisarufi wa Lugha

Uingizaji kwa wingi mno wa arki za kiistilahi za kigeni na istilahi mkopo kutoka lugha za Ki-magharibi, unaweza kusababisha mabadiliko katika muundo wa kisarufi wa lugha husika (Mwansoko 1990:66). Athari za kuingiza istilahi za mkopo za namna hii tayari zimetambulikana katika lugha nyingine. Kwa mfano, Kiindonesia na lugha nyingine nyingi za Kiaustronesia kijadi zina muundo unaopendelewa wa silabi kuishia na vokali (Ferguson, 1977:18). Hata hivyo, kwa vile istilahi nyingi mkopo kutoka Kigirikolatini (Kigiritini) na lugha za Ulaya za kisasa hazifuati ruwaza hii, kumetokea muundo mpya wa kimofolojia katika Kiindonesia (taz. matumizi ya **kwantitas**===*quantity*, **organik**===*organic*) (Pia taz. Alisjahbana, 1976:75-6; kwa maelezo zaidi kuhusu athari ya aina hii ya maneno mkopo kutoka Kiarabu katika Kiindonesia).

Uingizaji wa istilahi mkopo nyingi mno kutoka Kiingereza umeathiri ruwaza ya Kiswahili ya usilabishaji kiasi kwamba shada za vikwamizo pamoja na vikwamizo visivyoghuna, au kikwamizo na kitambaza au kimadede, ambavyo asilia havikutokea katika Kiswahili, kwa sasa vinatokea kwa wingi (kwa mfano, **sintaksia**===*syntax*, **silabi**===*syllable*, **brokasi**=== *brocase*). Hii ndiyo sababu Mbaabu (1992:119) hakosei anapodai kuwa:

> ...a haitumiwi kama kiishio cha kuunda nomino kutokana na vitenzi vyevye asili ya Kibantu. Tunapounda nomino za Kiswahili kutokana na vitenzi vilivyokopwa hii irabu a ndiyo hutumiwa kwa wingi sana. Nomino nyingi zilizoundwa kutokana na vitenzi vya kukopwa huishia kwa irabu a. ... Ikiwa kitenzi huishia kwa irabu i, hiyo irabu i ndiyo hutoweka (au hubadilika) na mahali pake huchukuliwa na kiishio a (taz. **fitini=fitina, hoji=hoja**).

Mabadiliko na ruwaza anayojadili Mbaabu imetokana na uingizaji wa istilahi mkopo na arki za kiistilahi za kigeni katika Kiswahili (taz. pia Polome 1967:59-70).

### 6.3.1.2 Visawe vya Kiistilahi

Kuwepo kwa istilahi mkopo nyingi za isimu zilizotoholewa kutoka lugha za kigeni pia hakupendelewi na wanalugha na watumiaji wa Kiswahili, kwa vile kunaweza kusababisha visawe vya kiistilahi vingi mno. Na kama alivyosema Mbaabu (1989:27), kuwepo kwa istilahi nyingi tofauti zenye kuwakilisha dhana ile ile ni tatizo kubwa katika ufundishaji wa sarufi na muundo wa Kiswahili. Kwa mfano, imebainika kwamba katika baadhi ya vitabu vya sarufi vilivyonuiwa vitumike katika shule za upili, vyuoni na vyuo vikuu, wanasarufi mbalimbali wametumia istilahi kama vile,

**kielezo** (Mbaabu, 1992), **kijalizo** (Kapinga, 1983), **kikamilishi** (Besha, 1994), **shamirisho** (Nkwera, 1978), **kishamirishi, chagizo** (Mdee, 1979), **ziyada ya kitendo, kiongezo cha kitendo, kisifa** (Abdulla, 1988), kurejelea dhana moja ya kisarufi ya "*complement.*"

Matumizi ya visawe vya kiistilahi vingi mno vya namna hii huwakanganya walengwa, hususani katika fani ya isimu, sayansi menyu na ya teknolojia, na huleta taswira mbovu kwamba kuna zaidi ya dhana moja. Kutokana na sababu hii, ni maoni yetu kuwa visawe vya kiistilahi vinafaa kuepukwa katika isimu ya Kiswahili. Mawasiliano ya kitaaluma ni swala la **uwazi** na wala siyo wingi wa visawe (Felber, 1984:180). Pia haifai chochote kuwa na visawe katika taaluma hii ya kigeni ya Kiingereza ambayo wasemaji wa lugha ya Kiingereza wenyewe wanatumia istilahi moja kwa dhana moja. Visawe havipo katika isimu ya Kiingereza kutokana na sababu kwamba isimu ya lugha hii iliasisiwa na kubuniwa Marekani peke yake. Hata hivyo, si ha lazima tofauti ziwepo katika isimu ya Kiswahili.

#### 6.3.1.3 Tatizo la Tahijia

Tatizo kubwa, ambalo kwa maoni yetu linakwamisha shughuli za kukuza istilahi za isimu, ni ukosefu wa uamuzi wa jinsi ya kuziandika istilahi mkopo kutoka lugha za kigeni (tahijia). Tahijia ni kaida zinazozingatiwa wakati maneno yakiwa katika umbo la matamshi yanayowakilishwa kimaandishi (Kitsao, 1995:36). Kamati ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliyoundwa 1930,

ilipendekeza kufanywe makubaliano ya pamoja ya kuwa na tahijia moja kwa maneno yenye tahijia zaidi ya moja ((usanifishaji wa tahijia) (taz. Mbaabu, 1991)). Inaelekea Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), mrithi wa Kamati hii, halikufuata pendekezo hili, ndiposa katika *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi* wa BAKITA (1990:9 na 14), ushauri unaotolewa unakanganya. BAKITA, kama chombo kinachoratibu na kudhibiti shughuli zote za ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili nchini Tanzania, kinashauri istilahi mkopo za isimu ziandikwe kufuatana na matamshi na/au maandishi ya Kiingereza (Mwansoko, 1990). Chombo hiki cha kukuza Kiswahili hakielezi lini istilahi ya mkopo ifuate matamshi ya Kiingereza na lini ifuate maandishi ya lugha hiyo. Wapo wanaoandika **deta** (<kufuatana na matamshi ya Kiingereza) na wapo wanaoandika **data** (<kufuatana na tahijia ya Kiingereza *data*) (rejelea Mohamed na Mohamed, 1998). Data ndilo linalofaa, manake hata ni neno la Kiswahili-Kibantu; likiwa na maana ya "nasa'" au "kamata" (taz. pia Chimerah, 1999). Kuruhusu na kupendekeza Kiswahili kiandikwe kiholela (taz. **tahajia** (Kitsao, 1989; Mbaabu, 1992) na **tahijia** (Tumbo na Mwansoko, 1992)) kadiri mtu anavyotaka, ni kushusha hadhi ya Kiswahili. Ndiposa kauli na swali analouliza Mbaabu (1995:50) kuwa "wanafunzi tofauti waweza kuchagua tahijia tofauti na tahijia aliyoichagua mwalimu wao. **Je huku si ni kuilemaza lugha?"** ni la kimsingi. Tofauti za kitahijia huilemaza lugha. Hali hii huwakanganya walengwa, kwani hushindwa kufahamu au kuamua ni uandikaji upi wa istilahi ulio sahihi au sanifu.

Kwa mujibu wa utafiti wa Mwansoko (1989, 1990), na kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi huo, mtaalamu huyu anapendekeza kuwa

istilahi mkopo kutoka Kiingereza ziingizwe kwenye Kiswahili kufuatana na matamshi yake ya Kiingereza. Pendekezo la Mwansoko hapa linahitaji uchunguzi wa kina zaidi, hasa ikichukuliwa kwamba utaratibu wa kuzitohoa istilahi kufuatana na tahijia ya lugha yake changizi pia una ubora wake. Utaratibu wa namna hii ni wa moja kwa moja (au ni wa kuliona tu umbo la nje la istilahi ngeni na kulitohoa) katika uzalishaji wa istilahi, kwa vile muundaji halazimiki kusikiliza kwanza matamshi ya istilahi anayohitaji kutoka kwa mzungumzaji au mzawa wa lugha changizi inayohusika ili aweze kuzitoa kwa usahihi. Tukio hili halihusu Kiswahili pekee. Kwa mfano, istilahi za Kibahasa Malaysia na Kibahasa Indonesia zilibuniwa kwa utaratibu huu (Omar na Noor, 1981).

Mifano zaidi:

**graviti**===*gravity* (Kiingereza).

**hidrogeologi**===*hydrogeology* (Kiingereza).

**nautikali**===*nautical* (Kiingereza).

(taz. pia Dewan Bahasa dan Pustaka, 1982; *Istilah Baru Hisab Moden*, rejelea pia 4.8.5.2, uk. 185).

### 6.3.1.4 Namna ya Kushughulikia Viambishi vya Kiistilahi

Tatizo lingine linalofanya istilahi mkopo kutoka lugha za kigeni zisipendelewe na wataalam na watumiaji wa Kiswahili huenda linatokana na jinsi ya kushughulikia viambishi vya kiistilahi. Je, viambishi vya kisayansi ambavyo ni vingi sana katika Kiingereza vitoholewe au vitafutiwe visawe vyake vya Kiswahili? Ilivyo sasa ni kwamba jibu thabiti la swali hili halijapatikana na kuna 'mchanganyiko' tu wa viambishi vya kiistilahi vya isimu

ya Kiswahili.

Uchunguzi kwa makini wa viambishi katika TUKI (1990) unaonyesha kwamba mbinu zote mbili (yaani, utohoaji na utafutaji wa visawe vya Kiswahili) zimeruhusiwa kutumika na zinatumika kiholela. Kwa mfano, istilahi za isimu zinazoishia kwa kiambishi tamati *"-ion"* hazikuwasilishwa kwa utaratibu uliosawa kama mfano huu **(51)** unavyodhihirisha:

(51a) *absorption*===**umezwaji**

(51b) *adaptation*===**utohozi**

(51c) *affixation*===**uambishaji**

(51d) *accomodation*===**rekebisho** (**urekebishaji**)

(51e) *apposition*===**mrejeosawa**

(51f) *aspiration*===**mpumuo**

(51g) *attraction*===**mvuto**

(51h) *convention*===**kaida**.

Kutokana na mfano huu, imebainika kwamba visawe vya Kiswahili vilivyotumiwa ni nomino zilizonyambuliwa. Maneno ya Kiingereza yaliyozalisha nomino hizo pia yanatokana na mnyambuliko. Aidha, kiambishi tamati *"-ion"* kinawakilishwa, wakati mwingine, na **u+...+ji**, (au **u+...+zi**). Vilevile huwakilishwa na **m+...+o**, na mara nyingine na **O+...+a**.

Uchunguzi wa hoja na vijelezi vinavyotumiwa unaonyesha kuwa utohozi wa viambishi hivi haufuati utaratibu uliosawa na hakuna ulinganifu wa mtiririko unaokubalika katika dhana zinazo-wasilishwa katika Kiswahili. Maoni yetu ni kwamba kiambishi tamati *"-ion"* katika vipengele vyote, ila tu **umezwaji**, **utohozi**,

na **kaida**, kinafaa kuwakilishwa kama **m+...+o**. (Rejelea 6.1.2, uk. 344, kuhusu tathmini ya 'usayansi' wa istilahi zilizotolewa hapa kama mfano wa **(51)**. Pia taz. Mugesera (1987:64-7) kwa maelezo zaidi juu ya viambishi vya kiistilahi vya Kiingereza na namna vinavyotafutiwa visawe vyake vya Kinyarwanda).

Kuhusu kiambishi tamati *"-ity"*, *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, TUKI (1990) inatoa mifano **(52)** ifuatayo;

(52a) *compatibility*===**upatanifu**

(52b) *affinity*===**uhusianolugha**

(52c) *ambiguity*===**utata**

(52d) *transitivity*===**uelekezi**

(52e) *opacity*===**ubuye** (utotoro)

(52f) *incompatibility*===**kutopatana**

(52g) *incongruity*===**mwachano**

(52h) *linearity*===**mfuatano**

(52i) *intensity*===**nguvumkazo**

(52j) *irregularity*===**ughairi**

(52k) *regularity*===**ukawaida**.

Kutokana na mifano iliyotolewa hapa juu, inabainika kuwa katika *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, kiambishi tamati *"-ity"* bado hakijapatiwa kisawe kifaacho cha Kiswahili, na hivyo basi kinawakilishwa kama:

(i) **u+...+ifu** (52a), (ii) **u+...+a** (52b, 52c, 52k),

iii) **u+...+O** (52d, 52e, 52j), iv) **O+...+a** (52f), na

v) **m+...+o** (52g, 52h) na (vi) **u+...+e**(52e).

Haieleweki ni kwa nini kiambishi tamati hiki kinawakilishwa na maumbo sita tofauti katika Kiswahili. Hakuna sababu maalum, kwa

mfano, inayofanya'**hali**' (taz. maelezo au vijelezi vya vipengele hivyo kama vinavyotoholewa katika TUKI, 1990) wakati mwingine kuwakilishwa kama **u+...+fu** (taz. 52a).

Pendekezo la Massamba (1996:95) kwamba kiambishi tamati *"-ity"* kipewe kisawe cha Kiswahili cha **u+...Vfu/Vvu** (au **u+...fu**) (ambapo V= vokali faafu, kwa kutegemea sheria ya usilimisho ifaayo) ni la kimsingi, na linafaa kuzingatiwa na wataalam wote wa Kiswahili iwapo lengo la kuitanua lugha hii litafanikiwa ipsavyo (pia taz. Kiingi, 1989: 173-180). Uendelezaji wa istilahi katika Kihebrania tayari unazingatia utaratibu au sera hii ya lugha kutafutiwa visawe vyake vya viambishi vya kiistilahi ndani ya lugha yenyewe (Fellman & Fishman, 1977). Kwa namna hii, imewezekana viambishi vya kiistilahi kubuniwa katika Kiswahili kwa kufuata mantiki katika uandishi.

### 6.3.2 Matatizo ya Kisiasa

Sababu za kisiasa aghalabu huchangia katika ukuzaji, ama uzoroteshaji, wa lugha kiistilahi. Ndiposa, kwa mfano, baada ya kipindi cha Meiji, na Vita vya Pili vya Dunia, jamii ya Kijapani ilijenga mikabala hasi kuhusu mataifa ya Magharibi. Kutokana na sababu hii, Wajapani waliepukana na istilahi za kimataifa zilizochimbuka kutokana na lugha za kisasa za Ulaya (Sugito, 1989). Istilahi mkopo kutoka lugha za Kimagharibi zilikataliwa, na uteuzi wa lugha changizi uliopendelewa katika ukuzaji wa istilahi katika Kijapani ukawa kama ufuatavyo:

Kwanza, kutafuta istilahi asilia zilizopo katika Kijapani; ikiwa hakuna istilahi mwafaka ya Kijapani ya kurejelea dhana, utafutaji wa istilahi nyingine uliegemezwa kwenye lugha nyingine za Kijapani. Ikiwa kulikosekana istilahi faafu katika lugha za kienyeji, jaribio lilifanywa la kupata istilahi katika lugha ya Kichina. Istilahi mkopo za kimataifa zilitumiwa kama hatua ya mwisho kabisa baada ya kukosekana istilahi asilia ya Kijapani. Kwa kifupi, istilahi/maneno ya Kijapani yanaweza kuainishwa kwa makundi manne yafuatayo:

**wago:** Maneno asilia ya Kijapani (**yamato-kotoba**).

**kango:** Maneno yenye asili ya Kichina.

**gairaigo:** Maneno mkopo kutoka Kiingereza na lugha nyingine za Kimagharibi.

**konshugo:** Maneno mchanganyiko (**wago** + **kango**, **kango** + **gairaigo**, **wago** + **gairaigo**).

(taz. pia Takada, 1989:104-116).

Katika Kiswahili, mambo si tofauti sana. Mkwaruzano, ambao una historia ndefu, ni baina ya Watanzania na Wakenya (taz. Ruo, 1989:96-8). Wataalam wa Kiswahili kutoka Kenya wanaelekea kutopendezwa na juhudi zinazofanywa na TUKI na BAKITA za ukuzaji wa lugha kwa kuiundia istilahi kwa mfanyiko wa utohoaji kutoka lugha za kigeni (taz. Mbaabu, 1995:51). Ni maoni ya Nabhany (1982), Mbaabu (1992) na Chimerah (1998) kwamba Kiswahili kijengwe kwa misingi ya Kiswahili chenyewe. Ndiposa si ajabu kwamba wataalam hawa, miongoni mwa Wakenya wengine, wanategemea mno mno lahaja za Kiswahili katika ukuzaji wa Kiswahili. Msimamo wa wataalam hawa ni kwamba istilahi nyingine za kimataifa (kwa

mfano, 'uana') ni makosa, na zinafaa kukosolewa, na mahali pake kuchukuliwa na istilahi faafu (Chimerah, 1998b).

Tahadhari iliyotolewa na wanalugha wa awali kuwa "tusipoangalia nchi yetu itakuwa koloni la nchi jirani" (katika Ruo, 1989:97) inaelekea kwamba haijawatoka Wakenya wengi. Kwa upande mwingine, baadhi ya wataalam kutoka Tanzania (taz. Mdee, 1980; MacWilliam, 1985; Massamba, 1989; 1996) msimamo wao, unaotokana na uchunguzi walioufanya, ni kwamba haina maana kubadili istilahi zilizozoeleka, ama kuunda istilahi mpya, pale ambapo tayari kuna nyingine zilizopata mashiko ya kimataifa. Kwa kutumia kigezo hiki, na kile cha ukubalifu wa istilahi, Massamba (1996:96) anauliza:

> Ni kwa nini, kwa mfano, watumiaji wa Kiswahili wahisi kwamba ni bora kwao kutumia **runinga** badala ya **televisheni** au TV ambalo limezagaa na kuenea katika fahamu za watu kwa muda mrefu?
>
> (Tafsiri yetu)

Kutokana na swali hili, ni dhahiri kwamba mtaalam huyu haoni haja ya kuzibadili istilahi kama **televisheni** ambazo zimezoeleka. Istilahi nyingine, japo zimezoeleka, ni makosa na si mwafaka kimaana. Kwa mfano, tukilichambua neno **televisheni**, tunaliona kuwa katika Kiswahili, linaweza kuwa na maana!

**visheni** *clothe the unclothed*

**tele** *full.*

Maana hii inaweza kumkanganya msemaji wa Kiswahili ambaye hata hajawahi kuona **"runinga."** Na hawa ni wengi sana! (kutokana na mazungumzo ya mtafiti na Chimerah, 1999).

Ni maoni yetu (taz. pia Chimerah, 1998) kwamba suala la 'kuogopa kutawaliwa kimawazo na nchi jirani' huenda hapo baadaye likaleta tofauti za kiistilahi. Kenya na Tanzania hapo baadaye zitakuwa na istilahi/msamiati mbalimbali kama vile Uingereza, Amerika na Australia, japo msingi wa lugha utakuwa huo huo mmoja. Tukio hili halitakuwa la kipekee kwa hali ya Kiswahili. Kwa mfano, maneno yote yanayoeleza sehemu za gari (taz. Sewangi, 1996:12-23) ni tofauti kabisa katika Kiingereza na Kimerikani, japo Wamerikani na Waingereza wanaelewana barabara (taz. Coulmas, 1989:188). Jambo hili likitokea, huenda halitazuia juhudi za kutatua tatizo la ulingano (au usawazisho) wa kimataifa unaotakiwa baina ya istilahi za isimu ya Kiswahili (taz. Mukama, 1989:6).

### 6.3.3 Matatizo ya Kijamii

Pia kuna matatizo ya kijamii ambayo huathiri mifanyiko ya ukuzaji wa leksikoni ya lugha. Ijapokuwa tunafahamu, kwa mfano, kuwa ni kawaida lugha kukopa maneno kutoka kwa lugha zilizoingilia mazingira yake (Langacker, 1968) lakini hata hivyo kundi la lugha za Runyakitara (Runyoro/Rutooro/Runyankore/Rukiga) limekopa istilahi chache sana kutoka kwa Kiswahili (k.m. **ekitabu** (kitabu), **egaali** (gari), **pikipiki**) (taz. Byakutaga, 1996:17). Jambo hili limesababishwa na ukosefu wa heshima na mikabala au mielekeo hasi walionayo Warunyakitara kwa Kiswahili (Mukwaya, 1996:69). Lugha ya Kiingereza, tofauti na Kiswahili, licha ya kwamba inahusishwa na ukoloni na ina waneni wachache kutokana na kiwango cha juu cha kutojua kusoma na kuandika kwa Kiingereza na Warunyakitara (taz.

pia Ndoleriire, 1996:53), imeheshimika na imepewa hadhi ya juu kama lugha ya wasomi na ya kuleta umoja wa Waganda. Si ajabu, kwa hivyo, kwamba idadi kubwa ya istilahi mkopo za Runyakitara zimetoka kwenye Kiingereza (k.m. **maapu**===*map*, **fairo**===*file*, **orupapura**===*paper*, **waranta**===*warrant*, na **peni**===*pen*) (taz. Byakutaga, 1996:16-19).

Aidha, ukuzaji wa istilahi, hususani za isimu ya Kiswahili, huenda usikwepe tatizo la **ukubalifu.** Ukubalifu ni dhana inayojikita katika shughuli za utendaji (Chomsky, 1965:11). Dhana ya ukubalifu ni suala la isimunafsia na ni telezi mno kulieleza (Mdee, 1980:51). Ukubalifu wa istilahi unaweza kuathiriwa na ujuzi wa mtumiaji wa kuelewa maana inayorejelewa katika dhana fulani. Ukubalifu wa istilahi unaweza pia kuathiriwa na utamaduni au mhemuko mkubwa wa mhusika (taz. Abdulaziz, 1989:44). Utafiti uliofanywa na wataalam wa Kiswahili (taz. k.m. Mdee, 1980; Mwansoko, 1993; Sewangi, 1996) umeonyesha kiwango cha chini cha ukubalifu wa istilahi kwa walengwa.

Kuna sababu nyingi zilizochimbuka kutokana na utafiti wa wataalam hawa na hapana haja ya kuzirejelea hapa (taz. pia Dunn, 1985; na Massamba, 1996; kwa maelezo zaidi juu ya sababu za kijamii za kukataliwa kwa istilahi mpya za Kiswahili). Hata hivyo, kauli ya Mwansoko (1996:29) kwamba istilahi zinazokataliwa aghalabu zibuniwe istilahi nyingine mpya na watu binafsi 'vivi hivi tu,' ina umuhimu wake, ila tu inapaswa kufanyiwa uchunguzi wa kina zaidi.

Tukio la kutokubalika kwa istilahi makosa au zisizo na 'usayansi' au 'faafu' zilizobuniwa na wataalam binafsi au vyombo vya kukuza lugha, hutokea katika lugha nyingi duniani. Katika Kijapani, istilahi zenye asili ya Kichina **(kango)** zilizoendelezwa na wasomi wa Kijapani waliobobea katika masuala ya Kichina, wakati mwingine zilikataliwa na umma na mahali pake kuchukuliwa na istilahi asili **(wago)** kama visawe bora. Mfano wa **(kango)** zilizokataliwa ni **"kiboo"** (matumaini) **"taisen"** (acha vita), **"jin-riki-sha"** (gari kubwa nzito) (taz. Sugito, 1989:119; Takada, 1989:109). Kuhusu mifano ya istilahi za isimu ya Kiswahili zisizo na 'usayansi' na zilizokataliwa na walengwa, rejelea 6.1.2, uk. 344.

Ingawa haya yanaonekana ni matatizo 'madogo' tu katika ukuzaji wa istilahi za Kiswahili, ni muhimu, hata hivyo, kuzingatiwa na wanaleksikografia na wataalam wa fani mbalimbali kwa ushirikiano, wakiwemo wanaistilahi kutoka Kenya, Uganda na Tanzania na kwingineko lugha hii inakotumika duniani. Labda suluhisho katika matatizo yaliyojadiliwa hapa juu huenda likapatikana siku za usoni kutokana na utafiti wa kina katika masuala haya.

## 6.4 Muhtasari wa Sura ya Sita

Katika sura hii, tumetathmini 'usayansi' wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kuwa neno 'usayansi' lina faliwati na vijelezi kadhaa. Katika tasnifu hii, neno hili 'usayansi' lina maana ya uwezo wa istilahi kufanyiwa majaribio au utafiti na kuweza kuelezwa kutokana na utafiti mahususi. Kadhalika, 'usayansi' wa istilahi umeelezwa kuwa ni

uwezekano wa istilahi kuelezwa kimantiki kwa kuzingatia vigezo maalum vya uundaji wa istilahi.

Aidha, katika sura hii, tumefafanua misingi ya kutathmini istilahi za isimu ya Kiswahili, na tumeonyesha umuhimu wa kuegemeza tathmini ya istilahi kwenye kanuni na misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi. Pia tumesisitiza kuwa misingi ya kutathmini istilahi sio taratibu za 'kisheria' ambazo lazima zifumbatwe na kila istilahi inayobuniwa. Hata hivyo, mantiki ya kuchunguza misingi ya kisayansi na kutathmini istilahi za isimu imefafanuliwa kwa mapana na marefu yake.

Katika sura hii, mna tathmini ya istilahi za isimu ya Kiswahili za chombo cha kukuza Kiswahili cha TUKI. Kutokana na tathmini hii, imedhihirika kuwa zipo istilahi za isimu ambazo zina 'usayansi' na huwaridhisha walengwa wake. Kwa upande mwingine, zipo ambazo hazina 'usayansi' (yaani mfumo wa sayansi haujatumika katika uundaji wake) ambazo huondokea kutowaridhisha watumiaji. Hata hivyo, tathmini hii imetusogeza mbele zaidi na kuonyesha kuwa kutosadifu kwa istilahi pia hutokana na kutozingatia vigezo vya PEGITOSCA vya ufaafu wa istilahi (taz. Kiingi, 1989). Imebainika, kutokana na utafiti huu, kwamba baadhi ya viambishi vya mkopo vinavyotumiwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) havijapewa visawe mahsusi vinavyobeba maana maalum za kisemantiki za lugha ya Kiswahili, hususani katika taaluma ya isimu.

Tumesisitiza kuwa istilahi za TUKI ambazo hazina 'usayansi', na zile zinazobuniwa moja kwa moja bila kuzingatia ufungamano wa kidhana, huenda zikahitaji masahihisho siku za usoni ili ziakisi vilivyo sifa za dhana zinazoziwakilisha. Hali kadhalika, imedhihirika, kutokana na utafiti huu, kwamba ingekuwa bora kama *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990) ingerekebishwa na kuandikwa upya. Tumesisitiza, vilevile, kuwa urekebishaji wa kamusi hii utahitaji kuzingatia viambishi vya kiistilahi vilivyobuniwa na kuasilishwa kutokana na lahaja za Kiswahili.

Katika sura hii pia, mna tathmini ya istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoundwa na wataalam binafsi, na aidha mbinu zinazotumiwa na wataalam hao katika uendelezaji wa leksikoni ya lugha ya Kiswahili. Tathmini hii imeonyesha kuwa istilahi za isimu zilizopendekezwa ama kubuniwa na baadhi ya watu binafsi zina kiwango cha chini cha 'usayansi' na hazikidhi mahitaji ya jaribio la PEGITOSCA. Tumesisitiza kuwa ukosefu wa usayansi katika baadhi ya istilahi za isimu zilizoundwa na watu binafsi walioteuliwa umesababishwa na kutozingatiwa kwa kanuni za uundaji istilahi na, vilevile, mbinu wanazozitumia kubuni istilahi hizo. Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba mfanyiko unaozalisha istilahi za isimu ya Kiswahili zenye 'usayansi' ni ule wa uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe ukifuatwa na mfanyiko wa uunganishaji na uambatanishaji, unyambuaji, ubunaji, upanuzi wa maana za maneno, na utohoaji/ukopaji, kwa mfuatano huo huo.

Aidha, katika sura hii, tumesisitiza kuwa 'usayansi' wa istilahi utumiwe na walengwa, waundaji istilahi binafsi, pamoja vyombo vya TUKI, BAKITA, BAKIKE kama msingi wa kuona na kuamulia istilahi zipi za isimu ni 'pendezi' zaidi ama zipewe nafasi katika Kiswahili.

Vilevile, tumejadili, katika sura hii, matatizo ya ukuzaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Tunatarajia kuwa utafiti huu utawafaa watumiaji wote wa Kiswahili katika uteuzi wa istilahi 'faafu' zaidi za isimu panapotokea haja ya kuchagua kati ya istilahi mbili, tatu, au zaidi zenye kurejelea dhana moja. Waaidha, tunatarajia kuwa taarifa zilizotokana na tathmini ya 'usayansi' katika istilahi, pamoja na kuonyesha kiwango cha usayansi, zitawafaa wabunaji istilahi binafsi, na vyombo vya kukuza lugha ya Kiswahili, katika kuteua mbinu zalishi na zenye 'usayansi' kati ya mbinu nyingi za kisifabia zinazotumika katika kuunda istilahi. Pia tunatarajia kuwa kazi hii itawasaidia wapenzi wa Kiswahili wote watakaoisoma kwa makini, hususani katika kuelewa mifanyiko yenye kuzalisha istilahi zenye 'usayansi' bila shida kubwa.

# SURA YA SABA

## TAMATI

### 7.0 Mchango wa Utafiti Huu

Jambo moja jipya ambalo limejitokeza kutokana na utafiti huu juu ya usayansi wa istilahi za isimu ya Kiswahili ni kwamba istilahi kukosa 'usayansi' huathiri ufaafu, kusadifu, na ukubalifu wake kwa walengwa. Kutokana na utafiti huu, tumetambua kwamba endapo mfumo wa sayansi utatumika na wabunaji istilahi za isimu ya Kiswahili, basi nyingi ya istilahi zitakazobuniwa zitakuwa na upeo wa juu wa ubora, na zitaeleweka kwa urahisi na watumiaji wake.

Jambo jingine ambalo tumeligundua kutokana na utafiti huu ni kuwa mifanyiko au mbinu inayoendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili zenye 'usayansi,' na zinazosadifu kimataifa, ni ile ya uasilishaji wa istilahi kutokana na Kiswahili chenyewe kurejelea dhana/istilahi za kigeni. Mbinu hii ya uasilishaji wa maneno inafuatiwa na mbinu za uunganishaji na uambatanishaji, unyambuaji, ubunaji, upanuzi wa maana za maneno, na ukopaji/ utohoaji, kwa mfuatano huo. Aidha, kutokana na utafiti huu, tumetambua ya kuwa mbinu za uundaji istilahi za uhulutishaji, uradidi na ufupishaji ni nadra katika matumizi; na zinapotumika, aghalabu, huzalisha istilahi za isimu zenye kiwango cha chini cha 'usayansi' na ufaafu wa kimataifa.

Jambo jingine jipya ambalo tumegundua kutokana na utafiti huu ni kwamba misingi ya uundaji wa istilahi ya Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO), ambalo ndilo linaloratibu uendelezaji wa istilahi kimataifa, na misingi iliyopendekezwa na Felber (1984), Picht & Draskau (1985), na Mwansoko (1990) si timilifu. Inafaa ifahamike, hasa na wanaistilahi, kuwa ingawa utafiti huu umejaribu kuiweka misingi hii pamoja na kuikamilisha ili iweze kurejelewa kwa urahisi, misingi hii sio taratibu za 'kisheria' ambazo sharti zifumbatwe na kila istilahi itakayobuniwa. Hata hivyo, mantiki ya kujiwekea misingi ya uundaji istilahi imeng'amuliwa kutokana na utafiti huu.

Aidha, kutokana na utafiti huu, tumegundua kwamba, ili kupata 'usayansi' katika istilahi za isimu ya Kiswahili, wanaistilahi hawana budi kuzingatia misingi ya kisayansi, na mbinu zalishi za ubunaji wa istilahi. Misingi hiyo ikitwe kwa nadharia za kiistilahi. Kutokana na utafiti huu, tumetambua pia kwamba kuna nadharia za istilahi zinazopaswa kutumiwa kama 'mwongozo' wa kubuni na kuendeleza istilahi za Kiswahili (rejelea sura ya 2). Hali kadhalika, imebainika, kutokana na utafiti huu, kuwa Kiswahili kinaweza, kwa kiasi kikubwa, kujiendeleza kiistilahi mumo kwa mumo kwa kuzingatia misingi teule ya kisayansi, na mifanyiko zalishi ya uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe. Utafiti huu pia umechangia katika ugunduzi kwamba kuna njia mbili kuu za kukuza lugha. Nazo ni: Kwanza, kwa kuizidishia visawe vya kiistilahi; na pili, kwa kujaza mapengo ya kiistilahi yaliyopo na yanayotokana na kuingizwa kwa dhana za kigeni ama kufa kwa istilahi fulani fulani katika lugha pokezi. Hata hivyo,

kutokana na utafiti huu, tumetambua kuwa tija ya visawe vya kiistilahi hutegemea fani au taaluma yenyewe. Katika fani ya isimu haifai chochote kuwa na visawe vingi kupindukia, hasa vile wenyeji wa taaluma hii wenyewe wanatumia istilahi moja kwa dhana moja. Vile vile, kutokana na utafiti huu, tumegundua kwamba kuwa na makundi mawili ya kiistilahi; istilahi za wasomi na istilahi za watu wasio wasomi, hususani katika fani ya isimu ya Kiswahili, ni upotofu mkubwa unaofaa kuepukiliwa mbali.

## 7.2 Mapendekezo

Kutokana na utafiti huu, imewezekana kugundua mambo kadhaa ambayo inabidi kuyataja na kuyatolea mapendekezo. Utafiti huu umebainisha kuwa lugha hukuzwa kiistilahi kwa kuizidishia visawe katika msamiati wake wa kimsingi. Vilevile, lugha huendelezwa kwa kujaza mapengo ya kiistilahi yaliyopo, na yanayotokana na kuingizwa kwa dhana za kigeni ama kufa kwa istilahi fulani fulani. Kutokana na ugunduzi huu, ni muhimu kutoa pendekezo kwamba juhudi za kukuza Kiswahili zisiachiwe 'mabingwa' wa istilahi (wanaistilahi) pekee (taz. Mbaabu, 1991). Watumiaji wengi wa istilahi na wataalam wa fani mbalimbali washirikishwe katika uundaji istilahi na kutoa ushauri kuhusu 'ufaafu' na ubora wa istilahi mpya. Istilahi mpya zinazozalishwa zisambazwe kitaifa na kimataifa kwa walengwa wake. Ni muhimu wanalugha binafsi wanapokamilisha orodha zao za istilahi wazipelekee orodha hizo BAKIKE, BAKITA, TUKI, CHAKITA ili zikathibitishwe kwa njia ya usanifishaji.

Aidha, licha ya kwamba visawe huweza kuwa na manufaa katika ukuzaji wa lugha, tunapendekeza kuwa ubunaji wa istilahi mpya za isimu usiendelezwe pale ambapo tayari dhana moja inarejelewa na istilahi 'faafu' mbili au zaidi. Jambo hili litapunguza 'utata' katika istilahi za isimu ya Kiswahili. Vilevile, litapunguza 'malalamiko' kuhusu kukanganya na udhaifu wa istilahi hizo. Kadhalika, iwapo patatokea haja ya kuchagua istilahi 'pendezi' kati ya istilahi mbili au zaidi zenye kurejelea dhana moja, tunapendekeza kuwa uteuzi huo uegemezwe kwenye vigezo vya istilahi 'faafu' vya **PEGITOSCA**, na vilevile kwenye misingi ya kisayansi ya uundaji istilahi.

Fauka ya hayo, suala la 'usayansi' katika istilahi, na mbinu za uundaji istilahi, linastahili liwe mwongozo wa kuwasaidia waundaji istilahi binafsi na vyombo vya BAKITA, TUKI, CHAKITA na BAKIKE katika kuendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika, lugha ya Kiswahili ikuzwe kwa kujaza mapengo yaliyopo kwa mifanyiko na ruwaza iliyodhihirika kuzalisha istilahi zenye 'usayansi.' Ruwaza hizo ni pamoja na uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe, uunganishaji, unyambuaji, na ubunaji. Uzingativu wa mbinu hizi, kama vielelezo vya kuundia istilahi, licha ya kwamba utachapusha kazi ya ukuzaji istilahi za isimu, bali pia utasaidia kuonyesha bayana mantiki ya uhusiano baina ya dhana na istilahi inayoiwakilisha.

Kutokana na ugunduzi kuwa lahaja za Kiswahili na lugha za Kibantu zina umuhimu na mchango mkubwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, utafiti wa kina kirefu unahitajika ufanyike katika

lahaja hizo. Utafiti wa aina hii utasaidia kuibua maneno ya Kibantu mahali ambapo katika eneo zima, maneno yanayotumika ni ya kigeni tu. Kiswahili kinaweza kubeba dhana zozote zile, za sayansi zikiwemo, vizuri sana. Utafiti wa aina hii utasaidia pia kuibua istilahi zinazohitajika ndani ya Kiswahili chenyewe kabla ya kutohoa istilahi mkopo kutokana na lugha za kigeni. Vilevile suala la 'usayansi' katika istilahi na mbinu za kubuni istilahi linastahili kufanyiwa utafiti na uchunguzi zaidi kwa kuzingatia nadharia mbalimbali za istilahi. Matokeo ya utafiti wa aina hii yatawapa wabunaji istilahi na walengwa fursa ya kuimarisha weledi wao na namna ya kubuni na kutambua istilahi zenye 'usayansi' na zinazosadifu kimataifa.

Aidha, kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa 'usayansi' wa istilahi ni hatua moja muhimu katika ujenzi wa usayansi katika lugha. Mataifa mengi (k.v. Japani na Korea) yameendelea kiviwanda kwa kujenga usayansi katika lugha zao asili na kwa kuzitumia lugha hizo kama chombo cha kusambaza maarifa yao ya kisayansi na kiteknolojia (Takada, 1989:114) Tunapendekeza utafiti wa baadaye kuhusu 'usayansi' wa lugha ya Kiswahili ufanywe ili lugha hii iweze kujieleza yenyewe katika shughuli za kisayansi na kiteknolojia. Kwa hivyo, utafiti huu ni kichocheo cha utafiti wa baadaye kuhusu usayansi wa lugha ya Kiswahili.

Ziara yetu katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki ilitupa fursa ya kushuhudia kuwa somo la leksikografia na othografia halijapewa uzito vyuoni ipasavyo. Kutokana na umuhimu wa istilahi na udurusu wa Kamusi ya Kiswahili, ingefaa somo la leksikografia na

othografia liendelee kufundishwa na kutafitiwa. Jambo hili litawapa wanaleksikografia, wananadharia, waundaji istilahi, wanalugha, wanaisimu, wahadhiri, na wanafunzi wa Kiswahili fursa ya kupanua umahiri wao wa jinsi ya kuendeleza lugha.

Aidha, imani kwamba istilahi zinazoundwa zinafaa kuhusishwa na vikundi vya walengwa wake, yaani kwa kujali tofauti zao za kielimu, huenda haina uzito. Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa istilahi zinazozalishwa kwa kuzingatia misingi ya kisayansi ya uundaji istilahi na vigezo vya istilahi 'faafu,' hukidhi matakwa ya watumiaji wote. Uundaji istilahi katika lugha nyingi duniani tayari umepiga vita imani hii ya istilahi za wasomi na za wasio wasomi (taz. Porksen, 1989:131). Ni kwa kufanya hivyo tu ndipo dhana kama vile "istilahi zisizo na usayansi" au "istilahi zenye usayansi" zitakuwa na maana halisi kwani 'usayansi' wa istilahi hautahusishwa ama kubanwa katika vikundi mahsusi vya walengwa wa istilahi.

Kutokana na utafiti huu, haja ya ushirikiano katika shughuli ya kuendeleza istilahi za Kiswahili imebainika. Jambo hili linadhihirisha umuhimu wa kuwepo kwa jopo la kitaifa na la kimataifa la wataalam, hususani wanaistilahi, la kutoa mwongozo thabiti, kujadiliana, kurasmisha, na kuidhinisha istilahi mpya zinazobuniwa na kupendekezwa na waundaji istilahi. Utaratibu wa istilahi kuundwa na kisha kupitishwa na jopo la wataalam una faida kuu nne:

- Kwanza, utasaidia kutambua haraka mapengo ya kiistilahi na haja kuu kimuktadha ya utumizi wa istilahi mpya.

- Pili, utasaidia kuona haraka ni istilahi zipi zina 'usayansi,' na tena ambazo ni 'pendezi' zaidi kwa walengwa.
- Tatu, utahimiza istilahi zisiundwe moja moja kukidhi mahitaji ya mbunaji istilahi, lakini ziundwe kwa kutazama mfumo wa lugha yote ili ziwe katika ufungamano wa kidhana.
- Nne, utasaidia kuleta upatanisho, usawazishaji, na usasaishaji wa lugha hii unaohitajika sana kimataifa.

Mtindo wa kubuni istilahi na 'kuisanifisha' baada ya kupitishwa na jopo la kitaifa, au kimataifa, la wanalugha ukizingatiwa utatuepusha na uundaji wa istilahi zisizo na 'usayansi,' na pia utata unaotokana na wingi wa visawe vya kiistilahi, hususani katika isimu ya Kiswahili. Hata hivyo, ni muhimu ieleweke kwamba, katika hatua ya utekelezaji, huenda jambo hili lisiwezekane na halina ulazima. Katika uundaji wa maneno kama vile *brunch*, *cyberspace*, *chunnel*, *infotainment*, *fantabulous*, wanalugha wa Marekani, Uingereza, Australia, New Zealand au Kanada hawakukutana na kushirikiana katika majopo (taz. Mwansoko, 1997). Jopo halibuni istilahi bali, hupitisha au kukataa tu. Licha ya kwamba lugha haikuzwi jinsi hii, pia jambo hili haliwezekani kwa sababu za kisiasa na kifedha, hivyo linahitaji uchunguzi wa kina zaidi.

Isitoshe, istilahi za isimu ya Kiswahili ambazo hazina 'usayansi' na, vilevile istilahi nyingine za Kiswahili ambazo zimeundwa kimakosa zinafaa kufanyiwa marekebisho, masahihisho, au ziondolewe katika machapisho, na mahala pake pachukuliwe na istilahi 'faafu.' Usahihishaji wa istilahi za isimu za namna hii ni muhimu na utaziwezesha kuakisi vilivyo sifa za dhana

zinazoziwakilisha. Hali kadhalika, *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990), kutokana na utafiti huu, inahitaji kufanyiwa marekebisho na, ikiwezekana, iandikwe upya ili kutosheleza mahitaji ya walengwa wake (taz. pia Kiingi, 1997). Wanaleksikografia na watunzi wa kamusi za Kiswahili hawana budi kuongozwa na nadharia maalum za istilahi ambazo zitawapa misingi ya kisayansi ya kuteua istilahi 'faafu' na zenye ukubalifu wa kimataifa kwa walengwa. Kazi hii inasisitiza kuwa istilahi ambazo hazina 'usayansi' zisipatiwe nafasi yoyote katika *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, na, kwa jinsi hiyo zinafaa kupembuliwa, ama kuondolewa, katika kamusi hiyo.

## 7.3 Hitimisho

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza usayansi wa istilahi za isimu na mbinu zinazotumiwa kubuni istilahi zenye 'usayansi' na ukubalifu wa kimataifa kwa walengwa. Imedhihirika, kutokana na utafiti huu, kwamba lugha ya Kiswahili kuwa na upungufu wa istilahi za isimu si kioja hata; kazi ni njia ya kulitatulia tatizo hili. Kwa vyovyote vile, wanalugha na wanaistilahi wa Kiswahili si mbumbumbu wa hayo, ndiposa wamo mbioni kukienzi na kukikuza kwa vyovyote vile. Aidha, tumeona kutokana na utafiti huu, kwamba tasliti ya Kiswahili kutaka kujieleza kikamilifu katika nyanja ya isimu itamalizika iwapo uundaji wa istilahi utafuata misingi timilifu ya kisayansi (na iliyokitwa kwa nadharia ya kiistilahi) na mbinu zalishi za uundaji istilahi. Tumeona kwamba, kama suala hili litafuatwa na kutekelezwa na wabunaji istilahi wote, basi nyingi ya istilahi

za isimu zitakazozalishwa zitakuwa na upeo wa juu wa 'ufaafu' na 'usayansi,' na zitaeleweka kwa urahisi kwa vile zitaweza kuelezeka kimantiki. Isitoshe, tumezungumzia umuhimu wa juhudi za koto (au za ziada) zinazofanywa na wanaistilahi binafsi pamwe na vyombo vikuu vya ukuzaji na uendelezaji wa istilahi za Kiswahili. Katika uchunguzi wetu, tumeona kwamba, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, kumekuwa pia na matatizo anuai katika ukuzaji wa istilahi za Kiswahili. Tumeona kuwa shughuli na kazi ya kuendeleza Kiswahili isiachiwe 'mabingwa' wa istilahi pekee. Vilevile, imebainika kuwa wabunaji istilahi wanapokosolewa, wasivunjike moyo bali wapate ndaro ya kubuni zaidi, kwani Kiswahili kinahitaji sana ujuzi wao ili kufikia upeo wake mustahiki. Ni matarajio yetu basi, kuwa tasnifu hii itachangia katika harakati za kuimarisha istilahi za isimu ya Kiswahili na, hivyo basi, kuikomaza lugha hii katika medani ya taaluma.

[CONCEPTUAL]



# A THEORY OF SCIENTIFIC TERMINOLOGY

⟨1⟩ **Basic Concepts:**

expression, concept, term

⟨2⟩ **Postulates:**

⟨2.1⟩ 20 Periods $\bar{N}$ $\bar{L}$ $\bar{T}$ $\bar{M}$ $\bar{K}$ $\bar{A}$ $\bar{W}$
$\bar{B}$ $\bar{R}$ $\bar{F}$ $\bar{Z}$ $\bar{H}$ $\bar{C}$ $\bar{V}$ $\bar{S}$ $\bar{Q}$ $\bar{E}$ $\bar{X}$ $\bar{P}$ $\bar{O}$

⟨2.2⟩ 24 Bonds R H X G S Ɛ N B
M Ë Ä V W D U L J P
O F T E K Y

⟨3⟩ **CFR:** $\bar{\pi}\,\Omega\,\bar{\pi}_o = \bar{\pi}\,\gamma\,\bar{\pi}_o\,\gamma_o$

⟨4⟩ The Periodic System of Conceptual Elements

⟨5⟩ **CTR:** $\varphi(\bar{\pi}_1, \bar{\pi}_2, \ldots) V \bar{\Psi}$

where $\bar{\Psi} = \bar{C}, \bar{V}, \bar{S}, \bar{Q}, \bar{E}, \bar{X}, \bar{P}, \bar{O}$

⟨6⟩ **CBR:** $\bar{X}\,\mathcal{E}\,\bar{\pi}$

⟨7⟩ **The PEGITOSCA Criterion**

$f_1(P, E, G, I, T, O, S, C)$ iff $f_2(C^*, E^*, S^*, L^*, A$

| Period | Group 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| I | $\overline{N}$z | $\overline{N}$r | $\overline{N}$h | $\overline{N}$x | $\overline{N}$g | $\overline{N}$s | $\overline{N}$ε | $\overline{N}$n | $\overline{N}$a | $\overline{N}$b | $\overline{N}$c | $\overline{N}$m | $\overline{N}$ë́ |
| II | $\overline{L}$z | $\overline{L}$r | $\overline{L}$h | $\overline{L}$x | $\overline{L}$g | $\overline{L}$s | $\overline{L}$ε | $\overline{L}$n | $\overline{L}$a | $\overline{L}$b | $\overline{L}$c | $\overline{L}$m | $\overline{L}$ë́ |
| III | $\overline{T}$z | $\overline{T}$r | $\overline{T}$h | $\overline{T}$x | $\overline{T}$g | $\overline{T}$s | $\overline{T}$ε | $\overline{T}$n | $\overline{T}$a | $\overline{T}$b | $\overline{T}$c | $\overline{T}$m | $\overline{T}$ë́ |
| IV | $\overline{M}$z | $\overline{M}$r | $\overline{M}$h | $\overline{M}$x | $\overline{M}$g | $\overline{M}$s | $\overline{M}$ε | $\overline{M}$n | $\overline{M}$a | $\overline{M}$b | $\overline{M}$c | $\overline{M}$m | $\overline{M}$ë́ |
| V | $\overline{K}$z | $\overline{K}$r | $\overline{K}$h | $\overline{K}$x | $\overline{K}$g | $\overline{K}$s | $\overline{K}$ε | $\overline{K}$n | $\overline{K}$a | $\overline{K}$b | $\overline{K}$c | $\overline{K}$m | $\overline{K}$ë́ |
| VI | $\overline{A}$z | $\overline{A}$r | $\overline{A}$h | $\overline{A}$x | $\overline{A}$g | $\overline{A}$s | $\overline{A}$ε | $\overline{A}$n | $\overline{A}$a | $\overline{A}$b | $\overline{A}$c | $\overline{A}$m | $\overline{A}$ë́ |
| VII | $\overline{W}$z | $\overline{W}$r | $\overline{W}$h | $\overline{W}$x | $\overline{W}$g | $\overline{W}$s | $\overline{W}$ε | $\overline{W}$n | $\overline{W}$a | $\overline{W}$b | $\overline{W}$c | $\overline{W}$m | $\overline{W}$ë́ |
| VIII | $\overline{B}$z | $\overline{B}$r | $\overline{B}$h | $\overline{B}$x | $\overline{B}$g | $\overline{B}$s | $\overline{B}$ε | $\overline{B}$n | $\overline{B}$a | $\overline{B}$b | $\overline{B}$c | $\overline{B}$m | $\overline{B}$ë́ |
| IX | $\overline{R}$z | $\overline{R}$r | $\overline{R}$h | $\overline{R}$x | $\overline{R}$g | $\overline{R}$s | $\overline{R}$ε | $\overline{R}$n | $\overline{R}$a | $\overline{R}$b | $\overline{R}$c | $\overline{R}$m | $\overline{R}$ë́ |
| X | $\overline{F}$z | $\overline{F}$r | $\overline{F}$h | $\overline{F}$x | $\overline{F}$g | $\overline{F}$s | $\overline{F}$ε | $\overline{F}$n | $\overline{F}$a | $\overline{F}$b | $\overline{F}$c | $\overline{F}$m | $\overline{F}$ë́ |
| XI | $\overline{Z}$z | $\overline{Z}$r | $\overline{Z}$h | $\overline{Z}$x | $\overline{Z}$g | $\overline{Z}$s | $\overline{Z}$ε | $\overline{Z}$n | $\overline{Z}$a | $\overline{Z}$b | $\overline{Z}$c | $\overline{Z}$m | $\overline{Z}$ë́ |
| XII | $\overline{H}$z | $\overline{H}$r | $\overline{H}$h | $\overline{H}$x | $\overline{H}$g | $\overline{H}$s | $\overline{H}$ε | $\overline{H}$n | $\overline{H}$a | $\overline{H}$b | $\overline{H}$c | $\overline{H}$m | $\overline{H}$ë́ |
| XIII | $\overline{C}$z | $\overline{C}$r | $\overline{C}$h | $\overline{C}$x | $\overline{C}$g | $\overline{C}$s | $\overline{C}$ε | $\overline{C}$n | $\overline{C}$a | $\overline{C}$b | $\overline{C}$c | $\overline{C}$m | $\overline{C}$ë́ |
| XIV | $\overline{V}$z | $\overline{V}$r | $\overline{V}$h | $\overline{V}$x | $\overline{V}$g | $\overline{V}$s | $\overline{V}$ε | $\overline{V}$n | $\overline{V}$a | $\overline{V}$b | $\overline{V}$c | $\overline{V}$m | $\overline{V}$ë́ |
| XV | $\overline{S}$z | $\overline{S}$r | $\overline{S}$h | $\overline{S}$x | $\overline{S}$g | $\overline{S}$s | $\overline{S}$ε | $\overline{S}$n | $\overline{S}$a | $\overline{S}$b | $\overline{S}$c | $\overline{S}$m | $\overline{S}$ë́ |
| XVI | $\overline{Q}$z | $\overline{Q}$r | $\overline{Q}$h | $\overline{Q}$x | $\overline{Q}$g | $\overline{Q}$s | $\overline{Q}$ε | $\overline{Q}$n | $\overline{Q}$a | $\overline{Q}$b | $\overline{Q}$c | $\overline{Q}$m | $\overline{Q}$ë́ |
| XVII | $\overline{E}$z | $\overline{E}$r | $\overline{E}$h | $\overline{E}$x | $\overline{E}$g | $\overline{E}$s | $\overline{E}$ε | $\overline{E}$n | $\overline{E}$a | $\overline{E}$b | $\overline{E}$c | $\overline{E}$m | $\overline{E}$ë́ |
| XVIII | $\overline{X}$z | $\overline{X}$r | $\overline{X}$h | $\overline{X}$x | $\overline{X}$g | $\overline{X}$s | $\overline{X}$ε | $\overline{X}$n | $\overline{X}$a | $\overline{X}$b | $\overline{X}$c | $\overline{X}$m | $\overline{X}$ë́ |
| XIX | $\overline{P}$z | $\overline{P}$r | $\overline{P}$h | $\overline{P}$x | $\overline{P}$g | $\overline{P}$s | $\overline{P}$ε | $\overline{P}$n | $\overline{P}$a | $\overline{P}$b | $\overline{P}$c | $\overline{P}$m | $\overline{P}$ë́ |
| XX | $\overline{O}$z | $\overline{O}$r | $\overline{O}$h | $\overline{O}$x | $\overline{O}$g | $\overline{O}$s | $\overline{O}$ε | $\overline{O}$n | $\overline{O}$a | $\overline{O}$b | $\overline{O}$c | $\overline{O}$m | $\overline{O}$ë́ |

'CONCEPTUAL
UAL ELEMENTS

| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| $\overline{N}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{L}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{T}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{M}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{K}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{A}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{W}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{B}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{R}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{F}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{Z}v$ | $\overline{Z}w$ | $\overline{Z}d$ | $\overline{Z}u$ | $\overline{Z}l$ | $\overline{Z}j$ | $\overline{Z}p$ | $\overline{Z}o$ | $\overline{Z}f$ | $\overline{Z}t$ | $\overline{Z}e$ | $\overline{Z}k$ | $\overline{Z}y$ |
| $\overline{H}v$ | $\overline{H}w$ | $\overline{H}d$ | $\overline{H}u$ | $\overline{H}l$ | $\overline{H}j$ | $\overline{H}p$ | $\overline{H}o$ | $\overline{H}f$ | $\overline{H}t$ | $\overline{H}e$ | $\overline{H}k$ | $\overline{H}y$ |
| $\overline{C}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{V}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{S}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{Q}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{E}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{X}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{P}v$ | | | | | | | | | | | | |
| $\overline{O}v$ | | | | | | | | | | | | |

K.B. Kiingi, Kenyatta University
September 1997

SEHEMU YA KWANZA

## Kiambatisho cha 2: Istilahi za Isimu ya Kiswahili

### 2.1 Orodha ya Istilahi za isimu ya Kiswahili Zilizotathminiwa

Jina la Mdadisiwa.............................................
Asasi ya Elimu................................................
Tarehe ya Mahojiano...........................................

| ISTILAHI | 1:<br>JE UNAITAMBUA ISTIALHI HII? | 2:<br>KAMA NDIYO Eleza MAANA YAKE AU TOA<br><br>KISAWE CHAKE CHA KIINGEREZA | 3:<br>VIFUATAVYO NI VIGEZO VYA "ISTILAHI FAAFU"<br><br>a) istilahi sharti ilenge maana ya dhana inayotumiwa kwa udhahiri<br>b) istilahi sharti ifuate utaratibu maalum wa istilahi zilizopo<br>c) istilahi sharti iwe na ulinganifu wa mtiririko<br>d) istilahi sharti iwe na ukubalifu wa kimataifa<br>e) istilahi lazima iangaze maana<br>f) istilahi lazima iwe na uwezo wa kuzalisha maneno zaidi kwa mnyambuliko<br>g) istilahi yafaa iwe fupi na yenye kueleweka<br>h) istilahi sharti iepuke maana ya matusi-iwe yenye stara<br>i) istilahi sharti ifuate muundo unaokubalika wa kimatamshi na kisarufi wa lugha ilimoundwa<br><br>ONYESHA, kwa kutumia vigezo hivi jinsi gani istilahi zifuatazo zimekidhi au hazikukidhi<br>ANDIKA kigezo/vigezo (a,b,c,d, e,f,g,h,au i ambavyo unafikiri istilaji imesadifu kwenye nafasi iliyotolewa | 4:<br>KAMA huzitumii istilahi zilizo-orodheshwa, Je ISTILAHI ZIPI UNAZITUMIA BADALA YAKE? |
|---|---|---|---|---|
| (1a) vimadende<br>(1b) vitambaza<br>(1c) vilainisho | | | | |
| (2a) kitendwa<br>(2b) yambwa<br>(2c) kishamirishi | | | | |
| (3a) kijalizo<br>(3b) kielezo<br>(3c) kikamilishi | | | | |
| (4a) usawazisho wa matamshi<br>(4b) uwiano wa irabu<br>(4c) upatanisho wa irabu | | | | |
| (5a) kiwakilishi<br>(5b) kijina<br>(5c) kibadala/ pronomino | | | | |
| (6a) kitamkwa<br>(6b) sauti<br>(6c) fonimu | | | | |
| (7a) majina<br>(7b) nauni<br>(7c) nomino | | | | |
| (8a) mchakato<br>(8b) mfanyiko<br>(8c) mnyumbusho | | | | |
| (9a) kidaka tonge<br>(9b) epiglotisi | | | | |
| (10a) kiingizi<br>(10b) kishangao<br>(10c) kihisishi | | | | |
| (11a) silabi<br>(11b) mizani | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (12a) viigizi<br>(12b) vielezi miigo<br>(12c) idiofoni | | | | |
| (13a) umaizilugha<br>(13b) uwezolugha<br>(13c) umilisi lugha | | | | |
| (14a) kihusishi<br>(14b) kihusiano<br>(14c) kiunganishi | | | | |
| (15a) nazali<br>(15b) kipua<br>(15c) king'ong'o | | | | |
| (16a) kiima<br>(16b) kitendaji<br>(16c) faali | | | | |
| (17a) kiarifu<br>(17b) kifungu kitenzi<br>(17c) prediketa | | | | |
| (18a) ubebwaji<br>(18b) uchopekaji<br>(18c) umezaji | | | | |
| (19a) mkazo<br>(19b) shadda | | | | |
| (20a) vijenzi<br>(20b) viambajengo sisisi | | | | |
| (21a) Jozi bainifu<br>(21b) Jozi za sauti<br>(21c) Jozi za nitoe nikutoe | | | | |
| (22a) sintaksia<br>(22b) sarufi miundo | | | | |
| (23a) mzizi<br>(23b) kiini | | | | |
| (24a) abjadi<br>(24b) alfabeti | | | | |
| (25a) nyakati sahihi<br>(25b) njeo sahihi | | | | |
| (26a) intonesheni<br>(26b) kiimbo<br>(26c) mkokotoo | | | | |

SEHEMU YA PILI

**Kiambatisho cha 3: Kidadisi Juu ya Mtazamo wa Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili na Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu**

## 3.1 Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili

Jina la Mdadisiwa..............................................
Umri..............................................................
Uwana............................................................

1. Je, ulianza kufundishwa masomo ya Kiswahili wakati gani? [Kidato cha 1, 2, 3, 4. au chuoni mwaka wa 1, 2, 3, 4.]

2. Kwa nini ulianza kufundishwa Kiswahili katika kiwango hicho cha juu?

3. Je, unapata ugumu wowote katika kutumia maneno mapya ya Kiswahili?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana

4. Kwa kuwa vitabu vingi vya Kiswahili vya rejea ni vya Kiingereza, je, unapataje visawe vya Kiswahili vya dhana za Kiingereza? [weka alama **x** kwenye jibu faafu)
[ ] Ninatumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) (1981)
[ ] *Kamusi ya Isimu na Lugha* (1990) ya TUKI
[ ] *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*, TUKI (1996) n.k.
[ ] Ninaunda mwenyewe istilahi za isimu na kuzitumia
[ ] Ninatohoa istilahi za Kiingereza kwa Kiswahili

5. Endapo umeshaisoma na kuitumia *Kamusi ya Isimu na Lugha* (TUKI 1990), je, maelezo ya istilahi yalitosheleza mahitaji yako?
[ ] Hapana [ ] Ndiyo
Iwapo **hapana** eleza ni kwa nini.

6. Je, unafikiri istilahi za isimu ya Kiswahili zinatosha?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana

7. Kama istilahi za isimu ya Kiswahili hazitoshi, unapendekeza pafanyike nini katika kujaza pengo lililoko.
[ ] Patumike istilahi za Kiingereza kama zilivyo
[ ] Istilahi za Kiingereza zinukuliwe katika Kiswahili
[ ] Wataalam wa Kiswahili waunde istilahi mpya za isimu ya Kiswahili kwa kuzingatia misingi ya kisayansi
[ ] Istilahi za zamani za Kiswahili zifufuliwe na kupanuliwa kimaana.

8. Je, unayo au umeshayaona machapisho yafuatayo ambayo yana istilahi za taaluma mbalimbali za Kiswahili:
(a) BAKITA (1976) *Tafsiri Sanifu*, Toleo la 2
(b) TUKI/Kapinga, M.C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*
(c) TUKI - *Mulika* Na. 16 na 23, *Kioo cha Lugha* UDSM

(d) TUKI - *Kiswahili*, Juzuu 51/1 na 51/2 (1984), Juzuu 58/1 na 58/2 (1991)
(e) Nkwera, F.V.M. (1978) *Sarufi na Fasihi*... DSM
(f) Mbaabu, I. (1992) *Sarufi ya Kiswahili* Longman Kenya
(g) Chimerah, R.M. (1998) *Kiswahili Past, Present & Future Horizons*
(h) Yote yaliyotajwa hapo juu.

9. Lugha ya Kiswahili inataka kujieleza katika kipengele cha isimu kwa kutumia Kiswahili. Juhudi hizo zitafaulu tu endapo:
[ ] Misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili itazingatiwa
[ ] Mbinu zalishi na ya kisayansi ya kuunda istilahi itatumiwa
[ ] Wanaleksikografia/waunda maneno wata kuwa wabunifu na kuepukana na ukopaji mwingi wa istilahi za kigeni.
[ ] Lugha hii itaendelezwa kiistilahi mumo kwa mumo kwa kuzingatia misingi teule ya kisayansi.
[ ] Yote yaliyotajwa hapo juu, ila ninaongeza kwamba...

10. Mbali na istilahi zilizochapishwa tayari kuna njia nyingine yo yote ambayo kwayo unajipatia istilahi za Kiswahili?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana
Kama jibu lako ni ndiyo, taja njia yenyewe.

11. Wewe ungependelea istilahi za isimu ya Kiswahili zitokane na lugha gani? [Zipange ukianza na ya 1, 2, 3, 4, hadi 5]
[ ] Kigiriki/ Kilatini (Kigiritini)
[ ] Kiswahili na lahaja zake
[ ] Lugha za Kibantu
[ ] Kiarabu
[ ] Kiingereza

12. Endapo utakopa istilahi kutoka Kiingereza, je, utapendelea istilahi hiyo iandikwe vipi? [Wekea alama **x** chaguo moja tu na toa sababu za chaguo hilo ikiwezekana]
[ ] Kufuatana na matamshi ya Kiingereza ya istilahi hiyo kama yanavyosikika na mzungumzaji wa Kiswahili (k.m. nyutroni, naitrojeni)
Sababu ........................................
[ ] Kufuatana na maandishi ya Kiingereza ya istilahi hiyo (nutroni, nitrojeni)
Sababu ........................................
[ ] Kufuatana na maandishi na pia maandishi ya Kiingereza ya istilahi hiyo (k.m. nitrojeni)
Sababu ........................................

13. Yaelekea baadhi ya waandishi wa vitabu vya Kiswahili, magezeti, walimu wa sekondari na wahadhiri wa vyuo vikuu hawajali **"usanifu" wa istilahi za Kiswahili** hivyo wanajiundia istilahi na kuzitumia. Je, wewe unapendekeza **hatua gani** ichukuliwe kukomesha jambo hili (uundaji kiholela)?
..................................................
..................................................

14. Wewe ungewashauri waundaji istilahi za Kiswahili watumie mbinu gani (yenye usayansi) ya kuunda istilahi zenye ukubalifu wa kimataifa? (Panga kwa upendeleo 1, 2, hadi 5)
[ ] Unyambuaji na uambishaji
[ ] Ufupishaji - Akronimu, uhulutishaji, na ukatizaji
[ ] Uambatanishaji
[ ] Ukopaji - kaleki na utohoaji
[ ] Upanuaji istilahi kimaana

15. Je, mbinu ya ukopaji ina umuhimu wowote katika kuendeleza istilahi za Kiswahili kwa wakati huu?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana
Sababu ..............................................

16. Wana **Jungu Kuu** (akina Sheikh Nabhany) wanasisitiza Kiswahili kipanuliwe kiistilahi kwa kufufua maneno asilia na kutafsiri maana ya viungo vidogo vidogo vya maneno kutokana na lahaja za Kiswahili. Je, una maoni gani kuhusu uendelezaji huo wa istilahi?
[ ] Ninawaunga mkono kwamba Kiswahili kiendelezwe mumo kwa mumo lakini wazingatie misingi teule ya kisayansi.
[ ] Nafikiri mbinu hiyo ya istilahi haifai, haina usayansi na inazidisha bure tatizo la wingi visawe.
[ ] Ninapendekeza......................................

17. Katika kuunda istilahi faafu na inayokubalika kimataifa wewe ungesisitiza vigezo gani vya kisayansi vitumike (panga upendeleo wa vigezo hivyo katika ngazi 9 (1, 2, 3, 4 ,5, hadi 9).
[ ] Ufupi wa istilahi - iktisadi
[ ] Uwezo wa istilahi kuzalisha maneno zaidi - uzalishaji
[ ] Uwezo wa istilahi kutotatanisha mtumiaji wake - udhahiri
[ ] Ujitoshelezaji wa istilahi kimaana - uangavu
[ ] Umataifa wa istilahi
[ ] Ustara wa istilahi - istilahi kuepuka utusani
[ ] Uundaji wa istilahi kufuatana na utaratibu maalum na utaratibu ulio sawa
[ ] Ulandaji wa muundo wa kimatamshi na kisarufi wa istilahi na ule wa lugha ya Kiswahili
[ ] Uundaji wa istilahi zisizo na wingi wa visawe

18. Wewe kama mtumiaji wa Kiswahili, unaweza kudai kwamba hupendi istilahi mpya ya Kiswahili kwa sababu:
[ ] Tayari kuna nyingine faafu ya kutumia aliyoizoea
[ ] Haelewi misingi ya kisayansi na mbinu iliyotumika kuiunda istilahi hiyo
[ ] Haina mwonjo/utamu
[ ] Hapendi muundo na matmshi yake
[ ] Mizizi ya istilahi haitokani na Kiswahili chenyewe
[ ] Yote yaliyotajwa hapo juu, ila naongeza kwamba....
.............................................
.............................................

19. Ili Kiswahili kiendelezwe kiistilahi na kiweze kujieleza katika kipengele cha isimu kikamilifu, wewe ungependekeza wataalam wa lugha hii wa Afrika Mashariki wafanye nini?

[ ] Wafufue Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ya uundaji na usanifishaji wa istilahi zenye ukubalifu wa kimataifa

[ ] Washirikiane katika kupiga msasa istilahi za Kiswahili

[ ] Watumie mbinu za kisayansi za kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili

[ ] Wachukue hatua nyingine kuongeza kwa zilizotajwa hapo juu (Taja hatua yoyote ikiwezekana)

20. Je, una ushauri wowote unaoweza kutoa kwa waundaji binafsi wa istilahi za Kiswahili popote walipo na kwa vyombo vya BAKIKE, BAKITA, TUKI, n.k. utakaosaidia katika kupunguza malalamiko juu ya udhaifu wa istilahi mpya za Kiswahili zinazoundwa?

..........................................................

..........................................................

### 3.2 Wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu

Jina la Mwanafunzi........................................
Umenke....................................................
Jina la Asasi ya Elimu....................................

1.(a) Je umewahi kujifunza somo la Isimu ya Kiswahili?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana

(b) Je, ulianza kujifundisha somo la isimu ya Kiswahili wakati gani?
[Kidato cha 1, 2, 3, 4. au chuoni mwaka wa 1, 2, 3, 4.]

2. Kwa nini ulianza kujifundisha isimu ya Kiswahili katika kiwango hicho cha juu?

3. Kama mwanafunzi wa isimu ya Kiswahili, ni vitabu vipi vya rejea unavyotumia kujifundishia (vitaje na ueleze kama vinatosha au la).

4. Kwa kuwa vitabu vingi vya isimu ya Kiswahili vya rejea ni vya Kiingereza, je, unapataje visawe vya Kiswahili vya dhana za Kiingereza? [weka alama **x** kwenye jibu faafu)
[ ] Ninatumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) (1981)
[ ] *Kamusi ya Isimu na Lugha* (1990) ya TUKI
[ ] *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*, TUKI (1996) n.k.
[ ] Ninaunda mwenyewe istilahi za isimu na kuzitumia
[ ] Ninatohoa istilahi za Kiingereza kwa Kiswahili

5. Endapo umeshaisoma na kuitumia *Kamusi ya Isimu na Lugha* (TUKI 1990), je, maelezo ya istilahi yalitosheleza mahitaji yako?
[ ] Hapana [ ] Ndiyo
Iwapo **hapana** eleza ni kwa nini.

6. Je, unafikiri istilahi za isimu ya Kiswahili zinatosha?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana

7. Kama istilahi za isimu ya Kiswahili hazitoshi, unapendekeza pafanyike nini katika kujaza pengo lililoko.
[ ] Patumike istilahi za Kiingereza kama zilivyo
[ ] Istilahi za Kiingereza zinukuliwe katika Kiswahili
[ ] Wataalam wa Kiswahili waunde istilahi mpya za isimu ya Kiswahili kwa kuzingatia misingi ya kisayansi
[ ] Istilahi za zamani za Kiswahili zifufuliwe na kupanuliwa kimaana.

8. Je, unayo au umeshayaona machapisho yafuatayo ambayo yana istilahi za taaluma mbalimbali za Kiswahili;
(a) BAKITA (1976) *Tafsiri Sanifu*, Toleo la 2
(b) TUKI/Kapinga, M.C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*
(c) TUKI - *Mulika* Na. 16 na 23, *Kioo cha Lugha* UDSM
(d) TUKI - *Kiswahili*, Juzuu 51/1 na 51/2 (1984), Juzuu 58/1 na 58/2 (1991)
(e) Nkwera, F.V.M. (1978) *Sarufi na Fasihi*... DSM

(f) Mbaabu, I. (1992) *Sarufi ya Kiswahili* Longman Kenya
(g) Chimerah, R.M. (1998) *Kiswahili Past, Present & Future Horizons*
(h) Yote yaliyotajwa hapo juu.

9. Lugha ya Kiswahili inataka kujieleza katika kipengele cha isimu kwa kutumia Kiswahili. Juhudi hizo zitafaulu tu endapo;
[ ] Misingi ya kisayansi ya uundaji wa istilahi za isimu ya Kiswahili itazingatiwa
[ ] Mbinu zalishi na ya kisayansi ya kuunda istilahi itatumiwa
[ ] Wanaleksikografia/waunda maneno wata kuwa wabunifu na kuepukana na ukopaji mwingi wa istilahi za kigeni.
[ ] Lugha hii itaendelezwa kiistilahi mumo kwa mumo kwa kuzingatia misingi teule ya kisayansi.
[ ] Yote yaliyotajwa hapo juu, ila ninaongeza kwamba...

10. Mbali na istilahi zilizochapishwa tayari kuna njia nyingine yo yote ambayo kwayo unajipatia istilahi za isimu ya Kiswahili?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana
Kama jibu lako ni ndiyo, taja njia yenyewe.

11. Wewe ungependelea istilahi za isimu ya Kiswahili zitokane na lugha gani? [Zipange ukianza na ya 1, 2, 3, 4, hadi 5]
[ ] Kigiriki/ Kilatini (Kigiritini)
[ ] Kiswahili na lahaja zake
[ ] Lugha za Kibantu
[ ] Kiarabu
[ ] Kiingereza

12. Endapo utakopa istilahi kutoka Kiingereza, je, utapendelea istilahi hiyo iandikwe vipi? [Weka alama **x** chaguo moja tu na toa sababu za chaguo hilo ikiwezekana]
[ ] Kufuatana na matamshi ya Kiingereza ya istilahi hiyo kama yanavyosikika na mzungumzaji wa Kiswahili (k.m. nyutroni, naitrojeni)
Sababu ............................................
[ ] Kufuatana na maandishi ya Kiingereza ya istilahi hiyo (nutroni, nitrojeni)
Sababu ............................................
[ ] Kufuatana na maandishi na pia maandishi ya Kiingereza ya istilahi hiyo (k.m. nitrojeni)
Sababu ............................................

13. Yaelekea baadhi ya waandishi wa vitabu (vya isimu ya Kiswahili), magezeti, walimu wa sekondari na wahadhiri wa vyuo vikuu hawajali **usanifu wa istilahi za Kiswahili** hivyo wanajiundia istilahi na kuzitumia. Je, wewe unapendekeza **hatua gani** ichukuliwe kukomesha jambo hili (uundaji kiholela)?

14. Wewe ungewashauri waundaji istilahi za isimu ya Kiswahili watumie mbinu gani (yenye usayansi) ya kuunda istilahi zenye ukubalifu wa kimataifa? (1, 2, hadi 5)

[ ] Unyambuaji na uambishaji
[ ] Ufupishaji - Akronimu, uhulutishaji, na ukatizaji
[ ] Uambatanishaji
[ ] Ukopaji - kaleki na utohoaji
[ ] Upanuaji istilahi kimaana

15. Je, mbinu ya ukopaji ina umuhimu wowote katika kuendeleza istilahi za Kiswahili kwa wakati huu?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana
Sababu ..................................................

16. Wana **Jungu Kuu** (akina Sheikh Nabhany) wanasisitiza Kiswahili kipanuliwe kiistilahi kwa kufufua maneno asilia na kutafsiri maana ya viungo vidogo vidogo vya maneno kutokana na lahaja za Kiswahili. Je, una maoni gani kuhusu uendelezaji huo wa istilahi?
[ ] Ninawaunga mkono kwamba Kiswahili kiendelezwe mumo kwa mumo lakini wazingatie misingi teule ya kisayansi.
[ ] Nafikiri mbinu hiyo ya istilahi haifai, haina usayansi na inazidisha bure tatizo la wingi visawe.
[ ] Ninapendekeza...

17. Katika kuunda istilahi faafu na inayokubalika kimataifa wewe ungesisitiza vigezo gani vya kisayansi vitumike (panga upendeleo wa vigezo hivyo katika ngazi 9 (1, 2, 3, 4 ,5, hadi 9).
[ ] Ufupi wa istilahi - iktisadi
[ ] Uwezo wa istilahi kuzalisha maneno zaidi - uzalishaji
[ ] Uwezo wa istilahi kutotatanisha mtumiaji wake - udhahiri
[ ] Ujitoshelezaji wa istilahi kimaana - uangavu
[ ] Umataifa wa istilahi
[ ] Ustara wa istilahi - istilahi kuepuka utusani
[ ] Uundaji wa istilahi kufuatana na utaratibu maalum na utaratibu ulio sawa
[ ] Ulandaji wa muundo wa kimatamshi na kisarufi wa istilahi na ule wa lugha ya Kiswahili
[ ] Uundaji wa istilahi zisizo na wingi wa visawe

18. Mtumiaji wa Kiswahili hudai kwamba **hapendi istilahi mpya** ya Kiswahili kwa sababu;
[ ] Tayari kuna nyingine faafu ya kutumia aliyoizoea
[ ] Haelewi misingi ya kisayansi na mbinu iliyotumika kuiunda istilahi hiyo
[ ] Haina mwonjo/utamu
[ ] Hapendi muundo na matmshi yake
[ ] Mizizi ya istilahi haitokani na Kiswahili chenyewe
[ ] Yote yaliyotajwa hapo juu, ila naongeza kwamba...

19. Tatizo la **wingi wa visawe** vya istilahi za Kiswahili linatokana na nini?
[ ] Ukosefu wa misingi ya kisayansi ya kuundia istilahi za Kiswahili
[ ] Uundaji kiholela wa istilahi za Kiswahili
[ ] Uhuru katika uteuzi wa lugha changizi
[ ] Yote yaliyotajwa hapo juu, ila naongeza...

20. Ili Kiswahili kiendelezwe kiistilahi na kiweze kujieleza katika kipengele cha isimu kikamilifu, wewe ungependekeza wataalam wa lugha hii wa Afrika Mashariki wafanye nini?

[ ] Wafufue Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ya uundaji na usanifishaji wa istilahi zenye ukubalifu wa kimataifa

[ ] Washirikiane katika kupiga msasa istilahi za Kiswahili

[ ] Watumie mbinu za kisayansi za kuunda istilahi za isimu ya Kiswahili

[ ] Wachukue hatua nyingine kuongeza kwa zilizotajwa hapo juu (Taja hatua yoyote ikiwezekana)

21. Je, una ushauri wowote unaoweza kutoa kwa waundaji binafsi wa istilahi za Kiswahili popote walipo na kwa vyombo vya BAKIKE, BAKITA, TUKI, n.k. utakaosaidia katika kupunguza malalamiko juu ya udhaifu wa istilahi mpya za Kiswahili zinazoundwa?

22. Je, una ushauri wowote unaoweza kutoa kwangu (kama mtahiniwa na mtafiti katika eneo la istilahi za isimu ya Kiswahili)?

..........................................................

..........................................................

**Kiambatisho 3.3: Mahojiano Juu ya Mtazamo wa Waandishi (wa Vitabu na Magazeti) na Watangazaji Redioni na Televisheni**

## 3.3.1 Mahojiano na Waandishi wa Vitabu na Magazeti

Jina la Mwandishi......................................
Umenke.................................................
Umri...................................................
Tarehe ya Mahojiano....................................

**Maswali ya Mahojiano**

1. Je, wewe huandika vitabu/magazeti
   [ ] Ndiyo [ ] Hapana

2. Unatumia lugha gani katika kuandika vitabu/magazeti? Na ni kwa nini?
   [ ] Kiswahili [ ] Kiingereza [ ] za Kiafrika
   [ ] yoyote

3. Je, wasomaji wako hufurahishwa na lugha unayoitumia katika kuandika vitabu/magazeti? Ikiwa jibu ni la, toa sababu

4. Je, unaweza kunieleza ni kwa nini idadi ya wasomaji wa vitabu/magazeti ya Kiswahili ni ndogo ikilinganishwa na ya wasomaji wa vitabu/magazeti ya Kiingereza? [weka x kwenye jibu faafu]
   [a] Lugha inayotumiwa ni ngumu kueleweka
   [b] Mikabala hasi ya muda mrefu kuhusu lugha hii
   [c] Matumizi na uteuzi mbaya wa istilahi/maneno
   [d] Mtindo wa uchapishaji ni chapwa
   [e] Yote yaliyotajwa hapo juu

5. Kama mwandishi wa vitabu, ni vitabu vipi vya Kiswahili vya rejea unavyotumia kuandikia? Vitaje na ueleze kama vinatosha au la
   ...................................................
   ...................................................

6. Kwa kuwa magazeti/vitabu vingi vya isimu ya Kiswahili vya rejea ni vya Kiingereza, je, unapataje visawe vya Kiswahili vya dhana za Kiingereza? [Weka / kwenye jibu mwafaka]
   [ ] Ninatumia Kamusi za Kiswahili
   [ ] Ninaunda mwenyewe istilahi za isimu na kuzitumia
   [ ] Ninatohoa istilahi za Kiingereza kwa Kiswahili

7. Inaonekana kwamba baadhi ya waandishi (wa vitabu na magazeti) hujiundia na kutumia istilahi zao za Kiswahili kwa sababu ya upungufu wa istilahi zilizopo. Je, una maoni gani kuhusu uundaji huu huria wa istilahi
   ...................................................
   ...................................................

8. Ni kwa sababu gani watumiaji hutumia maneno/istilahi zingine kwa urahisi na **hukataa** istilahi mpya zinazoundwa na watu binafsi au/na vyombo vya kukuza lugha vya BAKITA, BAKIKE na TUKI?

..................................................................

..................................................................

9. Mwandishi na msomaji/msikilizaji hudai kwamba hapendi istilahi mpya za Kiswahili kwa sababu:

[a] Tayari kuna nyingine 'faafu' ya kutumia aliyoizoea

[b] Haelewi misingi ya kisayansi na mbinu iliyotumika kuiunda istilahi hiyo

[c] Haina utamu/mwonjo

[d] Mizizi ya istilahi haitokani na Kiswahili chenyewe

[e] Yote yaliyotajwa hapo juu (ila naongeza kuwa

..................................................................

..................................................................

### 3.3.2 Mahojiano na Watangazaji Redioni na Televisheni

Jina la Mtangazaji.................................
Umenke.............................................
Umri...............................................
Tarehe ya Mahojiano................................

**Maswali ya Mahojiano**

1. (a) Je, umewahi kutangaza kwa kutumia lugha ya Kiswahili?
   [ ] Ndiyo [ ] Hapana

   (b) Kama jibu lako ni ndiyo, je, umeshiriki katika utangazaji kwa muda gani?
   ..........................................................
   ..........................................................

2. Endapo umeshaisoma na kuitumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na *Kamusi ya Isimu na Lugha* (1990), je, maelezo yalitosheleza mahitaji yako?
   [ ] Ndiyo [ ] Hapana

3. Kwa kuwa vitabu vingi vya isimu ya Kiswahili vya rejea ni vya Kiingereza, je, unapataje visawe vya Kiswahili vya dhana za Kiingereza? [Weka / kwenye jibu faafu]
   [ ] Ninatumia kamusi za Kiswahili
   [ ] Ninaunda mwenyewe istilahi za isimu na kuzitumia
   [ ] Ninatohoa istilahi za Kiingereza kwa Kiswahili

4. Yaelekea baadhi ya watangazaji redioni na televisheni hawajali 'usanifu' wa Kiswahili hivyo wanajiundia istilahi/maneno na kuyatumia. Je, wewe una maoni gani kuhusu uundaji kiholela wa maneno?
   ..........................................................
   ..........................................................

5. Wewe ungeshauri waundaji istilahi za isimu ya Kiswahili watumie mbinu gani? (Tumia mpangilio 1,2,3,4 hadi 5)
   [ ] Unyambuaji na uambishaji
   [ ] Ufupishaji - akronimu, uhulutishaji na ukatizaji
   [ ] Ukopaji na utohoaji
   [ ] Ufufuaji na upanuaji kimaana wa maneno asilia na ya Kibantu
   [ ] Kaleki na uradidi

6. Wasikilizaji wa vipindi vya Kiswahili redioni na televisheni hudai kwamba hawapendi istilahi/maneno mapya yanayotumiwa kwa sababu:
   [a] Tayari kuna maneno mengine 'faafu' ya kutumia waliyoizoea
   [b] Hawaelewi misingi ya kisayansi na mbinu zilizotumika kuyaunda maneno hayo

[c] Hayana ladha/mwonjo
[d] Mizizi ya maneno hayatokani na Kiswahili chenyewe
[e] Yote yaliyotajwa hapo juu (ila naongeza kwamba ............................................................ ............................................................)

7. Je, una ushauri wowote unaoweza kutoa kwa waundaji istilahi za Kiswahili popote walipo utakaosaidia katika kupunguza malalamiko juu ya udhaifu wa istilahi mpya zinazozalishwa? ............................................................ ............................................................

**Kiambatisho 3.4: Kidadisi Juu ya Mtazamo wa Wahadhiri wa Kiswahili wa Chuo Kikuu**

Jina la Mhadhiri: ..................................
Umenke:.............................................
Jina la Asasi ya Elimu: ............................

1.(a) Je umewahi kufundisha somo la Isimu ya Kiswahili?
[ ] Ndiyo [ ] Hapana

(b) Je, ulianza kufundisha somo la isimu ya Kiswahili wakati gani?
[Kidato cha 1, 2, 3, 4. au chuoni mwaka wa 1, 2, 3, 4.]

2. Kwa nini ulianza kufundisha isimu ya Kiswahili katika kiwango hicho cha juu?

3. Kama mhadhiri wa isimu ya Kiswahili, ni vitabu vipi vya rejea unavyotumia kufundishia (vitaje na ueleze kama vinatosha au la).

